Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Thelathini na Saba - Tarehe 1 Agosti, 2008**

(*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*)

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2008/2009.

**MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani Kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 317

## Majengo ya MMEM Kisasiga

**MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna dalili na matumaini ya kuwa na mwekezaji katika eneo la *Kisasiga Ranch,* na kwa kuwa, katika eneo hilo kuna Majosho na Maboma ambayo yalijengwa na wananchi katika Utekelezaji wa Mipango ya MMEM:-

Je, hayo majengo ya MMEM yatafanyiwa utaratibu gani kutokana na kuwa Kisasiga sasa inatafutiwa mwekezaji na wananchi pia watahamishwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Ranch* ya Kisasiga ipo katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ambapo lipo Jimbo la Uchaguzi la Bukene. *Ranch* hii ilianzishwa mwaka 1972 ikimilikiwa na lililokuwa Shirika la Maendeleo la Wilaya ya Nzega (*Nzega Development Corporation Limited (NZEDECO).* Mwaka 1972 Shirika la *NZEDECO* liliomba ardhi yenye ukubwa wa ekari 40,000 kwa ajili ya ufugaji wa Ng'ombe wa maziwa na kuwanenepesha ng'ombe hao.

Mwaka 1973 shirika hilo liliomba kuongezewa ukubwa wa ardhi kutoka ekari 40,000 hadi ekari 115,200 na kukubaliwa na Kamati ya Maendeleo ya Mipango ya Wilaya wakati huo kwa kuwa Shirika lilikuwa linahitaji kupata mkopo kutoka Benki ya Dunia katika kuendeleza *Ranch* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ranch ya Kisasiga yapo maboma na vyumba vya madarasa ambavyo vilijengwa na wananchi kinyume na msimamo wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. Kwa hiyo, wananchi hao walisimamishwa kuendelea na ujenzi huo.

Vilevile hakuna Shule ya Msingi katika *Ranch* hiyo inayotambulika kumilikiwa na Halmashauri ya wilaya ya Nzega. Kuhusu majosho yaliyopo hii ni sehemu ya miundombinu ya Ranchi iliyojengwa na *NZEDECO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji na uendelezwaji wa eneo la Ranchi ya Kisasiga Mkurugenzi wa Maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nzega aliagiza kwa barua yenye Kumb. Na. *D.3/20/141* ya tarehe 6 Novemba, 1979 wananchi wote waliokuwa wakiishi na kufanya shughuli mbalimbali katika eneo la *Ranch* ya Kisasiga wahamie maeneo mengine nje ya Ranchi. Hadi tarehe 7 Juni, 2007 taarifa ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega inaonyesha kuwepo kaya 831 zilizokadiriwa kuwa na wananchi 5,141 na mifugo kama vile Mbuzi 3,141, Kondoo 835, na Ng'ombe 16,910.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega mnano tarehe 29/9/2007 alitoa tena notisi kuwataka wananchi wanaoishi katika eneo la *Ranch* kuhama. Notisi hiyo ilisogezwa mbele hadi tarehe 30/6/2008 kuwapa nafasi wananchi wanaoishi katika eneo hilo wawe wamehama nakuhamisha mali zao. Hadi hivi sasa wananchi hao hawajahama kama ilivyoelekezwa.

**MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu hayo ambayo yanaonekana kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri hajapata historia kamili mpaka leo hii.

Kwa kuwa, zimetengwa pesa kwa ajili ya kupima upya eneo la Kisasiga na kwa kuwa wananchi na kufuatana na Sheria ya Ardhi Vijijini ya mwaka 1999 wamekubaliana kwamba vijiji hivyo viko *registered* tangu 1970 na *NZEDECO* ilikuwa *registered* tangu 1972. Kwa hiyo, wale siyo wavamizi ni haki yao kwa sababu walikuwa *registered.* Na kwa hivyo basi, pesa zile zimetengwa sasa hawatakiwi kuondoka kabla ya tarehe 30 mpaka waonyeshwe maeneo ya kuhamia.

Je, Serikali lini itawaonyesha vijiji na vitongoji viliyokuwa *registered* na makubaliano ya wananchi pamoja na Serikali ya Halmashauri ya *DC* yaliyofanyika kwenye Mkutano wao ambao unafuata Sheria ya Ardhi….

**MWENYEKITI – MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Swali sasa!

**MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lini Serikali itawapangia mahali pa kwenda na kugawa ardhi hiyo ili waondoke kama kijiji na vitongoji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapa *concern* ya Mheshimiwa Mbunge sisi tunaiona, tunafahamu kabisa kwamba yeye ni sehemu ya mpango huu wa kuanzisha hiyo ranchi ambayo tumeizungumza hapa ambayo imepitishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. Lakini wakati huohuo tunajua pia kwamba *concern* yake ni kuhakikisha kwamba wale wananchi wanatendewa haki.

Swali hapa lilikuwa linahusu yale maboma yaliyopo kule ndani pamoja na yale majosho yaliyopo ndani. Zimetolewa notisi mara mbili hapa zikiwataka hawa wananchi waende nje hii si maana ya kwamba wanatoka nje ya yenyewe, maana yake ni kwamba wanakwenda pembeni kwa hiyo lile eneo linakuwa limetwaliwa linawekwa pembeni ranchi inabakia na eneo kama ranchi ili tusije tukachanganya mambo pale.

Tumewasiliana mara mbili au tatu na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nzega , nina hakika kabisa kwamba kama hawa wananchi watakuwa wameondoka katika maeneo haya mapema watakapokuwa wamefanya hivyowakati huohuo mpango utakuwa umewekwa kwa sababu eneo lile lililowekwa pembeni pale ni kwa ajili ya wale wananchi pale. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu ashirikiane na Halmashauri yake waweke vizuri mpango wake na kama watahitaji msaada wetu kutoka *Centre* hapa tutasaidiana ili kuweza kuona haya yanayozungumzwa kama yanatekelezwa.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, ranchi iliyoko *West Kilimanjaro* ambayo inapakana na Longido na Siha imekaa muda mrefu bila kutumika na wananchi wamevamia, wameingia na kuwa eneo la mifugo. Je, Serikali itahalalisha lini eneo hilo ili liwe la wananchi ambao wanatumia mpaka sasa?

**MWENYEKITI – MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu! Na ninaomba uwe makini kwa sababu linahusu Siha.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kama ulivyosema naomba kwanza ni- *declare interest* kwamba mimi ndiyo Mwakilishi na Mbunge wa wananchi wa Siha na eneo na eneo linalozungumzwa hapa nalifahamu vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliohusika katika mpango mzima wa kuona kwamba eneo hili sasa linachukuliwa kwa maana ya kubinafsisha na kuona pia wananchi watapata maeneo gani lilikuwa ni Shirika ambali lilikuwa linaitwa *PSRC* ambalo sasa hivi halipo. Utaratibu huu wote sasa umehamia katika Wizara ya Fedha na Uchumi ambayo ndiyo kwa kweli inayosimamia na kuratibu mipango yote hii.

Bado mimi nafahamu kwamba mpango huu unaendelea na wakati utakapofika kwamba wadau wote tumehusishwa katika jambo hili ninaamini kwamba haya anayoyazungumza Mheshimiwa Michael Laizer, yatakuwa yamefanyika kwa utaratibu huu ninaozungumza.

Na. 318

**Kuboresha Kituo cha Madaba**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kituo cha Afya cha Madaba katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea kinategemewa sana katika kutoa huduma kwa wananchi wa Kata zilizo karibu na kwa

kuwa Kituo hicho cha Afya kiko katika barabara kuu ya Songea – Njombe – Makambako, ambapo mara nyingi kunatokea ajali na matukio mengine yanayohitaji upasuaji;

Je, Serikali iko tayari kuongeza huduma ya chumba cha upasuaji na vifaa vyake ili kusaidia matukio yanayohitaji upasuaji wa haraka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista J. Mhagama Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mwongozo wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Kituo cha Afya kinapaswa kuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa wagonjwa wa kulazwa *(IPD)*, Wagonjwa wa nje *(OPD)*, huduma za mama na mtoto, huduma za maabara na upasuaji mdogo (*minor surgery*). Huduma za upasuaji mkubwa (*major surgery*) zinapaswa kutolewa katika ngazi ya hospitali. Aidha, kulingana na mwongozo wa ramani za majengo ya vituo vya Afya, Kifuto cha Afya, Kituo kinapaswa kuwa na chumba kimoja kwa ajili ya upasuaji mdogo (*minor surgery*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kituo cha Afya cha Madaba kinatoa huduma wa wagonjwa wa kulazwa, wagonjwa wa nje *(OPD)*, huduma za mama na mtoto, huduma za maabara, na pia huduma za ushauri nasaha, upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa hiari na utoaji wa dawa za kurefusha maisha kwa watu walioambukizwa virusi vya UKIMWI. Huduma za upasuaji mdogo hasa kwa wajawazito zimekuwa zikifanyika pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwa na matukio ya ajali katika barabara kuu ya Songea-Njombe- Makambako, ambapo pengine majeruhi hao wangeweza kupata huduma za upasuaji katika Kituo cha Afya cha Madaba. Majeruhi wengi wanaotokana na ajali hizo mara nyingi wanakuwa wakihitaji upasuaji mkubwa na kwa ajili hiyo hatua za haraka za kuwasafirisha majeruhi hawa kwenda hospitali ya Mkoa wa Ruvuma zimekuwa zikifanyika wa kutumia *ambulance* ya Kituo hiki cha Madaba. Kwa kutambua tatizo hilo, Serikali inaviwezesha vituo vya Afya vilivyoko katika maeneo maalum (*Strategic position*) kutoa huduma za upasuaji mkubwa ikiwa ni pamoja na kupanua vituo hivyo ili viweze kuwa na chumba kwa ajili ya upasuaji mkubwa, kupeleka wataalam na vifaa vya upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za upasuaji zinahitaji vifaa maalum na pia wataalam wenye sifa zinazostahili. Kwa ajili ya upasuaji mkubwa katika vituo vya Afya ni lazima kuwepo na daktari Msaidizi mmoja na mtaalamu wa dawa za usingizi (*anaesthetist*) Ofisi yangu itawasiliana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuona uwezekano wa kutoa huduma kama anavyopendekeza Mheshimiwa Mbunge wa Peramiho.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Songea inategemea kuweka katika mipango na Bajeti ya mwaka 2009/2010 Bajeti kwa ajili ya ujenzi wa chumba cha upasuaji mkubwa katika kituo hicho cha Madaba.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba kituo hicho cha Afya kiko katika maeneo ambayo ni muhimu sana kuweza kuokoa maisha ya watu wengi wanaotumia barabara hiyo ya Songea kwenda Njombe na urefu wa kutoka hapo Madaba kwenda Songea ni takriban kilomita zisizopungua 200.

Sasa Mheshimiwa Waziri anakubaliana na mimi kwamba ombi hili ni muhimu sana na kwa kuwa hatuwezi kuwaacha majeruhi walioumia vibaya eti wasafirishwe na ambulance mpaka hospitali ya Mkoa badala ya kupewa upasuaji wa haraka kuokoa maisha yao katika kituo kile cha madaba? Je, yuko tayari sasa kuharakisha zoezi hilo?

La pili, kwa kuwa Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma wameona kabisa kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kusaidia huduma hiyo ya upasuaji katika Kituo cha Afya cha Madaba.

Je, Wizara sasa iko tayari kuja kukaa na wataalamu wetu na waganga wetu katika hospitali ile ya Ruvuma na kukamilisha huo mkakati mahususi wa kukipa uwezo kituo hicho cha Afya cha Madaba kutoa huduma kubwa zaidi kuliko zile zinazotolewa sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista J. Mhagama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu anaouzungumza Mheshimiwa Jenista Mhagama ni muhimu na ni utaratibu unaofanana na ule utaratibu tunaoutumia katika ile Hospitali ya Tumbi ambapo wagonjwa wakipata ajali pale tunawasaidia pale pale, ndicho anachozungumza hapa. Kwa hiyo, sipati taabu sana kumwelewa anachozungumza.

Utaratibu huo huo anauzungumzia sasa kwenye kituo cha Madaba ambapo historia inaonyesha kwamba kuna matatizo yanatokea pale yaani ajali zinatokea na kwa hiyo kuwasaidia.

Wala sihitaji kufikiri sana wala ku-*consult* katika jambo hili, hili jambo ni *obvious* kwamba tukiweka huduma pale itasaidia wananchi wale na ndiyo maana nakubaliana naye kwamba kuna haja ya Wizara yetu kwa maana ya kwa niaba ya Waziri Mkuu pamoja na Wizara ya Afya kukaa kwa haraka sana na kuimarisha kituo hiki kwa sababu kituo hiki kiko pale kinachotakiwa ni Chumba cha Upasuaji tu pale. Mimi niko tayari

kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili kuona kwamba huduma hii inapatikana kwa ajili ya wananchi wetu.

Na. 319

**Upatikanaji wa Maji Safi Karagwe**

**MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MHE. GOSBERT B. BEGUMISA)** aliuliza:

Kwa kuwa, Wilaya ya Karagwe imejaliwa kuwa na maziwa na mito yenye maji mengi wakati wote yakiwamo Maziwa ya Kajunju, Songambele, Burigi, Kaberenge na Mto Kagera na kwa kuwa, Jimbo la Karagwe hasa katika Kata za Nyakasimbi, Rugu, Ihembe, Nyakakika, Kibondo, Nyabiyonza na Kiruruma. Pia Kata za Ihanda, Nyakahanga, Bugene, Kayanga, Ndama, Kihanga, Kituntu, Igurzwa na Bweranyange hazina maji safi:-

(a) Je, Seirikali ina mkakati gani wa kuvuna maji ya Maziwa ya Kajunju Burigi, Kaberenge kwa faida ya wananchi wa Jimbo la Karagwe?

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Rais aliwaahidi wananchi wa Karagwe maji safi. Je ahadi hiyo itatekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Jimbo la Karagwe, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa *program* ya Maendeleo ya Sekta ya Maji itakayotekelezwa mwaka 2006-2025. Katika *Program* ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, Wilaya ya Karagwe imeandaa vijiji 13 vitakavyohusika katika hatua ya kwanza ya utekelezaji wa program. Vijiji hivyo vitafanyiwa uchunguzi na usanifu ikifuatiwa na ujenzi wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kati ya Vijiji 13 vilivyochaguliwa na Halmashauri ya Wilaya ili kutekeleza *program* ya Kuendeleza Sekta ya Maji katika hatua ya kwanza, vijiji vitano vya Chabuhora, Nyakakika, Chamchuzi, Nyakahanga na Chanika na Miji miwili midogo ya Kayanga na Bugene. Vipo katika Jimbo la Karagwe. Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe tayari imekwishapata kibali cha kuendelea na

mchakato wa kupata mapendekezo ya Kampuni zitakazofanya usanifu wa miradi ya maji. Matarajio yetu ni kwamba mchakato huo utakuwa umekamilika ifikapo Septemba, 2008 na kufuatiwa na utekelezaji halisi. Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ndiyo inayofahamu vizuri Vijiji vya kupewa kipaumbele, ili kutumia vyanzo vya maji ambavyo ni maziwa ya Kajunju, Songambele, Burigi, Kaberenge na Mto Kagera, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe inashauriana na kumwelekeza Mtaalamu Mshauri atakayepatikana na kuzingatia matumizi ya maji katika vyanzo alivyotaja. Serikali inaendelea kutekeleza ahadi ya kuwapatia wananchi Karagwe maji safi na salama. Kwa mfano, Mwezi Juni 2007, Serikali ilitoa Shilingi 349,886,000/= kwa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe. Fedha hizo zimetumika katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2007/2008 kufanya ukarabati wa miradi ya maji ya mtiririko sita, visima virefu na vifupi 48 kwenye Kata 24. Ujenzi wa mradi mpya mmoja wa maji ya mtitiriko na ujenzi wa vituo 9 vya kuchotea maji katika miradi miwili. Kata zinazohusika katika utekelezaji wa miradi hiyo ni Ndama, Kihanga, Ihembe na Kiruruma.Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Serikali ilitoa shilingi 179,950,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika vijiji vya Nyakasimbi, Kimuli, Rugera, Rukukraicho, Nyamaiaga, Kihinda na Kano. Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inaendelea kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maji, kuna matatizo ya Halmashauri kuchelewa kutumia fedha hizo kutokana na kushindwa kufuata taratibu za manunuzi na wakati mwingine uwezo mdogo wa Wakandarasi wa kuekeleza miradi ya maji. Namwomba Mheshimiwa Mbunge tusaidiane kufuatilia utekelezaji halisi wa miradi kwa kutumia fedha zilizotajwa katika sehemu (b).

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Serikali yetu ni makini naamini kabisa itatekeleza azma yake ya kupelekea Wilaya ya Karagwe maji.

Kwa kuwa, tatizo la maji lililopo maeneo ya Karagwe yanafanana kabisa na matatizo yaliyopo katika Mji wa Namtumbo sababu mitambo ya kusukumia maji mji wa Namtumbo kwa sababu iliyopo Kata ya Rwinga Daraja la Migeregere imekufa na Mamlaka ya Maji Mji wa Namtumbo tumeiomba Serikali ituweke katika mradi wa kufufua na kuendeleza miundombinu ya maji katika Miji.

Je, Serikali ipo tayari kuuweka Mji na Wilaya ya Namtumbo katika mradi huo mwaka 2008/2009?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita R. Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nafurahi kwamba mji wa Namtumbo tayari unayo Mamlaka ya Maji na Mamlaka hiyo pia inayo Bodi inayoendesha shughuli zile za maji safi na maji taka.

Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu sasa tumeanza kutekeleza mradi huu ambao unafadhiliwa na *World Bank,* mambo yote ambayo yanatakiwa kufanyika katika Halmashauri ile na katika Mji mdogo ule basi kipaumbele au vipaumbele vyote viandaliwe katika Halmashauri ya Wilaya na Mhandisi Mwelekezi atakayekuja wao ndiyo wamwambie kwamba tafadhali weka hiki na weka kile katika maandalizi.

Lakini pia nimshauri na nimwelekeze kwamba hatuwezi kupata washauri kila mahali tunachofanya sasa ni kujaribu kufanya *clusters* za maeneo.

Kwa hiyo, kwa Namtumbo basi mshauri atakayekuwa amepatikana katika miradi ya karibu kwa maana ya Wilaya na Mkoa basi huyo huyo apewe katika hadidu za rejea afanye haya anayoyaomba Mheshimiwa Mbunge.

Na. 320

**Hitaji la Huduma ya Simu – Mikumi**

**MHE. CASTOR RAPHAEL LIGALLAMA (K.n.y. MHE. CLEMENCE B. LYAMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, mawasiliano ya simu za mkononi yamechochea sana kuongezeka kwa ufanisi wa uzalishaji na biashara za mazao ya bidhaa vijijini na kwa kuwa Barabara ya km. 80 kutoka Mikumi hadi Kilosa inayofanyiwa upembuzi yakinifu hivi sasa ili kuwekwa lami na inapita katikati ya Kata za Mikumi, Zomba, Ulaya na Masanze zenye idadi ya watu wasiopungua 25,000; na kwa kuwa Kata za Uleling'ombe, Malolo na Vidunda, ni pweke ki-jiografia lakini zimesheheni bidhaa zenye sifa zote muhimu kiuchumi.

(a)Je, Serikali ainaweza kulieleza Bunge kuhusu hatua zilizofikiwa juu ya ombi la barua yangu iliyoambatanishwa na michoro ikiomba Serikali iyashawishi makampuni yenye mitandao ya simu kufunga minara kandokando ya Barabara hiyo ili kuboresha ufanisi wa mawasiliano utakaochochea Maendeleo Kiuchumi.

(b)Kwa kuwa, tayari wanavijiji wengi wanazo simu za mikononi na katika meneo ya Uleling'ombe na Vidunda wako tayari kushiriki katika kutoa mchango wa nguvu zao na malipo kidogo ili kuharakisha minara ya simu hizo. Je, Serikali iko tayari kufuatilia kwa karibu ili Kata hizo zipewe kipaumbele.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Beatusi Lyamba, Mbunge wa Mikumi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *CELTEL* inafanya tafiti za masoko katika maeneo hayo ili kupeleka huduma na kuondoa matatizo ya mawasiliano katika Kata hizo ifikapo mwezi Desemba, 2009.

Aidha, mara baada ya kumaliza tafiti za masoko katika maeneo hayo, kampuni ya *CELTEL,* itagharamia gharama zote za ujenzi wa minara katika meneo ya Uleling'ombe na Vidunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *VODACOM* imebaini maeneo husika pamoja na maeneo mengine yaliyo jirani hususani yale ya Kata za Mikumi, Zomba, Ulaya na Masanze na maeneo mengine yenye shughuli za kibiashara kama vile Msolwa. Tathmini ya kiufundi itafanyika ifikapo mwezi Desemba, 2008 kwa ajili ya kuweka mtambo (Mitambo) wa mawasiliano ili kukidhi mahitaji ya maeneo ya Kata za Mikumbi, Zomba, Ulaya na Masanze na mengine ya jirani.

Aidha, mwezi wa Aprili, 2008 Kampuni hiyo ilikamilisha utafiti wa kiufundi katika Kata ya Malolo na Vidunda na kabla ya mwisho wa Desemba 2008 inatarajia pia kufanya utafiti katika kata ya Uliling'ombe ili kubaini maeneo muafaka yanayokidhi vigezo vya kiufundi na kibiashara kwa ajili ya kujenga minara ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *ZANTEL* inaendelea kupanua mtandao wake katika meneo mengiya Tanzania katika awamu tatu. Katika awamu ya kwanza *Zantel* itafika katika maeneo ya Mikumi, Kidatu, Ifakara na Mahenge ifikapo mwezi Desemba, 2008 kwa kujenga minara mtatu ya mawasiliano. Maeneo mengine ya Tanzania yakiwemo ya Wilaya ya Mikumi yatafikiwa katika awamu zinazofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *TIGO* imekiri kupokea maombi mengi ya Mheshimiwa Mbunge na kutokana na umuhimu wa maeneo hayo kibiashara, kampuni hiyo imeyaweka katika mipango yake endelevu. Mwezi Machi, 2008 utafiti wa awali ulikamilika kwa ajili ya kubaini sehemu za kujenga minara ya mawasiliano itakayosambaza huduma za mawasiliano katika meneo ya Kata za Mikumi, Zomba, Ulaya na Masanze pamoja na maeneo ya jirani.

**MHE. CASTOR RAPHAEL LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, matatizo yaliyopo kimawasiliano katika Kata alizotaja Mheshimiwa Mbunge wa Mikumi yanafanana na matatizo yaliyopo Kata ya Uchindire, Taweta na idete katika Jimbo langu la Kilombero. Na kwa kuwa, maombi nilishawasilisha na kwa

kuwa sasa hivi Barabara ya kuunganisha Taweta na ile ya Njombe/Lupembe inamaliziwa kiasi cha kufanya watu wa pale kufungua biashara.

Je, katika maombi niliyowasilisha Waziri atanisaidia ili tupate mawasiliano ya simu haraka?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Castor Ligallama, kama ifuatavyo.

Napenda nikiri kwamba tayari Mheshimiwa Ligallama aliwasilisha kwangu maombi mbalimbali ya mawasiliano na simu katika maeneo ambayo ameyataja na tayari mawasiliano tumeshafanya na wahusika wote kuona ni namna gani wanaweza kusaidia maeneo hayo.

Lakini napenda nikiri kwamba napata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wenzangu Wabunge na ninajitahidi kwa kadri ninavyoweza kuona wanapata mawasiliano katika maeneo yao. (*Makofi*)

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ku-*declare interest* kabla ya kuuliza swali la nyongeza. Lakini kuna watafiti mbalimbali akiwemo mmoja anaitwa Mr. Tophlas Mlaki wamefanya utafiti wa kuangalia jinsi mawasiliano yanavyoweza kusaidia ukuaji wa uchumi katika vijiji. Maeneo ya Sengerema, Lugoba, Kilosa na wiki hii yuko Makambako na Njombe.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia watu kama hawa akina Mr. Mlaki katika juhudi za kuhakikisha kwamba wanaweka mawasiliano na kufuatilia tafiti ambazo wamezifanya ili kuongeza uchumi kwa watu vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, tunaomba majibu kwa makini.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nami ni-*declare interest* kwamba, Mr. Mlaki ni mwajiriwa wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ambaye yuko *COSTECH*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Rita kwamba tunamtumia Mr. Mlaki ipasavyo katika kupata ujuzi wake wa kusaidia mawasiliano vijijini. Yeye amehusika moja kwa moja katika masuala ya kupeleka *Telecentre* kule Sengerema na maeneo mengine. Kwa hiyo, tutaendelea kuchota Hazina ya Mr. Mlaki kuona wananchi wa Vijijini wanafaidika na teknolojia hii ya mawasiliano.

Na. 321

**Mali za Shirika la Simu *(TTCL)***

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA (K.n.y. MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa baada ya Serikali kurekebisha Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*), mali zote zisizohamishika za Shirika zilihamishiwa kwenye Kampuni ya Simu 2000 na kwa kuwa muda wa kuwepo Kampuni umekwisha kwa mujibu wa sheria:-

Je, ni mali zipi ziliuzwa na kampuni ya simu 2000 na ni kiasi gani cha fedha kilipelekwa Serikalini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Simu 2000 *Limited* ilianzishwa mwaka 2000 chini ya Sheria ya Makampuni *Cap*. 212. Majukumu ya Shirika hilo yalikuwa kama ifuatavyo:-

· Kuchukua mali za *TTCL* ambazo hazikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na biashara ya simu (*non-core assets*) kulingana na Tangazo la Serikali Na. 87 la Mwaka 2001 na baadaye Tangazo la Serikali Na.331 kwa ajili ya *Retained Assets* yaani mali ambazo *TTCL* iliruhusiwa kubaki nazo kwa muda wa miaka miwili tangu tarehe ya kusaini mkataba 23/2/2003 kabla haijaamuliwa kuzinunua au kuzirudisha simu 2000 *Limited*.

· Kuchukua dhamana na deni la wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kulingana na jedwali la pili la Tangazo la Serikali Na. 87.

· Kuchukua kesi za madai zilizokuwa Mahakamani kwa kupelekwa na *TTCL* au dhidi ya *TTCL* kulingana na kifungu Na. 5 cha Tangazo la Serikali Na. 87.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mali zilizohamishiwa Kampuni ya Simu 2000 *Limited* mali zisizohamishika ni:-

(i) Majengo 107 na viwanja 46.

(ii) Mali zilizobakizwa (*Retained Assets*) ni majengo nane na viwanja vitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya awali, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanzishwa kwa Kampuni hiyo (simu 2000) mwaka 2000 hadi ilipomaliza muda wake 31 Desemba, 2007 mali zilizouzwa ni:-

(1) Majengo 103 na viwanja 30.

(2) Fedha inayopelekwa Serikalini ni Sh. 18,327,520,531.90.

Kwa mchanganuo ufuatao:-

(1) Sh. 12,827,520,531.90 kwa ajili ya malipo ya wastaafu waliokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki waliohama Kampuni ya Simu Tanzania – fedha hii ililipwa *NSSF*.

(2) Sh. 5,500,000,000/= zililipwa Wizara ya Fedha kama gawio. Mali zilizobakia zimehamishiwa *Consolidated Holding Corporation* kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 2007. (*Makofi*)

Na. 322

**Mradi wa Kupeleka Umeme Shule ya Sekondari Soya**

**MHE. PASCAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Shirika la *TANESCO* ilianza kutekeleza mradi wa kufikisha umeme katika shule ya Sekondari ya Soya, Wilayani Kondoa na kwa kuwa mradi huo umesimama kwa muda hivi sasa:-

(a) Je, ni kwa nini mradi huo umesimama?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza mradi huo kama ilivyopangwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali kupitia Shirika la *TANESCO* ilianza kutekeleza mradi wa kufikisha umeme katika shule ya Sekondari ya Soya. Mradi huo ulikuwa unahusisha ujenzi wa njia kubwa ya umeme (*High Tension*) yenye urefu wa kilomita 0.8 hadi kwenye transfoma kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye transfoma iliyokuwepo baada ya kuwa na wateja wengi.

Vilevile, mradi ulihusisha ujenzi wa njia ndogo ya umeme (*Low Tension*) yenye urefu wa kilomita 0.8 kutoka kwenye transfoma na kusambazwa umeme kwenye maeneo mbalimbali. Mradi huo pia ulihusisha uwekaji wa transfoma ya *KVA* 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa baadhi ya vifaa vya kupunguzia nguvu ya umeme ikiwemo transfoma na nyaya za msongo mdogo (*Low Voltage Cable)* kutokana na ufinyu wa Bajeti ndiyo sababu iliyosababisha kusimama kwa mradi kabla ya kumalizika kwa muda wa miezi mitano uliowekwa.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Umeme la *TANESCO* imekwishakamilisha mradi huo wa kupeleka umeme katika shule ya sekondari ya Soya. Mnamo tarehe 30 Aprili, 2008 transfoma ilifungwa na kuwashwa umeme. Tarehe 20 Mei, 2008 Shule ya Sekondari ya Soya ilifungiwa umeme pamoja na nyumba za walimu watatu. Aidha, wananchi 26 wanaozunguka shule hiyo pia wamepatiwa umeme kupitia mradi huo. Mradi huo una jumla ya wateja thelathini na wananchi wanaendelea kulipia malipo ya kuunganishiwa umeme.

**MHE. PASCAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na naomba nilishukuru sana Shirika la *TANESCO* kwa kufanya kazi nzuri ya kuwaunganishia shule ya Sekondari ya Soya umeme wa uhakika.

Sasa swali, kwa kuwa kuna shule za sekondari nyingine sita ambazo ziko karibu sana na njia ya umeme, shule hizo ni Dalai, Goima, Songoro, Chandama, Mwailanje na Mrijo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ama Serikali itasaidia vipi ili kulishawishi Shirika la *TANESCO* ili kuziunganishia umeme shule hizo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru sana Mzee Degera kwa kufuatilia suala hilo ambalo baada ya swali lake kuulizwa mwezi Januari, mkazo ukafanyika na ufuatiliaji wa karibu, hatimaye shule hiyo kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuwa amewasilisha maombi ya Dalai, Goima, Songoro, Chandama Mrijo na Mwailanje na katika kuwasilisha maombi yake ametufahamisha kwamba umeme tayari umeshafika maeneo hayo ya karibu. Naomba nimfahamishe kwamba tumepokea na kwamba tutaiomba *TANESCO* ifanye kwanza tathmini ya gharama zinazotakiwa ili kufikisha umeme katika shule hizo hasa ikizingatiwa kwamba Mheshimiwa Degera ameshatufahamisha kwamba kuna mahitaji ya umeme kwa ajili ya maabara na kadhalika. Vitu ambavyo vinaboresha huduma ya elimu kwa ajili ya shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba atupe muda tufanye tathmini tumepokea, tutawapa *TANESCO* watupe maelekezo ya gharama zinazohitajika na tutaangalia kwenye vyanzo vitakavyotokana na ziada vya *REA* ambao ni Wakala wa Nishati Vijijini na tutalifanyia tathmini. Tutaendelea kuwasiliana na tunalifanyia kazi.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali vilevile iliahidi

kupeleka umeme kwenye shule ya Sekondari ya Iguguno ambayo ni kilomita moja tu kutoka njia kuu na tathmini ilishafanywa na niliahidiwa kwamba mwaka huu wa fedha ndiyo watapeleka umeme. Je, Serikali inasemaje juu ya hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ahadi ilitolewa, tumepokea ombi la kupeleka umeme katika shule ya Sekondari ya Iguguno na tumejiwekea malengo ya kwamba tutapeleka umeme huo katika kipindi cha Bajeti cha mwaka huu 2008/2009.

Na. 323

**Kupeleka Umeme Katika Kiwanda cha Samaki cha Nyamisati**

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kiwanda cha Kuhifadhia Samaki cha Nyamisati kinategemewa sana na wavuvi wadogo wadogo wanaozalisha samaki aina ya Kamba (*prawns*) na kwa kuwa kiwanda hicho kimeshindwa kufanya kazi kutokana na matumizi makubwa na gharama kubwa za mafuta ya jenereta:-

(a) Je, Serikali kupitia mpango wake wa usambazaji umeme vijijini iko tayari kupeleka umeme kiwandani hapo ili kuboresha mapato ya wavuvi hao na Taifa kwa ujumla?

(b) Kama Serikali ipo tayari. Je, ni lini utekelezaji wake utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kufikisha umeme katika Kijiji cha Nyamisati mahali ambapo Kiwanda cha Samaki kimejengwa ni Sh. 1.68m/=. Umeme utakaopelekwa katika Kijiji cha Nyamisati utatokea Kijiji cha Bungu ambapo kutapita njia ya msongo wa *KV* 33 utakaozalishwa kwa kutumia gesi asilia ya Songosongo katika kituo cha kuzalisha umeme wa Somanga Fungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hicho cha fedha kitatumika katika ujenzi wa njia ya msongo wa *KV* 33 yenye urefu wa kilomita arobaini na tano kutoka Bungu hadi Nyamisati. Vilevile, fedha hizo zitatumika kuweka transfoma ya *KVA* 200 katika Kijiji cha Nyamisati pamoja na ujenzi wa njia ya umeme ya *three phase* ya *Voltage* 400/240 yenye urefu wa kilometa moja kwa ajili ya kusambaza umeme katika Kijiji cha Nyamisati. Hivyo, Kiwanda cha Kuhifadhia Samaki cha Nyamisati kitapatiwa umeme mara baada ya umeme kufika katika Kijiji cha Nyamisati.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo utagharamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*). Aidha, tumewaagiza *REA* na *TANESCO* wakae waandae mpango kwa vipaumbele vya miradi ya upelekaji umeme vijijini. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Jimbo lake wavute subira.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kwa kufanya upembuzi yakinifu na kutoa majibu yanayoridhisha kutokana na upelekwaji wa umeme katika Kijiji cha Nyamisati lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa kuna utata mkubwa wa kupitisha umeme hasa katika Daraja la Mkapa katika Mto Rufiji baina ya Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Nishati. Je, Waziri ataniambia kama Serikali imeshakubaliana namna ya kuuvusha umeme huo katika Daraja lile la Mkapa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mradi huu ulikwama kwa maeneo mawili. Moja ulikwama kwa sababu ya ucheleweshaji wa kukamilisha kile kituo cha Somanga Fungu lakini pia katika tathmini iliyokuwa inafanywa na wataalam kuhusu kuvusha nyaya za umeme juu ya daraja tulikuwa tunatofautiana kidogo, wataalam wengine wanasema ni jambo ambalo haliathiri uimara wa daraja na wengine wanasema linaathiri uimara wa daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Abdul Jabiri Marombwa na wananchi wote wanaotegemea kufaidika na mradi huo kwamba, tayari tunaendelea kukaa na tumekaa na wataalam wa *NORAD* tumelinganisha na maeneo mengine ambayo utaalam huo wa kuvusha umeme juu ya madaraja umefanywa na tumefikia hatua sasa kwamba tunafikia kwenye usuluhishi wa tatizo hili na tunaamini kwamba tutapata ufumbuzi wa tatizo hili kwa gharama ambayo ni ndogo na kwa ufanisi mkubwa ili kuwezesha umeme huu kuvuka kwa haraka iwezekanavyo.

Na. 324

**Ulinzi wa Waandishi wa Habari**

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa Waandishi wa Habari ni watu muhimu sana kwenye maendeleo ya nchi na kwa kuwa wapo Waandishi wa Habari ambao wanapelekwa kwenda kuandika habari za kivita (vitani) kwenye nchi jirani, mipakani na hata kwenye chaguzi za nchi jirani na hapa nchini ambapo hukabiliana na vitisho mbalimbali vya uonevu, kupigwa na kuvunjiwa vyombo vya kutendea kazi zao:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwalinda Waandishi wa Habari kwa kuwawekea bima ya ajali na maisha hasa pale wanapopelekwa nje kuandika habari za vita na migogoro ya nchi jirani?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Waandishi wa Habari ni watu muhimu kwa maendeleo ya nchi na hivyo basi wanastahili kuwa na Bima.

Mikakati ya Serikali katika kuwalinda Waandishi wa Habari ili wawe na bima ya ajali ya maisha ni pamoja na kutoa ushauri kwa taasisi zote za umma na watu binafsi ambazo hazina sera inayohusiana na bima ya ajali au utaratibu wa kuwahudumia Waandishi wanaowaajiri, kuhakikisha kuwa wanafanya hivyo.

Aidha, kwa wale Waandishi wanaojitegemea nao wanalazimika kujiwekea bima ya ajali na maisha ili wanapopata matatizo wakati wakiwa kazini ndani na nje ya nchi waweze kupata huduma zote wanazostahili kupewa. (*Makofi*)

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kumwuliza hivi, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba, Waandishi wa Habari ni watu muhimu sana na kwamba wanastahili kuwekewa bima ya ajali na maisha kutokana na kazi zao ngumu wanazozifanya. Je, ni vyombo gani vya habari vilivyowawekea bima ya ajali na maisha Waandishi wao wa Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa kuna baadhi ya vyombo vya habari ambavyo haviwawekei bima ya ajali na maisha Waandishi wao. Je, Serikali inatoa kauli gani dhidi ya wamiliki wa vyombo hivyo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba Waandishi wa Habari nchini kote na duniani kote wapo takriban wa aina tatu.

Kuna Waandishi wanaojitegemea, wapo wanaoajiriwa na Mashirika na taasisi binafsi na kuna Waandishi ambao wanaajiriwa na shirika la umma kama vile hapa kwetu, magazeti ya Serikali, *TBC* na vyombo vingine kama vile *ITV*, *Star TV* na wengine. Makundi haya yote yana taratibu za uajiri. Kwa hiyo, inatakiwa kila kundi mwajiri aweke bima kwa ajili ya wanaohusika. Hiyo ni sera au utaratibu wa kuajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kila Mwandishi wa Habari anapoajiriwa analazimika kuwekewa bima na aliyemwajiri. Hiyo ipo kwenye taratibu zao za kuajiri.

Kwa hiyo, napenda kusema kwamba, makundi haya yote ni lazima yaweke bima kwa ajili ya Waandishi wao kwa sababu ni watu muhimu na wanafanya kazi nyeti

ambayo inahitaji kupata msaada kama huo. Kwa hiyo, ningependa nitoe wito tena mzito kweli kweli kwamba, waajiri wote waliowaajiri Waandishi wa Habari iwe ni vyombo vya umma au binafsi ni lazima wawawekee bima Waandishi wa Habari ili angalau waweze kupata msaada wa kuwasaidia. (*Makofi*)

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru na kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake muhimu. Lakini ametutajia makundi matatu ya waandishi wa Habari, wale wanaojitegemea, wanaoajiriwa na vyombo binafsi na wa mashirika mbalimbali. Lakini Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba hivi sasa kuna makanjanja wamevamia sekta hii ya uandishi wa habari?

Sasa ili kulinda hadhi ya Tanzania isije kutokea kama ilivyotokea kwa Rais wa Zambia kutangazwa kuwa amekufa lakini yuko hai. Mheshimiwa Waziri anaweza kuliambia Bunge hili Wizara yake inachukua hatua gani kuwazuia makanjanja ili wasiendelee kupotosha Taifa letu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kabisa kwamba kumezuka wimbi la Waandishi Makanjanja ambao hawana weledi yaani *professionalism* ya kuandika shughuli za uandishi.

Lakini nataka nimhakikishie kabisa kwamba, Serikali imelitambua hilo na ndiyo maana tunaleta sheria hapa Bungeni, sheria mpya ambayo itaweza kutatua matatizo yote kwa sababu vigezo vyote vitawekwa humo ili tuweze kuwa na sifa za Mwandishi wa Habari. Tutakapofikia hapo basi hawa makanjanja watajifuta wenyewe. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Swali langu lilikwenda sambamba na mwenzangu aliyeuliza sasa hivi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Haroub Said Masoud.

Na. 325

**Wanamuziki wa Tanzania**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa wachezaji wa mpira wa miguu wanaotaka kwenda nje ya nchi kucheza mpira wa kulipwa wanapangiwa utaratibu mzuri na *TFF* jambo linalosaidia kuwatambua wachezaji walioko na idadi yao:-

(a) Je, kwa upande wa wanamuziki wetu wa Tanzania ni vikundi vingapi viko nje vikifanya shughuli zake za muziki?

(b)Kama utaratibu wa kuwasajili wanamuziki wanaokwenda nje kuimba haupo. Je, Serikali haioni kuwa, sasa ipo haja ya kufanya hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na utaratibu uliopo wa wanamuziki wetu wa Tanzania kwenda nje ya nchi kufanya shughuli zao za muziki, kwa sasa hakuna kumbukumbu zozote za kimaandishi zinazoonyesha idadi ya vikundi kutoka Tanzania vinavyofanya shughuli zake za muziki nje ya nchi. Kwa mujibu wa utaratibu huo, kikundi au vikundi vilivyopata mialiko kutoka nje ya nchi au vikundi kutoka nje ya nchi vinapotaka kuja hapa nchini, huomba kibali kutoka Kamati Maalum iliyoundwa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii inayoongozwa na Mwenyekiti ambaye ni Mkurugenzi wa Utamaduni, hukaa kila yaletwapo maombi kutoka kwa vikundi vya Muziki vya hapa nchini au nje ya nchi. Wajumbe wa Kamati wanatoka Baraza la Sanaa la Taifa, Idara ya Uhamiaji, Chama cha Hakimiliki (*COSOTA*), Mamlaka ya Mapato (*TRA*) na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kiamtaifa.

Baada ya kupitia maombi yaliyoletwa na kikundi au vikundi vya ndani au nje ya nchi, Kamati hiyo hufanya maamuzi ya kukubali au kukataa kutoa kibali kutokana na sababu zitakazojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna wanamuziki wanaofanya maskani ya kudumu uko nje kwa shughuli za muziki, hawakupata kibali kupitia Wizara yangu. Hata hivyo, ni jambo jema wanamuziki hao kusajiliwa katika Balozi zetu endapo nao wenyewe watapenda.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa yeye mwenyewe amekiri kwamba hakuna kumbukumbu zozote za kimaandishi zinazoonyesha idadi ya vikundi vilivyo nje na kwa kuwa wanamuziki ni mali sana hasa wakiwemo na wanenguaji na kwa kuwa wanapopelekwa nje bila maandishi wanaofaidika na ajira hiyo au wanaofaidika na mali zao ni wale wanaowachukua peke yao. Je, Serikali haioni kwamba utaratibu unaotumika *TFF* na wao waanze kuutumia mara moja ili kuwahami wananchi wetu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na yeye kabisa kwamba ni lazima tuwe na utaratibu kama wanaofanya *TFF* wa kuwa na usajili maalum kwa wasanii wetu wanapotoka nje.

Suala hili tunalichukua ni suala zuri, tutalifanyia kazina ile Kamati yetu inayohusika na kuchambua maombi basi itakapofikia kimetungwa kitu kinachohusika na utaratibu maalum tutakuwa tunakitumia hicho.

Na. 326

**Sifa za Askari wa Jeshi la Kujenga Taifa**

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati Serikali ikijibu swali Na. 86 ilisema kuwa kuwapeleka Askari nchi za nje kushiriki na kusaidia ulinzi kunahitaji fedha nyingi na vifaa vya kisasa:-

(a) Je, elimu kwa askari wetu kwenda kufanya kazi nje siyo kikwazo?

(b) Je, Serikali inaweza kueleza wastani wa elimu ya askari wetu?

(c) Je, mpaka leo Serikali bado inaajiri askari wa Jeshi kwa sifa ya urefu na umbile tu?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa Chakechake, kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajeshi kwa ujumla wanapoingia jeshini lazima wawe na sifa ya kuanzia elimu ya msingi, sekondari hadi elimu ya juu. Wanajeshi pia hupatiwa mafunzo ya ujuzi mbalimbali wawapo kazini ambayo pia huwasaidia wanapohitajika kwenda kufanya kazi za ulinzi wa amani nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) hapo juu wastani wa elimu ya askari wetu ni kuanzia elimu ya msingi hadi elimu ya juu.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, JWTZ huajiri askari toka JKT, kigezo cha urefu na maumbile ni baadhi tu ya sifa wanazotakiwa kuwa nazo vijana wanaojiunga na JWTZ.

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kupeleka askari nje ni gharama sana. Je, baada ya vita Serikali yetu inafaidika nini kutoka katika nchi tunakowapeleka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Naibu Waziri amesema urefu ni moja katika sifa za kumwajiri askari. Je, Wizara haioni kwamba ni ubaguzi wa maumbile kwani askari wafupi hawawezi kuwa askari wazuri?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ukitilia maanani Mwenyekiti ni mfupi. (*kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza niseme katika shughuli za Kimataifa nchi yetu inashirikiana na Jumuiya ya Kimataifa ukiwemo Umoja wa Mataifa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika na hivyo mara nyingi tunaposhughulika na shughuli za kulinda amani gharama zetu zinafidiwa na nchi hizo. Lakini vile vile tumejenga mahusiano na nchi nyingine ambazo tunazisaidia na pia tumejenga uzoefu wa askari wetu kwa kwenda kujifunza zaidi nje ya nchi katika kujifunza kwa vitendo. Urefu na maumbile ni baadhi tu ya sifa ambazo zinahitajika katika Jeshi. Urefu unahitajika na ufupi pia unahitajika kutegemea kazi inayofanyika, kwa hiyo wote tunawahitaji.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa niwafahamishe pamoja na ufupi wangu mimi ni askari *AK 952* (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuuliza ni jinsi gani elimu hii ya ulinzi inawafikia wananchi wote tukianzia na watoto wa shule ya msingi au wanapomaliza sekondari kwani ulinzi ni jukumu la wananchi wote. Mwanzoni tulikuwa tunapata nafasi ya kwenda JKT, hali hiyo sasa hivi imefikia vipi kushirikisha wanafunzi wanaohitimu ili waweze kupata mafunzo hayo na kuweza kuwa walinzi wa awali katika maeneo yao?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kutoa elimu kwa raia wote kwa kuzingatia kwamba ulinzi ni wajibu wa kila Mtanzania na kwa sababu hiyo ndiyo maana tumesema kuanzia mwaka 2010 tunarudisha upya utaratibu wa JKT. Lakini vile vile tunatoa wito kwa watu wetu wengine wanaohusika wakiwemo Walimu katika maeneo mbalimbali kuendelea kuwafundisha wanafunzi wetu kuhusu umuhimu wao katika ulinzi wa Taifa lao.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge maswali yameulizwa kisayansi, majibu hivyo hivyo na Mwenyekiti ameongoza kisayansi muda wetu wa maswali umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo tuingie kwenye matangazo. Niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho Jumamosi kutakuwa na Semina ya Wabunge wote itakayoanza saa nne na nusu asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Semina hiyo, inahusu Sera na Sheria ya Ushindani, utetezi wa mradi na vita dhidi ya bidhaa bandia nchini waandaji wa semina hiyo ni Tume ya Ushindani *(Fair Competition Commission).* Pia ningependa kuwatangazia kwamba mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge saa saba leo Waheshimiwa Wabunge wote mpitie Ukumbi wa Pius Msekwa ili mpate makabrasha yote ya semina ya kesho ili msome vizuri, kesho mkija kwenye semina ifanyike semina fupi ya kisayansi.

Tangazo la kikao Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *LAAC* anaomba Wajumbe wote wa Kamati yake, leo tarehe 1 kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo saa 5.00 asubuhi katika ukumbi Namba 231 ghorofa ya pili, jengo la Utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Abdisalaam Khatib, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara kwamba leo saa 5.00 Kamati hiyo itakuwa na kikao chake ukumbi Namba 432 ghorofa ya nne jengo la Utawala.

Mheshimiwa Kamishna William Shellukindo Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini anawatangazia Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati leo tarehe 1 Agosti, 2008 saa 5.00 asubuhi chumba Namba 227 ghorofa ya pili jengo la utawala.

Mheshimiwa Hamza Mwenegoha Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Fedha na Uchumi anaomba wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo Ukumbi Namba 428 ulioko ghorofa ya nne jengo la Utawala muda saa 4.30 asubuhi hii.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira inaombwa kukutana Ukumbi Namba 227 kuanzia saa 7.00 mchana huu. Kesho kama mnavyojua mmeshasambaziwa ratiba. Kesho ni ile siku ambayo ni ratiba ya *Cargo Stars Five Kilometer VIP Race* ambayo tunaifanya kila mwaka mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Joel Bendera Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawatangazieni wote msisahau hiyo kesho kwamba saa 12.00 asubuhi katika uwanja wa Jamhuri hadi viwanja vya Bunge Waheshimiwa Wabunge wote tutaanza mbio za kilomita 5 za *VIP Race.*

Pia Mheshimiwa Bendera anasema Mgeni rasmi ni Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye naye kesho atakimbia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, narudia tena hapo Mgeni Rasmi wa mbio hizo ni Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda Waziri Mkuu ambaye na yeye atavaa trakisuti na kukimbia kesho. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tuwe pamoja ili tumpe moyo Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu.

Ratiba imeshagawiwa kama nilivyosema na inaorodhesha mambo yote ya kesho, vifaa vyote vya mbio za kesho raba, tisheti, kofia na bahasha kwa ajili ya kesho vitagawiwa leo saa 10.00 jioni katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Msikose kupitia pale ili mvipate wote.

Sasa kuhusu wageni waliotutembelea wapo wageni wa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Job Ndugai, wageni 28 kutoka Mashirika

yasiyokuwa ya Kiserikali yanayoshughulikia ufugaji ambao nikiwataja naomba wasimame ambao ni pamoja na *Pingos Forum.*

Wageni waliokuja kupitia *Pingos Forum* simameni ambao ni hao hapo. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni kutoka *Legal and Human Rights Centre* tunashukuru. Tuna wageni kutoka Haki ardhi, *TAFGO, CODES* na *ADUTALO,* tuna *HIMWA,* tuna *PAICO DEO* na wapo pia wafugaji kutoka Mikoa wa Mbeya na Manyara na Arusha.

Wapo wageni wafugaji 14 wageni wa Mheshimiwa Ole Telele wa kutoka Ngorongoro sijui kama walifanikiwa kuingia humu ndani. Natumaini watakuwa wako njiani.

Mheshimiwa Ephraim Madeje ana wageni 30 ambao ni Kwaya ya Safina ya Kanisa Kuu la Aglikana Dodoma, wakiongozwa na viongozi wafuatao. Kwanza kwaya ya Safina. Karibuni sana Kwaya ahsanteni mnaweza kukaa.

Viongozi wa Kwaya hiyo ni Ndugu yangu Elia Ngalya, Isaac Chalo na Mama Mwita. Viongozi karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Hamza Mwenegoha Gasper Njuu *Director of Corporate Banks City Bank Tanzania Limited* wapo *Speakers Lounge* karibu sana Mkurugenzi. Pia Frank Omar *Head of Public City Bank* karibuni sana Ndugu zetu Viongozi wa Benki.

Wageni wa Mheshimiwa Kaika Telele nimeshawatamka, na wapo pia waandaji wa semina yetu ya kesho wanaotoka Tume ya Ushindani ambao wataendesha semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote kesho. Naomba wote msimame hapo mlipo. Karibuni sana Dodoma, Waheshimiwa Wabunge wanasubiri kwa hamu semina itakayotolewa hapo kesho. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mwisho, pia ningependa kuwatambulisha wanafunzi kutoka shule ya msingi Kikuyu B wanafunzi 40 pamoja na walimu wao msimame hapo mlipo karibuni sana wanafunzi muone na kujifunza demokrasia katika nchi yenu inavyoendeshwa. Leo karibuni sana na wakati mwingine. Ahsanteni sana walimu kwa kuwaleta watoto hawa. (*Makofi*)

Sasa tunaendelea na Shughuli za Bunge. Katibu tuendelee na *Order Paper.*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 – Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo ikiwa ni Bunge la Bajeti la Tatu kwa Serikali ya Awamu ya Nne.

Aidha, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa inayohusu Wizara yangu iliyowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji, lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu na kuthibitishwa kwa kura nyingi na Bunge lako Tukufu.

Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude P. Rwakatare na Mheshimiwa Dr. Christine Gabriel Ishengoma na Mbunge aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais; Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir. Pia, nampongeza Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, kwa kushinda katika Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Kiteto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu Chacha Zakayo Wangwe aliyekuwa Mbunge wa Tarime; Marehemu Salome Mbatia aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto, pamoja na Marehemu Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo Kiteto.

Aidha, na Waheshimiwa Wabunge wote waliofiwa na ndugu zao, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maelezo juu ya hali ya maendeleo ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi nchini, naomba kutumia nafasi hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika maandalizi ya bajeti hii. Kamati ilitoa ushauri na maoni kwa Wizara yangu ambayo yamezingatiwa katika kuandaa bajeti hii. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu itazingatia na kutekeleza maoni, ushauri na mapendekezo yatakayotolewa na Kamati pamoja na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb) kwa hotuba yake nzuri yenye kutoa mwelekeo wa shughuli zitakazotekelezwa na Serikali

mwaka 2008/2009. Vilevile, nampongeza Waziri wa Fedha na Uchumi pamoja na Mawaziri wote waliotangulia kwa hotuba zao nzuri ambazo zimeainisha maeneo mbalimbali tunayoshirikiana katika kutoa huduma za kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia masuala ya maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi kupitia hotuba zilizotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa Mawaziri walionitangulia Mheshimiwa Anthony Diallo (Mb) aliyeongoza iliyokuwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na naibu wake Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa (Mb) na Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe (Mb) aliyeongoza Wizara ya Maliasili na Utalii ilikokuwa Sekta ya Uvuvi pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Zabein Mhita (Mb) kwa maendeleo yaliyofikiwa katika sekta hizi mbili. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali halisi ya Sekta za Mifugo na Uvuvi. Kutokana na Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2007, sekta ya mifugo imekua kwa asilimia 2.4 kama ilivyokuwa mwaka 2006 na imechangia asilimia 4.7 katika pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 4.8 mwaka 2006.

Hali hii inatokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi za sekta nyingine pamoja na kutokea kwa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa (*Rift Valley Fever (RVF*) ulioathiri mifugo, soko la mifugo na mazao yake. Aidha, sekta ya uvuvi imekua kwa asilimia 4.5 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2006 na imeendelea kuchangia asilimia 1.6 katika pato la Taifa mwaka 2007 kama ilivyokuwa katika miaka ya 2005 na 2006. Hali hii imetokana na kuendelea kwa vitendo vya uvuvi haramu, uharibifu katika mazalia ya samaki na matumizi ya zana duni za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na takwimu zilizopo nchi yetu ina zaidi ya ng’ombe milioni 18.8, mbuzi milioni 13.5, kondoo milioni 3.6, nguruwe milioni 1.4 na kuku wa asili milioni 33 na wa kisasa milioni 20.

Aidha, ulaji wa mazao ya mifugo kwa sasa ni wastani wa kilo 11 za nyama, lita 41 za maziwa na mayai 64 kwa mtu kwa mwaka. Vilevile, ulaji samaki ni wastani wa kilo 6.9 kwa mtu kwa mwaka. Viwango hivi bado viko chini sana ikilinganishwa na vinavyopendekezwa na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani *(FAO)* vya kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa, mayai 300 na kilo 10.96 za samaki kwa mtu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007 kulikuwa na wavuvi wadogo (*artisanal fishers*) 163,037 na wavuvi wa kibiashara 199 waliojihusisha na uvuvi kwa kutumia vyombo vya uvuvi 51,714 ambapo tani 328,690.0 za samaki zenye thamani ya shilingi bilioni 327.4 zilivuliwa. Kati ya hizo, tani 327,218.34 sawa na asilimia 98.7 zilivuliwa na wavuvi wadogo (Jedwali Na. 1). Aidha, tani 57,795 za samaki na mazao yake pamoja na samaki hai wa mapambo 25,502 waliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa shilingi bilioni 7.6 (Jedwali Na. 2a na 2b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha Sekta hizi kuchangia zaidi katika pato la Taifa, Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Uvuvi kulingana na Tamko la Sera ya Taifa ya

Uvuvi ya mwaka 1997 na Mpango Madhubuti wa Maendeleo ya Mwani wa mwaka 2005 iko kwenye hatua mbalimbali. Pia, Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo Nchini (*Livestock Sector Development Strategy (LSDS*) na Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Ukuzaji wa Viumbe kwenye Maji (*National Aquaculture Development Strategy (NADS*) inaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Bajeti katika mwaka 2007/2008. Ukusanyaji wa Maduhuli. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu ilikusanya shilingi 9,340,946,544 kutokana na vyanzo mbalimbali sawa na asilimia 102.7 ya lengo. Kati ya hizo, shilingi 1,036,801,000 kutoka Sekta ya Mifugo na shilingi 8,304,145,544 kutoka Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi. Katika mwaka 2007/2008, iliyokuwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo iliidhinishiwa jumla ya shilingi 22,397,516,000. Kati ya hizo, shilingi 12,621,516,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 9,776,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi 6,931,332,000 kwa ajili ya matumizi mengine (OC) na shilingi 5,690,184,000 kwa ajili ya mishahara (PE). Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo, shilingi 1,424,000,000 zilikuwa fedha za ndani na shilingi 8,352,000,000 fedha za nje.

Aidha, katika kipindi hicho, Sekta ya Uvuvi iliyokuwa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ilitengewa jumla ya shilingi 25,559,366,120. Kati ya hizo, shilingi 5,918,164,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 19,641,200,120 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 9,200,000,000 kwa ajili ya Tanzania Bara na shilingi 10,441,200,120 kwa ajili ya Zanzibar. Pia, kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi 4,966,117,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengine (*OC*) na shilingi 952,047,000 ni kwa ajili ya mishahara (*PE*). Kwa upande wa Mifugo, hadi kufikia mwezi Juni 30, 2008, jumla ya shilingi 12,621,516,000 za fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi 5,632,673,688.37 za fedha za maendeleo zimetolewa na kutumika. Kwa upande wa sekta ya uvuvi, jumla ya shilingi 5,918,164,000 za fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 4,678,864,217 za fedha za maendeleo zimetolewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kazi zilizotekelezwa. Kazi muhimu zilizotekelezwa na Wizara yangu katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 ni pamoja na:-

(a) Sekta ya Mifugo. Ardhi, Maji na Malisho.

§ Kuhamasisha matumizi bora ya ardhi ya ufugaji iliyotengwa na kupima kiasi cha hekta 930,276 katika Wilaya 24 kwenye mikoa 10.
§ Kujenga uwezo wa wataalam 10 kuhusu matumizi endelevu ya Nyanda za Malisho kutoka wilaya za Monduli, Bahi, Kiteto, Kishapu, Singida, Kilwa, Rufiji, Mkuranga, Kisarawe na Lindi.

- § Kuimarisha mashamba ya kuzalisha mbegu bora za malisho ya Serikali na taasisi zake ambapo jumla ya tani 42.7 za mbegu aina mbalimbali za malisho na marobota 338,152 ya hei yamezalishwa. Aidha sekta binafsi imezalisha marobota 172,820 ya hei.

- § Kuratibu na kuhamasisha uzalishaji wa vyakula vya mifugo ambapo tani 717,231 zimezalishwa kutoka katika viwanda 74.

- § Kuratibu ujenzi na ukarabati wa malambo 158 kupitia miradi ya *PADEP* na *DADPs*.

- § Kutoa mafunzo kwa wakaguzi 20 wa vyakula vya mifugo kutoka Halmashauri 15 za Dodoma, Ilala, Ilemela, Iringa, Kibaha, Kinondoni, Mbeya, Morogoro, Moshi, Muheza, Nyamagana, Sumbawanga, Tabora, Tanga, na Temeke ili kuwawezesha kusimamia ubora wa vyakula vya mifugo.

(b) Uzalishaji na Usindikaji wa Maziwa.

- § Kuratibu na kuhamasisha uzalishaji wa maziwa ambapo lita bilioni 1.5 za maziwa zilizalishwa.

- § Kuhamasisha usindikaji wa maziwa ambapo zaidi ya lita milioni 24.1 zilisindikwa katika viwanda 31 nchini.

- § Kuhamasisha utekelezaji wa Programu ya Unywaji wa Maziwa Shuleni katika shule 63 zenye wanafunzi 23,350.

- § Kuratibu usambazaji wa mitamba 8,731 kutoka mashamba ya Serikali na Taasisi zake pamoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

- § Kununua mitamba 240 aina ya Boran kwa ajili ya kuimarisha mashamba ya kuzalisha mifugo ya Nangaramo, Kitulo, Sao Hill na Mabuki.

- § Kuzalisha dozi 69,085 za mbegu bora za uhimilishaji na kuhimilisha ng'ombe 55,253 na kutoa mafunzo kwa wataalamu 137 wa uhimilishaji.

(c) Uzalishaji na Usindikaji wa Nyama.

- § Kuratibu na kuhamasisha uzalishaji wa nyama ambapo tani 410,706 zilizalishwa.

- § Kuratibu na kuhamasisha uzalishaji wa vifaranga ambapo vifaranga milioni 32.6 vya kuku wa kisasa vilizalishwa na kuuzwa.

- § Kupitia *NARCO* kuuza ng'ombe 9,030 wenye thamani ya shilingi bilioni 2.1 na kununua ng'ombe 1,044 wenye thamani ya shilingi milioni 199.4 kutoka kwa wafugaji kwa ajili ya kunenepesha.

§ Kuimarisha ranchi za Kongwa na Ruvu kwa kuzinunulia ng’ombe wazazi 820 aina ya Boran na kuboresha miundombinu ya mashamba hayo.

§ Kukamilisha utoaji hati miliki (*sub lease*) kwa wawekezaji katika vitalu vya ranchi za Mzeri, Misenyi, Kitengule, Mkata, Kikulula, Mabale na Kagoma. Pia, zoezi la kukamilisha utoaji wa hati miliki kwa vitalu vya ranchi za Uvinza, Usangu na Kalambo linaendelea.

§ Kuendeleza mchakato wa kugawanya ranchi ya West Kilimanjaro ili *NARCO* ibakiwe na hekta 20,000 na hekta 10,364 zitagawanywa katika vitalu 23 ambavyo vitamilikishwa kwa wawekezaji chini ya umilikishaji mdogo.

§ Kuuza asilimia 51 ya thamani ya mali za machinjio ya kisasa ya Dodoma kwa Kampuni ya *National Investment Company Limited* (*NICOL*) ambapo mkataba kati ya *NARCO* na *NICOL* wa kuanzisha Kampuni mpya ya kuendesha machinjio hiyo umesainiwa.

§ Kufanya tathmini ya mapendekezo ya kiufundi *(technical competence)* ya wawekezaji binafsi watano (5) waliojitokeza kuingia ubia na *NARCO* katika ujenzi wa viwanda vya nyama ambapo wawekezaji watatu (3) wana sifa zilizohitajika.

§ Kukamilisha ubinafsishaji wa Kiwanda cha Kusindika Nyama cha Shinyanga kwa Kampuni ya *Triple “S” Beef Limited.*

(d) Biashara ya Mifugo na Mazao Yake.

§ Kuratibu na kuhamasisha biashara ya mifugo na mazao yake ambapo mauzo nje ya nchi yalifikia thamani ya shilingi bilioni 23.8.

§ Kuratibu ukusanyaji wa ngozi ambapo vipande vya ngozi milioni 2.5 vya ng’ombe, milioni 1.85 vya mbuzi na milioni 1.5 vya kondoo vyenye thamani ya shilingi bilioni 13.5 vilikusanywa kutoka kwa wazalishaji.

§ Kuongeza ukusanyaji wa ngozi (*recovery rate*) kutoka asilimia 50 hadi 75 na kutoa mafunzo kwa wadau 448 juu ya uzalishaji na uhifadhi bora wa zao la ngozi.

§ Kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi Nchini kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo (*Livestock Development Fund).*

(e) Mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo na Mazao yake.

§ Kukamilisha taratibu za kusajili katika mfumo wa kitaifa mashamba 26 ya mifugo yenye ng’ombe 42,902, mbuzi 3,793, kondoo 1,134 na nguruwe 574 na wafugaji wadogo 368 wa mbuzi wa maziwa wenye mbuzi 2,404.

§ Kusambaza nakala 125 za rejesta za kusajili wafugaji na mifugo katika wilaya 125 kwa ajili ya majaribio.

§ Kutoa mafunzo kwa wadau 164 kuhusu matumizi ya rejesta za kusajili wafugaji na mifugo.

(f) Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo.

§ Kuzindua Mkakati wa Tahadhari ya Kuzuia Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege tarehe 28 Aprili, 2008 uliofanywa na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

§ Kuchukua na kuchunguza sampuli 4,380 za ndege pori, kuku, bata na kanga dhidi ya Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege.

§ Kuchanja mifugo 4,741,614 dhidi ya Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa (*Rift Valley Fever - RVF*) na kutoa mafunzo kwa wataalam 79 kutoka mikoa 9 iliyoathiriwa na ugonjwa.

§ Kuchanja ng'ombe 2,813,492 ili kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe.

§ Kuendelea kufuatilia viashiria vya Ugonjwa wa Sotoka katika mikoa ya mpakani ya Arusha, Mara na Kagera kuthibitisha kuwa huru na ugonjwa.

§ Kudhibiti ugonjwa wa Homa ya Nguruwe katika vijiji na mitaa 14 katika Halmashauri za Mvomero na Kinondoni.

§ Kuchanja ng'ombe 2,518 dhidi ya Ugonjwa wa Mapele-Ngozi katika Halmashauri 37 nchini.

§ Kuzalisha dozi 24,680,200 za chanjo ya Ugonjwa wa Mdondo katika Maabara Kuu ya Taifa ya Mifugo – Temeke na kusambaza.

§ Kuratibu na kufuatilia ukarabati na ujenzi wa majosho 205 kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Plans – DADPs*).

§ Kununua na kusambaza dawa za ruzuku za kuogesha mifugo lita 59,122 katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

§ Kuhamasisha na kuratibu uchanjaji wa ng'ombe 76,233 dhidi ya ugonjwa wa Ndigana Kali.

- Kuendelea kuzalisha mbung'o katika Taasisi ya Utafiti wa Mbung'o na Nagana – Tanga aina za *Glossina pallidipes* (3,979), *G. austeni* (89,627), *G. brevipalpis* (439) na *G. morsitans centralis* (4,374) watakaohasiwa na kusambazwa kwa ajili ya kudhibiti Ugonjwa wa Nagana.

- Kununua dozi 50,000 za chanjo ya kudhibiti Kichaa cha Mbwa na kuzisambaza katika wilaya 26 nchini.

- Kufanya uchunguzi wa ng'ombe 3,079 dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba (*Brucellosis*).

- Kuendelea na utafiti na uzalishaji wa chanjo za Ugonjwa wa Kutupa Mimba, Kimeta na Chambavu katika Maabara Kuu ya Taifa ya Mifugo – Temeke.

(g) Uimarishaji wa Miundombinu ya Sekta ya Mifugo.

- Kujenga mnada na kukarabati minada 5 ya mifugo ya Meserani (Arusha), Buhigwe (Kigoma), Mhunze (Shinyanga), Pugu (Dar es salaam) na Kirumi (Mara).

- Kuongeza minada 16 katika mfumo wa utoaji wa taarifa za masoko ya mifugo (*Livestock Information Network Knowledge System-LINKS*).

- Kuimarisha na kukarabati vituo 2 vya karantini ya mifugo na 6 vya ukaguzi wa mifugo na mazao yake.

- Kuimarisha Maabara Kuu ya Taifa ya Mifugo – Temeke na Taasisi ya Utafiti wa Mbung'o na Nagana (*TTRI - Tanga*) kwa kuzipatia vifaa vya kisasa na vitendea kazi ili ziweze kufikia kiwango cha Kimataifa.

- Kuanzisha kituo kipya cha Utafiti wa Mifugo na Udhibiti wa Mbung'o na Nagana, mjini Kigoma.

- Kuimarisha vituo 4 vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo vya Kanda (*VICs*).

(h) Usimamizi na Utoaji Huduma za Mifugo.

- Kusajili madaktari 28, kuandikisha na kuorodhesha wataalam wasaidizi 123 na kusajili vituo 12 vya huduma ya mifugo.

- Kufanya ukaguzi wa vituo vya kutolea huduma 25, machinjio 21, mabanda ya ngozi 25 na maghala 23 ya kuhifadhia ngozi.

- Kuhakiki na kutangaza kwenye gazeti la Serikali madaktari wa mifugo 222 na wataalamu wasaidizi 731.

- Kutoa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wataalamu 78.

- § Kuhamasisha Halmashauri za wilaya 46 kufanya ukaguzi wa huduma za afya ya mifugo.
- § Kuboresha viwango vya taaluma ya veterinari katika mitaala ya kufundishia wataalamu katika vyuo 6 vya mafunzo ya mifugo na viwili vya sekta binafsi vya Igabilo na Simanjiro.

(i) Mafunzo na Huduma za Ugani.

- § Kutoa mafunzo kuhusu ufugaji bora kwa wafugaji 21,106 kutoka Wilaya 41.

- § Kugharamia mafunzo ya stashahada kwa wanachuo 1,006 katika vyuo sita vya mafunzo ya mifugo.

- § Kuchapisha na kusambaza kwa wadau wa mifugo vipeperushi 52,110, mabango 30,130 na vijitabu 13,200 vya ufugaji bora.

- § Kutayarisha na kurusha hewani vipindi 52 vya redio na 12 vya Televisheni kuhusu ufugaji bora.

- § Kuandaa na kusambaza miongozo miwili (2) kuhusu mbinu shirikishi za shamba darasa la mifugo na utoaji huduma za ugani wa mifugo.

(j) Utafiti wa Mifugo.

- § Kufanya uchambuzi wa koo za ng'ombe wa asili aina ya *Ufipa* (Rukwa), *Iringa Red* (Iringa), *Mbulu* (Arusha na Manyara) na *Ankole* (Kagera).

- § Kusambaza madume 85 aina ya Mpwapwa katika wilaya 4 za Iramba, Igunga, Mvomero na Simanjiro.

- § Kuendeleza utafiti wa ng'ombe wa maziwa na wa nyama, katika vituo vya Mpwapwa, Tanga na Uyole ili kuongeza uzalishaji.

- § Kuendeleza utafiti wa mbuzi na kondoo katika vituo vya utafiti na kununua mbuzi 164 kwa ajili ya utafiti.

- § Kuendeleza utafiti wa kuku wa asili katika Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa na vituo vya utafiti vya Tanga na Naliendele.
- § Kuendeleza utafiti wa malisho katika vituo vya utafiti wa mifugo na vijijini.

(i) Sekta ya Uvuvi. Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi.

- § Kukusanya na kuchambua takwimu za uvuvi zinazohusu idadi ya wavuvi, zana mbalimbali, vyombo vya uvuvi na mialo ya kupokelea samaki.

- § Kufanya doria ya siku-kazi (mandays) 5,247 katika ziwa Victoria, Tanganyika na Baharini.

- § Nyavu haramu 150,219, mitumbwi 191, mikuki minne (4), samaki wachanga kilo 41,901 na baruti 154 zilikamatwa.

- § Kuteketeza zana haribifu za uvuvi zaidi ya 2,800 katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Rukwa, Bwawa la Nyumba ya Mungu na kadhalika.

- § Kudhibiti utoroshaji wa mazao ya samaki mipakani ambapo samaki tani 16.2 zilikamatwa na watuhumiwa 614 walifikishwa mahakamani.

- § Kutoa elimu ya jamii katika vijiji 13 katika Wilaya za Pangani, Tanga na Mkinga kuhusu athari za uvuvi haramu.

(ii) Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi.

- § Kuchunguza sampuli 1,526 kutoka viwanda vya kuchakata samaki vilivyoko Ukanda wa Ziwa Victoria na Pwani.

- § Kutoa mafunzo kwa wataalam 31 kuhusu ubora na usalama wa mazao ya uvuvi.

- § Kuhakiki ubora wa kambamiti (*prawns*) na mazingira yake kutoka kwenye shamba la ufugaji kamba miti katika Wilaya ya Mafia.

- § Kukagua viwanda 16 vya uchakataji samaki, vitano vya kusafirisha kamba koche (*lobsters*) na kaa, vinne vya kusafirisha samaki wa mapambo na maghala manne ya kuhifadhia mazao mbalimbali ya uvuvi.
- § Kukagua tani 57,795.5 za mazao ya uvuvi na samaki wa mapambo 25,502 na kutoa hati za afya ili kusafirisha nje ya nchi.

- § Kuandaa Mpango wa Taifa wa Kutathimini Mabaki ya Kemikali (*National Residue Monitoring Plan*) kwa ajili ya ufugaji wa kambamiti nchini na kuwasilishwa na kukubaliwa na Jumuia ya Nchi za Ulaya (*EU*).

- § Kujenga na kukarabati mialo 19 katika ukanda wa Ziwa Victoria na kuainisha maeneo sita kwa ajili ya kujenga mialo katika wilaya za Mafia, Rufiji na Kilwa.

(iii) Ukuzaji wa Viumbe Hai Kwenye Maji.

- § Kuzalisha na kusambaza kwa wafugaji vifaranga 603,010 vya samaki aina ya *perege* kutoka Kituo cha Ufugaji Samaki Kingolwira – Morogoro.

- § Kukamilisha na kusambaza kwa wadau mwongozo wa kutambua na kuchagua maeneo yanayofaa kufuga viumbe hai kwenye maji chumvi pamoja na kilimo cha mwani.

- § Kuendelea na majaribio ya ukuzaji wa viumbe kwenye maji na uzalishaji wa lulu (*pearls*) katika kisiwa cha Mafia.

- § Kutambua vijiji 16 katika Wilaya ya Rufiji vinavyofaa kwa ufugaji wa samaki na unenepeshaji wa kaa.

- § Kuratibu na kuhamasisha uzalishaji wa mwani ambapo tani 411.83 za mwani mkavu zilizalishwa katika mikoa ya Pwani, Tanga, Mtwara na Lindi.

- § Kukutanisha wadau 70 wanaojihusisha na kilimo na biashara ya mwani kutoka Tanzania Bara na Zanzibar ili kuimarisha na kuendeleza kilimo na biashara ya zao hilo.

(iv) Mafunzo kwa Wadau wa Uvuvi.

- § Kutoa mafunzo ya utunzaji bora na salama wa mazao ya uvuvi kwa wachakataji 50, wavuvi 85, wakaguzi 32 na wasafirishaji 150.

- § Kuandaa na kurusha hewani vipindi 6 vya redio kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

- § Kutoa mafunzo kwa wanavijiji 48 katika Wilaya za Mafia na Rufiji kuhusu ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia uvuvi endelevu ambapo vikundi 14 vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi (*Beach Management Units – BMUs*) vimeanzishwa.

(v) Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (Tanzania *Fisheries Research Institute - TAFIRI*).

Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi iliendeleza tafiti zifuatazo:-

- § Ukuzaji wa viumbe kwenye maji ikiwa ni pamoja na ufugaji wa samaki.

- § Kufanya sensa ya uvuvi katika Bahari ya Hindi iliyobaini kuwepo kwa wavuvi 36,247, vyombo vya uvuvi 7,342 na zana aina mbalimbali 60,819 *(Jedwali Na. 3).*

- § Kufanya sensa ya uvuvi katika Ziwa Victoria iliyobaini kuwepo kwa wavuvi 98,015, vyombo vya uvuvi 29,732 na nyavu aina mbalimbali 931,889.

- § Kufanya utafiti katika Ziwa Victoria na kubaini kuwa kiwango cha juu kinachoweza kuvuliwa kwa samaki aina ya Sangara ni tani 314,000, dagaa 860,000, furu na wengine 460,000 kwa mwaka 2007.

- Majaribio ya ufugaji wa samaki aina ya mwatiko katika wilaya za Kilwa, Rufiji na Mafia.

- Utafiti wa samaki aina ya Silikanti aliyedhaniwa kutoweka miaka milioni 60 iliyopita kwa ushirikiano na Taasisi za Uvuvi za Japan na Afrika Kusini.

- Utafiti katika ukanda wa pwani (*territorial waters*) ili kubaini uwingi wa samaki katika eneo hilo.

- Pia, TAFIRI iliandaa viwango vya utaratibu wa utafiti wa uwingi wa samaki kwa njia ya mwangwi (*hydro-acousatic surveys*) chini ya *Lake Victoria Fisheries Organization.*

    Aidha, kutokana na tafiti zake, TAFIRI ilibaini yafuatayo:-

- Kupungua kwa rasilimali ya kambamiti kutoka tani 1,320.1 mwaka 2003 hadi tani 202.5 mwaka 2007.

- Samaki wanaweza kuvuliwa kwa wingi kutoka kina kirefu cha Ziwa Nyasa kwa kutumia ndoana za kulambaza hususan nyakati za asubuhi kwa kuwa samaki hao wana tabia ya kuja juu kula dagaa.

(vi) Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu.

- Kufanya doria shirikishi jamii 125 katika maeneo ya hifadhi.

- Kupunguza matumizi ya zana haribifu kwa kubadilisha na zana bora za uvuvi ambapo vikundi 62 katika wilaya za Mafia na Mtwara vimenufaika.

- Kutoa elimu ya kazi mbadala ili kupunguza utegemezi kwenye uvuvi.

- Kutoa mafunzo ya utalii rafiki wa mazingira (*eco tourism*) kwa wadau 55 kutoka eneo tengefu la Dar es Salaam na hifadhi ya Bahari ya Mafia.

- Kuchapisha na kusambaza vipeperushi 4,500, majarida 6,000 na kalenda 5,000 kwa wadau na kurusha hewani programu 5 za televisheni na radio.

(vii) Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (*Marine and Coastal Environment Management Project – MACEMP*)

- Kuainisha eneo la kujenga makao makuu ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing Authority)* eneo la Fumba Zanzibar na kutangaza zabuni ya ujenzi.

- Kuwezesha kufanyika siku za doria 1,471 na za anga 30 ili kudhibiti uvuvi haramu katika ukanda wa pwani ikijumuisha maeneo tengefu.

§ Kurusha vipindi 5 vya redio na luninga na kusambaza nakala 4,000 za Jarida la Dodoji, fulana na kofia 400 na mabango 500 ili kuelimisha jamii umuhimu wa usimamizi bora wa rasilimali za uvuvi.

§ Kuwezesha wavuvi kuibua miradi 87 yenye thamani ya shilingi 794,656,644 katika wilaya za Kilwa, Mafia na Rufiji.

§ Kuwezesha utoaji wa mafunzo kwa wakusanyaji takwimu 17 zinazohusu uvuvi katika wilaya za Mafia, Kilwa na Rufiji.

§ Kuhamasisha Halmashauri 16 za Mkinga, Muheza, Jiji la Tanga, Pangani, Bagamoyo, Kinondoni, Ilala, Temeke, Mkuranga, Lindi Vijijini, Lindi Mjini, Mtwara Vijijini na Manispaa ya Mtwara zitakazoingia kwenye utekelezaji wa mradi wa *MACEMP* pamoja na Halmashauri za Rufiji, Kilwa na Mafia za awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi.

§ Kuwezesha uanzishaji wa vikundi 14 vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi (*Beach Management Units – BMUs*) katika Wilaya za Mafia na Rufiji.

§ Kuendelea na taratibu za kulitambua eneo la Kigombe (Muheza) kuwa eneo tengefu.

§ Kuimarisha maeneo Tengefu mapya kwa kuandaa mipango ya usimamizi wake, na kufanya tathmini ya kijiografia, kijamii na kiuchumi.

§ Kununua boti 6, pikipiki 6, baiskeli 30, kompyuta 6 na vifaa vyake na samani za ofisi kwa ajili ya Wilaya za Mafia, Kilwa na Rufiji.

(viii)Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi wa Ziwa Victoria (*Implementation of Fisheries Management Plan*)

§ Kushiriki kuandaa Mwongozo wa Kikanda na Kitaifa wa kuanzisha na kusimamia vikundi vya ulinzi wa rasilimali ya uvuvi (kwa Tanzania zaidi ya vikundi zaidi ya 506 vimeanzishwa).

§ Kuhuisha taratibu za utoaji leseni na usajili wa mialo.

§ Kuandaa Mpango wa Kikanda wa Kuthibiti Uvuvi haramu na Kasi ya Uvunaji katika Ziwa Victoria.

§ Kuendesha doria dhidi ya uvuvi haramu ambapo watuhumiwa 558 walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

§ Kukamilisha ujenzi wa madarasa mawili na nyumba ya mwalimu katika shule ya Nyakakarango (Chato) na jengo la Zahanati ya Mazinga (Muleba).

§ Kuandaa michoro ya mialo sita ya Bwai (Musoma), Sota (Rorya), Kigangama (Magu), Kahunda (Sengerema), Kikumbaitare (Chato) na Marehe (Misenyi).

- § Kununua magari 2, kompyuta 8, projector 1, kamera ya video na picha na injini 8 za boti.

- § Kutayarisha na kusambaza vipeperushi 6,000, mabango 16,000, fulana 12,000 na vipindi vya radio na televisheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni Masuala Mtambuka.

- § Kusambaza kwa wadau nakala 3,700 za Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006, kutoa elimu na kuendelea kutayarisha mkakati wa kutekeleza sera hiyo.

- § Kuendelea kuhuisha na kuandaa mapendekezo ya kutunga sheria 6 pamoja na kuandaa kanuni 5 na miongozo inayohusu sekta za mifugo na uvuvi.

- § Kugharamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 94 wa kada mbalimbali.

- § Kuajiri watumishi 491 wakiwemo 129 wa kada za mtambuka, 231 wataalam wa mifugo na 131 wataalam wa uvuvi.

- § Kuwapandisha vyeo watumishi 95 na kuwathibitisha 7 kazini.

- § Kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kupima na kuzuia maambukizi mapya ya UKIMWI kwa watumishi 250.

- § Kuimarisha dawati la jinsia kwa kuunda kamati na kuendelea kutoa mafunzo kuhusu masuala ya jinsia.

- § Kukamilisha uandaaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja (*Client Service Charter*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwelekeo wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2008/2009. Mwelekeo wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 inalenga katika kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Ibara ya 32 na 33 za Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, na Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA). Hivyo, kazi zifuatazo zitapewa kipaumbele katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni Sekta ya Mifugo:-

(i) Kuandaa mikakati na sheria zitakazoimarisha sekta ya mifugo;

(ii) Kuimarisha utafiti wa mifugo na kuboresha koosafu za mifugo;

(iii) Kuhamasisha uzalishaji mifugo kwa njia ya uhamilishaji na mfumo wa unenepeshaji mifugo;

(iv) Kuimarisha huduma za ugani kwa kuongeza idadi ya maafisa ugani tarajali;

(v) Kuendeleza uzalishaji, usindikaji na masoko ya mifugo na mazao ya mifugo;

(vi) Kuendeleza uzalishaji, usindikaji na hifadhi ya malisho bora na upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora za malisho;

(vii) Kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kuogesha na chanjo za mifugo;

(viii) Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo;

(ix) Kujenga uwezo wa Halmashauri na wadau wengine katika kutoa huduma bora za mifugo;

(x) Kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya usindikaji wa nyama na maziwa;

(xi) Kuendeleza matumizi sahihi na endelevu ya elimu ya asili katika ufugaji na kuboresha maisha ya mfugaji kwa kuhimiza shughuli mbadala za kiuchumi; na

(xii) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni Sekta ya Uvuvi:-

(i) Kuimarisha doria ili kudhibiti uvuvi haramu, ikiwa ni pamojana kuimarisha kikosi cha doria kwa kukipatia vifaa

(ii) Kufanya mapitio ya sera na sheria za uvuvi;

(iii) Kupunguza kasi ya uvuvi katika baadhi ya maeneo ya uvuvi;

(iv) Kuimarisha udhibiti wa ubora, usalama na kuongeza thamani kwa mazao ya uvuvi;

(v) Kuendeleza uanzishwaji wa vikundi vya usimamizi wa rasilimali kwa kushirikiana na jamii (*Beach Management Units*) kwenye maeneo mengine ya uvuvi na kutoa mafunzo;

(vi) Kuwezesha kufanyika tafiti zitakazowezesha kufahamu kiasi cha rasilimali ili kuwezesha kupanga mikakati endelevu ya uhifadhi, uvunaji na utumiaji wa rasilimali ya uvuvi;

(vii) Kuendelea kuboresha mialo iliyobainishwa katika ukanda wa pwani na maziwa tuliyonayo, ikiwa ni pamoja na miundombinu ya kupokelea, kuhifadhi na kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi;

(viii) Kufunga maeneo ya uvuvi kulingana na msimu na unyeti wa maeneo;

(ix) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi bora ya rasilimali ya uvuvi na utunzaji wa mazingira katika mikoa ya Mbeya na Ruvuma;

(x) Kuendeleza ukuzaji wa viumbe vya majini kwa kushirikiana na wadau wengine kwa kutumia teknolojia za kisasa;

(xi) Kuendeleza mchakato wa kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu; na

(xii) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Sera na Sheria za Mifugo na Uvuvi. Sera ya Taifa ya Uvuvi (1997). Katika mwaka 2007/2008 Wizara imeendelea kusimamia rasilimali ya uvuvi na maendeleo yake kwa kutumia Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 1997. Hata hivyo tangu kupitishwa sera hiyo kumekuwepo na mabadiliko mbalimbali katika sekta, sera ya uchumi ya kijumla, miongozo ya kitaifa pamoja na masuala ya kimataifa kama vile utandawazi hivyo, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itafanya mapitio ya Sera hiyo na kuandaa mkakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Mifugo (2006). Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu imeendelea kutoa elimu na kusambaza nakala 3,700 za Sera ya Taifa ya Mifugo kwa wadau. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itasambaza nakala 3,000, kutoa elimu kwa wadau, kukamilisha mkakati wa kutekeleza sera hiyo pamoja na kuandaa programu ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Sekta za Mifugo na Uvuvi. Katika kutekeleza sera za sekta ya mifugo na uvuvi, Wizara yangu inasimamia utekelezaji wa sheria mbalimbali zikiwemo:-

- Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2005. Katika mwaka 2007/2008 kwa kushirikiana na wadau Wizara yangu imefanyia mapitio kanuni zake za mwaka 2005. Katika mwaka 2008/2009 Wizara itaendelea kuzifanyia mapitio kanuni hizo.

- Sheria ya Veterinari Na 16 ya mwaka 2003. Katika mwaka 2007/2008 chini ya Sheria hii Wizara yangu imeandaa rasimu za kanuni 3 za kusimamia wakaguzi wa nyama, wataalam wa maabara na wahimilishaji. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaendelea kuandaa kanuni na miongozo chini ya Sheria hiyo.

- Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya mwaka 2003. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu imeandaa kanuni 5 chini ya sheria hii na rasimu ya kanuni ya usimamizi wa utotoaji vifaranga. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itakamilisha kanuni moja na kuandaa kanuni zingine chini ya sheria hiyo.
- Sheria ya Maziwa Na. 8 ya mwaka 2004. Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu imeshiriki kuhuisha viwango saba vya maziwa na bidhaa zake kwa nchi za Afrika Mashariki. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaandaa mwongozo wa usalama wa maziwa (*Milk Hygiene Code of Practice*).

- Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu imeunda na kuzindua Baraza la Mwaka la Wadau wa Nyama kwa mujibu wa Kifungu cha 4 chini ya sheria hii na kufanya kikao chake cha kwanza Morogoro mwezi Machi, 2008. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaandaa kanuni za kutekeleza sheria hiyo.

- Sheria ya Usimamizi wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994. Katika mwaka 2007/2008, sheria hii imefanyiwa mapitio ambayo yatakamilika katika mwaka 2008/2009.

- Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Na. 6 ya mwaka 1980. Katika mwaka 2008/2009, sheria hii itafanyiwa mapitio ili ikidhi mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria nyingine. Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhuisha na kuandaa mapendekezo ya kutunga sheria mbalimbali pamoja na kuandaa kanuni zake kama ifuatavyo:-

(a) Muswada wa Sheria ya Biashara ya Ngozi (*The Hide and Skins Trade Act*) umesomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 2008.

(b) Muswada wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama (*The Animal Welfare Act)* unatarajiwa kusomwa Bungeni hivi karibuni.

(c) Wizara kwa kushirikiana na wadau imekamilisha rasimu za mapendekezo ya kutunga sheria nne (4) ambazo ni:-

- Sheria mpya ya Maeneo ya Malisho na Vyakula vya Mifugo (*The Grazing Land and Animal Feed Resources Act*);
- Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo (T*he Livestock Identification, Registration and Traceability Act*);
- Sheria ya kuanzishwa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo *(The National Livestock Research Institute Act)*;
- Sheria ya kuanzishwa Maabara Kuu ya Mifugo *(The Central Veterinary Laboratory Act).*

(a) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaandaa Kanuni za kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority Act)* Na. 6 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau itakamilisha sheria zilizotajwa hapo juu na kuandaa sheria zifuatazo:-

(a) Sheria ya Uzalishaji Mifugo (*Animal Breeding*);

(b) Sheria ya Ukuzaji wa Viumbe Hai kwenye maji (*Aquaculture Development*); na

(c) Kufanya mapitio ya Sheria ya Mbung'o (Sura 100 ya mwaka 1943).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi zilizo chini ya wizara. Ili kuongeza ufanisi katika usimamizi kwa baadhi ya taasisi na maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi, Wizara yangu inazo Bodi zifuatazo ambazo zimefanya kazi zake vizuri katika mwaka 2007/2008:-

- Bodi ya *NARCO* (Sheria za Makampuni, Sura 212 ya mwaka 1968);

- Bodi ya TAFIRI (Sheria ya *TAFIRI* Na. 6 ya mwaka 1980);

- Bodi ya Udhamini wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994);

- Bodi ya Maziwa (Sheria ya Tasnia ya Maziwa Na. 8 ya mwaka 2004); na

- Baraza la Veterinari Tanzania (Sheria ya Veterinari Na. 16 ya mwaka 2003).

Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kusimamia Bodi hizo na itakamilisha uundaji wa Bodi ya Nyama chini ya Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Wizara. Maabara Kuu ya Mifugo – Temeke. Maabara Kuu ya Mifugo – Temeke ina jukumu la kufanya uchunguzi, utambuzi na utafiti wa magonjwa ya wanyama. Aidha, maabara inatoa mafunzo ya ufundi sanifu maabara. Katika mwaka 2007/2008, maabara imeendelea kuimarishwa kwa kupatiwa vifaa vya kisasa na vitendea kazi muhimu ili iweze kufikia kiwango cha Kimataifa. Aidha, maabara imetekeleza yafuatayo:-

(a) Kuchunguza sampuli 22,303 zikiwemo 6,468 za Homa ya Bonde la Ufa, 4,380 za Mafua Makali ya Ndege na 15,835 za magonjwa mengine. Matokeo ya uchunguzi wa sampuli za ndege kwa ajili ya ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege yamedhihirisha kuwa ugonjwa huo haujaingia nchini.

(b) Kuzalisha na kusambaza dozi 24,680,200 za chanjo ya Ugonjwa wa Mdondo, dozi 37,750 za chanjo dhidi ya Ugonjwa wa Kimeta na 65,000 za ugonjwa wa Chambavu.

(c) Kuhakiki ubora na usalama wa dozi 580,000 za chanjo ya Kimeta, dozi 385,000 za Chambavu na 740 za Ugonjwa wa Kutupa Mimba.

(d) Kufunga mashine ya kuchunguza na kuhakiki ubora wa mazao na vyakula vya mifugo, yakiwemo mabaki ya dawa na sumu *(High Performance Liquid Chromatograph)* pamoja na kuwapatia mafunzo watafiti wawili (2).

(e) Kuanzisha Kituo kipya cha Udhibiti wa Mbung'o na Ndorobo Kigoma.

(f) Kufanya maandalizi ya kuzalisha kwa wingi mimea ya dawa za asili katika maabara kwa kutumia njia ya kisasa ya *Tissue Culture Micropropagation* kwa kushirikiana na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Kahawa *(TACRI- Lyamungo).*

(g) Kufanya uchunguzi na kuthibitisha kuwa dawa ya asili ijulikanayo kwa kimasai kama Oltemwai *(Commiphora swynertonii)* ina uwezo wa kuua wadudu kama viroboto, kupe na chawa.

(h) Kukarabati maabara na kujenga chumba cha kuhifadhi na kutayarisha damu kwa ajili ya mbung'o katika Taasisi ya Utafiti wa Ndorobo na Nagana Tanga. Aina na idadi ya mbung'o waliofugwa kwa mwaka 2007/2008 katika kituo hicho ilikuwa *Glossina pallidipes* (3,979), *G. austeni* (89,627), *G. brevipalpis* (439) na *G. morsitans centralis* (4,374).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Maabara Kuu itazalisha na kusambaza katika Halmashauri mbalimbali dozi 300,000 za chanjo ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba, dozi 500,000 za Kimeta na 500,000 za Chambavu. Pia, Maabara itazalisha dozi milioni 30 za chanjo ya mdondo ili kudhibiti ugonjwa huo hususan vijijini. Aidha, Maabara itafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kuendeleza ufugaji wa aina mbalimbali za mbung'o kwa ajili ya utafiti;

(b) Kufanya uchunguzi, utambuzi na utafiti wa magonjwa mbalimbali;

(c) Kuchunguza na kuhakiki ubora wa mazao ya mifugo na vyakula vya mifugo pamoja na mabaki ya dawa na sumu;

(d) Kuanza ujenzi wa kituo cha kutengeneza chanjo za mifugo Kibaha; na

(e) Kukarabati na kuimarisha Maabara Kuu ya Mifugo, Taasisi ya Utafiti wa Ndorobo na Nagana Tanga na kujenga kituo cha Udhibiti wa Mbung'o na Ndorobo Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maabara ya Taifa ya Udhibiti wa Ubora wa Samaki Nyegezi. Katika mwaka 2007/2008, Maabara ya Taifa ya Udhibiti wa Ubora wa Samaki Nyegezi ilichunguza sampuli 1,526 za samaki kutoka viwanda vya kuchakata samaki vya kanda ya ziwa ili kuhakiki ubora kwa kubaini vimelea haribifu kwenye mazao ya samaki. Matokeo yalionyesha kuwa sampuli zote zilikuwa nzuri.

Aidha, maabara hiyo imepata ithibati Na. T 0327 iliyotolewa na *South African National Accreditation Services* (*SANAS*) na hivyo kutambulika kimataifa. Katika mwaka 2008/2009 maabara itaimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi na watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa na Vituo vya Utafiti wa Mifugo. Wizara yangu ina Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa na vituo 6 vya utafiti wa mifugo vya Kongwa, Tanga, West Kilimanjaro, Mabuki, Uyole na Naliendele. Katika mwaka 2007/2008, Taasisi na Vituo vya Utafiti vimeendelea kutathmini na kuhifadhi jamii mbalimbali za mifugo asili, kubuni na kusambaza teknolojia zinazolenga kuongeza uzalishaji wa mifugo. Aidha, madume 85 aina ya Mpwapwa yamesambazwa katika wilaya za Iramba (40), Igunga (20), Mvomero (15) na Simanjiro (10). Utafiti unaonyesha kuwa uzito wa kuzaliwa umeongezeka kutoka wastani wa kilo 15 kwa ndama wa asili hadi wastani wa kilo 25 kwa ndama chotara. Pia, ng’ombe chotara hufikia uzito wa kilo 350 – 400 wanapofikia miaka minne (4) ikilinganishwa na kilo 250 – 300 kwa ng’ombe wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi imeendelea kufanya uchambuzi wa koo za ng’ombe wa asili aina ya *Ufipa* - ng’ombe 71, *Ankole* - ng’ombe 20 katika Vituo vya Utafiti vya Uyole na Mabuki na aina za *Iringa Red, Mbulu* na *Singida White* katika mazizi ya wafugaji kwa lengo la kuainisha sifa zao za uzalishaji na kuwahifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, utafiti wa mbuzi aina ya *Malya* (*Blended Goats*), *Newala na Gogo White* uliendelea. Jumla ya mbuzi bora 163 aina ya *Malya* wamezaliwa na mbuzi 164 aina ya *Newala* walinunuliwa kwa lengo la kufanyiwa utafiti na kuhifadhi katika kituo cha utafiti cha Naliendele. Vilevile, mbuzi 69 jamii ya *Pare*, 35 jamii ya *Sonjo* na kondoo 219 jamii ya *Red Masai* wamenunuliwa kwa ajili ya tathmini, utafiti na kuhifadhi katika kituo cha West Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, kuku 600 aina za *Kinyavu, Mozambican Dwarf, Kishingo* na *Kuza* wamendelea kufanyiwa utafiti katika Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa na katika vituo vya utafiti vya mifugo ili kubaini sifa muhimu zinazoweza kutumika kuboresha uzalishaji katika mazingira ya vijijini.

Tathmini imebaini ukuaji wa kuku wa asili kuongezeka kutoka wastani wa gramu 4 hadi 9 kwa siku, kuongeza uzito kutoka kilo moja na nusu hadi kilo mbili wanapofikia umri wa miezi sita, na utagaji kuongezeka kutoka mayai 40 hadi 105 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa malisho ulifanyika kwa kukusanya aina 60 za mimea ya malisho kutoka maeneo mbalimbali ya Afrika kupitia Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo Nairobi na aina 15 kutoka Mkoa wa Dodoma kwa lengo la

kufanyiwa tathmini na kuhifadhiwa katika benki ya vinasaba (*Genebank*). Kilo 520 za mbegu bora za malisho zilizotokana na tafiti hizi zilisambazwa kwa wafugaji katika vijiji vya Iguguno (Iramba), Unyankhanya (Singida vijijini) na Mtumba (Dodoma).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendeleza tafiti za mifugo zifuatazo:-

(i) Kubaini teknolojia zitakazoongeza uzito wa ng'ombe wa asili kutoka kilo 250 kufikia kilo 450 wakiwa na miaka minne (4); uzito wa mbuzi na kondoo wa asili kutoka kilo 25 kufikia kilo 45 wakiwa na miaka miwili (2) na uzito wa kuku wa asili kufikia kilo 2 kabla ya mwaka na uzito wa yai kuwa gramu 150.

(ii) Kusambaza madume 90 aina ya Mpwapwa na mbuzi 60 jamii ya Malya *(Blended)* vijijini na kufuatilia uzalishaji wake.

(iii) Kuibua na kusambaza teknolojia za uzalishaji, usindikaji, uhifadhi wa mazao ya mifugo, malisho na vyakula vya mifugo.

(iv) Kuwajengea uwezo watafiti wa mifugo kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(Tanzania Fisheries Research Institute - TAFIRI).* Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)* ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 6 ya mwaka 1980. Katika mwaka 2007/2008, *TAFIRI* kupitia vituo vyake vya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Kyela na kituo kidogo cha Sota mkoani Mara iliendelea kufanya utafiti kuhusu kubaini uwingi wa samaki kwenye maji ya kina kifupi katika Bahari ya Hindi na ufugaji wa samaki aina ya mwatiko *(milk fish)* katika wilaya za Kilwa, Rufiji na Mafia.

Aidha, mabwawa ya mfano ya kufuga samaki aina ya mwatiko yamejengwa kwenye Chuo cha Mbegani na Kilongawima (Kinondoni) kwa ajili ya mafunzo kwa wafugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TAFIRI* ilichambua takwimu za uvuvi wa kambamiti na kuonyesha kuwa kambamiti wamepungua kutoka tani 1,320.1 mwaka 2003 hadi tani 202.5 mwaka 2007 sawa na upungufu wa asilimia 84.7 (Jedwali Na. 4). Kutokana na hali hiyo, Wizara yangu imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuzuia uvuvi wa kambamiti kwa meli kubwa za kibiashara katika ukanda wa pwani ili wazaliane na kufanya mazingira na mazalio yao na ya samaki kuboreka zaidi; na

(ii) Kuelekeza uvuvi sehemu nyingine ambayo rasilimali yake bado haijavunwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa samaki aina ya Silikanti, aliyedhaniwa kutoweka miaka milioni 60 iliyopita unaendelea kwa ushirikiano na Taasisi za *Tokyo Institute of Technology* ya Japan na *South African Institute of Aquatic Biodiversity*. Samaki hao wameonekana kwa wingi katika maeneo ya bahari ya Wilaya za Tanga na Muheza. Kutokana na historia ya pekee ya samaki hawa wanaweza kuwa kivutio kikubwa cha utalii, hivyo Wizara yangu kwa kushirikisha wananchi wa eneo la Kigombe (Muheza) imeainisha eneo hilo kuwa tengefu na taratibu za kulitambua kisheria zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Wizara yangu kupitia *TAFIRI* imefanya utafiti katika Ziwa Nyasa na kugundua kuwa samaki wanaoishi katika maji ya kina kirefu wana tabia ya kuja juu kula dagaa wakati wa asubuhi. Kutokana na hali hiyo, wavuvi wanashauriwa kutega ndoana za kulambaza asubuhi kabla jua kuchomoza kwa kutumia chambo hai hasa dagaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ziwa Victoria utafiti uliofanyika mwezi Februari, 2008 ulibaini kiwango cha samaki waliopo ni sangara tani 375,670, dagaa 1,381,709 furu na wengine 735,480. Tafiti kwa aina nyingine za samaki zinaendelea. Aidha, nchi yetu kwa kushirikiana na nchi za Afrika Mashariki kupitia *Lake Victoria Fisheries Organization* imetengeneza viwango vya utaratibu wa kufanya utafiti wa uvuvi katika Ziwa Victoria kwa njia ya mwangwi (*hydro-acoustic surveys*). Tathmini ya awali ya utafiti wa aina hii ni kama ulivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, TAFIRI itafanya sensa ya wavuvi na zana za wavuvi katika maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Rukwa na mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu. Aidha, mafunzo yatafanyika kwa wakusanya takwimu 186 wa sensa za wavuvi na zana za wavuvi kutoka maeneo ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara. Vilevile, TAFIRI itaendesha mafunzo kwa wataalam 20 wa kuchambua na kutunza takwimu za sensa ya uvuvi.

Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (*Marine Parks and Reserves Unit*). Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kinasimamia hifadhi mbili za bahari za Mafia (Mafia Island Marine Park) na Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma (*Mnazi Bay and Ruvuma Estuary Marine Park*,) iliyopo Mtwara. Pia, kitengo kinasimamia maeneo tengefu katika eneo linalozunguka Dar es Salaam na visiwa vidogo ambavyo havikaliwi na watu vya Mbudya, Bongoyo, Pangavini, Fungu Yasini, Sinda, Makatumbe na Kendwa na kisiwa cha Maziwe kilichopo Pangani. Pia, kitengo kinasimamia maeneo tengefu ya visiwa vya Shungimbili, Mbarakuni na Nyororo katika wilaya ya Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, doria shirikishi jamii 125 zilifanyika katika hifadhi na maeneo yanayozunguka hifadhi. Jumla ya wavuvi haramu 26 walifikishwa mahakamani na nyavu za kokoro/majuya 83, kilo 10 za majongoo bahari, boriti 800 za mikoko, mitumbwi 12, michinji (*spear guns*) 2 na baruti 5 vilikamatwa na kutaifishwa. Ili kupunguza kasi ya uharibifu wa rasilimali za bahari Wizara yangu iliimarisha utaratibu wa kubadilisha zana haribifu kwa zana bora za uvuvi endelevu.

Kutokana na utaratibu huo, vikundi 62 vyenye wavuvi 220 katika wilaya za Mafia na Mtwara wamenufaika. Aidha, elimu ya kazi mbadala ili kupunguza utegemezi kwenye uvuvi ilitolewa kuhusu ufugaji nyuki kwa wanavijiji 40 (Mafia) na 45 (Mtwara), ufugaji wa samaki wanavijiji 26 (Mtwara), ufugaji wa kuku kwa wanavijiji 40 (Mtwara) na ukulima wa mwani wanavijiji 80 (Mafia). Pia, mafunzo ya utalii rafiki wa mazingira yalitolewa kwa wanavijiji 25 (Dar es Salaam) na wanavijiji 30. (Mafia)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kupitia kitengo hicho itaendelea na usimamizi wa uhifadhi wa maeneo tengefu kwa kushirikiana na wadau. Aidha, uandaaji na ukamilishaji wa mipango ya usimamizi wa maeneo tengefu mapya ya visiwa vya Kendwa, Makatumbe, Sinda, Mbarakuni, Shungimbili na Nyororo utakamilishwa.

Vilevile, kitengo kitaendelea na mchakato wa kulitambua kisheria eneo la Kigombe Muheza kwa ajili ya kuhifadhi samaki aina ya Silikanti na viumbe wengine kwenye eneo hilo na kuendeleza utalii rafiki wa mazingira katika maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Mifugo na Uvuvi. Wizara yangu inavyo vyuo sita vya mafunzo ya mifugo vya Buhuri, Madaba, Morogoro, Mpwapwa, Tengeru na Temeke. Vyuo hivyo vinatoa mafunzo ya astashahada na stashahada za fani mbalimbali za mifugo. Pia, Wizara inasimamia vyuo viwili vya mafunzo ya uvuvi vya Nyegezi na Mbegani. Chuo cha Uvuvi Nyegezi hutoa mafunzo katika taaluma ya uvuvi katika ngazi ya astashahada, ushauri wa ufugaji samaki na uvuvi katika maji baridi. Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi Mbegani hutoa mafunzo katika taaluma za Ubaharia, Uhifadhi, Uchakataji Samaki na Masoko, Ufundi wa Mitambo ya Baharini na Ujenzi wa Boti. Chuo pia kinatoa mafunzo kwa wakaguzi wa mazao ya Uvuvi kwa nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu kupitia programu maalum ya mafunzo kwa wagani, iligharamia mafunzo ya stashahada kwa wanachuo 1,006 na wanaendelea na mafunzo katika vyuo vya Buhuri (29), Madaba (69), Morogoro (231), Mpwapwa (232), Tengeru (402) na Temeke (43). Madhumuni ya programu hiyo ni jitihada za kupunguza pengo la wataalam wa ugani wa mifugo 13,469. Aidha, katika mwaka 2007/2008 Vyuo ya Mbegani na Nyegezi vilikuwa na jumla ya wanafunzi 228, kati ya hao, 142 wapo Mbegani na 86 wapo Nyegezi. Vilevile, ukarabati unaendelea kwa meli za *Marine Vessel* (MV) Mafunzo na MV Elimu, karakana ya kutengeneza barafu na majokofu katika Chuo cha Mbegani kwa msaada wa Serikali ya Japan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaandika upya mitaala 5 kwenye mfumo wa moduli na kusimamia utekelezaji wake kufuatana na matakwa ya *NACTE* na kutayarisha vitabu 6 vya kiada na ziada .

Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza Programu maalum ya Mafunzo ya Wagani kwa kugharamia wanafunzi 1,185 katika vyuo vya mifugo. Pia, jumla ya wanafunzi 120 watadahiliwa katika vyuo vya Uvuvi. Vilevile, vyuo hivyo vitaimarishwa ili viweze kuendesha mafunzo ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Ranchi za Taifa *(National Ranching Company – NARCO)*. Jukumu kubwa la Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) ni kuzalisha, kunenepesha na kuuza mifugo kwa ajili ya nyama sanjari na kutoa huduma za ushauri kwa wafugaji wanaozunguka ranchi hizo. Katika mwaka 2007/2008, Kampuni imeendelea kuzalisha mifugo ya nyama katika ranchi zake 10 za mfano za Kikulula, Mabale, Kagoma, Misenyi (Kagera), Kongwa (Dodoma), Mzeri (Tanga), Ruvu (Pwani), Mkata (Morogoro), Kalambo (Rukwa) na West Kilimanjaro zenye eneo la hekta 230,384 na jumla ya ng'ombe 41,000. Katika mwaka 2007/2008, *NARCO* iliuza jumla ya ng'ombe 9,030 wenye thamani ya shilingi bilioni 2.1. Aidha, Kampuni ilinunua ng'ombe 1,044 wenye thamani ya shilingi milioni 199.4 kutoka kwa wafugaji wanaozunguka maeneo ya ranchi kwa ajili ya mradi wa kunenepesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ranchi za Kongwa na Ruvu, Wizara yangu imenunua ng'ombe wazazi 820 aina ya Boran (madume 120 na majike 700) na hivyo kuipa *NARCO* uwezo wa kuzalisha ng'ombe bora zaidi kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Pia, miundombinu ya mashamba hayo imeboreshwa ikiwa ni pamoja na kufyeka vichaka, kujenga uzio na kukarabati machinjio. Katika mwaka 2008/2009, *NARCO* itaongeza uzalishaji wa ngómbe, mbuzi na kondoo. Aidha, Ranchi za Kongwa na Ruvu zitaboreshwa kwa kununua ngómbe wazazi 1,200 na madume 49. Vilevile, *NARCO* watanunua maksai 10,000 kwa ajili ya programu ya kunenepesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008 Wizara imewezesha upatikanaji wa hati miliki ndogo (*sublease*) kwa vitalu vya Mzeri (9), Misenyi (21), na Mkata (11). Zoezi la utoaji wa hati miliki ndogo kwa vitalu vya ranchi za Uvinza, Usangu, Kalambo, Mabale, Kikulula na Kagoma linaendelea. Kwa upande wa ranchi ya West Kilimanjaro, upimaji wa vitalu 23 unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha mashamba, miundombinu na huduma zilizokuwa chini ya Wizara yangu na kubinafsishwa zinaendelezwa na kufanya kazi iliyokusudiwa, tulifanya tathmini ya mashamba 58 na viwanda viwili. Tathmini hiyo imeonyesha kuwa baadhi ya mashamba na viwanda havijaendelezwa kama ilivyotarajiwa na Wizara inaendelea kufuatilia na kutoa ushauri unaohitajika. Napenda nitoe wito kwa wote waliopewa mashamba na viwanda hivyo ambavyo havijaendelezwa au wanafanya shughuli nyingine tofauti na makubaliano yaliyoainishwa kwenye mikataba kuwekeza katika kipindi cha miezi miwili, ama sivyo watanyang'anywa na kupatiwa wawekezaji wengine wenye nia ya kuyaendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha biashara ya nyama na mazao yake Serikali ilikubali kuuza asilimia 51 ya thamani ya mali za machinjio ya Dodoma kwa Kampuni ya *National Investment Company Limited (NICOL)* na kubakiza asilimia 49 chini ya NARCO. *NARCO* na *NICOL* zimeanzisha kampuni iitwayo *Tanzania Meat Company Limited* itakayoendesha machinjio hiyo. Vilevile, wawekezaji binafsi watatu

(3) watakaoingia ubia na *NARCO* kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya nyama na machinjio wamepatikana. Wawekezaji hao ni:-

(i) Kampuni ya *Snowy Mountains PTY* kutoka Australia ambayo imeomba kuwekeza katika eneo la Ruvu (Bagamoyo);

(ii) Kampuni ya *Rockshield Quality Foods* ya Mkoani Kagera ambayo imeomba kuwekeza katika eneo la Kyaka (Misenyi); na

(iii) Kampuni ya *Live Support Systems (T)* ya Mkoani Arusha ambayo imeomba kuwekeza katika eneo la Themi (Arusha).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009 taratibu za kuiwezesha NARCO kuingia ubia na wawekezaji hao zitaendelea. Kwa upande wa maeneo ya Magu, Bunda na kiwanda cha nyama cha Mbeya ambako wawekezaji hawajapatikana, Wizara itatangaza tena zabuni upya ili kupata wawekezaji watakaoingia ubia na *NARCO* katika maeneo hayo. Serikali imetenga shilingi bilioni 3 kuiwezesha *NARCO* kuingia ubia na wawekezaji hao waliojitokeza ili kampuni ishiriki kama mbia. Aidha, katika mwaka wa 2008/2009 Wizara yangu itafanya zoezi la kuhesabu mifugo yote iliyo chini ya *NARCO* na Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kampuni nilizoainisha hapo juu, zipo pia kampuni binafsi zinazojihusisha na biashara ya nyama ambazo ni:

(i) Kampuni ya *Triple "S" Beef Limited* iliyokabidhiwa Kiwanda cha Kusindika Nyama cha Shinyanga tarehe 31 Desemba 2007 na mwekezaji anaendelea na taratibu za uwekezaji.

(ii) Kiwanda cha kusindika nyama cha Sumbawanga *Agricultural and Animal Feeds Industries* (SAAFI) chenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 150 kwa siku.

(iii) *Tanzania Pride Meat* cha Morogoro chenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 200 na kuku 16,000 kwa siku.

(iv) Machinjio ya Sakina, Arusha yenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 300 kwa siku.

(v) Mkuza *Chicks Limited* (Kibaha) yenye uwezo wa kuchinja kuku 8,000 kwa siku.

(vi) *Interchick Company Limited* (Kinondoni) yenye uwezo wa kuchinja kuku 3,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, Baraza la Veterinari limesajili madaktari 28 na kufanya jumla ya madaktari wa mifugo waliosajiliwa kufikia 582, kuandikisha na kuorodhesha wataalam wasaidizi 123 na kufanya jumla kuwa 906. Vilevile, vituo 12 vya huduma ya mifugo vimesajiliwa katika mikoa 7 ya Morogoro (2), Arusha (3), Kilimanjaro (2), Tanga (2), Kigoma (1), Mbeya (1) na Mwanza (1) na kufikia 291 na vituo 25 vilikaguliwa katika mikoa ya Dar-es-Salaam na Pwani. Aidha, wataalam 5 walikataliwa usajili na vituo 4 vilipewa muda wa kurekebishwa. Pia, Baraza limehakiki na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali madaktari wa mifugo 222 na wataalamu wasaidizi 731 na kutoa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wataalamu 78.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kurahisisha ufuatiliaji wa maadili ya kitaalam, Baraza limeanzisha mfumo wa kutunza takwimu. Katika mwaka 2007/2008, Baraza limehakiki takwimu za usajili kutoka Halmashauri za wilaya 46 za mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara, Mtwara, Lindi, Pwani, Dar-es-Salaam na Morogoro na kuingizwa katika programu maalum ya kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Mpango Mkakati wa Baraza la Veterinari utaendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kukagua na kusajili wataalam wa mifugo 300, maeneo ya kutolea huduma na kuorodhesha na kuandikisha wataalamu wasaidizi wa mifugo. Vilevile, ukaguzi wa mitaala ya wataalamu wa afya ya mifugo utafanyika katika vyuo vya mifugo vya sekta binafsi vya Kilacha (Moshi Vijijini) na Simanjiro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa mifugo. Uendelezaji wa ng’ombe na mbuzi wa maziwa. Uendelezaji wa sekta ndogo ya maziwa umeendelea kuratibiwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Bodi ya Maziwa nchini. Katika mwaka 2007/2008, kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji wa maziwa kutoka lita bilioni 1.42 mwaka 2006/2007 hadi lita bilioni 1.5 sawa na ongezeko la asilimia 5.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko la mahitaji ya mitamba takribani 15,000 kwa mwaka ikilinganishwa na wastani wa uzalishaji wa mitamba 6,721 mwaka 2006/2007, Wizara yangu imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika mashamba ya kuzalisha mitamba bora ya ng’ombe wa maziwa. Vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha mashamba yake ya kuzalisha mitamba ya Nangaramo, Ngerengere, Sao Hill, Mabuki na Kitulo kwa kukarabati majengo, miundombinu ya shamba, mitambo na kuweka umeme katika baadhi ya mashamba hayo. Aidha, jumla ya mitamba 230 aina ya Boran na madume 10 aina za *Friesian* na *Ayrshire* yamenunuliwa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mitamba katika mashamba hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ilisambaza jumla ya mitamba 8,731 kwa wafugaji wadogo. Kati ya hiyo, mitamba 7,009 ni kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali

na 1,722 kutoka mashamba ya Serikali na Taasisi zake. Vilevile, mbuzi 2,041 wa maziwa walisambazwa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza uzalishaji wa maziwa pamoja na ulaji wake, Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kusindika maziwa, uundwaji wa vikundi vya kukusanya na kusindika. Usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita 56,580 kwa siku mwaka 2006/2007 hadi lita 65,930 mwaka 2007/2008 sawa na ongezeko la asilimia 16.5. Usindikaji huu ulifanyika katika viwanda 31 kati ya viwanda 39 vilivyopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na Bodi ya Maziwa itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuzalisha, kukusanya na kufufua baadhi ya viwanda vya kusindika maziwa vinavyofanya kazi na vilivyosimama. Uzalishaji wa maziwa unakadiriwa kufikia lita bilioni 1.6. Aidha, mashamba ya uzalishaji mitamba ya Nangaramo, Ngerengere, Sao Hill, Mabuki na Kitulo yataimarishwa ili yaweze kufikia lengo la kuzalisha mitamba 1,000 na mbuzi wa nyama 400 kwa mwaka. Pia, tathmini ya uendeshaji wa mashamba ya kuzalisha mifugo itakamilishwa kwa lengo la kubaini mfumo unaofaa kuendesha mashamba hayo kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji kama njia ya haraka ya kuboresha mifugo. Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (*National Artificial Insemination Centre – NAIC*) cha Usa River, Arusha kimeimarishwa kwa kununuliwa mitungi 35 ya kuhifadhi hewa baridi ya Nitrojeni. Katika mwaka 2007/2008, uzalishaji wa mbegu bora umeongezeka kutoka dozi 58,500 mwaka 2006/2007 na kufikia 69,085 sawa na ongezeko la asilimia 18.1. Aidha, ng’ombe waliohimilishwa wameongezeka kutoka 50,500 na kufikia 55,253 katika kipindi hicho sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Vilevile, wataalamu 137 wa uhimilishaji kutoka katika Halmashauri na mashamba ya mifugo walipatiwa mafunzo ya uhimilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Kituo cha Uhimilishaji cha NAIC Usa River kitaimarishwa ili kiweze kuzalisha dozi 100,000 za mbegu, lita 40,000 za hewa baridi ya naitrojeni na kufundisha wahimilishaji 150 kutoka Halmashauri, mashamba ya Serikali, Sekta binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Aidha, vituo 5 vya kutolea huduma za uhimilishaji vya kanda vitaimarishwa ili kupanua huduma ya uhimilishaji kwa kuvinunulia mitungi 50 ya kuhifadhia mbegu na mitambo 2 ya kutengeneza hewa baridi ya naitrojeni kwa Kanda ya Kati na Mashariki. Vilevile, Mkakati wa kuimarisha uhimilishaji nchini utaandaliwa kwa lengo la kuongeza kasi na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa zao la nyama unahusisha ng’ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, kuku n.k. Katika mwaka 2007/2008 uzalishaji wa nyama uliongezeka kutoka tani 370,566 mwaka 2006/2007 na kufikia tani 410,706 sawa na

ongezeko la asilimia 10.8. Kati ya tani hizo, nyama ya ng'ombe ni tani 218,976, mbuzi/kondoo tani 81,173, nguruwe tani 33,307 na nyama ya kuku tani 77,250. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama na mazao yake na kupanuka kwa wigo wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008 takriban ng'ombe 29,600 walinenepeshwa ukilinganisha na 26,400 mwaka 2006/2007 sawa na ongezeko la asilimia 12.1. Unenepeshaji huu ulitekelezwa katika mashamba ya *Glienshils Ranch* na *Mtibwa Feedlot* (Morogoro), *Sumbawanga Agricultural and Animal Feeds Industries (SAAFI)*, ranchi za Manyara na Mzeri na wafugaji wadogo katika mikoa ya Mara, Mwanza na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, inakadiriwa kuwa tani 421,700 za nyama zitazalishwa. Aidha, Wizara yangu itahamasisha utekelezaji wa mipango ya unenepeshaji wa mifugo ya nyama na kutoa mafunzo kwa wadau wa sekta ndogo ya nyama pamoja na kutengeneza miongozo ya unenepeshaji mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa kuku nchini umeendelea kushamiri na kuwa kati ya vyanzo vikuu vya mapato na lishe kwa wananchi hasa wa vijijini. Katika mwaka 2007/2008 vifaranga milioni 32.6 vya kuku wa kisasa vilizalishwa ikilinganishwa na vifaranga milioni 28.7 vilivyozalishwa mwaka 2006/2007. Aidha, vifaranga milioni 1.9 na mayai ya kutotoa vifaranga milioni 5.4 yaliingizwa nchini mwaka 2007/2008 ikilinganishwa vifaranga 782,550 na mayai milioni 3.1 mwaka 2006/2007. Pia, uzalishaji wa mayai nchini uliongezeka kutoka mayai bilioni 2.23 mwaka 2006/2007 hadi mayai bilioni 2.69 mwaka 2007/2008 sawa na ongezeko la asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa kuku, mayai na vifaranga ambapo uzalishaji unatarajiwa kufikia mayai bilioni 2.7 na vifaranga milioni 34. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaandaa kanuni zitakazosimamia utaratibu wa kuendesha vituo vya kutotolesha vifaranga vya kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa nguruwe umeendelea kukua kutokana na ulaji wa nyama ya nguruwe kuongezeka kutoka tani 31,721 mwaka 2006/2007 hadi 33,307 mwaka 2007/2008. Ili kuboresha ufugaji huu, Wizara imeendelea kuzalisha mbegu bora za nguruwe katika mashamba ya mifugo ya Ngerengere na Kongwa ambapo nguruwe 317 walizalishwa. Katika mwaka 2008/2009 mashamba hayo yataimarishwa ili kuongeza uzalishaji kufikia nguruwe 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maji na Vyakula vya Mifugo. Katika kukabiliana na uhaba wa maji kwa ajili ya mifugo, Wizara yangu kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) katika mwaka 2007/2008 malambo 132 yalipangwa kuchimbwa. Pia, kupitia Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (PADEP) malambo yamechimbwa katika wilaya za Mwanga (1), Same (2), Uyui (6), Handeni (10) na Kilindi (7). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya

za Kilwa, Nachingwea na Lindi Vijijini imefanya usanifu wa ujenzi wa malambo ya Miteja (Kilwa), Mbondo (Nachingwea) na Mjimwema (Lindi Vijijini). Pia, nakala 2,650 za mwongozo wa ujenzi wa malambo na uvunaji wa maji zimesambazwa kwa wadau. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri itaendelea kuainisha maeneo ya kujenga malambo na mabwawa ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imehamasisha utengaji wa maeneo ya ufugaji na matumizi bora yenye ukubwa wa takribani hekta 930,276 kwenye vijiji 155 katika Wilaya 24 za mikoa 10 ya Dodoma, Iringa, Kagera, Kigoma, Lindi, Mbeya, Morogoro, Pwani, Singida na Tabora. Pia, wataalam kutoka wilaya za Monduli, Bahi, Kiteto, Kishapu, Singida, Kilwa, Rufiji, Mkuranga, Kisarawe na Lindi wamepata mafunzo kuhusu matumizi endelevu ya maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa malisho bora. Kutokana na uhamasishaji huo, kumekuwepo na ongezeko la wazalishaji binafsi wa malisho bora kutoka wawekezaji 6 mwaka wa 2006/2007 hadi 40 mwaka 2007/2008, ambapo jumla ya marobota 179,333 ya hei yamezalishwa ukilinganisha na marobota 90,000 ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuimarisha mashamba ya mbegu bora za malisho ya Vikuge (Kibaha), Langwira (Mbarali), Mabuki, (Misungwi) Buhuri (Tanga) Kizota (Dodoma Manispaa), Kongwa, Mivumoni (Muheza) na Sao Hill (Mufindi). Mashamba hayo yamezalisha tani 42.7 za mbegu aina mbalimbali ikilinganishwa na tani 26 zilizozalishwa mwaka 2006/2007 sawa na ongezeko la asilimia 65.4. Aidha, mashamba hayo yamezalisha marobota 338,152 ya hei ikilinganishwa na marobota 216,000 yaliyozalishwa mwaka 2006/2007 sawa na ongezeko la asilimia 56.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta binafsi imeendelea kuzalisha vyakula bora vya mifugo nchini. Kwa sasa, vipo viwanda 74 vya kutengeneza vyakula vya mifugo nchini vyenye uwezo wa kuzalisha tani 980,000 ikilinganishwa na mahitaji ya takriban tani milioni 1.2. Viwanda hivyo vipo katika mikoa ya Arusha (14), Dar es Salaam (29), Kilimanjaro (7), Mbeya (7), Mwanza (11) na Pwani (6). Katika mwaka 2007/2008 tani 717,231 za vyakula vya mifugo zilizalishwa ikilinganishwa na tani 606,566 za mwaka 2006/2007 sawa na ongezeko la asilimia 18.2. Aidha, mafunzo kwa wakaguzi 20 wa vyakula vya mifugo kutoka Halmashauri 15 za Wilaya za Ilala, Temeke, Kinondoni, Kibaha, Moshi, Tanga, Dodoma, Muheza, Sumbawanga, Morogoro, Ilemela, Nyamagana, Tabora, Iringa na Mbeya yametolewa ili kuwawezesha kusimamia ubora wa vyakula vya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itatoa mafunzo kwa wataalam 80 kuhusu matumizi ya maeneo ya malisho na usimamizi wa ubora wa vyakula vya mifugo. Pia, mashamba manane (8) ya mbegu bora za malisho yataendelea kuimarishwa ili yaweze kuongeza uzalishaji wa hei hadi kufikia marobota 400,000. Vilevile, kwa kushirikiana na Halmashauri, Wizara yangu itatoa mafunzo kwa wafugaji

wadogo kuhusu utengenezaji wa vyakula vya mifugo. Pia, mfumo wa tahadhari ya majanga kwa mifugo (*Livestock Early Warning System*) utaimarishwa na kutumika katika mikoa ya kanda ya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo na magonjwa ya mlipuko. Katika mwaka 2007/2008 Mkakati wa Tahadhari ya Kuzuia Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege umeandaliwa kwa lengo la kuzuia ugonjwa huo usiingie nchini. Sampuli 4,380 za ndege pori, kuku, bata na kanga zilichunguzwa na kuthibitisha kutokuwepo kwa virusi vya ugonjwa huo nchini. Ugonjwa huo unaendelea kuenea duniani ambapo hadi sasa nchi 61 zimeambukizwa na kati ya hizo, 11 ziko katika Bara la Afrika, zikiwemo Nigeria, Misri, Niger, Cameroon, Burkina Faso, Sudan, Cote d'Ivore (Ivory Coast), Djibouti, Ghana, Benin na Togo. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kutekeleza Mkakati wa Tahadhari ya Mafua Makali ya Ndege. Hivyo, naomba kutoa wito kwa wananchi wote na wadau wengine kuzingatia na kutekeleza maelekezo ya wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za kudhibiti ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya ng'ombe ziliendelea chini ya Mpango wa *'Roll Back Vaccination'* katika mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa, Singida, Tabora na Kigoma. Katika mwaka 2007/2008, Serikali ilinunua chanjo dozi milioni 3.2 kwa ajili ya kuchanja mifugo kwenye mikoa hiyo na mikoa ya Arusha na Mara inayopakana na nchi jirani ambapo kuna hatari ya kutokea ugonjwa. Jumla ya ng'ombe 3,025,190 walichanjwa dhidi ya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huo umeonyesha mafanikio ambapo kati ya ng'ombe 24,000 waliopimwa ni ng'ombe watano (5) tu (asilimia 0.02) walipatikana na viashiria vya ugonjwa ukilinganisha na mwaka 2004 ambapo kati ya ng'ombe 3,927 waliopimwa 24 (asilimia 0.6) walipatikana na ugonjwa. Kutokana na mafanikio hayo Wilaya za Kyela, Ileje, Rungwe, Ludewa na Makete zimeondolewa kwenye zoezi la kuchanja kuanzia mwaka 2006 na tunategemea Wilaya za Mbozi, Mbeya Mjini na Vijijini, Mbarali, Sumbawanga Mjini na Vijijini, Nkasi na Mpanda zitaondolewa kwenye chanjo mwaka 2008. Katika mwaka 2008/2009 Wizara itawezesha na kuratibu uchanjaji wa ng'ombe milioni 5 kuzuia ugonjwa huo chini ya mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Mbuzi (*CCPP*) ulitokea katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Mara, Ruvuma, Tabora na Tanga ambapo mbuzi 5,596 waliambukizwa na kati ya hao, 1,608 walikufa. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri iliwashauri wafugaji kutibu mbuzi wagonjwa kwa vile ugonjwa huo unatibika na hauna ulazima wa kuchanja. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaendelea kuwashauri wafugaji kupata ushauri kuhusu namna ya kudhibiti ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008 Ugonjwa wa Miguu na Midomo ulitokea kwenye wilaya za Chunya, Ilala, Iringa, Mbarali, Mbulu, Mpwapwa, Ngorongoro, Nzega, Rungwe, Same, Sengerema, Singida, Tabora na Temeke ambapo ng'ombe 10,840 walipata ugonjwa huo, kati ya hao 185 walikufa. Katika mwaka

2008/2009 Wizara itakamilisha mkakati wa kudhibiti ugonjwa huo na kutekeleza mkakati huo chini ya programu ya SADC ya kudhibiti ugonjwa huo. Vile vile Ugonjwa wa Mapele-ngozi ulijitokeza katika Halmashauri 37 nchini ambapo ng'ombe 1,539 waliugua na kati ya hao, 106 walikufa na 2,995 walichanjwa. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu athari na udhibiti wa ugonjwa huo na ng'ombe 4,000 wanatarajiwa kuchanjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008 Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe (*African Swine Fever)* ulitokea katika wilaya za Mvomevo, Kinondoni na Ilala ambapo nguruwe 1,288 walikufa. Hatua zilizochukuliwa kwa kushirikiana na Halmashauri hizo ni pamoja na kuweka karantini, kusafisha mabanda na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu athari za ugonjwa huo. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu athari na udhibiti wa ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008 Ugonjwa wa Mdondo uliendelea kujitokeza ambapo kuku 33,728 waliugua na kati ya hao, kuku 7,395 walikufa. Aidha, dozi 24,680,200 za chanjo dhidi ya ugonjwa huo zilizalishwa na kusambazwa. Katika mwaka 2008/2009 Wizara itakamilisha mkakati wa kudhibiti ugonjwa wa Mdondo na kuzalisha na kusambaza dozi milioni 30 za chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(OIE)* kuitambua nchi yetu kuwa mojawapo ya nchi ambazo hazina ugonjwa wa Sotoka duniani, katika kipindi cha 2007/2008 Wizara yangu imeendelea kufuatilia kutokuwepo kwa ugonjwa huo kwa kufanya uchunguzi katika mikoa ya mpakani ya Arusha na Mara katika mifugo na wanyama pori. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kuimarisha ufuatiliaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa yanayoenezwa na wadudu. Magonjwa yaenezwayo na kupe husababisha zaidi ya asilimia 72 ya vifo vyote vya mifugo hapa nchini. Kati ya vifo hivyo, asilimia 43.7 husababishwa na ugonjwa wa Ndigana Kali (*East Coast Fever*), asilimia 16.6 Ndigana Baridi (*Anaplasmosis*), asilimia 6.5 ugonjwa wa Maji Moyo (*Heart Water*) na asilimia 5.2 ugonjwa wa Mkojo Mwekundu (*Babesiosis*). Inakadiriwa kuwa hasara zinazotokana na kupe na magonjwa wayaenezayo ni takriban Dola za Kimarekani milioni 65. Katika mwaka 2007/2008 Serikali kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Plans – DADPs*) ilipanga kukarabati majosho 114 kwa shilingi 824,855,000 na kujenga mapya 92 kwa shilingi 1,443,605,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008 Serikali ilitoa shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kuendelea kutoa ruzuku ya dawa ya kuogesha mifugo kwa mikoa yote 21 Tanzania Bara ili kuwawezesha wafugaji kununua na kuogesha mifugo yao. Serikali imeingia mkataba na kampuni sita (6) za *Amilexin Traders*, *Anicrop Services*, *Bajuta International (T) Ltd, Bytrade (T) Ltd, Farmers Centre na Ronheam International* ambazo zimenunua jumla ya lita 59,122 za dawa za kuogesha mifugo na kuzisambaza. Wafugaji huuziwa dawa hizo kwa asilimia 60 ya bei halisi na asilimia 40 inalipwa na Serikali kama ruzuku. Aidha, sekta binafsi imetoa chanjo ya Ndigana Kali kwa ng'ombe

76,233 katika mikoa 11 ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Tabora, Kigoma na Kagera ikilinganishwa na ng'ombe 30,000 waliochanjwa mwaka 2006/2007. Katika mwaka 2008/2009 Wizara itaendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti kupe kwa kutoa ruzuku ya shilingi bilioni 1.4 kwa dawa ya kuogesha mifugo na sekta binafsi inatarajia kutoa chanjo ya ndigana kali dozi 100,000. Aidha, savei na ufuatiliaji wa ikolojia ya kupe na usugu wa kupe kwa dawa za kuogeshea itafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kuenea kwa mbung'o na ugonjwa wa Nagana katika mifugo limeendelea kuwapo hapa nchini. Katika mwaka 2007/2008 ng'ombe 2,994 waliambukizwa ugonjwa huo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Mbeya, Morogoro, Pwani, Shinyanga, Singida, Rukwa, Tabora na Tanga, kati ya hao, ng'ombe 93 walikufa. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Taasisi ya Utafiti wa Mbung'o na Nagana - Tanga iliendelea na ufugaji wa mbung'o wa aina mbalimbali kwa lengo la kutumia teknolojia ya madume ya mbung'o waliohasiwa ili kutokomeza mbung'o. Katika mwaka 2008/2009 Wizara itaanza kutekeleza Programu ya Umoja wa Afrika ya Kutokomeza Mbung'o na Nagana (PATTEC), kufuatalia mtawanyiko wa aina za mbung'o na kutoa ushauri kwa wafugaji kuhusu kutomeza mbung'o na kudhibiti ugonjwa wa nagana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu *(Zoonoses*). Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa (*Rabies*) bado unaendelea kuwa tishio kwa maisha ya wanyama na binadamu. Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu ilinunua dozi 50,000 na kusambazwa katika wilaya 26 nchini. Jumla ya mbwa 55,284 walichanjwa katika Halmashauri 12 za Iringa Vijijini, Kilolo, Tarime, Bunda, Kyela, Magu, Bariadi, Meatu, Singida Vijijini, Tabora Manispaa, Nzega na Uyui kutokana na chanjo hizo na nyingine kutoka sekta binafsi. Katika mwaka 2008/2009 Wizara itaendelea kudhibiti Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa kwa kununua na kusambaza dozi 50,000 za chanjo na kushirikiana na Halmashauri kutoa elimu kwa jamii juu ya athari za ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008 jumla ya ng'ombe 3,079 walifanyiwa uchunguzi wa Ugonjwa wa Kutupa Mimba (*Brucellosis*) katika mikoa ya kanda za Ziwa (286), Kaskazini (789), Kati (1,598) na Magharibi (406). Kati ya hao, 189 sawa na asilimia 6.1 waligundulika kuwa na ugonjwa huo. Ushauri ulitolewa wa kuchinja ng'ombe walioathirika ili kuepuka maambukizi kwa binadamu. Katika mwaka 2008/2009 ng'ombe 5,000 watachunguzwa dhidi ya ugonjwa huo na Wizara itaendelea kutoa ushauri wafugaji kuchanja mifugo yao dhidi ya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa (*Rift Valley Fever - RVF*) unatekelezwa kwa kufanya uchunguzi wa ugonjwa huo ambapo jumla ya sampuli 15,026 za damu kutoka kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo zimechukuliwa. Matokeo yameonyesha kuwa ugonjwa wa RVF haupo tena nchini. Pia, mafunzo yalitolewa kwa wataalam 75 wa mifugo, afya na elimu kutoka mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Singida na Tanga

kuhusu athari za ugonjwa huo. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaendelea kutekeleza mkakati na mpango wa kudhibiti ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji wa magonjwa na ukaguzi wa mifugo na mazao yake. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu imeendelea kufuatilia mienendo ya magonjwa ya mifugo kupitia vituo vyake vya kanda vya Arusha, Mwanza, Mpwapwa, Temeke, Tabora, Iringa na Naliendele (Mtwara). Aidha, vituo hivyo vimeimarishwa kwa kuvipatia vitendea kazi na watumishi 14 na kituo cha Tabora kimekarabatiwa. Katika mwaka 2008/2009 ukarabati na uimarishaji vituo hivyo utafanyika ili viweze kutekeleza majukumu yake. Aidha, ujenzi wa kituo cha Dodoma utaendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inasimamia vituo 41 vya ukaguzi wa mifugo na mazao yake vya mpakani na vingine 381 vya ndani vinasimamiwa na Halmashauri kwa lengo la kuzuia uingizaji na usambaaji wa magonjwa ya mifugo nchini. Katika mwaka 2007/2008, vituo vya Kwala (Kibaha) na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere vimeimarishwa na kupatiwa watumishi. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri itakarabati vituo 45 vya kukagulia mifugo na mazao yake pamoja na maeneo 13 ya karantini. Aidha, Wizara itaimarisha udhibiti na ukaguzi kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa wakaguzi 150 wa nyama, ngozi na mazao mengine ya mifugo kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya mifugo na mazao yake. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu imeendelea kuratibu biashara ya mifugo na mazao yake ikiwa ni pamoja na kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji. Juhudi hizi zimesaidia kukuza wigo wa biashara ya mifugo hai, nyama na ngozi katika nchi za Falme za Kiarabu, Oman, Kuwait, Umoja wa Comoro, Pakistan, Hongkong, India, Italia, Uturuki, Kenya, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Malawi, Burundi na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008 jumla ya ng’ombe 779,280, mbuzi 614,693 na kondoo 112,995, wenye thamani ya shilingi bilioni 216.1 waliuzwa katika minada mbalimbali nchini. Kati ya mifugo hiyo, ng’ombe 2,772, mbuzi na kondoo 874 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 waliuzwa nje ya nchi. Pia, tani 195 za nyama ya ng’ombe, mbuzi na kondoo zenye thamani ya shilingi milioni 500 ziliuzwa nje. Mapato kutokana na mauzo ya mifugo na nyama nje yameongezeka kwa asilimia 64.3 ikilinganishwa na mapato ya mwaka 2006/2007 ya shilingi bilioni 1.4. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa mauzo, kupanuka kwa wigo wa soko na kupanda kwa bei ya kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya vipande vya ngozi za ng’ombe milioni 2.5, mbuzi milioni 1.9 na kondoo milioni 1.5 vyenye thamani ya shilingi bilioni 13.5 vilikusanywa. Kati ya hivyo, vipande vya ngozi za ng’ombe milioni 2.3, mbuzi milioni 1.6 na kondoo milioni 1.1 viliuzwa nje ya nchi kwa thamani ya shilingi bilioni 21.5. Mapato kutokana na mauzo ya ngozi nje yameongezeka kwa asilimia 32.7 ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 16.2 mwaka 2006/2007. Ongezeko hilo kubwa linatokana na kuongezeka kwa ubora na uuzaji wa ngozi zilizosindikwa nje ya nchi. Katika mwaka

2008/2009, inakadiriwa kuwa vipande  milioni 2.8 vya ngozi za ng'ombe, milioni 2.0 vya mbuzi na milioni 1.6 vya kondoo vitakusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi Nchini umeanza kutekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Halmashauri 55 na Chama cha Wadau wa Sekta ya Ngozi (*Leather Association of Tanzania*). Mkakati huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo (*Livestock Development Fund)* ulioanzishwa mwaka 2003/2004 kutokana na makusanyo ya ushuru wa asilimia 20 ya mauzo ya ngozi ghafi nje ya nchi ambao uliongezwa kuwa asilimia 40 mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Juni, 2008 jumla ya shilingi bilioni 6.3 zimekusanywa na Serikali Kuu kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Kati ya hizo, shilingi 3,983,370,000 zilipangwa kutumika mwaka 2007/2008 kutekeleza mkakati, ikiwa ni pamoja na mafunzo kwa wataalam wakufunzi wa ngozi 110 wa Halmashauri na wadau, kuimarisha huduma za wagani kwa kununua pikipiki 55, baiskeli 275, magari mawili, vifaa vya kuchuna ngozi, kukarabati Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia ya Ngozi Mwanza na utekelezaji katika Halmashauri. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaendelea kushirikiana na wadau wengine kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuimarisha miundombinu ya masoko ya mifugo ili kuimarisha biashara ya mifugo na mazao yake. Katika mwaka 2007/2008 ujenzi wa mnada wa Mbuyuni (Chunya) na ukarabati wa minada ya upili ya Meserani (Monduli), Buhigwe (Kigoma), Mhunze (Kishapu), Pugu (Ilala) na Kasesya (Sumbawanga Vijijini) unaendelea. Kwa kushirikiana na Halmashauri kupitia Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) michoro ya miundombinu ya minada ya awali kwenye Wilaya za Lindi (Kitomanga), Kilwa (Mbwemkuru na Nangurukuru) na Rufiji (Umwekusini/Ikwiriri na Chumbi) imeandaliwa. Pia, miongozo ya kuendesha minada ya awali inaandaliwa kwa ajili ya kushirikisha watendaji watakaosimamia minada hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kuboresha mfumo wa utoaji wa taarifa za masoko ya mifugo (*Livestock Information Network Knowledge System-LINKS*) katika minada kwa kuongeza minada 15  ya Mbauda (Arusha), Endulen (Loliondo), Endagikoti (Mbulu), Dosidosi (Kiteto), Ndala (Nzega), Chamakweza (Bagamoyo), Mgagao (Mwanga), Masabi (Kahama), Parakuyo (Kilosa), Namanyere (Nkasi), Bukulu (Kondoa), Chipogolo (Mpwapwa), Mtana (Tarime), Ndereme (Handeni), Nyamuhongolo (Ilemela) na Rusahunga (Biharamulo). Hii inafanya jumla ya minada iliyoorodheshwa kwenye mfumo huo kuwa 29 ambayo hutoa taarifa za bei na aina ya mifugo iliyouzwa pamoja na madaraja kwa kutumia ujumbe wa simu za mikononi. Taarifa za masoko zinapatikana katika mtandao wa http://www.lmistz.net na kupitia tovuti ya Wizara http://www.mifugo_uvuvi.go.tz. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuimarisha mfumo wa kukusanya na kusambaza taarifa za masoko ya mifugo katika minada ya upili na kuhamasisha mauzo ya mifugo na mazao

yake. Pia, savei ya kuainisha maeneo yanayofaa kuwa huru na magonjwa ya mifugo (*Disease Free Zones/Compartments*) itafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaendelea kuimarisha miundombinu ya masoko ya mifugo kwa kukarabati minada ya upili ya Pugu, Meserani, Korogwe, Themi na Igunga na kujenga minada mipya ya Buzilayombo (Chato) na kukamilisha ujenzi wa mnada wa Nyamatara (Misungwi). Aidha, Wizara itashirikiana na wadau kuimarisha na kusimamia mfumo wa kukusanya na kusambaza taarifa za masoko ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake unaendelea kuimarishwa ambapo hadi sasa mashamba 26 ya ng'ombe, wafugaji wadogo 368 wa mbuzi wa maziwa, ng'ombe 42,902, mbuzi 3,793, kondoo 1,134 na nguruwe 574 wa kisasa wametambuliwa na kusajiliwa katika mfumo wa kitaifa. Nakala 125 za rejesta za kusajili wafugaji na mifugo vijijini zimesambazwa katika kijiji kimoja kila wilaya Tanzania Bara kwa ajili ya majaribio. Aidha, mafunzo kuhusu matumizi ya rejesta hiyo yametolewa kwa Washauri wa Mifugo wa Mikoa 4 na Maafisa Mifugo wa Wilaya 38 kutoka katika mikoa ya Dodoma (Mpwapwa, Dodoma, Kongwa), Morogoro (Mvomero na Kilosa), Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga. Pia, mafunzo hayo yalitolewa kwa wadau 122 kutoka mikoa ya Dodoma na Morogoro, kwa ushirikiano na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Vilevile, wadau wa mifugo walielimishwa kuhusu mfumo huo kupitia vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na radio, runinga na magazeti. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri itaendelea kuimarisha mfumo wa kitaifa wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Ugani wa Mifugo. Utoaji wa huduma za ushauri kwa wafugaji ni njia mojawapo ya kuwapatia wafugaji teknolojia sahihi na mbinu za ufugaji bora na huduma hizi hutolewa kwa kiasi kikubwa na Halmashauri. Hata hivyo huduma hizi hazitoshelezi kutokana na upungufu wa wataalam wa mifugo 13,469 katika ngazi ya vijiji. Ili kupunguza pengo hilo, kwa mwaka 2007/2008 Wizara imegharamia mafunzo ya stashahada kwa wanachuo 1,006 katika vyuo vya mafunzo vya Tengeru (402), Mpwapwa (232), Morogoro (231), Madaba (69), Temeke (43) na Buhuri (29). Katika mwaka 2008/2009 Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 1,185 katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu ilitoa mafunzo kwa wafugaji kupitia mashamba darasa 15 *(Farmer Field Schools - FFS)* katika Wilaya za Ilemela, Misungwi, Meatu, Ngorongoro, Tanga, Pangani, Handeni, Morogoro, Mvomero, Bahi na Kongwa. Pia, wakufunzi 10 walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu shirikishi ya shamba darasa la mifugo ili waweze kuanzisha mashamba darasa katika wilaya za Korogwe, Kilindi, Same, Hai, Arusha, Meru na Karatu. Vilevile, wafugaji 21,106 kutoka Wilaya 41 walipatiwa mafunzo kuhusu ufugaji bora na wa kibiashara katika vyuo vya mifugo na vya maendeleo ya wananchi. Aidha, vipeperushi 52,110,

mabango 30,130 na vijitabu 13,200 kuhusu ufugaji bora vilichapishwa na kusambazwa kwa wadau na vipindi 52 vya redio na 12 vya Televisheni viliandaliwa na kurushwa hewani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Halmashauri kupitia Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*Participatory Agricultural Development and Empowerment Project - PADEP*) imeendelea kuhamasisha wafugaji kuunda vikundi ili kuwa na nguvu ya pamoja na kuweza kutatua matatizo mbalimbali. Katika mwaka 2007/2008, jumla ya vikundi 880 vimeundwa na kufikia 1,728. Vikundi hivyo ni vya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa, uboreshaji ng'ombe wa asili, mbuzi wa maziwa, kuku wa asili na nguruwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri na wadau wengine itaimarisha huduma za ugani na kutoa mafunzo kwa wagani wakufunzi katika mikoa ya kanda za Ziwa, Kusini na Kaskazini kuhusu upangaji mipango ya ugani. Pia, Wizara itaendelea kuimarisha na kuratibu utoaji wa huduma za ugani zinazotolewa na Halmashauri na sekta binafsi. Vilevile, vipindi 52 vya redio na 12 vya luninga kuhusu ufugaji bora vitaandaliwa na kurushwa hewani. Vijitabu 13,000, vipeperushi 152,000 na mabango 30,000 kuhusu ufugaji bora yatachapishwa na kusambazwa kwa wafugaji. Aidha, wafugaji 21,000 wataelimishwa juu ya ufugaji wa kisasa na kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Wizara yangu ina jukumu la kusimamia rasilimali ya uvuvi nchini na kuhakikisha kuwa rasilimali hiyo inalindwa, inahifadhiwa na kuendelezwa kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Usimamizi huu unalenga kuwa na uvuvi endelevu utakaochangia kukuza uchumi wa Taifa, kuongeza kipato, lishe, ajira na hivyo kupunguza umaskini kwa wananchi. Katika mwaka 2007/2008 jumla ya tani 332,218 za mazao ya uvuvi yanayokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi bilioni 327.4 yalivunwa katika maeneo mbalimbali ya uvuvi nchini. Kati ya hizo, tani 57,795 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 25,502 waliuzwa nje. Mapato kutokana na mauzo hayo yalikuwa na thamani ya shilingi bilioni 213.2 na kuipatia Serikali shilingi bilioni 7.6 kama ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali ya uvuvi katika Maziwa. Mwaka 2007/2008 katika Ziwa Victoria, walivuliwa samaki tani 228,690.0 zenye thamani ya shilingi bilioni 224.7. Tathmini ya hali ya uvuvi iliyofanyika katika Ziwa Victoria ilibaini kwamba uvuvi haramu umekithiri katika nchi zote tatu na kasi ya uvuaji samaki aina ya sangara ni mkubwa kiasi cha kutishia uvuvi endelevu wa samaki hao. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda kupitia Taasisi ya *Lake Victoria Fisheries Organization* itaimarisha usimamizi wa rasilimali katika ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa mazao ya kibiashara hutegemea dagaa na migebuka ambayo ni maarufu kwa ajili ya chakula na

biashara ndani na nje ya Mkoa wa Kigoma. Ziwa Tanganyika kwa upande wa Tanzania linakisiwa kuwa na kiasi cha tani 80,000 za samaki ambazo zinaweza kuvuliwa bila kuathiri uwezo wa samaki hao kuongezeka. Katika mwaka 2007/2008 walivuliwa samaki wenye uzito wa tani 36,440 zenye thamani ya shilingi bilioni 21.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uendelezaji Uvuvi katika Ziwa Tanganyika chini ya Programu ya Maendeleo ya Uwiano katika Bonde la Ziwa Tanganyika ambao unashirikisha nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Tanzania na Zambia utaanza kutekelezwa mwaka 2008/2009 kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 68.4. Kati ya fedha hizi, Dola milioni 24.23 zitatumika kwa ajili kutekeleza kazi za maendeleo ya uvuvi na uhifadhi wa mazingira nchini mwetu. Fedha hizi zitatoka Benki ya Maendeleo Afrika *(ADF)*, Mfuko wa Mazingira *(GEF)*, Mfuko wa Maendeleo wa nchi ya Norway *(Nordic Development Fund)* na *International Union for the Conservation of Nature and Natural Resources (IUCN).* Utekelezaji wa mradi huo utasaidia kuinua hali ya uvuvi katika Ziwa na matumizi endelevu ya rasilimali ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007/2008 katika Ziwa Nyasa, walivuliwa samaki tani 4,390 zenye thamani ya shilingi bilioni 2.6. Kutokana na kina kirefu cha Ziwa hilo kwa upande wa Tanzania, upatikanaji wa samaki katika ziwa hilo ni mdogo. Aina kuu za samaki katika ziwa hilo ni mbasa, mbelele na dagaa. Kwa upande mwingine, Ziwa hili pamoja na Ziwa Tanganyika ni maarufu kwa upatikanaji wa samaki wa mapambo ambao wana soko kubwa nje ya nchi. Aidha, maziwa madogo, mabwawa na mito huchangia upatikanaji wa samaki tani 7,087 ambao ni muhimu katika kuimarisha lishe na pato kwa wananchi. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaimarisha uvuvi katika Ziwa Nyasa kwa kununua boti 2 na kutoa mafunzo kwa wavuvi ili kuwa na uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali ya uvuvi katika Bahari, uvuvi wa kibiashara katika maji ya kitaifa unahusisha kwa sehemu kubwa kambamiti (*prawns)*, kambakoche *(lobsters*) na pweza *(octopus*). Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu ilifuatilia uvuvi wa kambamiti katika ukanda wa pwani ambapo jumla ya meli 10 zilipewa leseni za uvuvi wa kambamiti na kuvua kambamiti tani 202.5 zenye thamani ya shilingi bilioni 2.6 na samaki tani 642.2 zenye thamani ya shilingi milioni 963. Uvuvi wa kambamiti ulishuka kwa asilimia 34 ikilinganishwa na mwaka 2006/2007. Hali hii imetokana na kupungua kwa rasilimali hiyo na hivyo, Wizara yangu imesitisha uvuvi wa kambamiti kwa wavuvi wakubwa kwa muda wa mwaka mmoja ili kuruhusu rasilimali hiyo iongezeke. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itasimamia na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi hayo na kutathmini uwingi wa rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, aina nyingine ya samaki wa kibiashara waliovuliwa ni pamoja na kambakoche tani 556 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.4 pweza tani 1,632 zenye thamani ya shilingi bilioni 8.0 na ngisi *(squids*) tani 54.7 zenye thamani ya shilingi milioni 211.8. Aidha, uvuvi wa samaki wa mapezi (fin-

fish) kutoka bahari yetu umelenga soko la ndani na huvuliwa na wavuvi wadogo. Aina muhimu ya samaki waliovuliwa kwa wingi ni jamii ya Kibua, Tasi, Nguru, Kolekole, Changu, Chewa, Taa, Kalambisi na Mzia ambapo tani 43,498 zenye thamani ya shilingi bilioni 39.3 walivunwa. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kusimamia uvunaji endelevu wa rasilimali hiyo. Aidha, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na vyombo vingine vya dola, ikiwa ni pamoja na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi, wananchi na wadau wengine katika kuhakikisha tunadhibiti uvuvi haramu unaofanywa na meli za kigeni pamoja na uvuvi unaofanywa kwa kutumia baruti katika bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuhimiza ukuzaji wa viumbe hai kwenye maji baridi kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa samaki na mazao mengine ya majini. Katika mwaka 2007/2008, vifaranga 603,010 vya samaki aina ya *Perege* vilizalishwa na Kituo cha Ufugaji Samaki Kingolwira – Morogoro na kusambazwa katika mikoa ya Morogoro (586,860), Pwani (3,150), Dar es Salaam (3,000) Tanga (7,500), na Kilimanjaro (2,500). Aidha, Wizara yangu imeandaa rasimu ya Mkakati wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe kwenye Maji (*National Aquaculture Development Strategy*) kwa lengo la kuzalisha mazao hayo kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendeleza ukuzaji wa viumbe hai kwenye maji chumvi, Wizara iliandaa na kusambaza kwa wadau mwongozo wa kutambua na kuchagua maeneo yanayofaa kufuga viumbe hai, ikiwa ni pamoja na kilimo cha mwani. Utambuzi wa maeneo yanayofaa kwa ufugaji samaki na unenepeshaji wa kaa katika vijiji 16 vya Wilaya ya Rufiji umefanyika. Vilevile majaribio ya ukuzaji wa viumbe kwenye maji chumvi na uzalishaji wa lulu (*pearls*) yaliendelea katika kisiwa cha Mafia. Vilevile, Mkakati wa Kuendeleza Ukuzaji wa Viumbe Hai katika maji chumvi, (*Mariculture Development Strategy*) unaandaliwa. Ili kuimarisha ugani kuhusu ukuzaji viumbe hai kwenye maji pikipiki 6 zilisambazwa katika wilaya za Mtwara, Tanga, Arumeru, Ngara, Lindi na Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Alphakrast ya Dar es Salaam imewekeza katika ufugaji wa samaki aina ya kambamiti katika eneo la Jimbo wilayani Mafia. Kampuni ina mpango wa kuchimba jumla ya mabwawa 76 yenye ukubwa wa hekta 1.5 kila moja yenye uwezo wa kuzalisha tani 912 za kambamiti kwa mwaka wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 8.5. Hadi sasa mabwawa 29 yamekamilika ambapo tani 140 zenye thamani ya takriban Dola milioni 1.5 zimezalishwa. Aidha, nchi yetu imekubaliwa kuuza mazao ya kufugwa (aquaculture products) kwenye soko la Jumuiya ya Ulaya *(EU)* kuanzia tarehe 3 mwezi Juni, 2008 Tanzania. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kufuatilia ufugaji wa mazao yanayotokanayo na ukuzaji wa viumbe hai kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha mwani kimeendelea kuchangia katika kuwapunguzia wananchi umaskini katika Ukanda wa Pwani. Katika mwaka 2007/2008, jumla ya tani 411.9 za mwani mkavu zilizalishwa katika mikoa ya Pwani (7), Tanga (160.7), Mtwara (18) na Lindi (226.2). Aidha, Wizara ilikutanisha wadau 70 wanaojihusisha na kilimo na biashara ya mwani kutoka Tanzania Bara na Visiwani kwa lengo la kuimarisha na kuendeleza kilimo na biashara ya zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine itaendeleza ukuzaji wa viumbe kwenye maji kwa kutumia teknolojia muafaka na kuimarisha ugani katika ufugaji wa samaki. Aidha, kazi zitakazofanyika ni pamoja na kufufua vituo vya ufugaji wa samaki vya Mtama (Lindi), Karanga (Moshi), Sikonge (Tabora) na Luhira (Songea); kuzalisha na kusambaza vifaranga 800,000 vya perege na 200,000 vya kambale kutoka Kituo cha Kingolwira. Pia, Wizara yangu itakamilisha rasimu ya Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe kwenye Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau itafanya utambuzi wa mabwawa mapya na yenye upungufu wa samaki na kupandikiza vifaranga, kuimarisha ukuzaji viumbe hai kwenye maji baridi na maji chumvi kwa kutoa mafunzo pamoja na kuainisha maeneo yanayofaa kwa ajili ya unenepeshaji wa kaa katika ukanda wa pwani. Vilevile, Wizara itaendelea kuhimiza kilimo cha mwani pamoja na kuwaunganisha wakulima na wanunuzi wa mwani kwa lengo la kuendeleza kilimo hiki kibiashara. Pia, mafunzo ya ujasiriamali yatatolewa kwa wanavijiji 200 wa ukanda wa pwani kuhusu kuboresha kilimo cha mwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi na usimamizi wa rasilimali ya uvuvi. Katika mwaka 2007/2008 Wizara iliendesha doria za nchi kavu na majini katika maziwa na ukanda wa pwani wa Bahari ya Hindi. Jumla ya siku za doria 5,247 zilifanyika na kuwezesha kukamatwa nyavu haramu 150,219, mitumbwi 191, mikuki 4, vifaa vya kuzamia 12, samaki wachanga kilo 41,901, samaki waliovuliwa kwa sumu kilo 552 na baruti 154. Vilevile, katika kupambana na utoroshaji wa mazao ya samaki mipakani, samaki wabichi kilo 1,550, dagaa wabichi kilo 405, samaki wakavu kilo 12,381 na dagaa wakavu 1,834 walikamatwa. Watuhumiwa 614 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu athari zinazosababishwa na utumiaji wa baruti kwenye shughuli za uvuvi imetolewa katika maeneo ya Wilaya za Temeke, Tanga, Muheza na Mkinga ambapo wananchi wameonyesha nia ya kupambana na uvuvi haramu. Pia, ufuatiliaji wa vyombo vya uvuvi vya kigeni 69 vilivyoandikishwa kuvua katika Bahari kuu umeendelea kufanyika kwa kutumia teknolojia iitwayo "*Vessel Monitoring System" (VMS).* Hivyo, naomba kutoa wito kwa wananchi na taasisi nyingine kushirikiana na Serikali kulinda rasilimali ya uvuvi katika maziwa, baharini na vyanzo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kuzishirikisha kwa karibu Halmashauri

na vijiji ili kudhibiti uvuvi haramu. Aidha, Wizara itaimarisha kikosi cha doria kwa kukipatia vitendea kazi muhimu na mifumo ya upanashaji habari za kiintelijensia pamoja na kuanzisha vituo vipya vya doria vya Kipili (Nkasi), Mafia, Kasumulo (Kyela), Tunduma (Mbozi), Kashenye (Misenyi), Horohoro (Mkinga), Sirari (Tarime), Sota (Rorya), Mtwara, Kilwa na Kasanga (Sumbawanga) na kuimarisha vilivyopo vya Mwanza, Musoma, Bukoba, Kigoma, Tanga na Dar-es-Salaam. Vilevile, jumla ya doria za siku 6,000 zitafanyika majini na nchi kavu. Aidha, leseni 69 zilizotolewa kwa vyombo vya kigeni zitapitiwa upya na kupewa masharti mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, Mwongozo wa Kitaifa wa Uboreshaji na Uendeshaji wa Vikundi vya Ulinzi wa Rasilimali ya Uvuvi (*Beach Management Units - BMUs*) umeboreshwa kwa lengo la kuwashirikisha wananchi na kuleta ufanisi katika usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi. Hadi sasa jumla ya vikundi 506 vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vimeimarishwa nchini ambapo vikundi 433 vipo Ukanda wa Ziwa Victoria, 29 Bwawa la Mtera, 19 Bwawa la Nyumba ya Mungu, 11 mto Ruhuhu, Mafia 6 na 8 Rufiji. Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vya usimamizi wa rasilimali kwa kuvijengea uwezo na kuvipatia mafunzo kwa kushirikiana na wadau wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na uvuvi endelevu, upatikanaji wa takwimu za rasilimali na nguvu ya uvuvi ni muhimu. Wizara yangu ilifanya sensa za uvuvi (*frame surveys*) katika vipindi vya miaka miwili miwili kati ya mwaka 1997 hadi 2007. Katika mwaka 2007/2008, sensa ya uvuvi katika bahari ilibaini kuwepo kwa wavuvi 36,247, vyombo vya uvuvi 7,342 na zana aina mbalimbali 60,819. Sensa hii imeonesha kwamba nguvu ya uvuvi imeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2005/2006 ambapo kulikuwa na wavuvi 29,754 na vyombo 7,190. Aidha, kwa upande wa Ziwa Victoria sensa inaonyesha kuwepo kwa wavuvi 98,015, vyombo vya uvuvi 29,732 na nyavu aina mbalimbali 931,889 ikilinganishwa na mwaka 2005/2006 ambapo kulikuwa na wavuvi 77,997 na vyombo 22,565.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi. Mazao ya uvuvi yanayouzwa yanapaswa kuwa na ubora unaokubalika kitaifa na kimataifa na hivyo umakini unahitajika katika utunzaji, uchakataji na usafirishaji hadi kumfikia mlaji. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu ilichunguza sampuli 1,526 kutoka viwanda vya kuchakata samaki vilivyoko ukanda wa Ziwa Victoria na ukanda wa pwani kuona kama zina vimelea haribifu na viuatilifu. Matokeo yalionyesha kuwa mazao hayo yalikuwa salama kwa matumizi ya binadamu. Vilevile, sampuli 15 za chakula cha kulishia kambamiti, 59 za kambamiti waliofugwa, 9 za maji na 6 za matope zilipelekwa katika maabara za *South African Bureau of Standards* na *CHEMIPHAR* ya Uganda kwa ajili ya kuhakiki ubora wa sampuli hizo. Aidha, wataalam 31 walipata mafunzo kuhusu ubora na usalama wa mazao ya uvuvi. Aidha, ukaguzi wa mazao ya uvuvi viwandani na kwenye maghala ulifanyika ambapo viwanda 16 vya uchakataji samaki, 5 vya kusafirisha kambakoche na kaa hai, 4 vya kusafirisha samaki hai wa mapambo na maghala 4 ya kuhifadhia mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliandaa Mpango wa Taifa wa Kutathimini Mabaki ya Kemikali (*National Residue Monitoring Plan)* kwa ajili ya ufugaji wa kambamiti nchini. Mpango huo unahakikisha kuwa kambamiti wanaofugwa kwenye mabwawa wanazalishwa katika mazingira yanayokidhi viwango vya kimataifa. Mpango huu unalenga kuiwezesha nchi yetu kuingizwa kwenye orodha ya nchi zinazoruhusiwa kuuza mazao hayo katika soko la Jumuiya ya Ulaya. Mpango huo uliwasilishwa katika Jumuiya ya Ulaya kwa ajili ya tathmini na umeridhiwa; na nchi yetu sasa inaweza kuuza kambamiti wanaofugwa katika soko hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea kuboresha usalama, ubora na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi kwa ajili ya soko la ndani na nje. Pia, sampuli 600 za minofu ya sangara, maji na matope zitafanyiwa uchunguzi katika Maabara ya Taifa ya Udhibiti wa Ubora wa Samaki Nyegezi na za nje ya nchi. Aidha, kaguzi 2,842 za samaki na mazao yake zitafanyika kabla ya kusafirishwa nje ya nchi na viwanda 84 zitafanyika kwenye viwanda vya kuchakata samaki. Aidha, Wizara itaendelea kufuatilia, kudhibiti ubora, usalama na kuhamasisha uongezaji wa thamani wa mazao yatokanayo na uvuvi. Vilevile, mialo 25 ya kupokelea samaki iliyobainishwa katika Ukanda wa Pwani na Ziwa Victoria itaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu kwa Umma. Katika mwaka 2007/2008. Wizara yangu iliandaa na kurusha hewani vipindi 6 vya redio kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania. Wachakataji 50 wa mazao ya Uvuvi, wavuvi 85 na wakaguzi 32 walipatiwa mafunzo kuhusu utunzaji bora na salama wa mazao ya Uvuvi. Aidha, wadau 150 walipatiwa mafunzo kuhusu namna ya kusafirisha mazao ya uvuvi nje ya nchi. Aidha, Wizara iliendesha mafunzo kwa wanavijiji 48 kutoka Wilaya za Mafia na Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo na elimu kwa umma kwa njia ya vipindi vya radio, luninga, majarida, kalenda na kushiriki kwenye maonyesho kuhusu matumizi bora ya rasilimali ya uvuvi, madhara ya uvuvi haramu, utunzaji wa mazingira na umuhimu wa kuanzisha vikundi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (*Marine and Coastal Environment Management Project – MACEMP*). Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu iliendelea kusimamia na kutekeleza Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani *(Marine and Coastal Environment Management Project* – MACEMP). Katika kipindi hicho, jumla ya shilingi 9,200,000,000 zilipangwa kutumika ambapo shilingi 4,678,864,217 zilitolewa na kutumika. Fedha hizo zimetumika kutekeleza miradi katika maeneo ya:-

(i) Uanzishwaji wa Mamlaka ya Usimamizi ya Ukanda wa Uchumi wa Bahari shilingi 720,111,000;

(ii) Usimamizi wa Rasilimali na Mazingira ya Pwani shilingi 2,300,535,573, ikiwa ni pamoja na kuwezesha Halmashauri za wilaya za Kilwa, Rufiji na Mafia na

taasisi nyingine (NEMC, TAFIRI, Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu,Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi, Wizara ya Maliasili na Utalii) kusimamia rasilimali za bahari na ukanda wa pwani;

(iii) Uendeshaji na usimamizi wa mradi shilingi 863,561,000 kwa kununua vitendea kazi, mafunzo, vyombo vya usafiri kwa Wizara na Halmashauri zinazotekeleza mradi huo;

(iv) Uwezeshaji wa vijiji kuendesha miradi midogo 87 ya kujipatia kipato katika wilaya za Kilwa, Mafia na Rufiji yenye thamani ya shilingi 794,656,644. Miradi hiyo imeibuliwa na imeanza kutekelezwa na wananchi katika wilaya za Kilwa (miradi 15 yenye thamani ya shilingi 130,828,634 kwa wanavikundi 245); Mafia (miradi 38 yenye thamani shilingi 334,942,585 kwa wanavikundi 412) na Rufiji (miradi 34 yenye thamani ya shilingi 328,885,425 kwa wanavikundi 702). Miradi hiyo inahusu ununuzi wa zana bora za uvuvi, ufugaji wa samaki, unenepeshaji wa kaa, ufugaji nyuki, ukaushaji samaki, kilimo cha mboga na ujenzi wa mashua. Aidha, fedha hizo hutolewa kwa vikundi kupitia TASAF. Vilevile, kazi zifuatazo zilifanyika;

(v) Mafunzo rejea kwa vikundi 15 vya Kilwa, 20 vya Mafia na 22 vya Rufiji vinavyotekeleza miradi midogo yametolewa. Aidha, wawakilishi wa vikundi 11 kutoka wilaya hizo vilifanya ziara za mafunzo ya ushirikishwaji jamii katika usimamizi wa rasilimali za bahari mkoani Tanga. Pia, mafunzo yalitolewa kwa wataalam 17 kutoka wilaya za Mafia, Kilwa na Rufiji kuhusu ukusanyaji wa takwimu za uvuvi;

(vi) Mafunzo kwa viongozi na watendaji wa Halmashauri za Mkinga, Muheza, Tanga, Pangani Bagamoyo, Kinondoni, Ilala, Temeke, Mkuranga, Lindi Mjini, Lindi Vijijini, Mtwara Mjini na Mtwara Vijijini ambazo zitaanza kutekeleza mradi mwaka 2008/2009; na

(vii) Kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa usimamizi bora wa rasilimali za uvuvi kupitia vipindi vya redio na televisheni, nakala 4,000 za Jarida la Dodoji, fulana na kofia 400 na mabango 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Mradi wa *MACEMP* utatumia kiasi cha shilingi 6,993,825,000 kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa mipango ya jumla ya usimamizi wa hifadhi za bahari na maeneo tengefu;

(ii) Kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo na kuandaa mpango wa mafunzo kuhusu usalama na ubora wa mazao ya uvuvi;

(iii) Kujenga ofisi za Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi na Hifadhi ya Bahari Mafia ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali katika maeneo tengefu;

(iv) Kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi litakalojulika kama *Mvuvi House;*

(v) Kuwezesha Halmashauri husika kuandaa mipango ya uendelezaji wa rasilimali na uibuaji wa miradi ya vikundi kwenye vijiji 129 katika wilaya zote zinazotekeleza mradi;

(vi) Kuimarisha mfumo wa kudhibiti mwenendo wa vyombo vya uvuvi kwenye bahari kuu;

(vii) Kutoa mafunzo na kuimarisha vikundi vya kulinda rasilimali kwenye wilaya 14 za ukanda wa pwani;

(viii) Kutoa mafunzo kwa maafisa doria 24 na waangalizi wa uvuvi 24 kuhusu mifumo wa kufuatilia mwenendo wa meli;

(ix) Kuendesha mafunzo kwa wataalam 28 kuhusu takwimu za uvuvi katika wilaya 14 zinazotekeleza mradi;

(x) Kuwezesha kufanyika tafiti za samaki waishio kwenye matumbawe kwa lengo la uhifadhi wa samaki hao; na

(xi) Kuwashirikisha wananchi na wadau wengine kuhusu uhifadhi wa samaki aina ya Silikanti kwenye eneo la Kigombe (Muheza).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi wa Ziwa Victoria (*Implementation of Fisheries Management Plan*), unatekelezwa katika Ziwa Victoria na unahusisha nchi za Tanzania, Kenya na Uganda ambazo zinamiliki ziwa hilo na kusimamiwa na Taasisi ya Uvuvi katika Ziwa Victoria (*Lake Victoria Fisheries Organization)*. Mradi huu unafadhiliwa na Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)* kwa gharama ya Euro milioni 29.9. Katika mwaka 2007/2008 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) Kuandaa Mwongozo wa Kikanda na Kitaifa wa kuanzisha na kusimamia vikundi vya ulinzi wa rasilimali ya uvuvi (*Regional and National BMU Guidelines*);

(ii) Kuhuisha taratibu za utoaji leseni na usajili wa mialo;

(iii) Kuandaa Mpango wa Kikanda wa Kudhibiti Uvuvi haramu na Nguvu ya Uvuvi katika Ziwa Victoria *(Regional Plan of Action to Deter and Control Illegal, Unreported and Unregulated Fishing);*

(iv) Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Ki-kanda wa Kudhibiti Uvuvi Haramu na Kasi ya Uvunaji wa Samaki kwa kupunguza nguvu ya uvuvi - *Regional Plan of Action for Reducing Fishing Capacity – RPOA – Capacity* katika Ziwa Victoria;

(v) Kuwezesha doria kufanyika dhidi ya uvuvi haramu ambapo watuhumiwa 558 walikamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria. Zana zilizokamatwa ni pamoja na makokoro 1,434, makokoro dagaa 141, nyavu chini ya inchi tano 6823, timba

(*monofilament nets*) 742, mitumbwi isiyokuwa na leseni 60 na magari 3 yaliyokuwa yakisafirisha mazao ya samaki kinyume cha sheria;

(vi) Kuwezesha uboreshaji wa mialo 12, miradi mitano ya huduma za jamii, ununuzi wa magari na vitendea kazi na kutoa elimu kwa umma na mafunzo kwa watalaam; na

(vii) Kuwezesha kuandaa Viwango vya Utekelezaji "*Standard Operating Procedures*" (SOPs) na miongozo, "*Code of Practices* na *Fish Inspectors' Guide"*, kwa matumizi ya nchi tatu za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kupitia Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi wa Ziwa Victoria itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa mialo sita ya Bwai (Musoma Vijijini), Sota (Rorya), Kigangama (Magu), Kahunda (Sengerema), Ikumbitare (Chato) na Marehe (Misenyi);

(ii) Kukamilisha miradi mitatu ya huduma kwa jamii ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika zahanati ya Kijiji cha Lugata (Sengerema); na ujenzi wa madarasa katika shule ya sekondari ya kata ya Nyahongo (Rorya), ujenzi wa madarasa katika shule ya msingi Soswa (Sengerema);

(iii) Kuendelea na ufuatiliaji na kutoa huduma za ushauri kwa wavuvi juu ya uvuvi endelevu na ulinzi wa rasilimali kupitia *BMUs*; na

(iv) Kuendelea kugharamia doria na mafunzo kwa wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sensa ya mifugo, kwa kutambua umuhimu wa sensa ya mifugo ili kupata takwimu sahihi kwa matumizi ya mipango ya maendeleo, Wizara yangu itaendesha sensa ya mifugo kwa njia ya sampuli (*Sample Census Survey*) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Taasisi ya Takwimu ya Taifa (*National Bureau of Statistics*). Sensa kwa njia ya kuhesabu mifugo kamili (*total livestock count/enumeration*) itafanyika mwaka 2010 kwa mujibu wa Kalenda ya Sensa ya Kilimo Duniani *(WCA-World Census of Agriculture*) inayoratibiwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya mazingira. Katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Mazingira na Vyanzo vya Maji kwa kuhimiza matumizi bora ya maeneo ya malisho, matumizi ya fursa mbalimbali katika maeneo kame ya ufugaji na matumizi ya nishati itokanayo na samadi ya mifugo *(biogas).* Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea kuhamasisha hifadhi ya mazingira kwa kuhimiza matumizi bora ya ardhi ya malisho na nishati mbadala ya biogas.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsia, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea kuboresha dawati la jinsia na kamati husika ziliundwa na mafunzo kutolewa.

Katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea kuimarisha dawati la jinsia na kuandaa viashiria muhimu vya jinsia katika Wizara ili kuweza kufuatilia na kupima mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Habari, Mawasiliano na Elimu kimeendelea kuimarishwa kwa kupeleka watumishi kwenye mafunzo na kukipatia vifaa muhimu. Kitengo kimeandaa vipindi maalum viwili (2) vya televisheni ambavyo vilirushwa kupitia runinga. Aidha, *Documentary* kwa ajili ya kituo cha Kuzalisha Mbegu za Madume bora NAIC Usa River imeandaliwa kusambaza nakala 1,000 za jarida la Wizara la kipindi cha Julai-Septemba 2007 na nakala 1,000 za Kalenda ya Mwaka 2008 ya Wizara. Pia, kimeandaa na kuchapisha kwenye magazeti makala tatu (3) kuhusu uhimilishaji ulivyowakomboa wanawake Arumeru, Chanjo ya Mdondo na Madume bora ya kuendeleza ufugaji wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaandaa na kurusha hewani vipindi vya radio 52 na 12 vya luninga, kusambaza vipeperushi, mabango, majarida na kalenda kuhusu Wizara. Pia itakamilisha na kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara na kuimarisha maktaba ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Utawala na Rasilimali Watu. Maendeleo ya Watumishi. Katika mwaka 2007/2008, Wizara imeajiri jumla ya watumishi 491, kati ya hao 129 ni wa kada za mtambuka, 231 ni wataalam wa mifugo na 131 ni wataalam wa uvuvi. Aidha, watumishi 95 wamepandishwa vyeo na 7 wamethibitishwa kazini. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira ya kazi, kupandisha vyeo watumishi 25 na kuajiri watumishi wapya 151 kujaza nafazi zilizo wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, watumishi wa kada mbalimbali wapatao 94 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu (19) na muda mfupi (75). Pia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi yametolewa kwa watumishi ili kuwaongezea ujuzi. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa wataalam kutoka katika Halmashauri za Wilaya 10 ili kujenga uwezo wa wataalam hao kuhusu matumizi endelevu ya nyanda za malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaanzisha benki ya takwimu za watumishi wa wizara kwa ajili ya kumbukumbu na kutoa mafunzo kwa watumishi 50 wanaoshughulika na utunzaji kumbukumbu juu ya utumiaji wa teknolojia ya kisasa ya utunzaji kumbukumbu. Pia, Wizara itashirikiana na Vyama Huru vya Wafanyakazi na Baraza la Wafanyakazi katika Wizara ili kuwezesha watumishi kuboresha utendaji wa kazi, kuongeza tija na kujenga uhusiano mzuri kati ya watumishi na kushiriki na kuhamasisha wafanyakazi kushiriki katika michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria na miongozo ya ajira Serikalini imeendelea kuzingatiwa ili kuepusha mazingira ya rushwa au upendeleo katika ajira. Pia, Mkataba wa Huduma kwa Mteja (*Client Service Charter*) wa Wizara umeandaliwa na unachapishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaandaa na kutekeleza Mkakati wa Kuziba/Kuzuia Mianya ya Rushwa katika Wizara kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa (*National Anti-corruption Strategic Plan – NACSAP*). Aidha, Wizara itaanzisha na kuimarisha mfumo wa OPRAS ndani ya Wizara kwa kutoa mafunzo kwa wakufunzi wa OPRAS katika taasisi za Wizara ili kuleta uwazi katika kutathmini utendaji kazi. Pia, Wizara itazindua Mkataba wa Huduma kwa Wateja (*Client Service Charter*), kuhamasisha wadau juu ya Mkataba huo na kufanya tathmini ya ubora wa huduma kwa wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, watumishi 250 walielimishwa kuhusu umuhimu wa kupima na kuzuia maambukizi mapya ya UKIMWI. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kuhamasisha watumishi kupima UKIMWI kwa hiari na kuelimisha walioambukizwa kuishi kwa matumaini, kuondoa unyanyapaa na kusambaza nyenzo za kuzuia UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikutano na maadhimisho mbalimbali. Katika mwaka 2007/2008 kulifanyika mikutano mbalimbali ya wataalam na wadau wa sekta za mifugo na uvuvi. Mikutano hiyo ililenga katika kujadili maendeleo na changamoto mbalimbali zinazozikabili sekta za mifugo na uvuvi pamoja na kubadilishana uzoefu. Baadhi ya mikutano hiyo ni:-

(i) Mikutano ya wadau wa sekta ya uvuvi. Wizara yangu ilifanya mikutano mbalimbali katika mwaka 2007/2008, mikutano maalum 2 ya wadau wa Sekta ya Uvuvi nchini ilifanyika Jijini Mwanza ambapo mkutano wa kwanza ulifanyika tarehe 21 Novemba, 2007 na kujumuisha Mawaziri wa Wizara za Maliasili na Utalii, Viwanda Biashara na Masoko na Wizara ya Fedha kwa lengo la kujadili jinsi ya kuboresha biashara ya samaki katika Ziwa Victoria. Mkutano huo pia uliwakutanisha viongozi, watendaji wakuu, wenye viwanda vya uchakataji samaki, wafanya biashara, wavuvi na wadau mbalimbali wapatao 200 kutoka kanda ya ziwa Victoria. Aidha, mkutano wa pili ulifanyika tarehe 5 Mei, 2008 na kujadili hali ya uvuvi na biashara ya samaki na namna ya kudhibiti uvuvi na biashara haramu katika ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano wa kuandaa Mkakati wa Kudhibiti Uvuvi wa Kutumia Baruti ulifanyika tarehe 2 Desemba, 2007 mjini Bagamoyo na kuhusisha viongozi wapatao 90 wa ngazi ya juu serikalini, mabalozi, mashirika na wadau mbalimbali ambapo kikundi kazi cha maafisa na watendaji wa serikali 13 kiliundwa ili kutekeleza mkakati huo. Aidha, tarehe 26 Aprili, 2008 kulifanyika mkutano Bandarini Dar es Salaam kati ya wadau wa uvuvi wa kambamiti na wajumbe wa Chama cha Wafanyakazi katika Meli za Uvuvi Tanzania (WAMEUTA). Katika kikao hicho, wanachama walipata nafasi ya kujadili kuhusu kupungua kwa rasilimali ya kambamiti na kufungwa kwa uvuvi wake, uvuvi haramu, hifadhi ya mazingira, uvuvi katika Bahari ya ndani na Bahari kuu. Katika kikao hicho, Wizara yangu ilitoa wito kwa wavuvi kuzingatia uhakiki wa ekolojia (*Eco-Labelling for Fisheries Certification*) ili kulinda soko la mazao ya uvuvi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukubwa wa tatizo la uvuvi haramu, tarehe 4 Julai, 2008, Mawaziri wa nchi za *SADC* za Angola, DRC, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Afrika Kusini na Tanzania tunaosimamia sekta ya uvuvi tulifanya mkutano Windhoek, Namibia kujadili tatizo la uvuvi haramu baharini na kutoa tamko la pamoja la kupiga vita uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao yake.

(ii) Mikutano wa wadau wa sekta mifugo. Mkutano wa wataalam wa sekta ya mifugo ulifanyika tarehe 27 – 28 Novemba, 2007 katika Manispaa ya Arusha na kuwashirikisha wataalam wa mifugo kutoka Halmashauri zote nchini, taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi. Mkutano huu ulijadili utekelezaji wa majukumu ya sekta katika Halmashauri, Sekretariati za Mikoa, Taasisi za Wizara na wadau wengine na namna ya kuyaboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa pamoja wa Vyama vya Wataalam wa Mifugo (*Tanzania Veterinary Association - TVA* na *Tanzania Society for Animal Production - TSAP*) ulifanyika tarehe 27 Novemba hadi 2 Desemba, 2007 katika Manispaa ya Arusha na kuwashirikisha wataalam wa mifugo kutoka ndani na nje ya nchi. Mkutano huo ulifunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na kufungwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mheshimiwa Isidory Shirima. Kaulimbiu ya mkutano huo ilikuwa ni: "*Sustaining Livestock Productivity in Challenging Tropical Environment as a Contribution Towards Achieving Millenium Development Goals"*. Katika mkutano huu, Mheshimiwa Rais alitoa maagizo mbalimbali ambayo Wizara yangu inaendelea kuyafanyia kazi.

(iii) Maadhimisho ya Shughuli za Wadau wa Sekta za Mifugo na Uvuvi. Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu ilishiriki katika kuandaa, kuonesha na kuadhimisha Siku ya Wakulima, Nane Nane ambayo kitaifa ilifanyika katika viwanja vya Themi-Arusha kuanzia tarehe 1 hadi 8 Agosti 2007. Maonesho hayo ambayo Kaulimbiu ilikuwa *"Punguza umaskini kwa kuzingatia kanuni za kilimo, ufugaji, ushirika na hifadhi ya mazingira"* yalifungwa na Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nachukua nafasi hii kuwashukuru viongozi wote, wadau mbalimbali na wananchi wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini kwa kushiriki na kufanikisha maadhimisho hayo. Aidha, nawashukuru wananchi na viongozi walioadhimisha maonesho hayo katika kanda mbalimbali. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itashiriki katika kuandaa maadhimisho hayo ambayo kitaifa yatafanyika katika Manispaa ya Dodoma. Kaulimbiu ya maonesho hayo ni *"Mapinduzi ya Kijani ndio Mkombozi wa Mtanzania"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Juni kila mwaka wadau wa maziwa huadhimisha Wiki ya Unywaji Maziwa duniani kote kwa lengo la kuhamasisha unywaji wa maziwa ili kupanua soko la ndani na kuinua viwango vya utumiaji wa maziwa na mazao yake. Katika mwaka 2007/2008, Wiki ya Unywaji Maziwa iliadhimishwa kitaifa mkoani Rukwa kuanzia tarehe 29 Mei hadi 1 Juni 2008. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa, *"Fuga ng'ombe wa maziwa uongeze kipato na lishe"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadhimisho mengine ambayo Wizara yangu ilishiriki ni pamoja na; Siku ya Unywaji Maziwa Mashuleni, Siku ya Chakula Duniani, Siku ya Veterinari, Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani, Siku ya Wanyama Duniani na Wiki ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, mikutano na maadhimisho yote niliyoyaeleza hapo juu yametoa changamoto, msukumo na mchango mkubwa katika kuboresha maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto katika utekelezaji. Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 zimeendelea kukabiliwa na changamoto nyingi ambazo ni pamoja na:-

(i) Gharama kubwa za pembejeo za mifugo na uvuvi zikiwemo dawa za kuogeshea, zana za uvuvi kumesababisha wafugaji na wavuvi kushindwa kuzimudu na hivyo kupunguza uzalishaji wenye tija na kupunguza mapato kwa wafugaji na wavuvi. Kulingana na bajeti ya mwaka 2008/2009 Serikali itatumia shilingi bilioni 1.4 kama ruzuku kwa ajili ya dawa za kuogesha mifugo ambazo zinatosha kununua lita 68,579 tu kwa bei ya sasa. Kiasi hicho kinatosha kuogesha ng'ombe takriban milioni 2.3 sawa na asilimia 12 ya ng'ombe wote. Hivyo, kuendelea kuogesha kwa aslimia hizo ndogo itakuwa ni vigumu kuonyesha matokea mazuri katika kudhibiti kupe na magonjwa wayaenezayo. Ili kufikia lengo la mafanikio ya uogeshaji ng'ombe kwa angalau asilimia 80 kiasi cha shilingi bilioni 12.4 kingehitajika na hivyo kufanya kuwepo upungufu wa shilingi bilioni 11;

(ii) Uhaba wa maeneo ya ufugaji na miundombinu umesababisha wafugaji kuhamahama na kusababisha uharibufu wa mazingira, kuenea kwa magonjwa ya mifugo na migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi;

(iii) Uwekezaji mdogo katika sekta ya mifugo na uvuvi umesababisha ukuaji mdogo wa sekta hizi kuliko ilivyotarajiwa;

(iv) Kuwepo kwa magonjwa mbalimbali ya mifugo na tishio la ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege kumeathiri pia maendeleo ya Sekta ya Mifugo nchini;

(v) Uhaba wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na uhifadhi wa samaki na mazao ya uvuvi, uzalishaji duni na ukosefu wa masoko ya uhakika kumepunguza mchango wa sekta hizi katika Pato la Taifa;

(vi) Kutokuwepo kwa taasisi za mikopo zenye masharti nafuu kwa wafugaji na wavuvi kumesababisha washindwe kupata mitaji ili kuzalisha kibiashara;

(vii) Tija ndogo katika uzalishaji wa mifugo hasa ya asili imesababisha sekta hii kutochangia kikamilifu katika pato la taifa. Aidha, mifugo mingi ya asili ina ukosaafu mdogo na hivyo kuwa na viwango vidogo vya uzalishaji; na

(viii) Kuendelea kuwapo kwa uvunaji na matumizi ya rasilimali za uvuvi yasiyoendelevu, ikiwa ni pamoja na kuibiwa samaki kunakofanywa na meli za kigeni katika Bahari *(EEZ)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Dkt. James Wanyancha (Mb), Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Katibu Mkuu Dkt. Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Jonas Melewas, Wakuu wa Idara na Taasisi za Wizara yangu, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi mbalimbali, Wafanyakazi na Wadau wote wa sekta za mifugo na uvuvi kwa juhudi na mshikamano wao katika kufanikisha malengo ya Taifa kwa ujumla katika maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi. Napenda kutoa shukrani zangu kwa:-

- Kamati ya Bunge ya Sekta ya Kilimo, Mifugo na Maji;

- Kuzitambua na kuzishukuru nchi za Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Serikali za Australia, Austria, Denmark, Japan, Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Ireland, Marekani, Misri, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi na Italia. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa mashirika ya Umoja wa Mataifa ya FAO, IFAD, CFC, UNICEF, UNDP, GEF na IAEA;

- Kutambua na kuzishukuru taasisi za kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB); Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japani (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DfID), Taasisi ya Rasilimali za Wanyama la Umoja wa Afrika (AU/IBAR), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GTZ), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark (DANIDA), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Norway (NORAD);

- Napenda pia kuyashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za *Vet Aid*, *Care International*, *OXFAM* na *Wellcome Trust* za Uingereza, Austro-*Project, Heifer Project Tanzania (HPT), World Vision, FARM Africa, Land 'O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), Association for Agricultural Research in East and Central Africa (ASARECA), Overseas Fisheries Co-operation Foundation of Japan (OFCF), World Society for Protection of Animals (WSPA), Worldwide Fund for Nature (WWF)* na *International Livestock Research Institute (ILRI)* ambao wameendelea kuisaidia Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misaada yao tunaiheshimu na kuienzi na ninaomba wadau wengine wajitokeze kusaidia jitihada za Serikali kuboresha huduma za maendeleo ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda kuwashukuru wapigakura wangu katika Jimbo la Biharamulo Mashariki ambalo nina uhakika hivi karibuni litaitwa Jimbo la Chato kwa sababu kwa sasa hatuko ndani ya Wilaya ya Biharamulo, kwa

ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kutoa kwangu. Ninajua bila wao haya yote ninayoyafanya nisingeyafanya lakini nawashukuru pia kwa sara zao katika kuniwezesha kufanya kazi hizi ngumu ambazo tunazikabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Sekta ya Mifugo na Uvuvi zinasimamiwa na Sheria mbalimbali kama zilivyoainishwa katika hotuba hii. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itasimamia kwa dhati na uadirifu Sheria na Kanuni zote zinazohusika katika maendeleo ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu mnipe ushirikiano katika kusimamia utekelezaji wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka wa fedha wa 2008/2009. Katika mwaka wa 2007/2008 iliyokuwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo ilitengewa Jumla ya shilingi 22,367,516,000 na Idara ya Uvuvi iliyokuwa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ilitengewa shilingi 25,559,366,120 na kuwa na jumla ya shilingi 47,856,842,120. Hivyo katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 Wizara yangu inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya shilingi 41,872,873,000 kama ifuatavyo:-

(i) Shilingi 9,334,915,000/= kama makusanyo ya mapato ya Serikali;

(ii) Shilingi 7,738,262,000/= kwa ajili ya mishahara ya Watumishi *(PE)*;

(iii) Shilingi 13,761,804,000/= kwa ajili ya matumizi ya mengineyo *(OC);*

(iv) Shilingi 20,372,501,000/= kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi 7,723,810,000/= ni fedha za ndani na shilingi 12,648,667,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara yangu kwa anuani: www.mifugo_uvuvi.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutakubaliana kwamba hotuba hii imesheheni masuala mengi ambayo kwa kweli yanajibu masuala mengi ya wafugaji na wavuvi wa nchi hii. Kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati husika, naomba niwatambulishe wageni wa Mheshimiwa Kaika S. Telele na Mheshimiwa Lekule Laizer ambao ni ndugu Edward Porokwa, Mratibu wa PINGOs pamoja na wafugaji wale ambao walikuwa hawajafika wakati tunawatambulisha baada ya kipindi cha maswali na majibu wa kutoka kule Ngorongoro na maeneo mengine. Wafugaji wote mlioko hapo juu msimame. Karibuni sana Bungeni na tunafurahi sana kwamba mnafuatilia masuala yanayohusu ufugaji jambo ambalo ni muhimu sana kwenu na tunatumaini mwakani wavuvi nao watakuja kutembelea Bunge, karibuni sana. *(Makofi)*

Baada ya maneno hayo, namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Mifugo na Uvuvi kwa niaba yake Mheshimiwa Kaika S. Telele, ndiyeatakayosoma hotuba ya Kamati hiyo.

**MHE. KAIKA S. TELELE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba niwasilishe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana Dar es salaam tarehe 05 na 06 Juni, 2008. Katika kikao hicho, Kamati ilipata maelezo ya kina kutoka kwa Wizara kuhusu Dira na Muundo wa Wizara, Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, Mafanikio na Changamoto za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Mwaka 2007/2008. Aidha, Kamati ilipata maelezo ya malengo na maeneo ya kipaumbele na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka 2007/2008, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Kamati ilitoa maoni na ushauri wa kuzingatiwa na kutekelezwa ili kuleta ufanisi na kuongeza tija katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara imeyafanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati kadri ilivyowezekana, baadhi ya hatua za utekelezaji ni kama zifuatavyo:-

(a) Sekta ya Mifugo

(i) Wizara katika kukabiliana na tatizo la kupotea kwa mifugo asili, imefanya uchambuzi wa koo za mifugo;

(ii) Serikali kwa kushirikiana na *VETA* imeendelea kuhamasisha wafanyabiashara wa nyama kujiunga na Chuo cha Ukataji Nyama cha Dodoma ili kujifunza namna bora ya kukata na kuhifadhi nyama kitaalam;

(iii) Maeneo ya ufugaji katika Wilaya 24 za Mikoa ya Mbeya, Iringa, Pwani, Lindi, Morogoro, Dodoma, Singida, Kagera, Tabora na Kigoma tayari yamepimwa. Aidha Halmashauri zinahamasishwa kujenga na kukarabati miundombinu ya mifugo katika maeneo yao kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)*.

(iv) Serikali inaendelea na mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Wakulima ambayo itatoa huduma za kibenki kwa wafugaji na wakulima;

(v) Serikali imeendelea kuhimiza wadau wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika sekta ya mifugo ikiwa ni pamoja na kuanzisha Ranchi, Machinjio ya kisasa na Viwanda vya kusindika mazao ya mifugo;

(vi) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kuhamasisha wafugaji kujiunga kwenye vikundi na kuomba mikopo kwenye Vyama vyao vya *SACCOS* ili kupata fedha za kununua matanki ya kupoza na kuhifadhi maziwa;

(vii) Serikali ilitenga kiasi cha shilingi billion 1.2 kwa mwaka 2007/2008 kwa ajili ya ruzuku ya madawa ya mifugo;

(viii) Katika mnada wa Pugu ilionekana ushuru wanaotozwa wafugaji ni mkubwa. Wizara imewasiliana na Wizara ya Fedha na Uchumi kuhusu suala hilo na utaratibu unaandaliwa kurekebisha suala hilo kulingana na hali halisi ya biashara ya mifugo ili kuboresha huduma za masoko; na

(ix) Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa na vituo vingine vya utafiti wa mifugo vimeimarishwa kwa kufanyiwa ukarabati wa majengo, miundombinu na kupatiwa vitendea kazi na vifaa vya kisasa.

(b) Sekta ya Uvuvi

(i) Uanzishwaji wa chombo cha kusimamia Uvuvi kwenye bahari kuu (*The Deep Sea Fishing Authority)* nao umetekelezwa kwani marekebisho ya chombo hicho

kilichoundwa mwaka 1998 yalipitishwa na Bunge tarehe 05 Februari 2007 na mchakato wa kuwapata watendaji wakuu wa Mamlaka hiyo unaendelea;

(ii) Wizara kwa kushirikiana na wadau wa mwani inaendelea kuhamasisha kilimo cha mwani kwa lengo la kuongeza tija na kipato kwa wakulima. Aidha Wizara imeandaa mkakati wa kitaifa wa kuendeleza ukuzaji wa viumbe hai majini na kutoa mwongozo wa maeneo yanayofaa kufuga viumbe hai wa maji chumvi ikiwa ni pamoja na kilimo cha mwani; na

(iii) Katika kuandaa Kanuni za kusimamia uvuvi kwenye Bahari Kuu na kuharakisha uanzishwaji wa Mamlaka katika Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing Authority)*, kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mchakato huo unaendelea ili kuharakisha uanzishwaji wa Mamlaka hiyo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio katika utekelezaji wa Bajeti wa Wizara kwa mwaka 2007/2008. Mafanikio katika Mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 22,397,516,000. Waziri aliieleza Kamati kwa undani kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2006/2007, mafanikio hayo ni pamoja na:-

(a) Sekta ya Mifugo

(i) Kuandaa mapendekezo ya kutunga sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za miongozo inayohusu sekta ya mifugo;

(ii) Kusambaza nakala 3,700 za Sera ya Taifa ya Mifugo ya 2006 kwa wadau na kutoa elimu kuhusu sera hiyo.

(iii) Kuanzisha mfumo wa kumbukumbu za utafiti wa Mifugo *(Research Database)* kwa kukusanya takwimu mbalimbali kutoka katika kanda tano za Utafiti, ikiwa na lengo la kuzihifadhi na kuzisambaza kwa wadau kupitia machapisho na tovuti ya Wizara;

(iv) Kupatiwa mafunzo wafugaji 21,106 kutoka Wilaya 41 kuhusu ufugaji bora wa kibiashara. Aidha, Wataalam 20 wa Ugani kutoka Wilaya 10 za Kanda ya Kati nao walipata mafunzo kuhusu upangaji Mipango ya Ugani na Wafugaji vijijini;

(v) Kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba nchini kwa kukarabati majengo ya ofisi na makazi, miundombinu ya shamba, mitambo na kuweka umeme katika mashamba ya Kitulo, Ngerengere na Mabuki;

(vi) Kwa kushirikiana na wadau wa Sekta, Wizara imeshiriki kuandaa Mpango kabambe wa Kukuza mauzo ya mifugo nje;

(vii) Mfumo wa unenepeshaji ngo'mbe umeanza ili kukidhi mahitaji ya soko;

(viii) Ranchi za Kongwa na Ruvu zimewezeshwa kununua madume bora aina ya Borani 120 na kuboresha miundombinu ya mashamba;

(ix) Mkakati wa kufufua na kuendeleza sekta na viwanda vya ngozi nchini umeanza kutekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, OWM-TAMISEMI na chama cha wadau wa Sekta ya Ngozi *(Leather Association of Tanzania);*

(x) Wizara imeendelea kuimarisha huduma za afya ya Mifugo kwa kuweka mikakati ya kudhibiti magonjwa kama Sotoka, Homa ya Bonde la Ufa *(RVF)*, Mafua makali ya ndege *(Avian Influenza)* na kadhalika;

(xi) Vituo vya Kanda vya Uchunguzi wa Magonjwa ya mifugo vimeimarishwa kwa kupatiwa majokofu, kabati maalum *(Biosafety cabinets)* na vifaa vya kujikinga wakati wa kufanya uchunguzi au kuchukua sampuli;

(xii) Kitengo cha utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake kimeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi;

(xiii) Maabara kuu ya Mifugo ya Taifa – Temeke imeendelea kuimarishwa kwa kupatiwa vifaa vya kisasa na vitendea kazi muhimu ili iweze kufikia kiwango cha Kimataifa.

(b) Sekta ya Uvuvi

(i) Serikali kwa kushirikiana na nchi za Uganda na Kenya zimeandaa na kuanza kutekeleza mpango wa ki-kanda *(Regional Plan of Action for Reducing Fishing Capacity)* katika Ziwa Victoria. Mpango huu unalenga kusimamia na kudhibiti uvuvi haramu na kasi ya uvunaji wa samaki usio endelevu;

(ii) Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hususan vyombo vya dola, Ubalozi wa Uingereza, mashirika yasiyo ya Kiserikali kama *WWF* imeandaa mkakati maalum wa kudhibiti uvuvi haramu wa kutumia mabomu;

(iii) Ili kudhibiti meli zinazovua katika maji makuu kwenye ukanda wa uchumi wa Bahari *(Exclusive Economic Zone)* mfumo wa kuratibu mwenendo wa meli baharini umeanzishwa na unafanya kazi;

(iv) Wizara kwa kushirikiana na wadau wa mwani inaendelea kuhamasisha kilimo cha mwani kwa lengo la kuongeza tija na kipato;

(v) Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani *(MACEMP)* nao umesaidia katika kudhibiti uvuvi haramu kwa kuweka doria katika ukanda wa Pwani na kusaidia shughuli nyingine za Maendeleo;

(vi) Mradi wa kutekeleza Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi *(Implementation of Fisheries Management Plan)* wa ziwa Victoria umeendelea kuboresha mialo 12 na miradi 5 ya huduma za jamii ikiwemo Shule na Zahanati. Aidha, mpango wa kikanda wa kudhibiti uvuvi haramu katika Ziwa Victoria umeandaliwa *(Regional Plan of Action to deter and control illegal, unreported and unregulated fishing and control of Fishing Capacity)*;

(vii) Maabara ya Taifa ya Uvuvi Nyegezi imethibitishwa na *"South African National Accreditation Services"* kuweza kuchunguza vimelea kwenye mazao ya chakula ikiwa ni pamoja na samaki;

(viii) Mapato. Katika kipindi cha 2007/2008 Wizara ilitarajia kukusanya shilingi 9,092,925,000 hadi kufikia mwezi Mei 2008 jumla ya shilingi 9,213,972,760 sawa na asilimia 101.3 ya lengo la makusanyo zilikusanywa. Haya ni mafanikio makubwa, Kamati iliipongeza Wizara kwa kuweka mikakati madhubuti ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

(ix) UKIMWI. Wizara imefanikiwa kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kupima na kuzuia maambukizi mapya ya UKIMWI kwa watumishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2007/2008. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Waziri alieleza kwa kina changamoto au matatizo yaliyojitokeza katika kutekeleza bajeti ya Wizara kwa mwaka 2007/2008, changamoto au matatizo hayo ni pamoja na:-

(i) Upungufu wa fedha katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara;

(ii) Uhaba wa maeneo ya ufugaji na miundombinu umesababisha wafugaji kuhamahama na hivyo kuleta uharibifu wa mazingira, kuenea kwa magonjwa ya mifugo na migogoro baina ya wafugaji na wakulima;

(iii) Uwekezaji mdogo katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi umesababisha ukuaji mdogo wa sekta hizi kuliko ilivyotarajiwa.

(iv) Kuwepo kwa magonjwa mbalimbali ya mifugo na tishio la ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege kumeathiri pia maendeleo ya Sekta ya Mifugo nchini;

(v) Uhaba wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na uhifadhi wa samaki na mazao ya uvuvi, uzalishaji duni na ukosefu wa masoko ya uhakika, kumepunguza mchango wa sekta hizi katika Pato la Taifa;

(vi) Kutokuwepo kwa taasisi za mikopo zenye masharti nafuu kwa wafugaji na wavuvi kumesababisha washindwe kupata mitaji ili kuzalisha kibiashara;

(vii) Tija ndogo katika uzalishaji wa mifugo hasa ya asili imesababisha sekta hii kutochangia kikamilifu katika Pato la Taifa;

(viii) Gharama kubwa za pembejeo za mifugo na uvuvi zikiwemo dawa za kuogeshea, zana za uvuvi kumesababisha wafugaji na wavuvi kushindwa kuzimudu; na

(ix) Kuendelea kuwepo kwa uvunaji na matumizi ya rasilimali za uvuvi yasiyo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo na mipango wa Wizara kwa mwaka 2008/2009. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara imeainisha maeneo ya kipaumbele yatakayotekelezwa ambayo yamezingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Dira ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Baadhi ya maeneo hayo ya kipaumbele ni kama ifuatavyo:-

(a) Sekta ya Mifugo

(i) Kuandaa Mikakati na Sheria zitakazoimarisha Sekta ya Mifugo;

(ii) Kuimarisha Utafiti wa Mifugo na kuboresha koosafu za Mifugo;

(iii) Kuimarisha huduma za ugani kwa kuongeza idadi ya Maafisa Ugani tarajali;

(iv) Kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kuogesha na chanjo za mifugo;

(v) Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo; na

(vi) Kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya usindikaji wa nyama na maziwa ili kuwepo soko la uhakika.

(b) Sekta ya Uvuvi

(i) Kuimarisha doria ili kudhibiti uvuvi haramu kwa kukipatia kikosi cha doria vifaa;

(ii) Kufanya mapitio ya sera na sheria za uvuvi;

(iii) Kuendeleza mchakato wa kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing Authority);*

(iv) Kuimarisha udhibiti wa ubora, usalama na kuongeza thamani kwa mazao ya uvuvi; na

(v) Kuwezesha kufanyika tafiti zitakazowezesha kufahamu kiasi cha rasilimali ili kuweza kupanga mikakati endelevu ya uhifadhi, uvunaji na utumiaji wa rasilimali ya uvuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Baada ya kueleza utekelezaji wa maoni ya Kamati na changamoto zilizoikabili Wizara katika utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2007/2008 na Matarajio ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka 2008/2009 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokana na tishio la upungufu wa chakula, Kamati inashauri Serikali ichukue hatua za makusudi kuwawezesha wafugaji na wavuvi kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo na uvuvi;

(ii) Elimu duni kwa wafugaji na wavuvi imesababisha jamii hizi kuendelea kutonufaika na kuwa maskini, Kamati inashauri elimu ya ufugaji bora na uvuvi endelevu itolewe kwa jamii hizi ili waweze kuwa na maisha bora ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya wataalam wa ugani;

(iii) Kutokana na kukwama kwa miradi mingi ya maendeleo kwasababu ya kuchelewa kwa fedha za Wafadhili, Kamati inashauri Serikali ijitahidi kupanga mipango yake bila ya kutegemea sana fedha za wafadhili; na

(iv) Huduma za Utafiti ni muhimu sana katika kuleta maendeleo ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi, suala hili litawezekana endapo watafiti watawezeshwa kwa kuwa na maisha bora na mazingira mazuri ya kazi. Kamati inashauri Serikali itenge fedha za kutosha katika shughuli za Utafiti ili kuhakikisha watafiti wanapata maslahi mazuri na kuboresha mazingira ya miundombinu ya utafiti.

(a) Sekta ya Mifugo

(i) Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya ruzuku ya madawa ya mifugo ambacho hakikukidhi mahitaji halisi ya wafugaji, Kamati inashauri kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Serikali iongeze ruzuku ya madawa ya mifugo ili iweze kukidhi mahitaji halisi ya wafugaji;

(ii) Kwa kuwa Maabara Kuu ya Mifugo ya Taifa-Temeke ni maabara ambayo inategemewa na nchi za *SADC*, Kamati inashauri Maabara hiyo iboreshwe kwa kuipatia vifaa vya kisasa na vitendea kazi muhimu ili iweze kufikia kiwango cha kimataifa;

(iii) Kwa kuwa Serikali ilishaunda Tume ya kuchunguza suala la uhamisho wa wafugaji kutoka IHEFU, Kamati inashauri Serikali itoe taarifa ya hali halisi ya zoezi zima na hatua ilizochukua. Aidha, kutokana na Mikoa iliyopangiwa kuwapokea wafugaji hao kutoka IHEFU kutokuwa na miundombinu na huduma za kijamii, Kamati inashauri Serikali ichukue hatua za makusudi na kupeleka huduma za haraka ili kuwaokoa wafugaji hao kutokana na janga kubwa la ukosefu wa huduma za shule, maji, afya, majosho na malambo;

(iv) Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, juu ya umuhimu wa kula nyama na kunywa maziwa kwa ajili ya afya zao, na kuhamasisha wananchi kuongeza kiwango cha matumizi ya mazao hayo yatokanayo na mifugo. Kwa mujibu wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)*, kiwango kinachopendekezwa ni lita 200 za maziwa na kilo 50 – 60 za nyama kwa mtu mmoja kwa mwaka. Hata hivyo, Tanzania inakadiriwa kuwa mtu mmoja anakunywa lita 39 za maziwa na kilo 10.3 za nyama kwa mwaka, hiki ni kiwango cha chini sana.

(v) Kamati inashauri Serikali iendelee kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ili kutekeleza Mradi wa Kimataifa wa kuendeleza zao la ngozi unaofadhiliwa na *Common Fund for Commodities (CFC)* kwani ngozi ni mojawapo ya zao nchini litokanalo na ng'ombe, mbuzi na kondoo linaloliingizia Taifa pesa za kigeni;

(vi) Kamati inashauri Serikali iondoe ushuru wa madawa na vifaa vya mifugo;

(vii) Kamati inashauri majosho na malambo kwa ajili ya mifugo yakarabatiwe na mapya yajengwe kwani kuwepo kwa miundombinu hiyo kutasaidia ufugaji bora na kukua kwa Sekta ya Mifugo;

(viii) Kamati inashauri Serikali iendelee kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa uhamilishaji *(Artificial Insemination*) kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mifugo iliyo bora;

(ix) Kamati inashauri Serikali imuhimize mwekezaji wa kiwanda cha kusindika nyama cha Shinyanga kuanza uzalishaji mapema. Aidha Serikali iendelee na juhudi za kutafuta mwekezaji wa kiwanda cha kusindika nyama cha Mbeya ili kusaidia wafugaji kuuza mazao yatokanayo na mifugo yao;

(x) Kutokana na kuongezeka kwa wimbi la wizi wa mifugo hasa katika maeneo ya mipakani na miongoni mwa makabila ya wafugaji, Kamati inashauri Kitengo cha Kuzuia Wizi wa Mifugo *(Stop Theft Prevention Unit)* kifufuliwe na kiimarishwe kwa kupatiwa vitendea kazi muhimu; na

(xi) Kamati inashauri Serikali iendelee kuelimisha wananchi kutotumia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo kwa shughuli za kilimo na wala yasitolewe kwa wawekezaji. Aidha, maeneo ya mifugo mapya waliyopangiwa wafugaji yapimwe upya, yamilikishwe kwa wafugaji na yawekewe miundombinu.

(b) Sekta ya Uvuvi

(i) Sekta ya uvuvi itaendelea vizuri endapo viwanda vya kutosha vitajengwa ili kusindika mazao ya uvuvi. Kamati inashauri Serikali ijitahidi kushawishi wawekezaji ili waweze kujenga viwanda hivyo katika ukanda wa Pwani kwani kuna rasilimali/hazina kubwa;

(ii) Udhibiti wa utoroshaji samaki nje ya nchi unahitajika sana, Kamati inashauri Serikali ichukue hatua za makusudi kuviwezesha vyombo vyake vya ulinzi na usalama kudhibiti uvuvi haramu kwenye ukanda wa *EEZ* na maziwa.

(iii) Kamati inashauri wananchi waishio Ukanda wa Pwani wasaidiwe kupitia mradi wa *MACEMP* na pia wadau wote waelimishwe na kushirikishwa katika kusimamia vizuri mradi huo ili uwafikie walengwa. Aidha, kupitia Mradi huo unaojumuisha Wilaya zote za Ukanda wa Pwani katika Bahari ya Hindi, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, Kamati inashauri Waheshimiwa Wabunge wajulishwe kwa kupata taarifa za matumizi ya fedha hizo;

(iv) Kamati inashauri Serikali ifufue Shirika la Uvuvi la Tanzania *(TAFICO)* pamoja na mitambo yake ili kiwe Kituo cha Kupakia na Kupakua Samaki kwa Meli zote zinazovua Ukanda wa Pwani, hii itasaida kujua kiasi cha samaki kinachovuliwa katika Ukanda huo;

(v) Kamati inashauri Serikali ikiwezeshe Chuo cha Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)* kwa kufanya yafuatayo :-

(a) Kufungua Kituo Dar es Salaam kitakachoshughulikia utafiti wa maji chumvi na ufugaji wa samaki katika maji hayo;

(b) Kukiwezesha kufanya utafiti wa samaki, mbegu bora, chakula cha samaki na kupambana na magonjwa ya samaki kwenye mabwawa;

(c) Kukipatia Boti itakayowezesha kufanya utafiti baharini;

(d) Kukiwezesha kufanya tathmini ya wingi wa samaki katika mabwawa, mito, maziwa na bahari (*Fish Stock Assesment)* badala ya kazi hiyo kufanywa na wafadhili wa nje ya nchi;

(vi) Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara kufanya utafiti wa Ziwa Rukwa kwani limekuwa likikauka kabisa na kujaa maji baada ya miaka kadhaa. Aidha, ziwa hili limekuwa na mamba waharibifu ambao wanaua watu na kuathiri kuongezeka kwa samaki. Kamati inashauri mamba hao wavunwe ili wasiendelee kuleta maafa zaidi kwa wananchi na samaki kwa ujumla;

(vii) Kamati inaona umuhimu wa kufufuliwa kwa vituo vya ufugaji samaki vya kanda. Aidha, inashauri ufugaji wa mbegu bora za samaki mfano "Cyprinus Carpio" uhimizwe;

(viii) Kamati inashauri Serikali kama ilivyotoa ushuru kwa zana za kilimo, basi itoe ushuru kwa zana za uvuvi, kwa mfano mashine za boti, kamba za plastiki, nyavu *(nylon fabrics)*, nyuzi, maboya, mishipi na ndoano. Hii ni kulingana na taarifa za kodi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo nchi kama Kenya na Uganda kodi hutozwa kwa asilimia 0 (0%), wakati Tanzania bado Kodi inatozwa kwa asilimia kumi (10%);

(ix) Kutokana na migogoro ya wavuvi inayoendelea, Kamati inashauri Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi (Serikali) ifanye vikao vya pamoja kwa kuwashirikisha wavuvi wadogowadogo na wawakilishi wao ili kutatua migogoro inayoendelea. Aidha, Kamati inashauri Serikali iangalie kwa makini dhana nzima ya vifaa vya uvuvi na uharamu wake kwani kila uvuvi unategemea aina fulani ya zana/nyavu. Ufumbuzi wa haraka unatakiwa kwani wananchi ambao maisha yao yote yanategemea uvuvi wanaathirika sana;

(x) Ili kudhibiti uvuvi haramu, Kamati inaiunga mkono Serikali katika kudhibiti uvuvi huo kwa kupiga vita matumizi ya uvuvi kwa kutumia mitungi ya gesi, uvuvi wa kutumia baruti, kokoro, kutumia sumu na kupiga samaki kwa kutumia bunduki za baharini (Mikuki) na pia kusaidia kupata zana za uvuvi zinazokubalika;

(xi) Kamati inashauri Serikali iendelee kuhamasisha Kilimo cha Mwani kwa lengo la kuongeza tija na mapato bora kwa wakulima wa zao hilo. Aidha, Serikali ijenge au ihamasishe ujenzi wa kiwanda/chombo kwa ajili ya kusindika mwani ili kuboresha na kulipa thamani zao la mwani nchini;

(xii) Kamati inashauri wananchi waelimishwe kulinda na kuhifadhi mazalio ya samaki katika maziwa na bahari;

(xiii) Kutokana na wazawa kushindwa kufaidika na uvuvi katika bahari kuu, Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Wawekezaji wazawa wawezeshwe.

(b) Wazawa watafutiwe wabia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka 2008/2009. Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2008/2009 ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi yameandaliwa kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yanayotarajiwa kufikiwa katika utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi – Fungu 99 jumla ya Shilingi 41,872,573,000. Kati ya hizo Shilingi 21,500,066,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 20,372,507,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, kati ya fedha za

maendeleo, Shilingi 7,723,810,000 ni fedha za ndani na Shilingi 12,648,697,000 ni fedha za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Baada ya maelezo hayo napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ambao maoni, ushauri na mapendekezo yao katika Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi yamewezesha Taarifa hii kuwasilishwa mbele ya Bunge lako tukufu. Wajumbe hao ni:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa, Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Teddy L. Kasella, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Fred T. Mpendazoe, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Juma S. Omary, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mheshimiwa Salum K. Salum, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah na Mheshimiwa Kaika S. Telele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kumshukuru Mheshimiwa John P. Magufuli (Mb), Waziri wa Maendeelo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. James M. Wanyancha (Mb), Naibu Waziri kwa ushirikiano mkubwa walioupatia Kamati. Nampongeza pia Katibu Mkuu wa Wizara Dkt.Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Jonas N. Melewas pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa kazi nzuri na ushirikiano wakati wote wa mchakato wa bajeti yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na Ofisi ya Bunge hasa Kaimu Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Frank K. Mbumi na Pamela E. Pallangyo kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati, pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za Maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na kwa niaba ya Kamati, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenye kupaswa kushukuriwa ambaye ni Rahimu, Mwenye nguvu, mwenye ukarimu na mwingi wa hekima ambaye ametupa uhai na afya njema siku ya leo tukaweza kukutana kutekeleza wajibu wetu tuliokabidhiwa na wananchi kwa manufaa yao na kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2008/2009, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99 (7) toleo la 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchache wa fadhila kama sikuchukuwa nafasi hii kukishukuru Chama changu cha *CUF* kwa kuniteuwa na hatimaye kuchaguliwa kuwa Mbunge. Nakishukuru sana Chama changu kwa hatua hiyo. Aidha, napenda kuwapongeza wananchi wa Jimbo langu la Wete, kwa kuendelea kuniunga mkono katika kutekeleza wajibu wangu. Nawaahidi kwa uwezo atakaonipa Mwenyezi Mungu, nitawatumikia vyema na kwa juhudi zangu zote na sitowaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa unaonipelekea kuzifanya kazi zangu kwa wepesi na kwa ufanisi zaidi. Bila ya kuwasahau Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu kwa uswahiba na urafiki tulionao unaonifanya kujiona ni miongoni mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukuwa fursa hii kuwashukuru viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani kwa kutuongoza, kutuelekeza na kutusimamia vyema katika shughuli zetu za kila siku. Ufanisi mkubwa unaoonekana katika Kambi yetu, ni kutokana na uongozi wao makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa ujumla kwa hotuba yao nzuri ambayo wamewasilisha leo katika Bunge lako Tukufu. Aidha, nikiri kwamba Wizara hii ni nyeti na muhimu sana katika kukuza uchumi wa mtu mmoja na Taifa kwa ujumla. Kwa kuwa muda nilionao hautoshi kuzamia kwa undani na kwa umahiri mkubwa, nitaelekeza mchango wangu katika maeneo machache yanayohitaji ushauri na ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe basi kusema kwamba natambua juhudi za Wizara hii na hasa kitendo chao cha kukubali na kupokea ushauri wetu, lakini kubwa zaidi na kuufanyia kazi. Kwa hilo, nawashukuru, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba naweza kuharibu mizania ya matumizi ya ofisi yako ya Bunge, sina budi nami kuomba maji angalau nipate kusuza koo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali Halisi ya Mifugo Nchini. Mwaka 2007 shughuli za kiuchumi za mifugo ziliathiriwa na ugojwa wa homa ya bonde la ufa. Hata hivyo, idadi ya mifugo iliongezeka kiasi, ng'ombe walifikia 19.1 milioni ikilinganishwa na 18.5 milioni mwaka 2006, mbuzi walikuwa 13.6 milioni ikilinganishwa na 13.5 milioni mwaka 2006, kondoo 3.6 milioni ikilinganishwa na 3.5 milioni mwaka 2006. Jumla ya idadi ya kuku ilikuwa 30 milioni ambao ni sawa na mwaka 2006, hii inaonyesha kuwa kwa kipindi cha mwaka mzima kuku hawakuongezeka na wala hawakupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa uliathiri uzalishaji wa nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku. Kupungua kwa asilimia 9.3 toka tani 388,294 mwaka 2006 hadi tani 370,566 mwaka 2007 hali hii ilisababisha ulaji wa nyama kupungua kwa wastani wa kilo 11.5 kwa mwaka hadi kilo 10.5 kwa mwaka. Kambi ya Upinzani, inataka kujua Serikali imechukua hatua gani madhubuti ili kukabiliana na maambukizo ya magonjwa ya wanyama kama vile Homa ya Bonde la Ufa, mafua ya ndege na kadhalika ili kutoathiri sekta hii muhimu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takriban asilimia 99% ya mifugo hapa nchini inamilikiwa na kutunzwa kienyeji. Kwa bahati mbaya, mifugo yetu ya asili uzalishaji wao ni mdogo. Kiwango cha kuzaa *(calving rate)* ni chini ya asilimia 40%; muda wa mzao *(calving interval)* ni miezi 18 – 24 na hivyo kuzaa ndama 4 – 5 katika uhai wao. Vifo vya ndama ni zaidi ya asilimia 25%. Aidha uzalishaji wa maziwa uko chini ya lita 500 kwa mwaka. Matokeo haya yote yamesababisha ukuaji wa *National herd* kubaki katika kiwango cha asilimia 0.02%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na rasilimali kubwa ya mifugo tuliyonayo, takriban zaidi ya asilimia 63% ya wafugaji wetu bado ni masikini. Hii ni changamoto kubwa, inatupasa tukae na kutafakari nini la kufanya kuondokana na hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2006/07, ukuaji wa Sekta ya Mifugo, ulishuka kwa asilimia 1.2 kutoka 5.2% hadi kufikia 4.0%.Kushuka huku kwa asilimia 1.2, si jambo dogo, athari zake katika Sekta kuu ya Kilimo na uchumi wa nchi kwa ujumla ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wanakabiliwa na tatizo la kuyafikia masoko na kukosekana taarifa za masoko *(limited access to market outlets and market information)*. Kwa kawaida wafugaji nchini mwetu huwa hawazalishi kwa sababu ya kibiashara. Mara nyingi huzalisha kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, hutafuta soko pale tu wanapokuwa na ziada. Wanapokosa kuuza hiyo ziada huwa ni sababu ya kupunguza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa muda mrefu haijawekeza ipasavyo katika kukuza masoko, kadhalika upatikanaji wa taarifa za masoko ya mifugo na mazao yake. Hali hii inaathiri kwa kiasi kikubwa juhudi ya kuongeza uzalishaji. Ipo haja basi kwa Serikali kuongeza juhudi za makusudi kuwashajiisha wafugaji kuzalisha zaidi ili kuuza katika masoko. Juhudi hizo zinaweza kuzaa matunda iwapo tu utunzaji wa mifugo, kukuza masoko, upatikanaji wa taarifa za masoko na usindikaji wa mazao ya mifugo utaendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwezeshaji kwa wafugaji wadogo wadogo, halijapewa kipaumbele cha kutosha kwani hakuna mkakati wa kuhakikisha kuwa wafugaji hawa wanapewa mikopo, mafunzo ya kutosha, wanatafutiwa masoko,

miundombinu na nyenzo nyinginezo ili kuweza kuboresha mifugo yao kwa minajili ya kuongeza kipato na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine kwenye sekta hii muhimu ni uwezo na utaalamu wa watendaji wa idara husika katika kuratibu na kusimamia sekta hii ndogo katika maeneo ya vijijini hususani ukosefu wa vitendea kazi, utafiti, uchache wa watumishi na malipo madogo kwa watumishi wetu. Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri kutueleza Wizara ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa watumishi hawa wanapatiwa nyenzo na vitendea kazi ili kuweza kuboresha sekta hii kwa manufaa ya Watanzania masikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo ambalo limekuwa likifukuta hapa nchini katika maeneo mbalimbali, nalo ni migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Tatizo hili linakuzwa zaidi na usimamizi mbovu kwenye sekta ya ardhi na ukosefu wa mikakati ya kujenga mahusiano mazuri baina ya wakulima na wafugaji. Kwa mfano, upo uwezekano wa kuzuka migogoro baina ya wakulima na wafugaji katika Mkoa wa Pwani na hata maeneo mengine kutokana na uhaba wa ardhi ambao unatokana na kwamba hivi sasa ardhi inatengwa kwa wawekezaji wa kilimo cha mazao ya miwa na mibono pasipo kuzigatia sheria na mahitaji ya ardhi kwa wakulima na wafungaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kwamba kiasi kikubwa cha ardhi kimegawiwa kwa makampuni makubwa ya nje hasa katika Wilaya za Rufiji, Kisarawe na Bagamoyo. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inaandaa sera na mikakati kabambe ya kulinda haki za ardhi za wafugaji wadogo dhidi ya udanganyifu wa wawekezaji wakubwa katika kilimo hasa kilimo cha mazao ya nishati. Vile vile Kambi ya Upinzani, inaishauri Serikali kurekebisha Sheria za Ardhi ili uamuzi wa kugawa na kusimamia rasilimali za ardhi uwekwe mikononi mwa wananchi kupitia vyombo vyao vya uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaamini kwamba rushwa na ufisadi katika sekta ya ardhi na hususan migogoro isiyoisha baina ya wakulima na wafugaji vinasababishwa zaidi na udhaifu wa Sheria za Ardhi ambazo zinatoa mamlaka makubwa kwa watendaji wa Serikali kusimamia ardhi pasipo na udhibiti wa kutosha kutoka kwenye vyombo vya uwakilishi wa wananchi. Vile vile Serikali inashauriwa kuchukua hatua mara moja pindi viashiria vya migogoro vinapoanza kuonekana ili kuweza kunusuru yasije yakatokea machafuko baina ya wakulima na wafugaji na kusababisha umwagaji damu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usindikaji wa Mazao ya Mifugo. Usindikaji wa mazao ya mifugo hasa maziwa na nyama unaongeza thamani ya mazao hayo na hivyo mahitaji kwa mlaji huongezeka na hatimaye kupanua uzalishaji. Kwa bahati mbaya, hapa nchini, viwanda vingi vya kusindika maziwa vilivyokuwa vinaendeshwa na Serikali vimekufa. Hali hii ilitokana na utaratibu mbaya ulokuwepo kwamba Serikali ndiyo pekee iliyokuwa inasimamia na kuendesha viwanda vya maziwa nchini. Kwa upande mwingine, viwanda vya kusindika nyama navyo ni vichache, hali inayopelekea kukwaza biashara ya nyama na bidhaa zitokanazo na nyama nje na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu zilizopo kwenye Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2007, jedwali namba 60 linalohusiana na idadi ya watu walioajiriwa kwenye sekta ya viwanda, utaona kuwa takwimu zinazoonyesha idadi ya watu walioajiriwa kwenye viwanda vya kusindika ngozi pamoja na bidhaa za ngozi. Takwimu hizo zinatia mashaka makubwa sana. Mathalani kwa mwaka 2003 walikuwepo waajiriwa 68, mwaka 2004 walikuwepo 20, mwaka 2005 walikuwepo 20, mwaka 2006 walikuwepo 20 na hali kadhalika mwaka 2007 walikuwepo waajiriwa 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizi inaonyesha kabisa kuwa Tanzania hainufaiki na ngozi ambazo zinapatikana nchini na viwanda vya kusindika ngozi vilivyopo havitoi ajira ya kutosha kwa Watanzania. Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri kuelezea Watanzania nini maana ya takwimu hizi kama kwa miaka minne mfululizo viwanda vinavyosindika ngozi nchini vimeajiri watu 20 tu. Hii haileti maana kwa nchi ambayo ina jumla ya ng’ombe milioni 19.1, mbuzi milioni 13.6 na kondoo milioni 3.5. Tujiulize, hivi ngozi za wanyama hawa huwa zinaenda wapi? Ama tunawafuga ng’ombe, mbuzi na mondoo ambao hawana ngozi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa hiyo hiyo ya hali ya uchumi wa Taifa ukiangalia viwanda vinavyohusika na utengenezaji wa viatu idadi ya watu ambao wameajiriwa kwenye viwanda hivyo waliongezeka kama ifuatavyo, mwaka 2003 walikuwa waajiriwa 851, mwaka 2004, walikuwa 1,130, mwaka 2005 walikuwa 1,146, mwaka 2006 walikuwa 1,157 na mwaka 2007 walikuwa 1,169. Kwa takwimu hizi, ni dhahiri kuwa ngozi zilikuwa zinatumika kwa wingi kwa ajili ya utengenezaji wa viatu hivyo na ndio maana sekta hii imekuwa ikitoa ajira ambazo zimekuwa zikiongezeka kila mwaka. Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri aweze kutupatia majibu kuwa je, ngozi hizi ambazo zimekuwa zikitengeneza viatu kwenye viwanda vyetu zimekuwa zikiagizwa kutoka nje ya nchi au hali ikoje huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo na mazingira. Tatizo la upatikanaji wa maji na malisho, limekuwa kwa kiasi kikubwa linaathiri mwenendo mzima wa ufugaji hapa nchini. Kutokana na hali hii, wafugaji wanalazimika kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine kufuata maji na malisho pale yanapopatikana. Kadhalika sehemu kubwa ya nyanda zilizokuwa zinatumika kwa kuchungia mifugo zimekuwa zinavamiwa na kutumika kwa matumizi mengine kama sehemu za Kilimo, hifadhi za wanyamapori, machimbo ya madini na kadhalika. Katika hali kama hii, wafugaji hulazimika kuhama kutafuta maeneo mengine ya kulisha mifugo yao. Kutokana na kuhama hama huko kwa wafugaji na kwa sababu hakuna utaratibu maalum ulioandaliwa katika uhamaji huo ndiko wakati mwingine kunakopelekea mazingira kuharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaona kwamba njia mahususi ya kupunguza ufugaji wa kuhamahama, ni kuongeza maeneo yanayotumika kwa malisho; Wafugaji wapatiwe ardhi ya kutosha na kupewa hati ya kumiliki maeneo hayo; kujenga mabwawa na malambo yanayoweza kuhifadhi kiasi kikubwa cha maji. Aidha, majosho ya kutosha yajengwe na yale yaliyoharibika yafanyiwe ukarabati wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la wafugaji waliohamishwa kwenye bonde la Ihefu, Mbarali Mkoani Mbeya. Unyanyasaji mkubwa wa Wafugaji uliotokea Ihefu mwezi March, 2006, kwa kuwaondoa bila utaratibu wala mipango mathubuti. Vitendo walivyofanyiwa wafugaji ambavyo ni kinyume na haki za binadamu bado vimeacha makovu mengi. Wananchi wengi waliopoteza mali zao, mifugo, familia kusambaratika na kuumia kisaikolojia. Tume ya Rais, iliyotumia mamilioni ya fedha za Watanzania iliyoongozwa na Mheshimiwa Jaji Chande hadi leo taarifa yake imewekwa kabatini Watanzania hawakujulishwa kilichojiri katika ripoti hiyo na wala hatua zilizochukuliwa kwa watendaji waliotekeleza vibaya agizo la Serikali. Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe Tamko la Serikali kuhusu Taarifa ya Tume/Kamati ya Rais iliyochunguza matukio ya Ihefu ili Watanzania na hasa Wafugaji waamini kuwa Serikali yao inawajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi ya uvuvi nchini. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za uvuvi katika mwaka 2007, kilikuwa ni asilimia 4.5 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2006. Sababu kuu za kushuka kwa ukuaji wa shughuli za uvuvi kulitokana hasa na kuendelea kwa vitendo vya uvuvi haramu, kupungua kwa mahitaji ya samaki na mazao ya samaki nje ya nchi. Uharibifu wa mazingira katika mazalia ya samaki na matumizi ya zana duni za uvuvi. Mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 1.6 mwaka 2007 kama ilivyokuwa katika miaka ya 2005 na 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007, idadi ya wavuvi waliosajiliwa nchini iliongezeka na kufikia 163,037 ikilinganishwa na 156,544 mwaka 2006. Wavuvi hao walivuna samaki wenye uzito wa tani 327,807.5 wakiwa na thamani ya shilingi 292.7 bilioni mwaka 2007 ikilinganishwa na tani 341,109.2 zenye dhamani ya shilingi 285.7 bilioni mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007 mapato yatokanayo na mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi yalikuwa shilingi 7,589 milioni ikilinganishwa na shilingi 6,236 milioni mwaka 2006. Kati ya mapato hayo mauzo ya Sangara nje yaliingizia nchi mapato ya shilingi 6,660 milioni mwaka 2007, ikilinganishwa na shilingi 5,491 milioni mwaka 2006;

Mheshimiwa Spika, ukiangalia takwimu hizi utaona ya kuwa Sangara ambao wanatoka Ziwa Victoria na Tanganyika ndio pekee ambao wanaongoza kwa mauzo kwa zaidi ya asilimia 87.8%, Kambi ya Upinzani, inataka majibu kutoka Serikalini ni kwa nini samaki ambao wanapatikana na/au kuvuliwa Bahari ya Hindi wanachangia kiasi kidogo sana cha mauzo nje ya nchi, ilhali meli nyingi za uvuvi zinaendelea kuvua na kupata vibali kila wanapohitaji ila uvuvi huo hauonekani ukileta faida ya kutosha kwenye mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jinsi ambavyo Sangara wamekuwa wakiliingizia Taifa fedha nyingi kama ilivyoonekana kwa kipindi cha mwaka jana 2007 kuna kila sababu ya kuhakikisha kuwa panakuwepo mkakati kabambe wa kuvuna Sangara ambao wanapatikana ziwa Tanganyika. kwa kuwa mpaka sasa uvunaji wa

sangara waliopo ziwa Tanganyika hawavuliwi kwa wingi pamoja na ukweli kuwa sangara hao ndio chimbuko la sangara waliopo ziwa Victoria. Kuvuliwa kwa sangara waliopo ziwa Tanganyika itaongeza ukuaji wa mauzo ya sangara nje na kuongeza ukuaji wa Pato la Taifa na wakati huo huo kipato cha wananchi wa Mkoa wa Kigoma kitaongezeka mara dufu kutokana na kupanuka kwa shughuli za kiuchumi. Kadhalika sekta ya viwanda itaweza kukua kutokana na ujenzi wa viwanda vya samaki kwenye Mkoa huo. Aidha hatua hii itapelekea kuimarishwa kwa uwanja wa ndege wa Kigoma ili kuruhusu ndege kubwa za mizigo kuweza kutua na kuruka kwa ajili ya biashara ya minofu ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema kwenye hotuba yetu ya Bajeti Mbadala kuhusiana na vyanzo vya mapato kutokana na Uvuvi wa Bahari Kuu, naomba kusisitiza tena yale ambayo yalisemwa na kuitaka Wizara husika itilie maanani hoja zetu hizi ili kuweza kuongeza mapato ya Serikali na kukuza uchumi wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, uvuvi katika Bahari Kuu ni moja ya maeneo ambayo kama Serikali ingekuwa makini na kuchukua maamuzi ambayo Kambi ya Upinzani ilipendekeza, mapato yatokanayo na uvuvi yaliongezeka marudufu kutokana na kusimamia vyema shughuli za uvuvi. Maeneo yenyewe ni kama haya yafuatayo:-

(i) Kuongeza ada ya leseni kwa meli za nje zinazovua katika bahari kuu hadi kufikia USD 50, 000, kutoka inayotozwa sasa ambayo ni *USD18*, 000 kwa mwaka. Kulingana na takwimu zilizopo ni kuwa kuna meli 140 za nje zilizopatiwa leseni za uvuvi katika bahari kuu ya Tanzania. Kwa maoni haya mapato yangelifikia Tshs 9.5bn. ambayo Serikali ingelikusanya;

(ii) Kuongeza tozo la mrahaba wa mauzo la asilimia 10 katika bidhaa za Samaki zinazovuliwa katika Bahari Kuu. Kila meli kwa mwezi inavua wastani wa tani 2000 za samaki, kwa makisio ya chini sana. Bei ya soko kwa kilo ya samaki ni USD2.5. Kwa tozo hilo Mapato yangelifikia shs**.** 370 bn. ambayo Serikali ingelikusanya;

(iii) Katika kuhakikisha kuwa Sekta Uvuvi inaleta mabadiliko ya kiuchumi kwa nchi na wananchi kwa ujumla, inashauriwa bandari za Mtwara, Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar zitenge maeneo ya bandari za samaki *(Fish Ports and Fish Processing plants),* ili meli zote za uvuvi wa bahari kuu zilazimike kununua mahitaji yao yote ya mafuta, maji, chumvi na vyakula wanapo kuja kukaguliwa kwa ajili ya kukusanya mapato. Kwa uamuzi huu mapato yanakisiwa kuwa Tshs.3bn ambayo Serikali ingekusanya. *(Makofi)*

(iv) Uvuvi katika ziwa Victoria na ziwa Tanganyika, haujadhibitiwa vizuri. Hivi sasa kuna uvunaji haramu wa samaki wastani wa Tani 36,000 kwa mwaka. Kama uvunaji huu haramu ukidhibitiwa Serikali inaweza kujipatia kiasi cha shilingi 45 bn kwa mwaka. Kutokana na uvunaji huu haramu katika maziwa hayo kunasababisha viwanda vyetu kukosa mali ghafi ya kutosha kuzalisha minofu. Tunaitaka Serikali kuchukua hatua za dharura kuikabili hali hii kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na *TRA* ili kuongeza mapato na ajira. Zoezi hili litaongeza wingi wa samaki hivyo basi viwanda vya samaki vitaongeza uzalishaji na hatimae kodi itaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni haya Kambi ya Upinzani sio tu yamepanua wigo wa kodi, lakini pia kwa hatua hizo tutakuwa tumedhibiti uvunaji endelevu wa raslimali zetu ambapo sasa hazivunwi kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Hali Halisi ya Wavuvi Wadogo Wadogo. Hali ya wavuvi wadogowadogo hapa nchini kwetu ni ya kusikitisha sana kwani hakuna juhudi zozote za kina zinazochukuliwa na serikali kuhakikisha kuwa wavuvi hawa wanasaidiwa kupata mitaji ya kuweza kujiendeleza na kupata nyezo na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kukuza shughuli za uvuvi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa kina utaona kuwa badala ya Serikali kuwawezesha wavuvi hawa wadogo wadogo wanachofanya ni kuwawekea vikwazo vinavyopelekea washindwe kufanya kazi zao kwa ufanisi. Pia yapo malalamiko mengi kutoka kwenye jamii za wavuvi wadogowadogo kuhusu vitendo vya unyanyasaji wanavyofanyiwa na baadhi ya Maafisa wa Idara ya Uvuvi kwa visingizio vya kuthibiti uvuvi haramu. Kambi ya Upinzani, inaishauri Serikali kuimarisha mikakati yake ya kudhibiti uvuvi haramu na kufanya hivyo kwa mujibu wa kanuni za utawala bora na haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli kuwa wavuvi wadogo wadogo huchangia kwa kiasi kikubwa sana kwenye mapato ya Serikali lakini bado wananyanyasika sana. Mfano halisi ni barua iliyoandikwa na Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi Makao Makuu yenye kumbukumbu namba KA/594/01/87 ya tarehe 13 Mei 2008 inayowaagiza Wakurugenzi Halmashauri zote Tanzania Bara na ninapenda ninukuu waraka huo:-

*"Waraka huu unawapa uwezo maafisa walio chini yenu na vyombo vya dola kuthibiti na kuhakikisha kuwa matumizi ya nyavu za aina ya mtando na ringnet, juya au juya la kojani au kokoro na uvuvi wa kuzamia kwa kutumia mitungi ya gesi aina ya oxygen, viatu vya kuogelea na au miwani ya kiupiga mbizi yanapigwa marufuku kuanzia sasa".* Mwisho wa kunukuu!

Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri alieleze Bunge hili na wananchi wote kwa ujumla ni jinsi gani vifaa hivyo vinahusika na kuharibu mazingira. Kadhalika tunamtaka Waziri achukue hatua ya kuifuta barua hiyo ya Mkurugenzi wake kwani kwa kiasi kikubwa itaathiri kipato chao kutokana na shughuli zao za uvuvi. Aidha, hatua hiyo itapunguza mapato ya Halmashauri za Wilaya ambazo shughuli za uvuvi zinafanyika kutokana na kukosa ama kupungua kwa mapato yatokanayo na shughuli za uvuvi, kwani wavuvi hawa wamekuwa wakilipa mpaka zaidi ya shilingi 100,000 kwa siku kama ushuru wa mauzo ambapo wanakatwa asilimia 5 ya mauzo ya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inataka maelezo ya kina kutoka Serikalini, ni kwa nini Serikali inawawekea vikwazo wavuvi wadogowadogo na huku ikiwapa uhuru mkubwa wavuvi wa bahari kuu wenye meli kubwa na ambao hawalinufaishi taifa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama wa wavuvi wetu wawapo kwenye shughuli zao, ni mdogo sana kwani zimekuwa zikitolewa taarifa mara kwa mara kuwa kuna wavamizi wanawavamia na kuwanyang'anya vifaa vyao na hata wakati mwingine wavuvi hawa hupoteza maisha yao. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa panakuwepo mpango maalumu na shirikishi wa kuhakikisha kuwa ulinzi unaimarishwa na haswa katika maeneo yale ambayo vitendo hivi vya kiharamia vimekuwa vikitokea mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa tunayalinda maisha ya Watanzania wenzetu wawapo kwenye shughuli zao za kujitafutia riziki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imesikitishwa na kustushwa sana na taarifa iliyopo kwenye randama ya mpango na bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2008/2009 (kifungu 1003 Sera na Mipango) iliyowasilishwa kwenye kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge kuwa miongoni mwa kazi za kipindi hiki cha bajeti ya mwaka 2008/2009, ninapenda kunukuu:-

*“Kupitia Sera ya Taifa ya Uvuvi (1997) na kuandaa mkakati wa kutekeleza sera hiyo”.* Mwisho wa kunukuu.

Hivi tujiulize kwa kipindi chote cha zaidi ya miaka kumi inawezekana vipi Serikali haikuwa na mkakati wa kuitekeleza Sera ya Uvuvi? Sasa huu si uzembe na kuna kila sababu ya wahusika waliofanya uzembe huo wachukuliwe hatua mara moja kwani wanarudisha nyuma juhudi za kukuza uchumi wa Taifa letu hili, tunamtaka Waziri atupe majibu ya kina juu ya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inahoji hivi ni kweli kwa zaidi ya miaka 10, Sera hiyo haijawahi kutekelezwa? Ama walikuwa wanafanya kazi kwa kutumia muongozo gani kama hakuna mkakati wa kutekeleza sera ambayo ndio muongozo na dira ya utekelezaji wa shughuli za Uvuvi hapa nchini? Kama sera inasema kuwa, nanukuu:-

*“The overall goal of the National Fisheries Policy is to promote conservation, development and sustainable management of the fisheries resources for the benefit of present and future generations”***,** Mwisho wa kunukuu.

Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri kulieleza Bunge na wananchi je, lengo hili limeweza kufikiwa kwa kiasi gani kama hakukuwa na mkakati wa kutekeleza sera husika? Ni vigezo gani vinatumika kupima utekelezaji wa sera hii kama mkakati haukuwepo tangu miaka kumi iliyopita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Nichukue nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa wake zangu, Bi. Asha Mohammed Haji na Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, watoto wetu na familia yangu kwa ujumla kwa kunipa moyo na kuniunga mkono kwa muda wote, nikifanya shughuli zangu za kuwakilisha wananchi katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kuwa, Waziri ataweza kutupatia majibu ya kina juu ya mambo yote ambayo Kambi ya Upinzani imeyauliza au kutaka ufafanuzi juu ya mambo kadhaa kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Jecha kwa uwasilishaji wako. Sasa kabla hatujaendelea na uchangiaji ambapo mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa

Mheshimiwa Lucas Selelii, naomba Mheshimiwa Mwenyekiti Pacha, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, aje anipokee Kiti.

*Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mchangiaji wetu wa mwanzo asubuhi hii atakuwa Mheshimiwa Lucas Selelii, atafuatiwa na Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro ajiandae.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya awali kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nitoe salamu za rambirambi kwa msiba mkubwa ambao tumeupata sisi Wabunge. Mwenyezi Mungu alitoa, Mwenyezi Mungu ametwaa, Jina la Mungu libarikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi wangu wa pili, naomba kuwashukuru Watanzania wote wanaitakia heri na kuiombea nchi yetu mema. Naomba waendelee kuiombea nchi yetu na kuitakia heri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba wote wenye mapenzi mema na nchi hii, wasiogope kusema. Waseme, wasiogope kukamatwa, wasiogope kushitakiwa na hata wasiogope kufa kwa sababu msemakweli ni mpenzi wa Mungu. Kwa hiyo, jipeni moyo, yasemeni maovu yote, yawe yamefanywa na viongozi wakubwa, yawe yamefanywa na viongozi wa kati au viongozi wa chini na hata na mwananchi yeyote yule, lazima tuseme, tusiogope na wala tusione aibu. Semeni kwa namna yoyote ambayo mnaweza na Mwenyezi Mungu atatubariki, atalinda nchi yetu, ikaondokana na ufisadi na maovu ambayo yako kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu katika utangulizi, sekta ya mifugo, imepata wenyewe. Naamini sekta hii ni muhimu sana katika kujenga uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na hata katika kujenga uchumi wa nchi, ni muhimu sana. Kwa hiyo, nina imani sana na safu ambayo Mheshimiwa Rais ametuteulia kuanzia Waziri, Naibu wake pamoja na Maofisa, Makatibu Wakuu wote ni watoto wa wafugaji. Kwa rekodi aliyonayo Mheshimiwa Magufuli, naamini Wizara hii itaenda na haitakuwa tena sekta ndogo, naamini baada ya mwaka mmoja/miaka miwili itakuwa ni sekta kubwa ya mifugo ambayo itainua pato la wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza kuchangia. Mifugo kwa wananchi hasa wananchi wa kule kwetu, nina imani Mikoa ile ya Kanda ya Magharibi, Mikoa ya Kanda ya Ziwa, nina imani hata kwa ndugu zetu wa Singida, Wagogo na Wamasai, mifugo ni mbadala wa Benki. Mkulima yeyote ambaye ni mkulima stadi, akishavuna, akishapata mazao yake, akilima akifanikisha mazao mengi ya kutosha, akatosheleza chakula chake na bado mazao yakabaki, hujiwekea akiba kwa mifugo kwa maana ya kununua ng’ombe, mbuzi, kondoo, kuku na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui sana wenzetu wa Mikoa ya Arusha na Manyara, lakini kwa Mikoa ya wakulima wa kawaida hawa ambao mazao yao ni ya kulima kila mwaka, kule kwetu ukilima pamba na mwaka huu utalima pamba, ukilima tumbaku na mwaka huu utalima tumbaku, ukilima mahindi na mwaka huu utalima mahindi, naamini wakipata mazao ya kutosha, huwa wanageuza mazao hayo kuwa Benki ambayo wanajiwekea kwa ajili ya matumizi ya baadaye. Kwa hiyo, katika hili, sekta hii ni muhimu sana hasa kwa wananchi wa kipato cha kawaida, kwa wananchi wakulima wa kawaida katika kuimarisha maisha yao, kuimarisha familia zao kwa kuweka akiba kwa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mifugo yao, wakulima hawa au wafugaji hawa, imekuwa inapata athari za mara kwa mara, nyingi tu ikiwemo ukame wa mara kwa mara. Kwa maana hiyo, hawapati maji ya kutosha, hawapati malisho ya kutosha, ikiwemo ukosefu wa miundombinu mfano malambo na mabwawa, magonjwa mbalimbali yanayosakama ng'ombe, mbuzi, kuku na kwa muda mrefu sana Serikali kwa kweli haijawekeza kuwasaidia wafugaji kuondokana na adha hiyo ya ufugaji wa kubahatisha, kuingia kwenye ufugaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nimeanza kumsifu Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wake, lakini sasa pokeeni changamoto hiyo. Muwaondoe wafugaji hawa, muwaondoe wakulima hawa ambao wanaweka Benki yao kwa mifugo, waweze kuwa na mbadala wa kuwa na malisho, malambo na uhakika wa kutibu mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mrefu changamoto hii imewakabili wafugaji wetu, ndio maana hata ukienda kwenye masoko, minada tunaita, kule kwenye minada, ng'ombe au mbuzi anauzwa kwa udalali kwa bei ya kusemwa, "wenye shilingi mia moja, mia mbili, mia tatu" anauzwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona hata sehemu moja anaelekeza kubadilisha minada hii ya kizamani iliyopo sasa hivi ya kuuza mifugo kwa kuangalia sura na unene wa ng'ombe kwenda kwenye uuzaji wa mizani, sijaona, labda akimaliza anieleze, ufugaji mzuri wa soko zuri, atauza ng'ombe wake kwa uhakika kama atamuuza kwa kilo, amenenepesha ng'ombe wake ama mbuzi wake aende kwenye mnada akiwa na uhakika wa kupata pesa kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sasa anaangaliwa na wachuuzi wale kwa kukisiwa na hili ni jambo hatari sana ambalo halina mwendelezo mzuri kwenye masoko hasa kwenye minada yetu. Mimi sina hakika kama kuna mnada ambao unauza kwa kilo sasa hivi ukitoa mnada wa Pugu, sina hakika katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Singida, Tabora na pengine hapa Dodoma kwenye machinjio tu ndiyo kuna minada ambayo inauza kwa kilo na Mkoa wa Mara vile vile ambako Katibu Mkuu wa Wizara hii anatoka, sina hakika kama kweli kuna minada ambayo inauza kwa kilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kuondokana na ufugaji wa kizamani tuweke minada ambayo italazimisha wanunuzi wa mifugo wanunue kwa kilo hapo tutakuwa tumemsaidia mfugaji wetu. *(Makofi)*

Jambo la pili ni lazima tuweke viwanda vingi vya nyama na viwanda vingi vya ngozi, bahati nzuri benki hii ya wananchi wetu wa kawaida, benki yetu ya wakulima ina mazao mengi sana ya kutosha, ukimchunguza ng'ombe ana mazao zaidi ya matano, ana nyama, ngozi, maziwa, samadi na kwato.

Lakini katika mazao yote hayo hatuna sehemu ambayo tumewekeza kwa ukamilifu wa kutosha kuamini kwamba ili kuongeza thamani ya mifugo hawa, tuwe na minada mizuri lakini tuwe na sehemu nzuri ya viwanda vya nyama, ngozi, ili akiuzwa yule ng'ombe kwa bei ya kilo badala yake apelekwe kwenye kiwanda ambacho kiko karibu cha nyama au cha ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana maeneo yetu yote kule Kanda ya Magharibi, ninapozungumzia Kanda ya Magharibi ni mikoa ya Tabora, Singida, Dodoma, Shinyanga, Mara, Mwanza hakuna hata kiwanda kimoja cha nyama zaidi ya hiki cha Shinyanga kinachojengwa. Kujenga kiwanda kimoja tu kwa Kanda kubwa kama ile bado hujaitendea haki Kanda kubwa kama ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuongeze viwanda vingine kwa maana ya Mwanza au Mara au Shinyanga au Singida au Tabora hapo tutakuwa tumewaTendea haki wafugaji wetu watakuwa na uhakika wa kuuza mazao yao mahali pa karibu na kwa bei ya uhakika, nasisitiza kiwanda cha Shinyanga kifunguliwe haraka lakini bado hakitoshi. Zaidi ya robo tatu ya mifugo ya Tanzania inatoka Kanda ya Magharibi na Kanda ya Ziwa, kama sijakosea nitakuwa tayari kusahihishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningewaambia siri moja Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kule kwetu mwenye mifugo anaheshima ya ziada. Unaweza ukawa mkulima mzuri sana lakini kama huna mifugo bado, ukiwa mfugaji una ziada ya heshima, kule kwetu wanamwita Nsavi na Nsavi tafsiri yake ni tajiri na tajiri tafsiri yake ni mfugaji ndiyo maana yake, kwa hiyo, kilele cha kumfikisha mkulima penyewe ni kwenda kwenye ufugaji, kwa hiyo, cha Mheshimiwa John Magufuli kilele cha kumfikisha mfugaji umtengenezee minada, umtengenezee viwanda vya ngozi na viwanda vya nyama hapo utakuwa umemfikisha kilele kizuri cha mkulima ambaye ni Nsavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo hawa na wafugaji wake wamekuwa ni watu wa kuzalilishwa mara kwa mara, lakini ajabu kwenye michango au kodi ni watu wa kwanza kushikwa, hata kwenye vita vya Idd Amin, wafugaji wetu walichangishwa ng'ombe wawili wawili wakaenda kupigana lakini mifugo bado wapo, imetokea wafugaji na mifugo yao wanadhalilishwa na kufukuzwa ovyo ovyo tu wakati Serikali hujaweka miundombinu wakaanza wenyewe wakaenda mpaka Ihefu na mahala pengine kwa ajili ya kutafuta malambo ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekwenda kule mimi kweli siwatetei kwa sababu ya kuvunja mazingira au nini lakini nasimama kwa hali ambapo kwa nini wakati wanakwenda mnaona na kwa nini mmefika mahali ambapo wamefukuzwa tena kwa kudhalilishwa ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ambayo imewakuta kule baada ya kuingia kwenye hifadhi ya Ihefu na yaliyotokea Serikali iliunda Tume. Ripoti ile ya Tume mpaka leo hii haijawasilishwa hadharani kuna nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona kuna vitu vinajificha ujue kuna mambo nimekutana na wahusika waliotoka kule Ihefu wanasema viongozi wa Serikali na viongozi wa Wizara walicheza rafu, ilifikia mahali ambapo viongozi wa Serikali na watendaji wa Wizara kwa kuwafukuza waondoke Ihefu wanaenda na wachuuzi ama walanguzi, ng'ombe alifikia hadi shilingi elfu kumi. Hebu tuone thamani ya ng'ombe, elfu kumi anauziwa mchuuzi mlanguzi kwa niaba ya kiongozi ni aibu katika nchi hii tunaojali utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako ripoti hii itoe kwenye Bunge hili na tuijadili kama kuna mtu amehusika kama kuna mtu wa Serikali alihusika kama kuna kiongozi yeyote amehusika tujadili ili watu wachukuliwe hatua, turudishe imani kwa wafugaji wetu ambao wamedhalilika kwa muda mrefu, wamehangaika kwa kipindi kirefu na bado tunawapeleka mahali ambapo wanakuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo tunaihitaji itolewe iwe ya wazi kama vile taarifa zingine zilivyotolewa. Mbona kuna taarifa nyingi sana zimetolewa baada ya kuundwa hii, hii imeundwa siku nyingi sana mwaka 2006/2007 imekuwa kimya, imetoka taarifa ya *Richmond* hapa tumesema yaliyotokea tukayasema wazi tu, imetokea taarifa ya madini tumesema na tukaijadili wazi tu kwa nini taarifa hii inafichwa? Ileteni na mimi kwa kupitia Bunge lako nitasema kutoa hoja ili Bunge lako liunde Tume tuchunguze kilichotokea ni kitu gani kwa wananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalisema kwa uchungu sana kwa sababu haiwezekani taarifa ikafichwa kwenye kabati kama ina mapendekezo ya kufanyia kazi ili jambo hili lisije likatokea kwenye maeneo mengine kwa kuwanyanyasa na kuwadhulumu wananchi ambao wanajitafutia kwa jasho lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala lingine la uvuvi, tunapozungumzia Wizara hii ya Mifugo nashukuru Rais aliitania akaaita Wizara ya Kitoweo kwa sababu inaunganisha mifugo kwa maana ya mbuzi, kuku ng'ombe, kondoo na kadhalika, lakini vile vile kwa maana ya mifugo inaunganisha suala la uvuvi wa samaki, kumbe samaki nao ni mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la samaki mimi huwa nashangaa sana kitu kimoja nadhani Mheshimiwa Waziri atanisaidia kujibu hiki kitendawili, tumezungukwa na Bahari ya Hindi, tumezungukwa na Ziwa Victoria, tumezungukwa na Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika, tumezungukwa pia na mito mingi tu siwezi kuitaja yote lakini ni mingi ya kudumu na mito ya muda, tumezungukwa na mabwawa, tumezungukwa na malambo kila pahali na kila sehemu ambapo ndiyo sehemu ya mifugo hawa samaki wanaishi, kwa sababu sehemu ya kuishi samaki ni kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajabu yake ni kwamba kwa nini bei ya samaki iko juu sana, kuliko hata kilo moja ya nyama ya ng'ombe. Ukinunua samaki na ukinunua hata kilo moja ya nyama ya ng'ombe samaki iko juu zaidi kuliko nyama ya ng'ombe. Ninajuiliza kwa nini samaki wanakuwa na bei kubwa wakati samaki hahitaji kuchungwa, hahitaji kulishwa, hahitaji malambo, hahitaji pembejeo, hahitaji josho na haihitaji chanjo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wataalamu wote katika Wizara hii kwa kufanya kazi nzuri lakini katika mazingira magumu ya ufinyu wa Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wa mtani wangu Mheshimiwa Lucas Selelii na mimi nichangie machache kuhusu sekta ya mifugo, sekta ya mifugo ni muhimu sana kwa sababu inachangia Pato la Taifa lakini kutokana na ufugaji wetu ambao si wa kisasa sekta hii inachangia kwa kiwango kidogo Pato la Taifa kwa sababu wananchi wengi au wafugaji wengi wanataka kuwa na makundi ya mifugo lakini siyo ufugaji wa kisasa na siyo ufugaji bora. Kwa hiyo, ipo haja ya kuwaelimisha wafugaji wetu kuhakikisha kwamba wanakuwa na ng'ombe wa kisasa ili waweze kuchangia Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na taasisi za mifugo, Wilaya ya Mpwapwa bahati tuna taasisi tatu za mifugo. Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ya Taifa, Chuo cha Mifugo, Kituo cha Uchunguzi wa Maradhi ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu waliojenga taasisi hizi walikuwa na malengo maalum, kwanza taasisi ya utafiti wa mifugo ni kwa ajili ya utafiti wa mifugo na mimi nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri taasisi hizi zilikuwa hazitengewi fedha za kutosha lakini katika Bajeti ya mwaka 2008/2009 napenda niipongeze Wizara angalau Bajeti iliyotengwa pamoja na kwamba haiwezi kutosheleza mahitaji yote lakini itasaidia kutekeleza majukumu katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi ya utafiti ya mifugo ya Kitaifa ina matatizo mengi, hiki siyo kituo cha utafiti sasa ni taasisi ya Kitaifa ya utafiti wa mifugo kwa hiyo, iko haja ya kuimarisha na kuipatia vitendea kazi, kuajiri watafiti wa kutosha, magari ya kutosha pamoja na matrekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Mifugo nashukuru kwa sababu chuo hiki miaka iliyopita kilikuwa chuo ambacho kilikuwa na wanafunzi wachache sana, sasa chuo

hiki wamekifufua na sasa kina wanafunzi zaidi ya 200 na mwaka huu 2008/2009 wanatarajia kupokea wanafunzi zaidi ya 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri akiimarishe Chuo hiki kwa kukipatia vitendea kazi, kuboresha na kuimarisha maabara ya chuo, kuwapatia magari pamoja na vitendea kazi vya kufundishia ili kuimarisha na kuboresha ufundishaji katika chuo hiki, kwa sababu tunahitaji wataalam wa mifugo, maafisa wa mifugo kila kijiji, maafisa mifugo ni wachache sana na wananchi wanakula nyama bila kukaguliwa. Kwa hiyo, nina hakika chuo hiki ni muhimu kwa sababu kinatoa wataalamu wengi wa mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha uchunguzi wa maradhi ya mifugo, kituo hiki nacho ni muhimu sana kwa sababu maradhi yote kama kuna magonjwa ya kuambikizwa ya mifugo basi wenzetu wanasaidia kwa ajili ya kuchunguza maradhi haya na kuweza kudhibiti kinga pamoja na tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoanza mwanzo kwamba taasisi hizi ni muhimu sana na wenzetu waliojenga taasisi hizi walikuwa na malengo maalum, Chuo cha Mifugo ni cha wanachuo ambao wanajifunza mafunzo ya *animal health* pamoja na *animal production* na wanategemea kituo cha uchunguzi wa maradhi ya mifugo kwa ajili ya *field practical* na *clinical study* zote zinafanyika pale, hivi karibuni nimepata taarifa sina uhakika sana lakini kuna wazo la Kituo cha Uchunguzi wa Maradhi ya Mifugo na kujengwa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wazo hilo lipo mimi ninalipinga kwa asilimia mia moja na hilo wazo alilolitoa ni nani, kusema kwamba kituo kipo pembezoni, ofisi zote za Serikali zipo Dar es Salaam watu wanatoka Ngara wanasafiri mpaka Dar es Salaam, leo kituo hiki ambacho kinashughulikia mikoa miwili Singida na Dodoma mnasema kiko pembezoni kiletwe Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana ni kwa nia njema lakini kwa kweli kama mtakuwa na uwezo wa kusafirisha wanafunzi kutoka Chuo cha Mifugo Mpwapwa kuwaleta *field practical* Dodoma basi fanyeni hivyo, lakini itakuwa ni gharama kubwa sana. Mimi napinga kwa sababu wenzetu waliojenga Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, Chuo cha Mifugo pamoja na Kituo cha Uchunguzi wa Maradhi ya Mifugo walikuwa na malengo maalum kwa ajili ya wanachuo wetu kujifunza pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli hapa Bungeni je, mpango huo upo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1981 Serikali iliunda mashirika mawili, Shirika la Utafiti wa Mifugo *(TARIRO)* na Shirika la Utafiti wa Mifugo *(TARO)* wafanyakazi/watumishi wote walihama kutoka Serikalini wakaingia *TARIRO* na wengine wakaingia *TARO* miaka nane mwaka 1981 mpaka mwaka 1989, watumishi hawa wanapostaafu mafao yao ya miaka nane kutoka mwaka 1981 hadi 1989 hawalipwi, hayakuunganishwa katika mafao yao ya kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo haya mafao ya miaka nane watumishi walipokuwa *TARIRO* ni nani anayewalipa na kuna sababu gani za msingi kwa nini wasilipwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine mwenzangu amezungumzia katika uboreshaji wa sekta ya mifugo, kwanza tuhakikishe mifugo inapata maji kwa hiyo, suala zima la kuchimba mabwawa ni muhimu hasa maeneo kame. Mabwawa ambayo yatasaidia mifugo pamoja na wananchi kupata huduma ya maji, kwa hiyo, ipo haja kwa Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuchimba mabwawa, Wilaya ya Mpwapwa ikiwepo, Kata ya Mima, Kata ya Berege, Kata ya Matomondo, Gode gode, Kata ya Chunyu, wote wachimbiwe mabwawa ili waweze kunywesha mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mifugo inategemea sana uboreshaji wa tiba pamoja na kinga mwaka 2007/2008 watu zaidi ya 600 waliumwa na mbwa katika Wilaya ya Mpwapwa na bahati mbaya sana Mheshimiwa Naibu Waziri ulipotembelea taasisi ya utafiti wa mifugo, chuo cha mifugo na kituo cha uchunguzi wa maradhi ya mifugo tulipata taarifa kwamba kulikuwa na upungufu wa *vaccines* za *rabbies*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tuwe na dawa ya chanjo kwa ajili ya kupambana na maradhi haya, ugonjwa wa kichaa cha mbwa ni ugonjwa hatari sana na ni tatizo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mazao ya mifugo, nakubaliana kabisa na Serikali kwamba mifugo inatusaidia mambo mengi, nyama, maziwa, ngozi, kama nilivyosema mwanzo mifugo inachangia Pato la Taifa, lakini suala la unywaji maziwa kwa kweli iko haja ya kuwaelimisha wananchi kwamba maziwa ni muhimu sana na yana *protein* na yanajenga mwili kwa hiyo, ni vizuri maziwa haya yatumike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa ajili ya machinjio ya kisasa hapa tumejengewa machinjio ya kisasa lakini ni vizuri tusijenge Dodoma tu hata katika Wilaya zetu Serikali itenge fedha kwa ajili ya kujenga machinjio ya kisasa, watu wanachinja tu bila ng’ombe kukaguliwa, watu wanakula nyama tu na wengine wanakula mizoga kama mwaka jana tulikuwa na tatizo la homa ya bonde la ufa lakini tunashukuru sana Serikali imejitahidi kudhibiti hali hiyo. Hali ya kudhibiti ugonjwa kama huo wa homa ya bonde la ufa si la Serikali peke yake na si la viongozi, ni la wananchi wote kuhakikisha kwamba hawali mizoga ili kupambana na magonjwa kama haya ya bonde la ufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la udhibiti wa magonjwa ya mifugo kwa mfano magonjwa ya kupe, kuzuia magonjwa ya kupe ni kuogesha mifugo lakini ni aibu kubwa sana mifugo inakufa kwa sababu hawakuogeshwa, tuhakikishe kwamba majosho yote yanafufuliwa tunapata dawa za kutosha ili mifugo iweze kuogeshwa na kupambana na magonjwa haya ya kupe. Gharama za dawa, kinga na tiba ni gharama kubwa sana kwa hiyo, Serikali ifikirie kupunguza gharama za dawa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri ameshatembelea vituo vitatu,

namkaribisha mtani wangu Mheshimiwa John Magufuli atembelee taasisi hizo tatu ili aweze kupata maelezo na matatizo atajionea mwenyewe badala ya kusoma kwenye makaratasi. Kwa sababu unaposoma taarifa kwenye makaratasi na kuona mwenyewe kama Naibu Waziri alipofika Mpwapwa alipewa taarifa nzuri sana kwa hiyo, anaelewa ninapozungumza hapa taasisi tatu za Mpwapwa anaelewa kuliko kusoma kwenye makaratasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache nakushukuru tena na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kwanza uniruhusu nitoe rambirambi na pole kwa Bunge lako Tukufu kwa familia ya Marehemu Chacha Wangwe na kwa wananchi wa Tarime kwa msiba huo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia uniruhusu nimpongeze Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na waandamizi wengine katika Wizara kwa kazi nzuri kubwa waliyoifanya kwa sababu hotuba yake ya Bajeti imetupa sura kamili juu ya suala na hali ya mifugo na uvuvi nchini lakini pia tumepata picha juu ya mwelekeo wa Wizara kwa kipindi kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo na uvuvi kwa kweli ni vitu vinavyochangia sana katika uchumi wetu wa Taifa na katika maisha ya Watanzania wengi kwa ujumla, nikitazama suala la mifugo tu kwa kipindi kirefu sasa mifugo haikupata mkazo na mtazamo unaopaswa kupewa katika ngazi ya sera na katika sheria mbalimbali zinazogusa mifugo kama zao, mifugo kama uchumi na hii inadhihirika zaidi kwamba kwa kipindi kirefu mifugo imebebwa na sekta nyingine, kwa kipindi kirefu mifugo imebebwa ndani ya kilimo cha mazao, imebebwa katika sekta ya maji na sasa pia inabebwa na uvuvi na hii inaonesha kwamba mahali fulani mifugo haikutambulika rasmi kama sekta inayopaswa kusimama yenyewe ili iweze kupata mtazamo, iweze kupewa jitihada na kupewa rasilimali za kutosha kuweza kuikuza sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokeza katika suala zima la ardhi kwamba tukitazama mifugo inahitaji ardhi na tena ardhi kubwa kwa jinsi tunavyofuga huku kwetu, lakini ardhi nyingi inaonekana kwamba mara nyingi itoke chini ya sekta hii ya ufugaji na kwenda katika maeneo mengine iwe ni ya utalii, wanyamapori, kilimo, misitu na hii inaonyesha kwamba imekuwa ni sekta kidogo ambayo inaonekana kwamba badala yake kuna kitu kingine kinachoweza kikawa kizuri zaidi, kikazalisha vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba mifugo hasa kutokana na tafiti zilizofanywa hivi karibuni sekta ndogo kama ya nyama choma utafiti umefanyika ikaonekana kwamba ni sekta inayochangia sana katika Pato la Taifa na katika uhakika wa chakula kwa Watanzania walio wengi, pia kuna tafiti zilizofanywa katika sekta ndogo ya ngozi, sekta ndogo ya maziwa, sekta ya samadi na jinsi inavyochangia katika kilimo cha mazao na kwa kweli tukitazama sekta hizi ndogo zenyewe tu zinatuonyesha kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kujaribu kutoa mkazo na picha kamili katika suala zima la

mifugo ili mifugo iweze kupata mahala pake pia katika uchumi mzima wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Waziri katika kipindi hiki kinachokuja Wizara ichukue hatua za makusudi kabisa kufanya kazi kwa karibu na Wizara ya Ardhi ili kuhakikisha kwamba sheria ambazo zipo tayari Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 kwamba zitatumika kumpatia mfugaji na kuipatia mifugo nafasi halali katika vijiji husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kwamba kama kuna uwezekano sheria hizo zitumike, moja kuhakikisha kwamba vijiji vyote na maeneo yote ya kifugaji yanapimwa na kupatiwa hati kufuatana na sheria ya ardhi ya vijiji ya mwaka 1999 ili kuweza kulinda mifugo na wafugaji kutokana na matumizi mengine ya ardhi, kwa sababu kutofanya hivyo ni kuruhusu migongano inayotumika na matumizi mbalimbali ya ardhi iweze kuendelea kukua na kuleta madhara makubwa kwa mifugo lakini pia kwa Pato la Taifa na kwa wahusika wanaofuga na wanaolima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuhakikisha kwamba vijiji vyote vinapata ardhi na kupata hivyo vyeti, kuna haja pia ya Wizara ya Mifugo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi angalau kuweka mkazo kwamba maeneo yale ya kufugia pia yatambulike kama ni *zones* rasmi zinazotumika kihalali kama vile maeneo mengine kwa mazao ya kahawa, pamba, tumbaku korosho yanavyotambulika Kitaifa kwamba ni maeneo yanayotumika kuzalisha mazao haya niliyoyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya pia ya kifugaji ningeomba pia yatambulike kama ni maeneo ya uzalishaji na hivyo yanastahili kulindwa na kupangiwa matumizi bora ya ardhi na ionekane kwamba ufugaji ni njia mojawapo iliyo endelevu ya kutumia ardhi katika maeneo hayo na kwamba uzalishaji unaotokana na mifugo unaweza pia ukahalalisha maeneo hayo yatambulike hivyo bila kuvamiwa na bila kuingiliwa tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi yenyewe haitoshi kama mkazo usipowekwa katika suala zima la malisho na suala zima la maji, kwa upande wa malisho kuna haja ya kushirikisha wahusika wa maliasili kwa sababu kama ni majani na mimea mara nyingi inaangukia katika shughuli zinazofanywa pia na watu wa maliasili na kuna haja ya kujaribu kuondosha mgongano ambao umekuwepo kimapokeo kwamba eneo linapoonekana kwamba ni zuri kwa wanyamapori ni zuri kwa misitu, ni zuri kwa *flamingos* tabia iliyokuwepo ni kwamba kama kuna mifugo na wafugaji waondoke na kutoa nafasi kwa matumizi hayo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wakati umefika kwa sasa kwanza kukiri na kukubali kwamba maeneo hayo ni mazuri kwa sababu mifugo na wafugaji wamehifadhi maeneo hayo, wamewahifadhi hao wanyama kwa sababu kitoweo kimetokana na mifugo kwa hiyo, digidigi hawauwawi na tukitambua hivyo itasaidia kuona mshikamano unaokuwepo na mkamilishano unaokuwepo kati ya ufugaji pamoja na wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ikitambulika itakuwa ni njia moja rahisi ya kukuza mifugo katika maeneo hayo kwa sababu mifugo itaendelea kuwa ni kinga kubwa kwa wanyamapori pamoja na mazingira yale na uoto huo wa asili. Maji ni kitu kingine ambacho ni sharti nadhani Wizara iweke mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba maji yanakuwepo kwa matumizi ya watu lakini pia kwa matumizi ya mifugo.

Kama Wizara ya Maji itahusika nadhani ni jambo zuri na sahihi ili kuhakikisha kwamba kule kuhamahama kunakotokana mara nyingine na ukame na ukosefu wa malisho kutapungua maana si rahisi uhamaji upungue endapo mifugo ipo, inahitaji maji, inahitaji malisho na maji hayapo na malisho hayapo. Kwa hiyo, nadhani njia nzuri ya kukazania kutunza hayo mazingira na kupunguza uhamaji ni kule kwa Wizara nadhani kushirikiana na Wizara nyingine, lakini kuhakikisha kwamba maji yanakuwepo malisho yanaboreshwa, malisho yanakuzwa na kulindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia niongelee suala la magonjwa. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ni kweli ametoa picha halisi juu ya magonjwa yale makuu yawe ya mlipuko ama yale yanayojirudiarudia na athari inayotokana sana kwa wafugaji kwamba magonjwa kwa kweli yanaua mifugo kwa kiasi kikubwa na magonjwa haya yanawafanya watu kila mara warudi katika hali ya umaskini.

Ningeomba nadhani mkazo uwekwe na huwezi kuboresha hali ya afya ya mifugo nchini endapo tutaendelea kubaki na tatizo la watumishi kwamba watumishi vijijini hawapo na kama wapo ni wachache watabaki katika ngazi ya Wilaya na ningeomba mkazo uwekwe mmoja katika kuwaandaa watumishi watakaowasaidia wale wafugaji katika kuchambua hayo magonjwa kusaidia katika upatikanaji wa dawa lakini pia kushauri jinsi mifugo itakavyotibiwa na kupunguza hasara hizo. *(Makofi)*

Lakini tukiangalia mipango ya Wizara, Mheshimiwa Waziri amesema wanahitajika watalaam zaidi ya 13,469 lakini uwezo wa vyuo vilivyopo ni kuwaandaa watalaam 1108 kwa mwaka. Kwa hiyo, tukibaki katika hali hii ina maana kwamba tutahitaji walau miaka 10 kuweza kuwapata watumishi tunaowahitaji kwa sasa. Lakini bila shaka baada ya miaka hiyo kumi mahitaji ya mifugo na mahitaji ya watalaam yatakuwa yameongezeka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeomba kama kuna uwezekano Wizara ijaribu kutazama kuwa na programu jinsi ya kuwa na programu ya kuhakikisha angalau kwamba kwa kila Wilaya kunakuwepo na watalaam wa mifugo na kunakuwepo na maafisa ugani ili kuweza kuwasaidia wafugaji kuboresha mifugo kama zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la masoko kwamba ni kweli mifugo ni zao, ni chakula ndiyo lakini wanaofuga wanauza pia mifugo waweze kupata fedha za kutumia kwa mahitaji mengine. Ningeomba Wizara ijaribu kutazama tena upya vitu viwili sera ya mifugo lakini sheria hiyo ya *veterinary* ambayo ukitazama kwa karibu vitu hivi viwili hasa sheria inakwaza na kufanya vigumu wafugaji kuweza hata kufikia masoko yale yanayokuwepo. Basi sheria inasema mifugo ni lazima isafirishwe kwenye

malori na maeneo mengi hakuna barabara, hakuna malori, kwa hiyo, nadhani ni kutumia falsafa kidogo ya mbuni tukisema kwamba hawa wote watatumia tu usafiri wa barabara wanapopeleka mifugo yao sokoni kwa sababu hakuna barabara sehemu nyingi na hakuna usafiri maeneo mengi. *(Makofi)*

Ningeomba Wizara ijaribu kutazama sera na sheria ili hivi vyote viwili viweze kuwa ni vitu vya kuwezesha badala ya kuwa ni vitu vya kukwamisha ni vitu vya kukwaza. Hapo baadaye itakuwa kwamba miundombinu itakapokuwa ipo ya kutosha tunaweza tukasema kwamba tubadilishe sera, tubadilishe sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maadam havipo kwa sasa na itachukua miaka mingine karibu 20 bila ya vitu kuwepo katika maeneo ya wafugaji nadhani ni vizuri na ni busara kuanza kutazama kwamba yanayowezekana kwa hali yetu ya sasa ni yapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba tu tena nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na watalaam katika Wizara ya Mifugo na kuwaambia kwamba wajaribu kutumia kipindi kinachokuja walau ku-*transform sector* ya mifugo ili kwenye Bajeti ya mwaka mwingine tuweze kuitazama ikiwa na sura mpya, ikiwa na mwelekeo mpya zaidi, lakini pia ikiwa hai zaidi na wafugaji na mifugo yao wakiwa na nafasi maalum katika jamii ya Tanzania bila kuonekana kwamba ni watu wa kusukumwa huku na huku. Wasukumwe na kilimo, wasukumwe na wanyamapori, wasukumwe na madini, wasukumwe na kitu kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi nichangie kidogo katika hoja hii. *(Makofi)*

Kwanza kabisa kwa niaba yangu mimi binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwimba naomba nitumie nafasi hii kutuma salaam za pole kwa wafiwa, jamaa na wapiga kura wa Tarime waliofiwa na Mbunge wao Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marehemu Chacha Wangwe alikuwa ni Diwani wangu mwaka 1994 nilipohamia Tarime. Nilikuwa Mkuu wa Shule moja kule Tarime. Kwa hiyo, nilikuwa namfahamu sana na alikuwa ni rafiki yangu wa karibu sana, lakini kila mtu ana mwisho wake, mwisho wake umefika lililopo sasa hivi ni kumwombea hifadhi ya kheri kwa Mwenyezi Mungu. Ndugu wa Marehemu ningependa wawe na utulivu na wawe na amani. Naamini kwamba kazi aliyoifanya Mheshimiwa Chacha Wangwe ilikuwa ni nzuri sana. Naamini kwamba Mwenyezi Mungu atampatia kheri huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri

wanayoifanya katika kuendeleza sekta hii ya mifugo na uvuvi. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwamba kila mahali pote alipopita kazi zake kwa kweli zimekuwa nzuri sana. Labda tuseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri ana karama ya uongozi, mimi ninampongeza sana kwa hilo na kila mahali anapokwenda anabuni vitu fulani vinaonekana. Naamini kwamba Mwenyezi Mungu yupo pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii vile vile labda nianzie na *ranch* ya Mabuki, lakini ya *ranch* ya Mabuki haipo katika Jimbo langu, ipo katika Wilaya ya Misungwi ambayo ilikuwa ni sehemu ya Wilaya ya Kwimba.

Kwa hiyo, jinsi ilivyoingia tunaifahamu kwa kiasi fulani, lakini kwa Misungwi hii ni *ranch* ya awamu ya pili. *Ranch* ya kwanza ilianza mwaka 1931 ililetwa na wakoloni haikuwa na faida sana kwetu. Kwa bahati mbaya sana ufugaji huo ulituletea hasara sisi. Historia kama ikipitiwa vizuri itaonyesha kwamba Malkia wa Uingereza alileta ng'ombe wake mwaka 1931 Mabuki wakafa wote. Baadaye Gavana akaamua miti yote ifyekwe kwa sababu ng'ombe hao walikufa kwa sababu ya mbung'o**.** *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanashangaa kwa nini Shinyanga na Wilaya ya Kwimba hivi leo haina miti, Mungu hakuumba Wilaya ya Kwimba isiwe na miti wala Shinyanga sehemu za Maswa isiwe na miti. Kulikuwa na *operation* maalum ya kuua mazalio ya mbung'o**,** kulikuwa na *operation* ikaitwa senga senga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo ukienda Shinyanga utakuta watu wanaitwa Senga waliozaliwa katika kipindi kinachoitwa senga senga. Kwa hiyo, watu wa upande huo wakapata utamaduni wa kufyeka miti siyo kwamba sisi Wakusuma tulizaliwa na utamaduni wa kufyeka miti, tulifundishwa. Kwa hiyo, tunafyeka miti siyo kwa sababu tulizaliwa hivyo ni utamaduni tulioletewa katika *operation* ya senga senga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kwenye awamu ya pili ya *ranch* ya Mabuki ilipo hapo imeanzishwa zaidi ya miaka 20 iliyopita ilikuwa na malengo maalum. Mimi nilitarajia kwamba watu ambao wanazunguka eneo hilo watu wa Misungwi na watu wa Kwimba angalau wangeweza kuonekana kwamba wamenufaika na matunda ya *ranch* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabuki ina *fence* kwa tafsiri zangu inaelekea ile *fence* yake haizuii ng'ombe tu kutoka nje na wasiingie ndani lakini vilevile inazuia maarifa yanayotoka ndani ya *ranch* yasiende nje kuwafikia wananchi. Hii ni kwa sababu ng'ombe ndani ya *ranch* wapo tofauti sana na wale ng'ombe wengine wanaotoka nje ya *fence*. Maana yake ni kwamba hata wale ambao wapo karibu na ile *ranch* hawajaona faida sana ya *ranch* ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mimi kuna wakati niliuza swali hapa, hivi kwa nini eneo hilo Serikali isikubali ikalitoa kwa Wizara ya Miundombinu ujengwe Uwanja wa Kimataifa wa Ndege ile *ranch* iondolewe pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hivyo kwa sababu tumekuwa na *ranch* nyingine Malya ikafungwa na watu wa Malya walitegemea labda wangeweza kupata

mashamba, lakini mashamba hayo walipewa watu wengine ambao hivi sasa wanakodisha kwa utaratibu wao kitu kilichosudiwa kujengwa katika maeneo hayo na wale waliopewa hayo maeneo hakuna hata kitu moja na sasa hivi ni zaidi ya miaka mitatu. Kwa hiyo, imekuwa ni hasara kwa watu ambao wanazunguka eneo hilo. Wanaona watu wanatoka mbali wanakuja kulima katika eneo hilo wakati wenyewe hawanufaiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kwamba baada ya huko Mabuki na lenyewe linaweza shamba hilo lote kufungwa au kuchukuliwa na watu wengine na watu ambao wanazunguka eneo hilo wasinufaike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilipouliza hilo swali nilipata majibu mazuri sana kwamba hilo ni eneo pekee ambalo ni la kufanyia utafiti kwa ajili ya mifugo na kwamba faida zake zinaweza kuwa kubwa sana kwa watu wa Kanda ya Ziwa na sehemu zingine hapa nchini nikaridhika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimi ninaomba kutoka kwa Mheshimiwa Waziri mle ndani kuna mbuga za nyasi kwa ajili ya wafugaji. Eneo la Kwimba ni kame. Hao wananchi wa Jimbo la Kwimba ambalo eneo lao ni kame watanufaikaje na nyasi hizo ili angalau kama ni kupanda wakati wa masika waweze kulihifadhi. Hilo ni moja. Lakini la pili hivi mtu wa nje anayetaka kunufaika na elimu inayotolewa kutokana na utafiti unaofanyika katika *ranch* hiyo anaipataje, je, wanaokwenda kujifunza pale ni watu gani, je, ni wafugaji au kuna watu maalum ambao wanakwenda pale? Kwa sababu ningependa kufahamu ule uhusiano uliopo wa moja kwa moja kati ya mambo yanayofanyika ndani ya *ranch* ile na wafugaji ambao wako kando kando ya *ranch* hiyo. Ningependa sana kupata maelezo ili nianze kuhamasisha hao wafugaji wa Wilaya ya Kwimba waanze kwenda pale kwenda kupata mafunzo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nirudie suala moja ambalo limesemwa mauzo mazuri sana ni kwa kilo, Mheshimiwa Lucas Selelii ameliongelea vizuri sana na mimi nashangaa kwa nini mpaka sasa hivi mifugo iendelee kuuzwa kwa ngozi kwa kuangaliwa tu bila kuangalia uzito wake?

Mimi naendelea kumuomba Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuangalia ni kwa namna gani minada yetu inaweza kuanza kutumia mizani kwa ajili ya upimaji wa mifugo kabla ya kuuzwa. Mimi naamini kwamba kwa kufanya hivyo tutawatendea haki wafugaji ambao wanakopa katika mazao na wanakopa katika mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya mifugo na hapa mimi naongelea juu ya ng’ombe, mbuzi, kondoo na wanyama wote ambao wanatoa ngozi. Zao hilo la ngozi kuna mipango gani hasa ambayo inaweza kuanza mara moja. Miaka ya 1960 tulikuwa na kiwanda cha ngozi Mwanza, mipango yake mimi hata sifahamu inaendeleaje. Lakini mimi nilichokuwa nafikiri maeneo mengi ambayo yana mifugo kama Mwanza na Shinyanga viwanda kama hivyo vingeweza kutafutiwa wawekezaji haraka ili mazao haya yasiendelee kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee juu ya ufugaji wa samaki, kwa bahati mbaya sana Kwimba ndiyo Wilaya pekee ambayo haigusani na Ziwa Victoria pamoja na kwamba ni ya Mkoa wa Mwanza. Samaki tunawapata wameshakufa au waliokauka na wakati mwingine wanakuwa wanafika hata wale panki ingawa tunashukuru kwamba siku hizi hawapo tena, tunashukuru sana Serikali imesaidia kwa hilo. Ombi langu lilikuwa ni hivi, hivi Kwimba hatuwezi kupata mabwawa makubwa ambayo tunaweza kuyatumia katika kufuga samaki tusilazimike kula samaki ambao wamekufa saa nne, tano zilizopita? Mimi naamini kwamba inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunaandaa utaratibu wa kupata bwawa kwa ajili ya mji wa Ngudu, kwa sababu bado tuko katika hatua ya mwanzo sana, inawezekana kabisa watalaam wa Wizara hii wakatusaidia katika kuandaa ramani nzuri ili litakapokuwa linajengwa vile vile tuweze kufuga samaki kwa ajili ya wakazi wa Kwimba na hasa Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nafikiri inawezekana kwa sababu bado ni mapema. Tutaomba msaada sana wa Wizara hii, Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana ututumie watalaam wako kuja kuangalia hili eneo kama linaweza kufaa kwa wafugaji wa samaki. Nataka niishie hapo tu lakini naunga mkono hoja hii kwa asilimia karibu zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bujiku Sakila.

Waheshimiwa Wabunge, muda tulionao haumtoshi mchangiaji anayefuata kwa sababu kila mtu anatakiwa apate robo saa ya kuchangia. Kwa hiyo, tunazo dakika 10 tu ambazo hazitatosha mchangiaji. Lakini napenda nichukue wakati huu kutangaza wachangiaji watano watakaofuata jioni.

Kwanza kabisa nitamuita Mheshimiwa Ruth Msafiri, atafuatiwa na Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Abdulkarim Shah na Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo nasitisha kikao hiki mpaka saa 11. 00 jioni.

*(Saa 6.50 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Ahsante sana, simuoni Mheshimiwa Ruth Msafiri. Kuna wakati nilipata ripoti kwamba angependa kuchangia Jumatatu. Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kwa mchana huu wa leo kuweza kuchangia katika hoja hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ningependa kutoa pongezi kubwa katika Wizara hii. Ni Wizara mpya lakini imenaza vizuri. Ni Wizara ambayo imeundwa katika mtiririko ambao kwa kweli umetuwezesha sisi ambao tunakaa katika maeneo ya wafugaji pamoja na wavuvi kuweza kuyaunganisha masuala hayo.

Napenda nitoe pongezi kubwa kabisa kwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ndugu yangu Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Katibu Mkuu, watendaji wote katika Wizara hii. Naomba kabisa Wizara hii iwe ni mfano kama ilivyo mifano katika Wizara zingine alizoongoza Mheshimiwa John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Nipende tu kuzungumza machache kuhusu Wizara hii. Hasa nikimwangalia Waziri, Mheshimiwa John Pombe Magufuli ni mtu ambaye ni mbunifu, ametusaidia sana wananchi wa Geita hasa ukiangalia kwamba kila kitu anachokibuni unakuta kwamba kinatekelezeka. Alisema kwamba tungeweza kutoka kwa *taxi* kutoka Mtwara mpaka Mwanza. Kwa kweli katika kipindi chake mambo yalikuwa ni mazuri sana. Alituambia kwamba tungepata barabara ya lami kutoka Kiamnyorwa mpaka Mwanza na kweli ilikuwa hivyo, pamoja na kwamba alianzia Kiamnyorwa kwenda Mwanza, watu wakawa kubeza. Wengine wakaanza kutushawishi kwamba tumwone sisi kwamba hafai. Lakini lilikuwa lengo zuri kwa sababu angeanzia Mwanza ile barabara isingeisha, kwa sababu ya watu ambao walikuwa na tamaa ya kuweza kuendeleza maeneo yao na kutuacha sisi tunaathirika. Hilo nataka kumpongeze sana aendelee na moyo huo wa maendeleo katika maeneo yote. Hachagui hapa ni watu au ni sehemu gani. Anataka maendeleo ya Watanzania wote. Napenda nimshukuru sana kwa kazi nzuri anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninajua kabisa kwamba sasa Wizara hii imepata mwenyewe. Imepata mwenyewe katika masuala ya uvuvi na masuala ya ufugaji. Ningependa tu nimweleze machache Mheshimiwa Waziri kwamba katika Ziwa Victoria, kuna wavuvi ambao wako kule. Lakini tatizo moja kuibwa kuna hizi zana za uvuvi ambazo zimepigwa marufuku. Unakuta kwamba bado zinatengenezwa madukani. Sasa nilikuwa namwomba kama mnawapiga faini hawa wanaozinunua, hawa waliotengeneza wanapigwa faini gani? Kwa hiyo, hilo liwe ni jambo lingine la kuangalia ili tusiwe tunaumiza upande mmoja tukaacha upande mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo nilikuwa naliomba sana. Lakini nilitembelea vijiji kama 30 nilipokwenda, nilienda Kata ya Bulela, nilikuwa Bumanji na Nyaseke, nilikuwa Kata ya Kasamwa, sehemu za Mshinde na Ibanda. Nilikuwa Kata ya Rubanga, Ibisabageni na Isubotundwe na Nyakaduha. Kata ya Kamuhanga, nilikuwa Kijiji cha Kishinda na Mkolani. Lakini wote wale walikuwa wanalalamikia kwamba sasa hivi wananchi wa Geita tutakuwa na matatizo, kitoweo wanachokipata ni hawa wavuvi wadogo wadogo na sisi kama jadi yetu tuna kawaida ya kuwabatiza, wamewabatiza kama *nchimwabuyu* yaani inachoma fizi, vina miba migumu sana.

Sasa wanajiuliza hawa samaki wanapatikana katika mitego ipi? Au katika nyavu zipi? Sasa kama wamekatwa wale hata hiki kitoweo kidogo ambacho kinawaumiza watakulaje sasa hivi kama wataendelea kuvua samaki hao? Sasa nilikuwa naomba kabisa Mheshimiwa John Magufuli ufanye juhudi zako zote angalau wananchi wa eneo la Geita au Geita kwa ujumla wapate kitoweo cha kuridhisha. Lakini kumekuwa na utaratibu wa kwenda sokoni, unakuta kuna aina fulani ya hawa sangara wadogo wadogo, sisi tunaita joa. Wale unakuta kwamba akifika Afisa Uvuvi, anamwaga kwa sababu kwamba ni wadogo wadogo sana au wengine wa *size* kubwa, lakini wanamwagwa. Lakini wameshatolewa ziwani ambao ni kitoweo na wananchi wanawapenda. Kwa nini wananchi wasiachiwe wakala tu, badala ya kumwaga kitoweo yote?

Sasa unakuta kwamba jina zuri ambalo unalo wanakuchafulia wengine. Naomba Ndugu yangu John Magufuli uwasaidie wananchi hawa. Lakini unakuta kwamba sasa hivi kuna mfuko wa kusaidia hawa wavuvi wadogo wadogo, naomba wavuvi wa sehemu za Mharamba, Nzela pale Kogona pale Lwenzera, Mkome wasaidiwe na Asenga wasaidiwe angalau kupata mikopo kuweza kujiendeleza katika dhana hii ya uvuvi. Wavuvi hawana ruzuku ukilinganisha na wakulima. Wakulima wengi wanapata ruzuku katika maeneo mbalimbali. Kwa nini hawa wavuvi ambao wako maeneo machache yanayoeleweka katika Kanda ya Ziwa wavuvi wangepewa ruzuku wakaweza kuvua samaki wa kuweza kujitosheleza na isitoshe katika Ziwa Victoria unakuta kwamba samaki sasa hivi karibu wanakwisha au kama hawaishi unakuta kwamba wanapungua sana na unakuta sasa hivi makundi mengine ya samaki hayaonekani na wanaomaliza hawa ni hivi viwanda vikubwa vikubwa ambavyo vinachukua samaki kila siku.

Kwa nini kusiwe na utaratibu wa kuweza kufanya *quarters* kwamba miezi fulani wenye viwanda wapewe nafasi ya kuweza kuvuna, miezi inayobaki basi na wananchi na wenyewe wavune na kwa sababu kutakuwa na samaki wengi itakuwa bei ndogo kwa sababu samaki watakuwa ni wengi. Lakini sasa hivi unakuta kila siku hao wenye viwanda wanakuja kuchukua samaki pale na wakija wenye pesa ujue kwamba mwananchi wa kawaida hawezi akawanunua wale samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri kama kuna uwezekano kuwe na *quarters* kama wanavyofanya katika mapori ya uwindaji. Kuwe na *quarters.* Bahari na maziwa haya ni sawa sawa na mapori yetu, sawa sawa na misitu yetu ya wanyama. Hawa ni wanyama wa majini. Kwa nini kusiwe na *quarters* kwamba mwezi fulani ndiyo uvunaji, miezi iliyobaki basi waachiwe wananchi na wenyewe wapate kitoweo chao. Hilo nilikuwa naliomba sana kwa upande wangu na kwa upande wa Mheshimiwa Waziri. Najua ni msikivu anaweza akayatekeleza yote haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda upande wa wafugaji. Bahati mzuri sana Geita imekuwa na pande zote. Geita ina wafugaji, ina wakulima, ina wavuvi, ina wachimba madini na ina wafanyabiashara. Sisi kule tunasema hiyo ni kama nchi. Kwa sababu hata idadi yetu inatutosheleza kabisa.

Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa John Magufuli sasa hivi naenda upande wa mifugo. Wafugaji unakuta kwamba ni watu ambao wamedharaulika sana. Ni watu ambao

wamekuwa wanafukuzwa kila sehemu. Ni watu ambao hawaeleweki, akifika sehemu basi unakuta kana kwamba hastahili kuishi kwa wananchi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anawekwa katika hali ambayo basi yeye ni kama ni mtu tu wa kuja. Naomba kwa upande wa wafugaji wa Geita na nchi nzima waweze kuthaminiwa, mifugo yao tusiwe tunawalaumu tu. Mimi nasikia wengine wanasema kwamba punguzeni mifugo, lakini sijamsikia mtu anasema kwamba punguza mashamba au punguza pesa zako. Wengine wanajaza pesa kwenye benki, wapi mbona hatuwaambii kwamba mpunguze pesa zenu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba kabisa kwamba hilo lazima litiliwe maanani. Kinachohitajika ni kuwafundisha mbinu za kuweza kuboresha mifugo yao kama inavyoeleweka kwamba kuna madume ambayo yanazalisha, halafu mnayahasi.

Mimi nilikuwa naomba msiyahasi hayo madume. Hayo madume yanayozalishwa yote yapelekwe katika vijiji kwa wafugaji katika kila Kata kwamba kuna wafugaji labda wawili, wanapewa madume wawili ambayo yanaweza yakazalisha katika Kata kwa muda, ukiweka miaka mitano utakuta kwamba Tanzania tuna mifugo ambayo ni bora zaidi. Lakini leo hii tukianza kuwaambia tu kwamba punguza mifugo. Kwa kweli tunakuwa hatuwatendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la sivyo basi hata hawa wakulima tuwaambie wapunguze mashamba ili waweze kutumia ile ardhi katika ustaarabu. Lakini tunazidi kuwapa ardhi kubwa, tunawafukuza wafugaji, maana yake nini. Hilo kwa kweli siyo jambo zuri na kwa sababu uko upande ule najua utazungumza na wenzako ambao wanaweza wakaeleweka vizuri zaidi ili kuweza kusaidia wafugaji wetu. Wafugaji kwa kweli mpaka sasa hivi hawana ruzuku yoyote. Wafugaji unakuta wanazunguka tu hamna mtu wa kuwajali. Najua wewe umetoka katika ukoo wa wafugaji na Mwenyekiti ni mfugaji. Nina uhakika kabisa suala hili unaweza kulititilia maanani kiasi ambacho kwamba wafugaji wanaweza wakathaminiwa wakaonekana katika Tanzania kwamba ni wazalishaji wa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kabisa kwamba tukimtunza mfugaji au tukichukua kwamba ufugaji ndiyo chanzo chetu cha Pato katika Taifa hili. Nina imani kwamba Tanzania tutakuwa ni mfano mzuri. Kwanza ng'ombe wetu kama ulivyobainisha, lakini ng'ombe hawa unakuta kwamba Serikali haijali, ingejali kama sehemu zingine sidhani kama ng'ombe hawa wangeweza wakasema kwamba wanapotea bure tu. Kwa kweli mimi nimesikitika sana, lakini kilichonisikitisha zaidi ni hawa wanaowashika wafugaji na kuweza kuwatoza faini kubwa halafu wao wenyewe wanajinufaisha. Hii imetokea sehemu za Biharamulo, sehemu za Mbarali ambao watu waneleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa naongea na Mheshimiwa Ndugu yangu Lekule Laizer, akaniambia ninyi Wasukuma hamfai kabisa, unafukuzwa na mwanamke, kwa kweli alinikasirisha. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa nikaangalia kweli jamii iliyoteseka, kule Mbarali ni Wasukuma watupu, halafu waliowanyanyasa ni huyo huyo, kwa kweli iliniudhi. Kwa kweli nilikuwa nasema kwamba kama kuna uwezekano, Serikali imshinikize huyo mtu aliyejitajirisha kutokana na mikono ya wafugaji. Sasa hivi ana ng'ombe kibao, basi arudishe mali hiyo kwa wahusika na wale waliodhulumiwa naiomba Serikali kwa sababu ndiyo ilianzisha zoezi hilo. Warudishie gharama zote za usumbufu kwa sababu wamesumbuka sana hawa ndugu zangu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi hawana sehemu nyingine ya kukaa na wengine ukiwahoji unakuta kwamba wameshaishiwa hata mali kwa ajili ya kusafiri kutoka hapa mpaka Lindi wapi na ukifika kule hamna hata vigezo vyote, hamna miundombinu. Kwa hiyo, unakuta kwamba ni watu ambao wanasumbuka tu. Nilikuwa naomba watu kama hawa kwa kweli wachukuliwe hatua kali, kali, kali kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu kitu kimoja katika suala hili. Zamani enzi za ukoloni wakati mimi nazaliwa nimekuta sehemu za nyumbani kwetu kuna malambo mengi tu yanafanya kazi. Nyumbani kwetu nasema malambo ya mzungu. Lakini siyo ya mzungu, wananchi wenyewe ndiyo walikuwa wanashirikishwa, wanayachimba yale malambo na ndiyo yaliyokuwa yanasaidia katika kunywesha mifugo yetu katika maeneo mbalimbali na ndiyo katika mpango wa kujenga majosho ndiyo iliyosaidia kujenga yaani sehemu gani tujenge wapi josho ni sehemu ambayo kuna lambo.

Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuyaangalia malambo kama haya yafuatayo ambayo sasa hivi yameshabomoka hayafanyi kazi, lambo la Buzyasoga, sehemu za Sengerema, lambo la Chikobe, lambo la Nyamhwale, lambo la Isotundwe Labulela, Kasamwa, Bulegezi, Mbabane, Senga, Idoselo, Nyarugusu na Kamena. Haya yote sasa hivi hayafanyi kazi na ni malambo ambayo yapo. Nilikuwa naomba katika ule mtiririko najua Geita tumesahaulika, hata malambo hamna na majosho hamna. Hata Chato hakuna hata lambo. Sijui wewe utatengeneza wapi lambo, nilikuwa naomba basi hata malambo mawili Chato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Michael Lekule Laizer na atafuatiwa na Mheshimiwa Abdulkarim Shah. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Lakini kabla sijachangia, labda nisahihishe usemi aliyosema mchangiaji aliyenitangulia. *(Makofi)*

Kwanza alitaka kunichonganisha na akinamama kabisa, huu usemi niseme tu ni uzushi, kanizushia, sikusema hivyo. Nilichomwambia, nilimwambia ninyi Wasukuma hamfai kwa sababu hamjawatetea Wasukuma wenzenu waliofukuzwa Ihefu. Ndiyo tulitaniana hivyo, siyo suala la akinamama. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia tu na mimi niseme kwamba kwa kweli Waziri na Naibu Waziri walioko sasa katika Wizara hii tuna imani kubwa nao. Tuna imani kubwa na Waziri kwa sababu alifanya mambo ya ajabu katika Wizara ya Miundombinu, alipokuwa Miundombinu alifanya mambo ya ajabu. Hata barabara zote zilizoko Tanzania anazifahamu kwa kichwa, kilometa na majina na nini akisimama hapa hahitaji karatasi yoyote ya kumbukumbu. Kwa hiyo, tuna imani sana kwamba Wizara hii ambayo imeshindikana miaka na miaka nadhani utaiweza.

Kila Bajeti mimi nachangia mifugo na ninasema kila siku kwamba hakuna awamu yoyote kati ya Awamu ya Kwanza na ya Pili na ya Tatu na hii ya Nne inayothamini mifugo, sijawahi kuona. Kila wakati mifugo katika Bajeti zote haijaliwi, mpaka wafugaji wenyewe hawajaliwi. Hakuna kinachofanyika, ni Wizara mojawapo ambayo mifugo inawekwa tu kwa jina kwa makaratasi na kwa Bajeti. Ilipokuwa kilimo, fedha zote zinakwenda pembejeo za kilimo mpaka na mfuko wa pembejeo inakwenda kilimo hakuna wafugaji wanaopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilipowekwa maji, maji ni maji mijini. Majitaka, mabwawa ya uvuvi, hakuna ya mifugo. Hakuna kitu kinachofanyika katika mifugo. Naomba Mheshimiwa Waziri ubadilishe hali hiyo. Jambo lingine ningependa kuzungumzia ni suala la uhamisho wa wafugaji waliohamishwa kule Ihefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamisho huo umeleta unyanyasaji mkubwa sana kwa Watanzania ambao kwa kweli tukinyamaza nasema uhamisho huo umezidisha umaskini nchini kwa wafugaji, wameteswa, wamenyang'anywa mali zao. Wamehamishwa hawajui pa kwenda. Hakuna miundombinu, umaskini umejaa na wengine hawana mifugo mpaka sasa, wengine hata familia zao hawajui wako wapi? Siku moja nimezungumzia tu uhamisho huu kwenye Kamati mpaka nikalia nikikumbuka jinsi ambavyo wananchi walivyoteswa. Lakini labda niseme kama walivyosema wenzangu, hiyo taarifa iletwe hapa ijadiliwe na kama kuna watu waliowanyanyasa wafugaji ichukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hakuna mafisadi zaidi ya hao, kama mnawatafuta mafisadi na hao waingizwe katika mafisadi wa nchi hii. Jambo lingine ni Bajeti, hii Bajeti ya mifugo kawaida yake ni ndogo na ikiwa ndogo hakuna miundombinu inayofanyika kwa upande wa mifugo. Majosho hayatakuwepo, malambo hayatakuwepo, dawa za mifugo hazitakuwepo. Minada haitakuwepo, hata katika Bajeti ya Mheshimiwa Waziri, miundombinu ya mifugo ni chache mno.

Kwa hiyo, napenda kusema kwamba hii Bajeti, tukisema kwamba imeongezwa kipindi hiki, imeongezwa tofauti na Bajeti zingine, lakini kama imeongezwa na hakuna kilichowahi kufanyika miaka na miaka, matatizo yanakutana kila wakati, inahitaji Bajeti kubwa kwa sababu hakuna majosho nchini na hakuna malambo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye dawa za mifugo. Kupitia kwako nataka Mheshimiwa Waziri anisikilize kuhusu dawa za mifugo. Ruzuku inayotolewa japokuwa

ni kidogo inapita kwenye njia tofauti kabisa ambayo wafugaji hawafaidi. Hawa watu mnaowapa zabuni kusambaza dawa kwanza hamhakiki kwamba hizo fedha mlizowapa za ruzuku zimenunua dawa? Hivyo wakienda kujenga magorofa mijini itakuwa kweli tumepata dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wasijulikane katika kila Wilaya kwamba mtu aliyechukua fedha za ruzuku za dawa ni fulani, yawepo maduka ya dawa. Tunajua kwamba duka hili kuna dawa ya ruzuku. Mtu mmoja anapewa Kanda ya Kaskazini hatumjui ni nani. Hatujui duka liko wapi? *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunataka utaratibu kwa fedha hizo kidogo tunataka utaratibu tujue kwamba hizo fedha za ruzuku na sisi tufaidi. Sio tu kwamba watu tu waende kutajirika kwa ajili ya kupata dawa. Jambo lingine kuhusu dawa, kodi. Nilishangaa kusikia kwamba kodi ya dawa ya mifugo bandarini wanatozwa asilimia 10. Hivi kwa nini kwenye dawa ya mifugo inatozwa kodi. Pale bandarini asilimia 10 mpaka walipe na dawa za kilimo zimetolewa kodi, mpaka matrekta yametolewa kodi, kwa nini?Nashangaa kwa sababu tulipopitisha Bajeti hapa hatukuona *item* hiyo. Tungefuta wakati huo huo lakini nasikia sasa imekuja kuwekwa. Nani kaweka tena baada ya Bajeti kupita? . *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, naomba kama kuna hiyo kodi ya dawa ifutwe kabisa. Jambo lingine kuhusu dawa za mifugo ni dawa za kinga. Kuna dawa ya kinga ya ndigana kali *(ECF),* iko. Serikali ingefaa inunue dawa hizo na izisambaze nchini, sio walanguzi kwenda kutafuta dawa wanakuja kutuchanjia mifugo, ndama kwa bei ghali. Siku hizi sasa ni shilingi 10,000/= kwa ndama mmoja na ni dawa ambayo ukichanja mifugo, ndama hawafi tena. Sisi kabla hatujapata hiyo dawa wanapozaliwa, ukipata ndama 200 wanakufa mpaka wanabaki 25 au kama una bahati wanabaki mpaka 50. Baada ya hiyo dawa kupatikana, sasa una hakika ya kupata asilimia 80 mpaka asiliamia 90 ya ndama wanaozaliwa. Lakini mpaka dawa itoke Kenya iletwe na walanguzi. . *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali isilete dawa hizo na kusambaza nchini? Dawa ya kinga, kinga ya ugonjwa wa miguu na midomo ipo, Kenya wanachanja kila wakati na kila mwaka, lakini Tanzania hawachanji, kwa nini wasichanje? Sisi kule mpakani watu wa Kenya wanatulalamikia sana kwa sababu malisho ni sehemu moja. Lakini sisi hatuchanji, wao wanachanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la malambo, sikuona katika Bajeti. Ningeomba katika Wizara hii ni lazima kuwepo na malambo. Katika Wizara ya Maji kuna malambo kwenye maeneo kame, sasa haya malambo yote yanalenga mifugo kwa nini isiwe kwenye Wizara moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipopitisha Bajeti ya Maji hapa kulikuwa na malambo kwa ajili ya maeneo ya wafugaji. Hapa kuna malambo kwa ajili ya maeneo ya wafugaji. Kwanza anasema zile zilizoko kwenye Wizara ya Maji ndiyo mengi kuliko ya Wizara ya Mifugo. Wizara ya Mifugo haina malambo hapa. Nashangaa, halafu hizo fedha ziko tena TAMISEMI. Kwa nini izunguke isiwe katika eneo moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka kwa sababu naona muda unakwenda. Suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la masoko, masoko ya ndani ya masoko ya nje. Tunahitaji masoko yaimarishwe, na hili soko la nje tunasikia tu kwamba kuna soko la nje lakini bado hatujui kwamba hao ng'ombe wanatoka wapi? Kwa sababu ukiangalia katika Wilaya yangu ya Longido. Wilaya ya Longido ndio wameboresha ng'ombe Tanzania, ndiyo kuna ng'ombe Tanzania. Nafahamu kwa sababu Wilaya zote wanakwenda kuangalia ng'ombe kule Longido, Serengeti wamekuja, Kiteto wamekuja, Simanjiro wamekuja. Huko ndiyo wanakwenda kuangalia mifugo bora. Sasa kama mnataka Tanzania ijulikane kwamba kuna mifugo, mtupe hilo soko la nje, kwa sababu mkitupa ng'ombe, sio wadogo wadogo kama hawa ng'ombe wa Wasukuma na Waberbeig hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ng'ombe wakubwa, hakuna ng'ombe wa Kisukuma anayefikisha kilo 800 hakuna. Lakini wa kwangu wanazidi kilo 800 si watatangaza Tanzania. Jambo lingine ni suala la mbegu. Hii mbegu ambayo ipo pale Nike, msambaze sasa nchini. Sisi tunanunua dume la mbegu kwa milioni moja na laki tatu mpaka laki tano, ndiyo maana ni wazuri. Wasukuma hawawezi kununua, sasa badala ya kununua dume milioni moja na laki tano hizo mbegu zisambazwe. Sisi hatununui madume ya Kongwa hapa wala hatutaki ya Mpwapwa, kwa sababu ni wadogo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni maeneo ya wafugaji. Maeneo ya wafugaji yaheshimike. Jamani mnavamia maeneo ya wafugaji, kila wakati mnavamia maeneo ya wafugaji halafu mnasema kwamba wafugaji ni wakorofi. Hamuwawekei miundombinu, hawana maji, wanakwenda kwenye vyanzo vya maji. Hivi ukikosa maji utakufa? Si unakwenda kwenye chanzo cha maji kama hakuna maeneo mengine, unakwenda. Wakulima wanaona mbuga za malisho, wanasema ni *open area.* Haya ndiyo malisho. Kwa hiyo, ningependa muheshimu hayo maeneo. *(Makofi)*

Jambo lingine ni viwanda. Kila mwaka unakuta kwamba kuna Bajeti kiwanda Shinyanga, kuna kiwanda Arusha, kuna kiwanda wapi, lakini ni vitu vinavyowekwa kwenye Bajeti sijui ni kwamba haitekelezeki au hamtafuti, sijui ni nini? Jamani wafugaji tunateseka, sisi tunataka kuboresha mifugo na kuvuna mifugo, sio kupunguza mifugo. Huu usemi mnaousema kila siku kwamba wafugaji wapunguze mifugo ni kosa kubwa sana kama alivyosema mwenzangu. Tunataka kuboresha mifugo halafu tuvune mifugo na tuvune mifugo wakiwa kwenye *quality* ya hali ya juu. Lakini hatuna msaada, tumekosa msaada wa Serikiali, Serikali ianze sasa kuwasaidia wafugaji, sio kuwafukuza tu kana kwamba sisi hatukuwepo pamoja nanyi mlipopata uhuru. *(Makofi/Kicheko).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mikopo. Mheshimiwa Waziri, nilishangaa nimeona vikundi na vikundi vya wavuvi mliowapa mikopo, vikundi na vikundi, na wewe sasa umeanza kuangalia upande wa uvuvi kwa sababu wewe ni mvuvi na mfugaji, sasa umeanza na wavuvi. Hivi ni kwa nini nchi hii hakuna mfuko wa wafugaji, mmenza mfuko wa samaki, eeh, pembejeo hatupo, mfuko wa samaki hatupo, hata wa wawajasiriamali hatupo, tunakuwa tu sijui tupo tu anagani. Kwa hiyo, naomba kama umeanza mfuko wa uvuvi naomba uanzishe tena mfuko wa wafugaji. Hatuko

kwenye mfuko wa JK, hatuko kwenye mfuko wa uvuvi, hatuko kwenye mfuko wa pembejeo, tumebaki tu angani tunahangaika tu sisi hatuna chochote. *(Makofi).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Michael Laizer, hasa kwa msisitizo kuwa ng'ombe wa wasukuma hawana afya nzuri. Kabla sijamuita Mheshimiwa Shah, kuna wageni 10 wa Mheshimiwa Abdulkarim Shah, ningewaomba wasimame pale walipo. Karibuni sana Dodoma, nilisema asubuhi habari ya wafugaji kuwepo nikasema mwakani huenda tutapata wavuvi lakini tumewapata jioni hii, karibuni sana. *(Makofi)*

Basi moja kwa moja naomba nimuite Mheshimiwa Abdulkarim Shah, kwa mchango wake.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba na mimi kabisa kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mzee wangu John Pombe Magufuli, Mheshimiwa Dokta James Wanyancha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote wa Wizara kwa Idara zote Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na wataalamu wetu kuanzia Wizarani hadi vijijini. Nawapongeza kwa kuandaa Bajeti hii katika kitabu hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea siku zote hapa mara nyingi nikiongea huwa naongea na kuanza na mahadithi na aya za *Quran*, hadithi za Mitume, lakini leo nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri wangu wa Mifugo kwamba naanza na ubeti wa nyimbo ya Msondo Ngoma unaosema hivi, *"Ukiona mtu mzima analia basi ujue kuna jambo."* Sasa hilo naomba ulielewe na hali ya wavuvi wetu katika wilaya ya Mafia au nchi nzima kwa ujumla hasa katika Ukanda wa Pwani. *(Makofi).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haraka haraka naomba ninukuu ukurasa wa 27 sekta ya uvuvi na hii wanakwambia ndio mwelekeo wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2008/2009. Ukiangalia kutoka *roman one* mpaka *roman twelve* hakuna kipengele kilichowekwa kwamba kutakuwa na mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba mvuvi wa Tanzania amepewa mfuko maalumu wa kuja kumuendeleza, na labda tu katika kumuweka sawa Mzee wangu pale Mheshimiwa Michael Laizer kwamba hakuna mfuko wa uvuvi ambao upo, isipokuwa kuna miradi ambayo ipo kwa ajili ya kuwaendeleza wavuvi na miradi hiyo kama itatekelezwa vizuri basi itawasaidia lakini kama miradi hii itakuwa ni kwa ajili ya kuimarisha majengo, magari, warsha, makongamano, pesa zote hizi zitakwenda kwa watu na majengo. Hakuna lolote katika mradi huo hasa sidhani kama utaweza kuwakomboa wananchi wa Ukanda wa Pwani, hasa baada ya leo kupata fununu kwamba kumbe pesa zitakazolenga moja kwa moja kwa wananchi ni bilioni nne na nusu tu katika ukanda mzima kwa miaka sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu jamani tuangalie, tuzipige bilioni 4,500 gawanya kwa wilaya zilizokuwepo halafu uje kuzigawanya kwa miaka sita, kila wilaya itapata kiasi gani? Na katika pesa hizo usifikirie kwamba labda ndio zitakwenda moja kwa moja

pengine kutakuwa na vitu vingine vidogo vidogo vya kuimarisha ofisi. Sasa mengi yaliyozungumzwa hapa ni ya kumbana mwananchi, maana yake wanasema kuimarisha doria, kufanya mapitio ya sera, kuimarisha udhibiti wa ubora na usalama wa kuongezea thamani ya mazao ya uvuvi, kuendeleza uanzishwaji wa vikundi, *BMU* hizo, *BMU* hizi zote katika kudhibiti maeneo, japokuwa wakati mwingine vinasaidia katika mambo ya uvuvi haramu. Kuwezesha kufanya tafiti mbalimabli, kuendelea kuboresha mialo, kufunga maeneo ya uvuvi, kuendelea kutoa elimu kwa umma, kuendeleza ukuzaji wa viumbe vya majini, kuendeleza mchakato wa kuanzishwa kwa mamlaka ya kusimamia uvuvi wa bahari kuu na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara ili kuongeza ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ni mzuri. Lakini sasa twende moja kwa moja kwa wananchi, Mheshimiwa Waziri wetu Magufuli, naomba sana wakati unaandaa mpango huu, najua wewe ni mwanasiasa na umeingia ndani humu kwa siasa, si utaalamu, sasa wataalamu wetu wanavyokueleza naomba sana waangalie maeneo. Leo mwananchi wa wilaya ya Mafia, ni kisiwa kilichozungukwa na bahari, wananchi wa Songosongo, Kilwa Kisiwani, Koma, Kwale, Ukerewe, umwambie asivue afanye nini? Leo mtu wa Rufiji, samahani sisemi vibaya kwasababu wote wananihusu, lakini mtu wa Rufiji ukimwambia asivue atakwenda kulima mpunga, atapasua mbao, atafanya kazi zingine juu. Lakini mtu wa Mafia unamwambia asivue, wewe uko katika kulinda mazingira tu basi mazingira na mazingira, hivyo mazingira ya nyavu zile zinavyoharibu zile tunazoziita mtando sijui kitu gani, uharibifu ule wa nyavu zile na mashimo yanayochimbwa kwenye dhahabu ni nani anayeharibu mazingira duniani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tupime, tupime milima ya Geita inavyong’olewa, Mheshimiwa Ernest Mabina, kila siku anapiga kelele jamani mnaharibu mazingira lakini madini yanachimbwa na watu wananufaika, sisi tumelenga kuwabana. Mheshimiwa haki ya Mungu, naona aibu leo kwa sababu hali ni mbaya sana na ukiangalia wengi tunakusifu Mheshimiwa John Magufuli kwamba umekuja kutukomboa katika Wizara hii sasa huo ukombozi kwa kitabu hiki, sijui? Ndio najipa mtihani mzito sana na ukiangalia Mheshimiwa, unajua kila jambo na lenyewe ni lazima ukae na wenzako. Sasa Mheshimiwa Waziri, wewe umetoka Chato, Biharamulo, najua kuna kipande kidogo cha bahari, lakini ukimuangalia Naibu Waziri, katoka Serengeti, ukija kwa Katibu Mkuu katoka Mara, ukienda kwa Naibu Katibu Mkuu katoka Moshi, ukija kwa Mkurugenzi katoka Manyara, hebu niambieni bahari uwakilishi wake ukoje? Sasa ni utaalamu wa kwenye madaftari tu, sasa huu unaleta shaka kwamba hali ya wananchi wa Ukanda wa Pwani bado itaendelea kuwa na matatizo na laiti kama ungekuwa unaweza kuomba, ningeomba hata Mbunge, mwingine angeniachia nikaongea kwa nusu saa lakini maskini kanuni haziruhusu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sana sana uangalie hili suala la nyavu. Naomba twende, nyavu tuzifanye haramu kwa matumizi lakini tusiifanye nyavu kwa ukubwa wa tundu. Leo *trolling* ndizo zilizomaliza nguva, samaki jamii ya nguva ambaye alianzia Kilwa Mtoni, Somanga, Kombwe, Jaja, Mbwera, Dima, Kiasi mpaka Nyamisati lakini leo tunasema tukimvua nguva basi anakuwa kama kiumbe adimu anayetoweka, waliommaliza sio wavuvi wa Mafia au Rufiji kilichommaliza ni *trolling*. *(Makofi)*

Sasa ninachokuomba ushauri wangu kwa Serikali, tuwasaidie wananchi wa Mafia na soko la feri linatosheleza, mradi wa Masempo uende moja kwa moja kwa wananchi lakini tusiwabane wao, tufunge meli zote za uvuvi. Tufunge meli za uvuvi kwa sababu wale ndio wanaomaliza samaki, jamani msisikie kulikuwa na meli moja ya utafiti iliyokuwa inakuja kufanya utafiti wa sehewa. Mafia kuna jodari, sisi kule kienyeji tunawaita virungu Mpweke unasikia, natumaini mnawafahamu eeh, basi wale wamejaa kwenye bahari ya Hindi, lakini hakuna Mmafia anayevua au mtu wa Tanzania Bara au Visiwani, wanaovua ni meli kutoka nje, sasa tunasema funga meli za uvuvi zote kama mlivyofunga katika Ukanda wa Rufiji. Sasa na kule Bagamoyo zuia kwa sababu *trolling* inavua kwa nyavu ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *trolling* inavua kwa nyavu sawa sawa na ya mtando pengine hata hiyo *ring net* na mtando tundu lake ni kubwa, sasa tunaomba kama kufunga, zuia yote lakini kama kuweza naomba ziruhusiwe zile nyavu kwa sababu ya kwenda kuvua kwenye maeneo ya maji mengi. Kwenye maji madogo watazuiwa na mimi nipo na ninakwambia Mheshimiwa mimi ni mwana mazingira mzuri sana. Nilikosa kura za kijiji cha Jibondo kwa kuwaambia kwamba msiende kuugusa mwamba wa Kitutia kwa sababu ndio mahali wanapozaliwa samaki na sikuwaruhusu jamaa zangu na wakaninyima kura na nikawaambia hewala lakini nikakataa kuwaongopea, lakini mimi ni mvuvi, taaluma yangu ni uvuvi ninafahamu vizuri sana. *9Makofi)*

Kwa hiyo, ninaomba unisikie na ukimaliza tu hapa naomba haraka iwezekanavyo twende. Wavuvi wa Mafia hivi leo wananisikia na wanasema Jumanne, Jumatatu jioni utoe kauli ya lini unakwenda Mafia, haraka iwezekanavyo kwa sababu hali ni mbaya sana na hivi wanajeshi wamefika Mafia, leo wamekamata na wameshakamata mashine moja katika kijiji cha Tumbuju. Naomba Mheshimiwa waruhusiwe warudishiwe zile nyavu na vifaa vyao. Utakataa sawa, lakini hata ukikataa tunaleta, yaani sijui niseme nini? Kwa sababu nikisema siungi mkono, mimi mwenyewe ni mjumbe wa Kamati na ninaona haya, lakini nitaunga mkono kwa shingo upande lakini ninachosema naomba, uharibifu wote wa mazingira unaanzia Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mna ubavu anzeni kukamata feri pale nyavu zote, mabomu yote, sumu zote, zinaanzia Dar es Salaam, acheni kuwaonea watu wa visiwa vya Mafia, Ukerewe, Koma, Kwale, Songosongo na vingine, sisi ndio shamba letu, uvuvi bahari ndio shamba letu nakuomba sana Mheshimiwa utusaidie katika hilo. Wavuvi waruhusiwe kwenda kuvua katika maeneo ya maji mengi kwa nyavu zile haziharibu mazingira. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini meli zile katika *EZ* tunasema zinavua *deep sea?* Kwani wanavulia nini? Si manyavu hayo hayo ya *trolling,* hawavui kwa nyavu za nchi tatu, wanavua kwa nyavu ya chini ya robo nchi, mimi nimeshaziona. Kamba huwezi ukamnasa kwenye tundu kama hili ninalokuonesha, kamba unamnasa kwenye tundu la nchi kasoro robo au robo nchi, sasa tunafahamu zuia meli zote tuwasaide wananchi sasa na nchi hii haiwezi kuangamia kwa kukosa pesa za wale wenye meli ambao wanakuja kwanza kutoa takwimu za uongo, wanavua tani 10 wanakwambia wewe tani moja. Wewe

mwenyewe shahidi na ulituambia pale *mission to sea men* vitendo wanavyovifanya, sasa zuia zote. Bahari yote wawezeshe Watanzania hasa wavuvi wa Ukanda wa Pwani, Unguja na Pemba, wananchi wa Tanzania waweze kufaidika na ninakwambia tunajitengenezea mazingira magumu ya baadaye, tusaidie. Kila mtu anatetea ugali wake na mimi natetea ugali wangu hapa, sasa wote tumeingia kwa siasa hatukuingia kwa utaalamu hapa. Kwa hivyo, kama wewe umesifiwa sana, bahati nzuri hata Mheshimiwa Lucas Selelii, alifurahi sana kwamba sekta hii sasa imepata watoto wa wafugaji, sasa mimi nikaleta shaka, ina maana uvuvi hili jina Magufuli ndio kaja kutupiga kufuli huku Pwani? Sasa hili naomba sana Mheshimiwa kwa heshima zote, na kuheshimu Mzee wangu, kaka yangu Wanyancha. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Mheshimiwa ongea na Mwenyekiti.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, kwa kupitia kwako kwamba mpiganaji wake ni Dokta Wanyancha, anajua jinsi tulivyohangaika katika kumpeleka kule *AU.* Sasa naomba sana kwa heshima hii wavuvi wangu wa wilaya ya Mafia na Ukanda mzima pamoja na Ukerewe kabla sijasimama hapa nilikuwa nje, nimeongea na mama Mongella, nikamwambia hivyo niambie wavuvi wako leo wakiambiwa wasivue watafanya nini? Akasema ni bora wachukue sumu waikoroge waje kutupa kwenye visima tufe basi wao waendelee, huko waendelee kufuga sisi wavuvi wote tufe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nakuomba kwa heshima yako uwapigie simu Serikali ya Mafia wale wavuvi waendelee kuvua wakati leo jamani Mafia kuna dhiki, dhiki imeingia watu hawajui udokozi. Mtu wa Mafia alikuwa hajui neno polisi lakini juzi nasikia walikuwa na magongo wanataka kupigana na polisi, ni miaka mingapi toka Mungu kaumba dunia, kwa nini leo mtu wa Mafia ndio anajua kukamata jiwe? Tena anamlengeshea polisi anamwambia nitakupiga jiwe, kitu ambacho hakijawahi kutokea, mtu wa Mafia ukimwambia nitakupeleka polisi, mpaka kiama huongei nae. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana kwa heshima zote wavuvi wale wote waruhusiwe kuvua kwa kipindi maalumu wakati tunasubiri mbadala wa wale ambao mtakwenda kuwapa, bila ya hivyo Mafia kutakuwa hakuna kitoweo, Mafia kuna dhiki, watu watakuwa hawawezi kula, tutakabana au twende basi kwa kuwa mna ofisi ya Serikali, tuwaambie wananchi waende kwa *DC* wale wavuvi wote wakakae pale na familia zao waende wakale kwa sababu bila ya hivyo hakuna kinachoendelea. Riziki yetu inapatikana baharini Mheshimiwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sina mengi ya kusema isipokuwa hayo tu. Kwa hiyo, ninachokuambieni ni kwamba suala la mazingira tutajitahidi kutunza lakini wenzetu huku mlima mnaharibu zaidi mazingira kuliko sisi na nawaambieni wapiga bomu wanatoka Dar es Salaam. Na nyavu zote kama tunataka kuanza *operation* hiyo tuanze madukani twende feri, jeshi limetoka hapa, makao yake makuu yako hapa feri Kigamboni, wanakwenda Mafia kufanya nini? Wakati boti ziko pale pale si nendeni mkawakamate pale, wakamateni pale choma moto hakuna atakayekuja. Na wavuvi kwa uchache

tuliokuwa nao Mafia, hatuwezi kuharibu mazingira, bahari yetu imevamiwa na watu kutoka nje ya Mafia au tuseme kuanzia leo ni marufuku mtu yeyote wa kutoka nje ya wilaya ya Mafia kuja kuvua Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono lakini roho inaniuma. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Toka nimepata akili uvuvi ulikuwa thamani yake kama chumvi, anayepika biriyani, pilau, ukitoa ugali chakula cha wenzetu hawa, bila chumvi chakula hakiliki. Lakini thamani ya chumvi dukani ndogo na ikija mle ndani kukaa kwake jikoni, mende haitaki, haisifiwi labda ikiongezeka ndio inapigiwa kelele. Uvuvi ulikuwa maliasili hata kwenye jina la Wizara, uvuvi ulikuwa hautambuliki, leo kuna Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali walau uvuvi kwa mara ya kwanza kutokea katika jina la Wizara, lakini naishukuru vile vile Serikali kwamba imetuwekea mtu anaitwa Pombe Magufuli, ni mchapakazi kweli kweli lakini ni msikivu, akiambiwa anasikia. Na kwa hapa inabidi aongeze kusikia kwenye sehemu ya uvuvi kwa sababu nina uhakika hana utaalamu wa bahari na kwa bahati mbaya waliomzunguka vile vile nao hawana utaalamu wa bahari, kwa hivyo wadau wenyewe wavuvi ndio sisi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi ukiwa wa kisasa sisi watu wa mwambao, wenzetu wanaozungukwa na Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria, tutabadilika. Badala ya huu utani unaokuja uvuvi mkaita uvivu, hayo yote yatakwisha vile vile lakini tunahitaji uvuvi wa kisasa. Nendeni katika Jimbo la Mchinga, nusu ya wakazi wa Jimbo la Mchinga ni wavuvi na wanaishi kwa kutegemea uvuvi. Ukianza kijiji cha Mbanja, Mamburu, Kikwetu, Masasi ya Leo, Likong'o, Mto Mkavu, Mchinga, Ruvu, Kilolambwani, Maloo, Mvuleni, Kijiweni, watu wote hao wanaishi kwa uvuvi. Hakuna hata mtu mmoja hapo Wizarani anayevijua vijiji hivyo, labda Mchinga kwa jina kwa sababu ni Makao Makuu ya Jimbo. Basi katika hali hiyo siwezi kuitegemea Wizara kutusaidia wananchi wa Jimbo la Mchinga katika sekta hii ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiit, lakini ukienda katika Tarafa ya Milola kuna bwawa pale la Rutamba, bwawa la maji baridi na bwawa la maji ya chumvi, na wao wanaishi kwa uvuvi. Toka nimeingia Ubunge hiki ni kipindi changu cha tatu, sijawahi kusoma kwenye kitabu chochote kinachozungumzia sekta ya uvuvi wakataja vijiji hivyo. Sasa kuunga mkono kwa sababu tu ya urafiki wangu na Mheshimiwa John Magufuli, ninaunga mkono na unyonge kweli kweli na ukifanya kitu kwa unyonge hata kama ni kusaidia mtu maskini hupati thawabu kwa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baharini kama Serikali imedhamiria kuondosha umaskini kwa mvuvi ni jambo rahisi zaidi, maana sisi hatuna ukame kule, sisi hatuhitaji malambo baharini, sisi hatuhitaji majosho, sisi hatuhitaji dawa za kupiga sindano samaki, sisi baharini hatuna ukame, naona katika waraka huu ulioandikwa na rafiki yangu Mkurugenzi anazungumzia kuwepo jangwa baharini, bila shaka amekusudia kuisha kwa samaki. Sisi kule hatuna ukame kabisa sisi tuna mabadiliko ya pepo tu, Kaskazi, Kusi,

Maleleji, Umande, Matlai, Mwanashanga na kila ikitokea mabadiliko hayo tunahama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ndio maana utamkuta Mpemba anakuja kuweka dago Mchinga, ujue kule Kaskazi amepamba moto. Utamkuta Mmachinga kule anakwenda kuweka dago Mtambwe, kwa sababu kule Kusi amepamba moto, ndio kazi yetu kwa hiyo, sisi mkiongeza nguvu kidogo tu umaskini kwa watu wa Mwambao umekwisha. *(Makofi)*

Mimi nakushangaeni sana mnang'ang'ania kuweka viwanda kule Ziwa Victoria kule samaki wenyewe hamna wanakwisha. Sasa kule wakiisha mnapiga marufuku nyavu mnapiga marufuku na Mchinga, inahusu nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi unapoandika waraka unasema kuanzia leo ni marufuku mvuvi kutumia miwani, chupa ya gesi, viatu vya kuogelea, unataka mimi nikiingia mle ndani papa aje aone nyayo zangu kwa mbali papa aje anitafune. Katika waraka Mkurugenzi anasema ni marufuku kwenda na mtaimbo kwa sababu unavunja matumbawe wakati nyavu zikinasa, sio kazi ya mtaimbo hiyo, mie nimchokoe pweza, namchokoaje bila mchokoo? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikae kwenye chombo mle kwenye ngalawa halafu unasema kaka pweza njoo nikakutafune, inawezekana kweli? Wenzetu mnaweza kumuita ng'ombe kwa jina, Linda, akaja pweza humuiti akaja, hata kidogo. Kwa hiyo, wewe unapochukulia tu kwamba mtaimbo unavunja tumbawe basi unaona ni zana haramu kabisa mvuvi kuwanayo, unakosea na tunakusamehe kwa sababu tunajua Mkurugenzi huijui bahari. Kwa hiyo, tunaomba kabla hamjaandika nyaraka za kutisha kama hizi muwasiliane na sisi wadau tuwaelekezeni. Leo unaposema mvuvi basi ni mshipi ndio halali, jarife halali, wando na dema, enhee, mie leo nikitaka kumvua dagaa namvua na jarife? Mshipi, dagaa hali mshipi. Nikitaka kuvua tonge kwa tonge, nakwenda kuchukua jarife? Mtihani mkubwa sana, sasa mimi nasema aliyegawa mamlaka haya hakukosea kwa sababu amefuata utaalamu wenu, lakini na wewe mwenyewe ujijue basi, kwamba mimi hili silijui uende kwa wanaolijua, kosa liko wapi? Ndio moja ya faida ya kusoma ni kutambua hili silifahamu nikamuulize anayefahamu ndio usomi. Tutamsaidia vizuri sana ndugu yetu Waziri Magufuli, kwa sababu yeye akishapata uhakika anakuwa hana wasiwasi. Lakini hii, mimi nafikiri huu waraka umeandikwa hakupata ushauri wa kutosha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu bwana mifugo akienda kule amevalia na yale majoho yake wanajua wanakwenda kupata ushauri. Sisi watu wa mwambao tukiona bwana samaki anakuja ufukweni tunajiandaa kwenda kupiga mbizi baharini kukimbia, maana tunajua kinachokuja hapo sio heri kwetu ni shari. Tuje tupigiwe mashoka mamitumbwi yetu, tuje tutiwe kamba tupelekwe Mahakamani, yaani ukimsikia tu anakuja mtaalamu wa uvuvi, au anakuja kutoza ushuru au kukamata nyavu atie moto. Sasa hata kama baba ukiwa mkali namna hiyo nyumbani mwako, utaogopwa tu hupendwi. Na sisi Serikali hii ya awamu ya nne tusingependa wataalamu wetu waogopwe na wananchi, tunataka wapendwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema hapa watu wanatuangalia tu na ushauri atakaopewa Waziri, katika kutujibu Jumatatu, kitakuwa ni kiama cha ajabu sana kwamba

sie tunaojua bahari tutakuwa tumekosea, wao wasiojua bahari wanaosoma vitabuni na kutuchorea picha kwenye kitabu, hiki ni kiti cha pweza nani amekwambia pweza anakaa ana makaadi ya kukalia huyu? Watakuja watufuje sisi, lakini jamani sisi ni sehemu ya Watanzania. Sisi watu wa mwambao ni wapiga kura wa nchi hii, mnatugeuza kama Lepido wa Julius Ceasar kule Urumi na mimi hapa ningependa kumnukuu Antonio alivyokuwa anamponda Lepido, anasema; "Tungempa mtu huyu utukufu wote huu ili kujipunguzia mzigo wa malawama ataubeba kama punda anavyobeba dhahabu, akilalama na kutoka jasho kwa uzito wake. Akiongozwa na kuswagwa vile tutavyomuonesha na mara tu afikishapo amana tupapendapo, tutamtua mzigo wake na kumuachilia sawa na punda mtupu atikise masikio, ajiendee mbugani akale majani yake."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wavuvi hatutatikisa masikio kwa sababu sio punda, hatutakwenda mbugani kula majani kwa sababu tunacho chakula chetu, samaki. Ndugu yangu Ole Telele hapa wakati anasoma taarifa ya Kamati, alikuwa anashangaa kuona eti kuna watu wanamaliza mwaka wanakula kilo 10 tu ya nyama, ndio mazoea kwa sababu kwake yeye protini ni nyama tu, hajui kwamba kwenye pweza kuna protini kubwa zaidi, hajui kwenye ngisi kuna protini kubwa kabisa na kumbadilisha mtu tabia ni kazi ngumu sana. Wanasema ni rahisi zaidi kumkamata mtu kidole kuliko kumbadilisha mtu tabia. Na haya ni maneno ya waarabu; *"Kuswab'a wala tuhalifu tub'a,"* ni rahisi sana kumkata mtu kidole kuliko kumbadilisha tabia yake. Jamani sisi tuna protini zetu kule, sasa tusikie huyo anayesema tutafunga baadhi ya maeneo ya uvuvi, msije bwana, msije kabisa kufunga, mtatufunga na siye wawakilishi wa watu, maana hatutakubali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji. Sisi jamani Lindi kule tumewapokea watu mliowakimbiza huku, mimi Jimboni kwangu pale Mji Mwema, ninao pale akina Mabina. Yuko mzee wao pale anaitwa mzee Mkelemi, sisi hatuna ugomvi na ng'ombe, sisi hatuna ugomvi na wafugaji, kaka yangu Lekule, sisi ugomvi wetu wachungaji. Wanaotaka kuchunga ng'ombe wabaki huku huku wachunge ng'ombe wao, anayetaka kuja Lindi aje kuwa mfugaji, kwamba eneo hili linatosha ng'ombe 100 uwe na ng'ombe 100, lakini ukiwa unaongeza unaongeza tu unatudhiki sisi. Sisi hatuna ugomvi kabisa na wafugaji waje wafugaji lakini wasije wachungaji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa mwenyekiti, nimeangalia kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri hapa ukurasa wa 121, vituo vyake vya utafiti wa mifugo, kule Kusini kipo Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimjulishe Mheshimiwa Waziri kwamba wale ng'ombe waliotoka Ihefu hakuna hata mmoja aliyekwenda katika Wilaya yoyote ya Mtwara, wote wamekuja Mkoa wa Lindi. Sasa safari hii muache ule *Mtwaraism,* ule ugonjwa wa Mtwara Mtwara, hamishieni kile kituo kije Lindi ili kiwasaidie wale watu wawe wafugaji wasiwe wachungaji. Tunavumilia mengi kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatuna ugomvi na wafugaji. Tulikuwa hatujaona mtu akifa ng'ombe wanatolewa kwenye zizi, pale katikati panachimbwa shimo anawekewa na kigoda anakaa pale anafukiwa halafu ng'ombe anarudishwa. Lakini hatujapiga kelele sisi kwa sababu tunaona huo ndiyo utaratibu wenyewe sisi wote Watanzania. Kwa hiyo, tunaomba tafadhali waje wafugaji na ufugaji uwe wa kisasa, mtuletee watalaamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda wangu umekwisha, lakini naomba kurudia tu. Uvuvi usipigwe marufuku, zana zisionekane mbaya, ubaya uonekane katika matumizi. Kisu ni kizuri akiwa nacho muungwana, lakini kisu akipewa mwendawazimu ni kibaya. Mtaimbo ni mzuri kama mchokoo wa pweza, akipewa mvunjaji wa matumbawe ndiyo ukamate na sisi tutakusaidieni mkipenda. Wafugaji tunaomba muwalete watu, lakini waje wawe wafugaji na mifugo, wapunguze. Sisi mashamba yetu hatupunguzi kule na ukija na wafugaji wako kama umepewa eneo la kufugia ng'ombe basi fuga ng'ombe mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa hivyo hivyo tena. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI – MHE. JOB Y. NDUGAI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, japo sina hakika na Kiswahili chako kama mtani wangu Magufuli amekuelewa, masuala ya jarife, ngisi, pweza na mchokoo. *(Kicheko)*

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila na atafuatiwa na Mheshimira Felister A. Bura.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Wizara muhimu sana kama tunavyozungumzia habari ya Kilimo, tunapoingia katika Wizara hii, tunazungumzia masuala ya msingi ambayo yanawagusa Watanzania, hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri awe msikivu na atusaidie sana katika Mikoa yetu ambayo tunazungumza mambo ambayo yanatokea hasa kwa mifugo na uvuvi.

Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri Magufuli, mtani wangu, kaka yangu ambaye ni makini sana na ni msikivu kwa wale watu wanaompa ushauri. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. James Wanyancha, Katibu Mkuu pamoja na wataalamu wote waliopo katika Wizara hii mpya. Wameanza vizuri lakini Wizara ina matatizo mengi sana, tunaomba wawe wasikivu kwa Wabunge na wananchi wanavyolalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naanza na mifugo. Mkoa wa Rukwa ni Mkoa ambao kwa asili tumekuwa na ufugaji wa wastani. Tumekuwa tukifuga ng'ombe wa aina ya Zebu ambao wanahimili sana magonjwa na wanafaa katika mazingira yale, lakini walikuwa sio ng'ombe wengi. Wanyama hawa wametusidia kwa namna mbalimbali. Kwa taarifa yako Mkoa wa Rukwa ndiyo Mkoa ambao wananchi wake wanatumia wanyama kazi hasa ng'ombe kwa kilimo kwa 78%, nadhani tumeshavuka kiwango hicho, tunaelekea kiwango labda pengine 80%. Asilimia 78 wanatumia ng'ombe kwa kilimo, ni ng'ombe wale wa Zebu ambao wana umbo kubwa na wanahimili maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaomba majosho ili waweze kuogesha mifugo yao na madawa ili waweze kutibu mifugo yao pia. Suala hili kama Wizara ya Kilimo inatoa mbolea ya ruzuku, tunaomba na Wizara hii ifikirie jinsi ya kutoa madawa ya kuogesha mifugo ya ruzuku pamoja na madawa ya kutibu wanyama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka ya hivi karibuni, kama miaka 20 iliyopita Mkoa wa Rukwa umepata wageni wanachunga na wanaohama kutoka Mikoa yao kuja katika Mkoa huu ili kufuata malisho. Jambo lililojitokeza, ndugu zangu hawa wamekuja na mifugo mingi sana. Akija kuomba nafasi ya kuleta mifugo 50, mkimpa tu kibali cha kuleta mifugo ng'ombe 50, baada ya mwaka mmoja ana ng'ombe 5,000 halafu ukimwuliza hawa wanatoka wapi? Anakwambia hawa wamezaliwa hapa hapa. Lakini kila usiku ng'ombe wanaongezeka. Hii ni hatari!

Sasa Mkoa wa Rukwa *caring capacity* au uwezo wa malisho ya mifugo umekwisha. Sasa nchi hii inaanza kugeuka jangwa kama ilivyo Shinyanga na Mwanza. Tunaomba sasa Mheshimiwa Waziri atumie busara yake na uwezo wake atunusuru kwa sababu Mkoa wa Rukwa ni Mkoa wa wakulima, hatutaki kugombana na hawa watu kwa sababu hatukuwaleta, wao walikuja wamedanganya na wanatumia fedha kuwahonga watu mbalimbali ili waweze kupata vibali vya kukaa katika maeneo.

Wananunua maeneo hata ya vijiji wakijua kabisa eneo hili ni la kijiji, wanamshawishi mtu anawauzia eneo ambalo wanajua halitoshi, lakini analeta mifugo mingi anakuja kuharibu. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mifugo achukue hatua zinazostahili ili wasiwe ni watu wanaozunguka na mifugo sehemu zote za nchi hii ya Tanzania. Wawe ni watu wanaotumia ufugaji wa kisasa, kuwa na maeneo maalumu kwa ajili ya mifugo yao. La sivyo, nchi hii itaanza kupata njaa ambayo haijawahi kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni eneo la Ihefu. Tunazungumza habari ya Ihefu kwa sababu ni suala ambalo Serikali imechukua hatua, lakini nenda katika bonde la Ziwa Rukwa, jamani inasikitisha na lile ziwa sasa limeanza kupoteza kina chake kwa sababu mifugo wamekuwa wengi sana katika bonde lile, wanaharibu ardhi, sasa mvua ikija inasomba udongo inaingiza katika ziwa. Ziwa lile linaanza kupoteza kina chake na ni hatari siku moja tukasikia kwamba ziwa lile limekauka, nani watakuwa wamesababisha ziwa lile likauke? Mimi sina jawabu isipokuwa Mheshimiwa Waziri ndiye atakayeweza kutoa jibu hilo.

Hivyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri tusaidie watu wafuge kama unavyoeleza, siyo kuchunga kama wanavyofanya ndugu zangu hawa wafugaji waliopo ambao wamekuja katika Mkoa, ni wakatili kwa wenyeji, wanalisha kwenye mashamba yao na akilisha anasema mtanifanya nini? Mkienda Polisi nitakwenda kuwahonga, mkifanya hivi nitahakikisha nawashinda. Sasa anatumia kule kuogopa kwenda Polisi kushtaki kuwanyanyasa wananchi katika maeneo yetu. Kwa kweli jambo hili halikubaliki.

Tatizo lingine ambalo limeanza kujitokeza, mito, vijito na chemichemi zimeanza kukauka, mito tunayokuwa nayo si mikubwa sana, mvua zikikatika maji yote

yanakwenda ziwani kwa sababu hatuna mabwawa. Sasa ng'ombe wale wakienda katika mabwawa haya kwa makundi ya maelfu kwa maelfu maji yanazidi kupungua na kupungua, vijito vinakauka, chemichemi zinaziba. Wewe fikiria katika eneo ambalo kuna chemichemi ng'ombe 3,000 wanakuja kukanyagakanyaga pale, chemichemi zote zinaziba halafu sasa pale panakuwa ni mahali kame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, anaelewa kilio chetu kwa sababu sisi Mkoa wa Rukwa ni wa kilimo, hivyo tunamwomba sana aje atusaidie tuweze kuona ni jinsi gani ya kutatua tatizo hili. Wapunguze mifugo au wahame wakatafute sehemu nyingine kwa sababu sisi hatukuwaalika waje kuanza kutuletea migogoro na tunajaribu kufanya maelewano tuzungumze ili tuweze kukubaliana lakini ni watu ambao wanavunja Kanuni na Sheria mara kwa mara.

Tunakuomba sana suala hili lizingatiwe tusaidiwe tuweze kuondokana na tatizo hili ili tuendelee kulima chakula kitakachokwenda kuwanusuru watu wasiokuwa na chakula kingi katika Mikoa ya Shinyanga, Tabora, Singida na sehemu nyingine. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la uvuvi. Jimbo langu la Kalambo linapakana na Ziwa Tanganyika upande wa Magharibi, ninavyo vijiji saba. Kijiji cha Kipwa ni kijiji ambacho kipo mpakani kabisa kipo mahali ambapo Mto Kalambo unapoingilia katika Ziwa Tanganyika na sehemu hiyo ndipo mpaka wa Zambia na Tanzania unapoingilia, mpaka katika korongo lile la Maanguko ya Kalambo *(Falls).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo Kijiji cha Kapele na kipo Kijiji cha Kilewani. Vijiji hivi vipo karibu na Zambia sana, uvuvi wote unaofanyika katika vijiji hivi, samaki wanakwenda kuuzwa katika nchi ya Zambia kwa sababu hakuna namna yoyote ya kuwaleta samaki katika masoko ya Kasanga, Matai na Sumbawanga au sehemu nyingine kwa sababu ya usafiri mgumu. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri uangalie ni jinsi gani ya kuanzisha soko kubwa la samaki katika kijiji cha Kasanga, kuanzisha mitambo ya kusindika samaki pale, tuwatafute wawekezaji ili waje watusaidie samaki hawa ambao wanapelekwa Zambia kwenda kuuzwa kwa bei ya kutupa halafu hawalipi ushuru wowote kwa nchi yetu. Hii ni hasara kubwa sana, tunapoteza fedha na ushuru mwingi ambao Serikali ingeweza kupata kuendesha Serikali yake.

Vipo vijiji vya Kasanga, Muzi, Kipanga na Samazi, vijiji vyote hivi vinajishughulisha na uvuvi, lakini angalia zana zinazotumika ni zana duni sana. Angalia soko lao wanapeleka mazao yao haya wapi? Wanapeleka nchi ya Zambia na Congo. Mheshimiwa Waziri nimeshalalamika kwa kipindi cha miaka saba kwamba samaki wanaovuliwa katika Ziwa Tanganyika upande wa Tanzania wanapelekwa katika nchi ya Burundi, Zambia na Congo. Nchi ya Tanzania hatupati chochote kwa sababu kwanza hata nikikuuliza Mheshimiwa Waziri hivi unafahamu ni kiasi gani cha samaki wanaovuliwa katika upande wa Tanzania na kupelekewa katika nchi hizi za Zambia na Congo? Hakuna takwimu kwa sababu hatuna wataalamu wanaofuatilia, hatuna *patrol boats*.

Ninachoomba, Wizara hii itusaidie tupate wawekezaji ili tuanze kusindika samaki kama ilivyo katika ziwa Victoria, viwanda ambavyo vitasindika samaki wa aina mbalimbali. Tunao Migebuka samaki watamu sana, tunao dagaa na samaki wengine wengi sana katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziwa hili halijawa *polluted*, halijapata uchavu wa miji mikubwa, kumbe maji yake ni safi na samaki wake ni salama na wanaweza kuuzwa katika nchi za Ulaya, itakuwa ni rahisi kabisa, mimi nina uhakika na samaki hawa wanachukuliwa kwa njia mbalimbali mpaka wanafika katika nchi ya Ubelgiji na Ufaransa ambapo kuna wakongo wengi na watu wa nchi za Magharibi ambao wanatumia samaki kutoka Ziwa Tanganyika. Lakini sisi wenyewe Watanzania tunaovua samaki kwa wingi na ambao tuna *portion* kubwa ya ziwa hatufaidiki na uchumi wa ziwa hili.

Tunamwomba Mheshimiwa Waziri kuanzia sasa aanze kuangalia ni jinsi gani atakavyotusaidia tuwe na viwanda vya kutosha vya samaki katika Mji wa Kigoma, Karema, Kipili na Mji wa Kasanga. Tupate umeme ufike katika sehemu hizi ili samaki wasindikwe na tuuze katika masoko ya nje ili tuweze kuwanusuru wananchi katika maeneo haya ambao wanavua kwa zana duni na hawana soko la uhakika kwa samaki wao isipokuwa kupeleka Zambia ambako wananyanyaswa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nina uhakika Mheshimiwa Waziri amenisikia, amesikia kilio cha wananchi wa Jimbo la Kalambo na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla nina uhakika atafanya lolote ili kutusaidia kuondokana na matatizo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja nikitarajia kwamba atasikiliza haya ya wavuvi, lakini pia afikirie kutujengea mabwawa na majosho ya kutosha kwa mifugo yetu kwa sababu sasa maji yameanza kuwa shida. Ukienda katika Wilaya ya Nkansi kuna matatizo makubwa sana ya maji kwa sababu wafugaji wamejazana sana, lakini hakuna miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Ludovick Mwananzila. Kama nilivyosema mwanzo, Mheshimiwa Felister A. Bura ndiye atakayefuata na ajiandae Prof. Idris A. Mtulia ambaye simwoni kama atakuwa hajafika, basi Mheshimiwa Kaika Telele ajiandae. Mheshimiwa Felister A. Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Lakini kabla sijachangia, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ambayo ameshaonyesha kuifanya na niungane na Wabunge wenzangu kwamba Mheshimiwa John Magufuli alipokuwa Wizara ya Miundombinu alionyesha utendaji mzuri sana wa kazi na aliweza kutambua barabara zote za nchi hii kichwani na fedha zinazotakiwa kutengeneza barabara hizo na kwa sababu Mheshimiwa Rais ameona kwamba wavuvi na wafugaji wana matatizo, tunaamini kabisa kwamba kuletwa kwake

katika Wizara hii, wavuvi na wafugaji watapata nafuu na matatizo yatapungua katika Wizara hii ya Uvuvi na Mifugo.

Nampongeze pia Mheshimiwa Dr. James Wanyancha kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri na pia naamini kwamba ni mchapakazi mzuri na kwa sababu na yeye ni mtoto wa mfugaji na yeye mwenyewe ni mfugaji, naamini Wizara hii itafanya kazi nzuri na malalamiko yote ambayo tunayasikia leo kwa Waheshimiwa Wabunge kuna wakati tutasimama kwa kupongeza tu kwa kazi nzuri ambayo imefanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 65 amesema kwamba katika mwaka 2007/2008 Serikali ilipata shilingi bilioni 1.8 kwa kuuza mifugo, yaani ng'ombe 2,772, mbuzi na kondoo 874 nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufugaji tulionao Watanzania Mikoa karibu sita wanafuga na sasa Lindi kuna wafugaji na hata Rukwa, ni Mikoa zaidi ya kumi kuna wafugaji. Lakini pato la Taifa tulilolipata kwa mwaka jana ni shilingi bilioni 1.8. Ni kiasi kidogo sana, yaani kiasi kidogo sana! Hii inadhihirisha jinsi ambavyo Serikali haijafanya juhudi kubwa kutafuta masoko nje ya nchi kwa ajili ya wafugaji na mimi naamini kabisa wafugaji wana uwezo sana au mifugo ina uwezo mkubwa wa kuendeleza nchi yetu, yaani kuongeza pato la Taifa. Lakini hatujatumia mifugo yetu ipasavyo, nadhani sasa ufike wakati ambapo tuone namna ya kutafuta soko nje ya nchi na pato la Taifa liongezeke kutokana na mifugo tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika mwaka huo wa fedha uliopita Serikali iliuza tani 195 nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo na tukapata shilingi milioni 500 tu kwa mwaka kwa kuuza nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo nje ya nchi. Hii siyo haki kabisa tunayowatendea wafugaji katika nchi yetu. Nadhani pesa hizi zilizopatikana katika mifugo ni karibu Korosho ya Mkoa wa Mtwara tu. Korosho ya Mkoa wa Mtwara tu ingeweza kuleta zaidi ya shilingi bilioni 1.8 ambayo imepatikana kwenye mifugo. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie namna ya kutafuta masoko kwa ajili ya mifugo yetu kwa sababu Tanzania ni nchi ya tatu katika Afrika kwa ufugaji, lakini mifugo haijamwendeleza Mtanzania, haijamsaidia Mtanzania. Mimi ni mfugaji na ni mtoto wa mfugaji. Sitauongelea uvuvi kwa sababu sijawahi kuvua tangu nizaliwe.

Lakini katika huo ukurasa wa 65 Mheshimiwa Waziri hajaeleza kwamba wale wanaofuga kuku wameleta nini katika nchi yetu, kwa sababu tunao wafugaji wa Kuku Singida, akina Killimbah ni wafugaji wazuri sana wa kuku Mkoani Singida na kila siku treni ikipita pale kuna wanaonunua kuku, kuna wanaokula pia, lakini hatujaambiwa wafugaji wa Kuku wameliingizia Taifa hili kiasi gani cha pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposoma, pia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Waziri anasema katika ukurasa wa 90 kwamba madume na mbuzi 60 kutoka Mpwapwa katika Chuo cha Utafiti Mpwapwa wamegawanywa katika vijiji mbalimbali, lakini Mheshimiwa Waziri ametufumba, hakusema ni vijiji gani. Je, tuamini kwamba umegawa tu katika vijiji bila kusema ni vijiji gani au Mikoa gani? Tutaamini vipi kama madume

hawa umegawanya? Je, kituo hiki ni kikubwa na ni cha muda mrefu? Nilitegemea kwamba angepata madume zaidi ya 90 kwa mwaka. 90 kwa mwaka ni kiasi kidogo sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, umesikia Wabunge wengi wanalalamika kwamba wafugaji ni wachungaji, hawafugi, kwa sababu madume 90 tu wanagawa kwa mwaka, hivi tukigawa madume 90 kwa mwaka tuje tumalize Mikoa zaidi ya 10 Tanzania kuwagawie madume, tutamaliza mwaka gani? Nadhani ni wakati mzuri sasa Wizara iangalie upya namna ya kugawa madume hayo na kuyazalisha kwa wingi zaidi.

Lakini pia Mheshimiwa Waziri amesema kwamba anasambaza teknolojia ya uzalishaji na usindikaji na uhifadhi wa mazao ya mifugo, lakini hakutuambia ni katika Mikoa gani, hakutuambia ni katika Wilaya zipi na vijiji gani. Inawezekana akapeleka teknolojia hii katika Mikoa isiyo na mifugo na Mikoa isiyo na mifugo, sidhani kama wanahitaji teknolojia hii na utakaposambaza hiyo taknolojia naamini utawasaidia wafugaji kwa hali ya juu sana. Wananchi wengi wanafuga, lakini anapochinja ng'ombe au mbuzi wake au kondoo wake sana anachofanya ni kula nyama hiyo kwa siku mbili iishe kwa sababu hawajui namna ya kusindika.

Lakini wananchi hao wangejua namna ya kusindika mazao ya mifugo yao wangeuza hata ndani ya nchi. Wenye mazao wanakausha mazao yao wanauza ndani ya nchi, lakini wafugaji hawajui namna ya kusindika mazao yao wakauza ndani ya nchi na wanaweza wakajipatia fedha nyingi tu kwa sababu kuna wafugaji wenye ng'ombe, 1,000 lakini hana namna ya kusindika nyama hajui namna ya kusindika nyama. Lakini atakapofundishwa namna ya kusindika nyama naamini kabisa kwamba watajiendeleza na watapata mahitaji ya muhimu na hata mifugo hiyo tunayosema kwamba ni mingi itapungua kwa sababu watakuwa na teknolojia ya kusindika mazao yanayotokana na nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti Mpwapwa pia Mheshimiwa Waziri amesema kwamba alipata pia madume 85 na kusambaza Iramba, Igunga, Simanjiro na Mvomero, lakini idadi aliyoisema kwa kweli imenisikitisha. Ni kiasi kidogo sana ninaomba Wizara ione namna ya kusambaza madume hayo ili iwasaidie wafugaji walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Dodoma wananchi wengi ni wafugaji na hata Mkoa wa Singida. Lakini Mikoa hii miwili au aidha, ni zaid ya miwili ni Mikoa mikavu, yaani hakuna mvua ya kutosha na kama zikitokea, basi ni za wiki mbili au tatu na baada ya hapo hakuna mvua tena. Kwa hiyo, wanyama wanapata taabu sana na wafugaji pia wanapata taabu sana. Lakini nilipoangalia kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri sikuona maeneo wanayochimba Malambo na hata kule kwenye Wizara ya Maji sikuona wakochimba Malambo ya kutoka kwa ajili ya Mikoa hii yenye ukame. Sasa tunategemea nini? Tunategemea kuwasaidiaje hawa wafugaji? Siku zote watakuwa wachungaji kwa sababu wanatafuta maeneo yenye maji, siku zote watafuta maeneo ya kulisha mifugo yao kwa sababu hakuna malambo majirani, hakuna namna ya kupata maji na wala hakuna namna yoyote ya kusaidia mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Dodoma hakuna wataalamu wa mifugo na kama wapo, basi wapo wachache mno na hao wachache waliopo hawana hata baiskeli, hata toroli ya kusukuma hawana, tunategemea kwamba huyu mtaalamu atakwenda kilomita 80 kwa kutumia usafiri gani? Atamfikiaje mfugaji na amsaidie mfugaji wakati hana hata baiskeli, wala toroli ya kubeba mbolea, hana na bado tunasema tunamsaidia mfugaji, tunahamasisha mfugaji afuge ufugaji wa kisasa?

Huyu mtaalamu anayetegemewa kusaidia yupo mjini, hakuna watalaamu wanaokaa kijijini, atamsaidiaje bila usafiri? Naomba Mheshimiwa Waziri, awasaidie hawa watalaamu wake wapate usafiri na vijijini huko ng'ombe wanalishwa dawa za kienyeji bila vipimo maalumu kwa sababu madawa mpaka uje mjini, mtaalamu yupo mjini utampata wapi huyo mtaalamu akusaidie kumtibu ng'ombe wako? Wananyweshwa miarubaini huko vijijini! Tuwasaidie hawa wataalamu wapate usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majosho Mkoa wa Dodoma ni machache mno. Nikupe mfano mmoja kwamba katika Manispaa ya Dodoma kuna Kata 30 lakini katika Kata 30 kuna majosho 15 tu. Sasa sijui wafugaji wanatakiwa kuchangia majosho au kila kijiji kiwe na josho ili iwasaidie wafugaji katika maeneo husika! Ninaomba Wizara hii iangalie namna ya kuwatibu ng'ombe ama mifugo kwa ujumla. Madawa yenyewe hata tukisema wanunue mjini, ruzuku hawajui ni duka gani Serikali imetoa ruzuku ya madawa ya mifugo, hawajui. Hawa wachache wanaojua ni hawa wanaofuga ng'ombe wa kisasa mjini, yaani hawa wa *Zero Grazing* lakini wanaofuga au wanaochunga hawajui lini wapate dawa ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara iangalie namna ya kuwasaidia wafugaji kwa dawa ya mifugo, majosho, wataalamu na hao wataalamu wapate usafiri.

Mheshimiwa mwenyekiti, katika Mkoa wa Dodoma tuna ng 'ombe wengi sana lakini cha ajabu hatuna hata kiwanda cha kusindika maziwa, acha nyama, tuna machinjio ya kisasa tu, lakini baada ya kumchinja ng'ombe, mbuzi au kondoo hiyo nyama unaihifadhi vipi? Hatuna kiwanda chochote ! Tulikuwa tunategemea kiwanda cha Kawe, kile kiwanda kimekufa ; tunategemea kiwanda cha Shinyanga, kiwanda kile hakijaanza kazi.

Sasa hawa watu jamani, wenzetu wengine wenye mazao wana namna ya kusindika mazao yao lakini wafugaji hawana mpaka waende Arusha, ndiyo kuna kiwanda cha maziwa ; Mwanza kuna kiwanda cha maziwa, Dar es Salaam siyo wafugaji, lakini kuna kiwanda cha maziwa. Kwa nini Serikali isiwahamasishe wawekezaji wakajenga viwanda maeneo ambapo kuna wafugaji kuliko kumbeba ng'ombe kumpeleka Dar es Salaam, Mtwara na hata maeneo yasiyo na mifugo ? Kwa nini Serikali isijenge viwanda maeneo ambayo kuna wafugaji ? Tunategemea na tunasubiri kiwanda cha Shinyanga kianze kazi, sasa sitabidi turudi kinyumenyume kupeleka ng'ombe Shinyanga, kitu cha ajabu kweli kiasi kwamba tungejengewa kiwanda hapa au kwenye ranchi yetu wakaruhusiwa wawekezaji, wakashirikiana na ranchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Ranchi ya Kongwa. Ranchi ya Kongwa pale wakijenga kiwanda cha kusindika nyama na maziwa itawasaidia wafugaji wa Singida, Manyara na itawasaidia wafugaji wa Dodoma. Lakini hatuna kiwanda mpaka cha Kawe na cha Kawe kimekufa sijui kitafufuka mwaka gani, lakini tunaomba basi wafugaji wafikiriwe sasa kupata viwanda vya kusindika mazao ya mifugo, tena mazao ya mifugo kuna ngozi, maziwa, pembe, nyama na hata kwato, yaani mnyama huyo huyo mmoja ana faida chungu nzima. Lakini pamoja na faida zinazoonekana kwa mnyama huyo, bado mfugaji huyu hajathaminiwa akapata nyenzo za kumsaidia kupata dawa na msaada kutoka kwa Serikali. Ninaiomba Serikali iangalie hayo.

Mheshimiwa mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Felister Aloyce Bura. Nimemwona Profesa Idris Mtulia akiingia humu ndani, baada yake kuzungumza, atafuata Mheshimiwa Kaika Telele. Mheshimiwa Mtulia karibu.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kidogo. Watu wanashangaa hapa eti kwani Rufiji kuna ng’ombe! Jibu ni kwamba Rufiji wapo ng’ombe, tumeletwa ng’ombe. Kwanza, ilikuwa tupate ng’ombe 50,000 lakini sio hao tu, wapo na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hapo, nataka nimshukuru na kumpa hongera Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kutuletea hotuba hii ambayo inatia matumaini, lakini nilikuwa nataka niseme machache, kwamba wananchi wa Rufiji tumedanganywa. Tuliambiwa tutaletewa ng’ombe 50,000, kwa bahati mbaya kabisa sasa wapo kati ya 80,000 na 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyojitokeza ni kwamba, hawa wachunga ng’ombe kwa bahati mbaya sana hawajui majani ya mahindi ndiyo yanayotoa mahindi. Wao majani ni majani tu. Yaliyotokea, naomba niyaeleze ili baadaye tutafute jawabu, nayo ni kwamba, kule Rufiji ni sehemu yenye maji mengi na ardhi yenye rutuba. Kwa hiyo, majani ni mengi. Lakini walivyokuja hawa ndugu zetu wakapokewa, wakapewa sehemu yao ya kuchungia na sehemu nyingine wakapewa wananchi wa Rufiji kwa ajili ya kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya kabisa wakawa wanachunga tu na ndiyo wakaanza kuvuruga mambo. Wametoka katika sehemu waliyopewa, wakaenda katika mashamba ya watu, ng’ombe wakala mazao yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna mambo mengine ya ajabu au fikra mpya ambayo sijaipata kuona toka nimezaliwa. Kumbe wenzetu wakati wa kiangazi wanachoma mbuga ili mvua ikija ioteshe majani mapya. Kwa bahati mbaya kabisa wakachoma mashamba ya mikorosho. Nimetembelea katika vijiji hivyo nilitaka kulia. Huyo mzee hana kitu kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ubishi. Ukiwaeleza ng'ombe wako kala shamba langu la mahindi wanasema hakula mahindi, huyu kala majani tu. Nadhani *we needs to educate them*. Lazima tuwasomeshe kwamba majani ya mahindi ndiyo yanatoa mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la….

**MWENYEKITI:** Lakini Profesa majani si majani, hebu liweke vizuri hilo.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mahindi yakipandwa yanaota majani kabla hajatoa mahindi yenyewe. Sasa wale wachunga ng'ombe hawajali hilo shamba la mahindi, wanalisha wanyama mle ndani. Ukimwambia, anasema hajakula mahindi huyu, amekula majani tu. Hilo ndilo tatizo lililoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukawa na utata na ugomvi. Huyu anasema amekula shamba langu, mchungaji anasema hakula, amekula shamba langu, hakula!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugomvi umetokea Kijiji cha Muhoro, kwa hesabu, watu watatu wameuliwa kwa mishale na mikuki. Kuna kesi moja, mtu alipigwa mkuki sikioni akaenda Polisi, baada ya kujua yeye amekwenda Polisi, wale wachungaji wakamchinja ng'ombe porini, wakambeba na kumweka katika shamba la yule bwana na wao wakaenda Polisi, wakasema huyu ametuibia ng'ombe wetu na kachinja, tumemkuta katika shamba lake. Sasa utakuta mambo haya yanakuwa magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona sasa hivi tumefikia mahali tukubali kwamba, kila ukizidisha wanyama katika ardhi, ardhi inaharibika, haiwezi kuotesha mimea kwa urahisi. Vilevile kwa kuwa hakuna malambo tuliyoahidiwa na Wizara kule Rufiji, hawa jamaa kule kule tunapolima mashamba yetu nao ndiyo wanaleta mifugo yao. Halafu mkulima ambaye shamba lake limefyekwa na ng'ombe, huyu mtu anakuwa maskini, uchumi wake unarudi chini, kwa bahati mbaya watoto wake kusoma itakuwa taabu na halafu huyu jamaa aliyelisha ng'ombe hana habari, yaani *no sympathy at all*. Haonekani kuona kosa limefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunahitaji kuelimisha wafugaji wetu. La kwanza, lingekuwa somo linalohusu idadi ya ng'ombe. Serikali itamke mtu mmoja awe na ng'ombe wangapi, kwa nini wanakuwa na ng'ombe wengi tu na wanaruhusiwa kuharibu ardhi. Kwa hiyo, Serikali iweke angalau kwa uchache mtu mmoja awe na ng'ombe kadhaa kwa sababu kuwa na ng'ombe wengi halafu hawana fedha mfukoni, eti nina utajiri wa ng'ombe wanatembea, ile *idea* ya kizamani. Sasa hii elimu itolewe na Serikali kwa wafugaji, waachane na fikra za zamani za kufuga ng'ombe wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuwe na elimu vilevile ya *existence*. Wakulima na wachungaji ni ndugu waheshimiane, ng'ombe waheshimiwe na mimea iheshimiwe. Likikosekana hili ndiyo unapata matatizo ya ugomvi kati ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, sina hakika wale watoto wanaochunga ng'ombe kule Rufiji kama wanakwenda shule. Hivi kweli Serikali yetu imeshawalaani hawa watoto kwamba wao shule basi! Nilikuwa nadhani hapa inatakiwa Wizara ikubali na Serikali nzima itie nguvu kwamba, watoto wa wachunga ng'ombe nao wasiwe wachunga ng'ombe, wapatiwe shule. Vilevile kupatikane elimu ya afya, maana yake sijui usiku ukifika inakuwaje! Maana yake wale wanatoka misituni tu, itabidi tujitahidi sana kama Serikali kuwasaidia hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hili suala la hivi vifo vinavyotokea. Ikwiriri alikufa mtu mmoja mbele yangu, amepigwa na wachungaji, (wachunga ng'ombe) maana ukisema Mchungaji anakuwa mtu wa Kanisa, nadhani tuseme wachunga ng'ombe. Wachunga ng'ombe walipiga mtu, akafa mikononi mwangu katika hospitali ya Muhimbili kama ndugu yangu, watu wanavyosema, fidia yake ni nini? Nillieta madai haya kwa Wizara ya Mifugo, kwani zile maiti nne nazijua nataka tuombe fidia kwa sababu haya mambo tumeletewa na Serikali, yalikuwa hayapo haya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, kule Rufiji kuna mabwawa ya asili. Kwa bahati mbaya mabwawa hayo yapo katika shamba la bibi, yaani *the Selous Game Reserve*. Mabwawa haya yana samaki wengi, zamani watu walikuwa wanavua katika mabwawa haya, lakini tangu ilipofika *operation* uhai, watu wote walitolewa *Selous* na mabwawa yale mpaka leo yana samaki mpaka wanaruka ruka tu. Sasa naona kabisa kwamba wakati umefika Wizara hii ikubali kuzungumza na Wizara ya Maliasili ili watu wa Rufiji waruhusiwe kuvua samaki katika mabwawa ya *Selous*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo, itakuwa faida kwa wananchi na tutachunga maliasili. Jambo kubwa sana na baya ni kwamba, wale samaki wanaliwa na mamba na mamba akishashiba wale samaki, saa nyingine anatafuta watu. Sasa kuna faida gani kuweka mali ambayo inaliwa na mamba, mamba ambaye hatupi faida moja kwa moja? Nadhani sasa wakati umefika Mheshimiwa Waziri akubali kuongea na Waziri wa Maliasili ili tuweze kuwaruhusu wananchi wa Rufiji waende kuvua hata kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili sio jambo geni, kule *Selous* watu walikuwa wanavua kila baada ya miezi mitatu halafu wanapata leseni tena kila baada ya miezi mitatu. Sasa ile *population* ya samaki ilikuwa endelevu. Sasa hivi unaweza kwenda katika bwawa ukakuta samaki amezeeka anakufa, anaelea. Sasa tunapata faida gani? Kwa hiyo, inabidi tuwaruhusu watu wa Mloka na Ngorongo ambao wananisikia naiambia Serikali, iwaruhusu wakavue katika mabwawa yetu kule *Selous*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka kusisitiza kwamba kuwe na elimu maalumu kwa wafugaji wote ili wajue kwamba, hakuna ruhusa ya mtu kufuga zaidi ya ng'ombe kadhaa kwa ajili ya kuweka ardhi yetu katika hali ya usalama.

Pili, tutaomba sana kwamba, kuwe na elimu ya *existence*, wachunga ng'ombe wajue kuna wakulima na wafanyiane heshima. Wakulima hawana taabu lakini hawa

wenzetu wana mishale, hawa ni *nomadic,* kwa kweli mambo yao ni ugomvi ugomvi sana. Kwa hiyo, nadhani suala la elimu ni muhimu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kusisitiza tena kwamba, hawa watoto wa wafugaji wamepiga laana wasisome? Tutafute namna ya kuwapa elimu na huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Idris Mtulia. Mheshimiwa Michael Lekule Laizer ameniandikia hapa tena kwamba, anataka kuchangia kwa mara ya pili. Sasa nafunuafunua kanuni nione kama inaruhusiwa. Lakini basi tumsikilize Mchungaji ng'ombe, Mheshimiwa Kaika Telele na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed ajiandae.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Nilipokuwa nawasilisha taarifa ya Kamati leo asubuhi, nilishampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanyia Wizara hii na kwa maana hii sina sababu ya kurudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo kwa maana ya ng'ombe wana mahitaji yao. Kwanza kabisa, wana mahitaji ya malisho, maji na ni maji mengi ya kutosha, wana mahitaji ya dawa, chanjo na tiba, chumvi, kupumzika, lakini kubwa zaidi wana mahitaji ya ulinzi kutokana na wanyama wakali na vilevile kutokana na binadamu ambao ni wezi wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea vilevile uondoshaji wa wafugaji katika maeneo yao ya asili. Kama mnataka wafugaji wasiendelee kuhamahama na kuja kwenye Mikoa ambayo wazungumzaji wanasema ni lazima wapunguze mifugo, basi ni vizuri mkarejesha maeneo ya wafugaji ambayo kwa muda mrefu Serikali imeyatoa kwa wawekezaji, imeyatoa kwa mashamba makubwa ya kilimo, hifadhi za Taifa na kama maeneo hayo yatarejeshwa, basi hatuna sababu ya kuja katika Mikoa yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Nangoro leo asubuhi alieleza mambo ambayo yanasukuma mifugo au yanamwondoa mfugaji katika eneo lake la asili. Alizungumzia kilimo na ni kweli, jembe likiingia katika maeneo ya wafugaji watahama tu, wataondoka kwa sababu jembe na mifugo kwa kweli ni vitu viwili tofauti. Lakini vivyo hivyo kwa madini. Serikali ikitoa leseni kwa wachimbaji wakubwa, kwanza ana-*fence* eneo lile na kama lilikuwa ni eneo la wafugaji, hakuna tena kukanyaga eneo lile. La pili, anaondoa wachimbaji wadogo wadogo ambao nao wenyewe hawana tofauti na ng'ombe wanaoondolewa katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Serengeti ambako Serikali sasa hivi inajidai kwamba, Serengeti ni eneo la urithi wa dunia *(it is a world heritage site),* lakini hakuna

anayesema kwamba Serengeti pia ni urithi wa Taifa hili. Urithi wa watu ambao walishaondolewa katika eneo lile! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, afadhali hata Serikali ya kikoloni wakati ule, kwa sababu walipokuwa wanataka kuchukua eneo la Serengeti ambalo ni eneo la wafugaji, walifanya majadiliano na wenyeji na viongozi wa Kimasai kwa zaidi ya miaka kumi. Serikali ya sasa inapotaka kuondoa wafugaji mahali popote, *there is no negotiation*, wala hakuna ushirikishwaji wa aina yoyote. Sasa ipi bora? Serikali ya Kikoloni au Serikali yetu ya sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hao wakoloni walipokuwa wanachukua maeneo yale waliwaonyesha wafugaji maeneo mbadala ya kwenda na sio kuwaonyesha tu, waliwawekea miundombinu kwa maana ya mabwawa, majosho, *veterinary centres* na hawa Wamasai wakaenda kukagua, wakaridhika na maeneo yale na ndiyo wakakubali kuhama kwenda Ngorongoro *Highlands*. Lakini sasa hivi hakuna kitu cha namna hiyo. Kila kitu ni kutoka juu kuteremka chini. Sasa namna hii kwa kweli hata ungekuwa wewe, hushirikishwi lolote unaambiwa tu ondoka, kwa kweli wafugaji watafika mahali watasema, basi na hali itakuwa ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *crater* ya Ngorongoro, ni eneo dogo, lakini zamani Wamasai walikuwa wanaishi kwenye *floor* ya Ngorongoro *Crater*. Ni eneo la kilomita 250 tu. Lakini wakati huo kabla Wamasai kuondolewa pale kulikuwa na faru 200. Sasa Wamasai wameondolewa na jeshi pale, Wasomali wameingia wamemaliza faru pale. Kwa hiyo, wanyamapori na mifugo ni vitu vinavyokwenda pamoja, lakini sasa ninyi mnaanza kuleta utaalam wa mashule, mnaanza kuwatenganisha hawa, wanyamapori na mifugo watakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hata pale *crater* walikoambiwa tokeni kwenye *crater floor* nendeni juu ya *rim*, sasa hivi wanaanza tena kitu kinaitwa *zoning* ambapo sasa wanasema *either side of the crater*, mnakwenda *25 kilometres, we might go back to* Serengeti maana yake mnawa-*push* tu, tunakwenda hivyo. Sasa kwa kweli watafika mahali watasema hapana na liwe litakalokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, wakati wa *immigration* ya nyumbu, *wildebeast and zebras* wanakuja kwa maelfu na mamilioni, *seven million wildebeast and zebras* wana-*cross* Masamara wanaingia Serengeti, wanakuja wanakaa huku, wanazaliana huku, watoto wakishakuwa wakubwa wanarudi, wanakaa miezi sita. Kipindi chote cha mvua wako huko wanamaliza majani, mvua zikikatika, ukame unaingia na wenyewe wanarudi, kwa nini msiwazuie hao? Mnazuia tu mifugo isi-*move* kwa nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Telele nakukumbusha tu kwamba, Mwenyekiti ni Afisa Wanyamapori. *(Kicheko)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Ehe, ndiyo sawa sawa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengine kama nilivyosema wanaochukua maeneo ya wafugaji ni wawekezaji na wanaanzia juu, wanatafuta vibali, wana-*corrupt* sijui nani huko juu, basi wanakuja tu na vibali na yeye kazi yake inakuwa ni kukuonyesha tu kibali, hiki nimeshapewa. Kwa hiyo, huna la kufanya. Sasa kwa kweli hatuna haki na maeneo na ndiyo maana hakuna ushirikishwaji katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimegundua kwamba watu wanatumia elimu duni ya wafugaji kufanya wanayoyafanya. Lakini kama alivyosema Profesa hapa, wafugaji nao wameanza kusoma na sio lazima tuwe wengi mno, hata hao wachache waliopo wanaweza kuwa *pressure group* mambo yakaanza kubadilika katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha pia zinatumika sana kununua maeneo ya wafugaji, lakini laiti basi hata hizo fedha zingetumika, wakanunua maeneo ya wafugaji wakaanzisha *ranches* za mifugo kama ilivyo Kongwa, Ruvu na nyingine za Mkoa wa Kagera labda ingekuwa nafuu, lakini fedha zinatumika wananunua maeneo haya, halafu sisi wanatusukuma kwa kweli tutafika mahali hatutakubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malambo, inaonekana Serikali imeshindwa kuchimba malambo kwa ajili ya mifugo. Naiomba Serikali itoe tamko, wale makandarasi wanaojenga barabara katika maeneo ya wafugaji, wanapochimba *moram* wasifukie mashimo yale ili tuweze kupata maji ya mvua yaweze kusaidia mifugo yetu kwa sababu inaonekana Serikali imeshindwa kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambapo nilizungumzia sana habari ya mifugo, kuna mtu mmoja alinitumia meseji, akaniambia Mheshimiwa Mbunge huna la kusema huko? unazungumzia mifugo, mifugo, imepitwa na wakati! Unatakiwa uzungumzie umeme na barabara ambazo hatuna. Sasa sijajua mpaka sasa kama huyu ni mpiga kura au ni mtu tu ambaye anataka kumkoroga mtu. Lakini Mbunge ni mtu ambaye anakuwa na watu wote hao wanaohitaji umeme, watu wa mifugo na wanaohitaji barabara za lami. Kwa hiyo, kupanga ni kuchagua. Nataka nimfahamu mwananchi huyo ili nimwelimishe, kwamba mifugo haijapitwa na wakati na naomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania isiendelee kuona mifugo kama zao ambalo halina maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na mapungufu ya hapa na pale, lakini hii yote ni kwa sababu Wizara ni mpya. Kwa hiyo, inawezekana kuwe na matatizo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, ni vizuri sasa Serikali ikawa na utaratibu mzuri kidogo wa kuweka mifumo ambayo itakuwa endelevu. Hizi Wizara na Idara zinapohamishwa hamishwa kila wakati, kupima matokeo yake kunakuwa kugumu sana na nafikiri hili nalo ni tatizo la msingi. Tulipokuwa na Wizara

ya Kilimo na Mifugo, inategemea aliyekuwa pale alikuwa na hamu na mifugo au na kilimo. Kwa hiyo, *priority* atatoa pengine kwenye kilimo, mifugo akasahau. Ukichanganya Maliasili na Utalii na Uvuvi, aliyekuwepo akiwa hana hamu ya uvuvi, uvuvi atausahau na kushughulikia utalii. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia hizi *structures* vizuri ili tuhakikishe kwamba zinakuwa endelevu na wataalam wanajengwa ili kukidhi mahitaji ya Taifa letu. Hili ni jambo moja la jumla ambalo nimeona niliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumepata Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Ukiangalia *structure* ya juu haina matatizo, lakini nenda kwenye *Local Government*, msimamizi wa *Local Government* inawezekana kabisa ni mtaalam pengine anashughulika na mifugo tu, habari ya uvuvi hajui au anashughulika na uvuvi tu, mifugo hajui. Sasa huku juu inawezekana kuna watalaam wanaohusiana kabisa, lakini ukienda chini, yule mkuu anayeshughulika, pengine eneo lake la kushughulikia ni lile ambalo yeye haku-*specialize* kabisa. Nafikiri hilo nalo linahitaji liangaliwe na ndiyo matatizo ambayo tumeyapata katika *structure* yetu nzima. Kwa hiyo, napenda kuzungumzia kwanza jambo la *structure*.

Mheshimiwa Mwnyekiti, la pili, katika ukurasa wa 103 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna takwimu hapa, kuna hali ya uvuvi Tanzania Bara kwa mwaka 2007/2008. Katika takwimu hizi kuna angalizo chini linasema, uvuvi katika bahari kuu *EEZ* kupitia vyombo vya uvuvi 69 vilivyopewa leseni, Serikali ilikusanya ada ya leseni ya jumla ya Sh. 981m/= na kadhalika.

Sasa nilikuwa najiuliza, ikiwa wavuvi wadogo wadogo wanatozwa leseni na asilimia tano ya rasilimali wanayoipata, hivi vyombo 69 kwamba takwimu hazionyeshi wamevua tani ngapi za samaki? Kwa hiyo, inaonekana kwamba ule ukanda wa kilomita 200 za *nautical miles* tulizoachia bahari kama ni rasilimali au sadaka tumewapa wavue wanavyotaka, waondoke mradi tunakusanya ada ya leseni. Hivi kweli tupo *serious* katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *nautical mile, two hundred miles* umewaachia watu sadaka tu, unawapa leseni ya dola zako 18,000 halafu unasema vueni mnavyotaka. Mvuvi mdogo mwenye kiboti chake kidogo, unamwambia ukirudi huko hata kama umepata kilo 100 ulipe asilimia tano ya pato ulilovua, hawa wengine unawaachia sadaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Waziri wakati anajibu swali langu, alisema mapato haya ni pamoja na leseni. Hapana. Nimeshawahi kuvuna na *trawler* mwaka 2003. Leseni ya chombo inalinganishwa na uzito wa chombo chenyewe, sio samaki unaovua. Huwezi kusema dola 18,000 ndizo hizo hizo zinazochukua meli ya tani 500, ndiyo *revenue* ambayo Serikali inapata kutokana na uvuvi huo, sio sahihi hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo meli 20 *trawler* au 10 mlizonazo mnazitoza vitu vitatu; leseni, *royalty* na wakifika hapa wakivua kamba, wanalipa na *royalty* ya *five percent* kwa sababu meli za uvuvi *trawlers* ndogo ndogo za *prawns* wanakuja kuegesha hapa, meli kubwa haziegeshwi hapa. Kwa hiyo, hamuwatozi ile *royalty* na ndiyo sisi wa

Kambi ya Upinzani na Wabunge humu ndani, mara zote tunasema kwamba, kwa nini hizi meli kubwa wanaovua kule Mtwara, kwa nini wasiende kwenye Bandari ya Mtwara wakatozwa hii *levy* ili Halmashauri pale wakapata mapato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *net* zao zinakwenda kilomita tatu mpaka zinakwenda kilomita tatu mpaka tano, zinakokoa kila kitu halafu zinaleta na hata ukichukua takwimu za Mheshimiwa Waziri hapa, *trawler* inavua *prawns* tani 159, lakini inavua samaki tani 840, takwimu hizi hapa. Kwa hiyo, ina maana unavua *prawns,* lakini unavua na vitu vingine, sasa hawasemi samaki wangapi hapa wametupwa baharini kwa sababu anayevua *prawns* hana haja ya samaki. Kwa hiyo, akivua *prawns* wakifika juu yeye wale samaki wengine wanamharibia biashara, hana hamu nao na bei yake ni ndogo. Kwa hiyo, anawatupa baharini na ndiyo maana Wizara inaweka mtu ndani ya meli ili atazame kama kweli hakuna uharibifu wa kutupa samaki baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa kama chombo chake kina *capacity* ndogo anaamua kuwatupa baharini samaki ili apate *prawns* aweke kwenye *storage tank* yake. Sasa hizi takwimu hazitusaidii kama hakuna ufuatiliaji sahihi. Njia moja ya kufuatilia vyombo hivi ni kuhakikisha vinakuja bandarini, kuegesha na kuvikagua na kuhakikisha tani ngapi zimepatikana ili samaki wale wasafirishwe chini ya ukaguzi wetu, vinginevyo tunapoteza *resources* za nchi bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi, vyombo hivi ambavyo ndiyo vina uwezo wa kuharibu mazingira zaidi ndivyo vinabobembelezwa kuliko hawa wavuvi wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Tanga kuna vijana wetu wavuvi hawa walikamatwa na neti zao zikachomwa. Kila mmoja iligharimu shilingi milioni 17, wamekwenda kutaka kushitaki, wakaambiwa hamwezi kufungua mashtaka ya aina yoyote. Sasa mimi nataka Mheshimiwa Waziri atusaidie mtu anapokamatwa sheria hii ya *fisheries* inampa mamlaka Afisa anayehusika kuhukumu? Au inampa mamlaka kumpeleka mtu kwenye chombo cha sheria? *(Makofi)*

Pili, hao maskini wa Mungu wanaochomewa zana zao bila ya kuwapa fidia yoyote: Je, ni haki? Nilifanya mawasiliano na Wizara ya *Fisheries* ya Zanzibar, nikawauliza ninyi mnafanyaje? Wakasema sisi tunapowakamata tunamwambia bwana hizi hazifai, chukua hizi. Sasa huyu ndiyo anamkomboa kiuchumi. Lakini hapa mfugaji mdogo anaburuzwa, mchimbaji mdogo anaburuzwa, mvuvi mdogo anaburuzwa, watu wakubwa tunawabembeleza mpaka leo sheria za madini hapa zinasuasua hatutaki kubadilisha. Sasa nasema, *we are not doing justice to this people*. Tena na sheria yenyewe tumekubali mwaka 1995, Wizara hii iliruhusu *ring net,* leo wanaambiwa *ring net* haifai. Sasa kwa nini Wizara haifanyi utafiti ni nini hasa wanakitaka? Kwa nini hamjengi mahusiano na hawa wavuvi wadogo ambao takwimu bahati mbaya hazionyeshi lakini idadi yao sio chini ya shilingi milioni 3.4 ukichukua ukanda wote pamoja na maziwa. Hawa ndiyo wanaotupa chakula hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatuwasaidii. Ukiangalia miradi yote tuliyonayo, fedha zote tulizonazo, unazungumzia *peanut* kutokana na mahitaji ya wavuvi haya waliyohitaji. Lakini baya zaidi unaviacha vyombo vikubwa vinaharibu mazingira, vinachukua samaki na kadhalika. Tulikuwa na meli 144 leo Mheshimiwa Waziri katika taarifa yake anasema meli 66. Meli 66 alizonazo zina wastani wa tani 500 kila meli moja. Kwa sababu zinakaa zile ni viwanda vyenyewe vinafanya *packing*, kila kitu. Hakuna takwimu za mapato humu ndani. Sasa nasema hii ni hatari. Nimesikia Mheshimiwa Waziri akisema kwamba hili atashughulikia. Kwa hili moja mimi nilitaka alifanye.

La kwanza, hili tangazo alilotoa Mkurugenzi kwa mujibu wa sheria hebu Mheshimiwa Waziri akae na hawa wavuvi wadogo, kidogo walilalamika wakasema hupendi kukutana nao, hebu Mheshimiwa Waziri akutane nao sasa. Akae nao wasikilize matatizo yao, namna gani tunaweza kuwasaidia hawa wavuvi wadogo wako sio chini ya milioni tatu hapa Tanzania wakishughulikiwa vizuri, tutaondoa umaskini kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Lakini pili, lazima tuhakikishe sasa meli zinazopewa leseni zinakuja kwenye bandari kuu ili ziweze kutoa *royalties* tuweze kuwauzia mafuta, tuweze kuwapa maji, tuweze kuwapa vyakula ili soko letu na mapato yetu yaweze kuongezeka. Sasa hivi meli hizi zote zinachukua mafuta nje huko huko kwenye bahari kuu, wanapata maji huko huko nje wanafanya kila kitu nje. Kwa hiyo, hatupati rasilimali hapa. Sasa nasema hii ni rasimali kubwa ni mapato makubwa tunayapoteza bila ya sababu. Nashukuru kama Mheshimiwa Waziri analikubali.

Kwa hiyo, naomba *circular* aliyoitoa Mkurugenzi bado iwe *reviewed*, mkae na wavuvi, msikilizane mwone njia gani mnaweza kuwasaidia. Hamuwezi mkachukua vitu tu mkavichana chana, mkavichoma moto bila ya kukaa nao mkaona: Je, mtamsaidiaje? Hivi ukishachoma moto ukishamuacha pale ndiyo umemsaidia? Kwa nini hatuendi kule Mwadui basi, Williamson nao tukawafukuza wakaondoka kesho asubuhi, *why are you doing to this small people*? Hebu fanyeni *justice* katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana twende tukakae na wavuvi, tukakae na wafugaji, wafugaji hapa wanalalamika sana, mimi ningetegemea sasa kuna *program* ya kusema hivi Tanzania tunataka kuwa na wafugaji bora wangapi wa maeneo gani? Tunawawezeshaje? Hii mifugo mingine ambayo haitupendi iweje? Tunaiondoaje kwa utaratibu badala ya kuwasukuma tu watu? *These are things we have to do it*. Hatuwezi tukafanya tu mambo hivi kiholelaholela, lazima tufanye vitu kisayansi. Mkoa wa Pwani wao hawana tatizo kwa mfano kufuga kisasa, waelekeeni basi ili muwachukue wengine huko waje wajifunze huyu aliyepata manufaa mkulima na mfugaji anapenda sana kubadilika kwa kuona kama hakuona hawezi kumbadilisha kwa urahisi. Mchukueni mfugaji wa kimasai ambaye anafuga ng’ombe wengi mkamweke na mfugaji wa Kimasai ambaye tayari amebadilika katika ufugaji wake, atabadilika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivyo hivyo wavuvi, Mheshimiwa Waziri ametaja idadi kubwa, hizi *data* zake naomba kidogo wakazifanyie kazi. Ukichukua idadi

ya vyombo na wavuvi havioani sana. Nilikuwa nafunga hesabu hapa, labda chombo kimoja kina watu watatu kwenye ziwa. Halafu takwimu zake hizi ni ziwa Victoria, mapato yote ni Ziwa *Victoria. Why* Ziwa Victoria? Bahari, ukanda wote unafanya nini? Ziwa Tanganyika linafanya nini?  Tujiulize maswali kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba leo nimwunge mkono rafiki yangu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Labda nianze kwa kusema hivi kwa nini nimesimama hapa kuongea? Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja. Lakini kuna sababu zifuatazo zilizonifanya niongee, moja, Wamasai wanapiga kelele sana kiasi kwamba inakuwa kama vile Wamasai ndiyo wenye ng’ombe wengi sana wakati Wasukuma waliwaazimisha Wamasai ng’ombe na sasa wakijidai sana kusema kama vile ng’ombe hizi ni za kwao na wao ndiyo matajiri sana! Hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Shinyanga ndiyo unaoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya ng’ombe, Wamasai tuliwaazima tu, lakini wanapiga kelele kweli kweli, sababu moja hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili, kwa sababu za makusudi kabisa, nalazimika kuongea kuitetea Wizara hii kwa sababu nafahamu changamoto walizonazo. Kwa hiyo, ni vizuri tushirikiane pamoja kuyajadili mambo na hususan kuwapigia debe. Namfahamu kaka yangu Mheshimiwa Waziri uchapa kazi wake hauna mashaka. Lakini kuna kitu kimoja muhimu sana. Nyenzo za kufanyia kazi. Kwa bajeti hii bado ni ndogo kama ilivyokuwa huko nyuma.  Kwa hiyo, kwa kuwa bado tunaendelea, ni vizuri tuwatetee wenzetu ili kusudi wapate fedha za kutosha ili waweze kukabiliana na changamoto nyingi walizonazo. Sina mashaka na utalaam ndani ya Wizara hii, watalaam nawafahamu wote uwezo wao wa juu sana, wanajitahidi kadri inavyowezekana, lakini bado hela haitoshi. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii na sekta nzima ya mifugo bado kama ninavyosema inatengewa fedha kidogo hii ni bahati mbaya kwa sababu mimi huwa napenda kusema na narudia kusema hapa mifugo hii mingi tuliyonayo ni fedha iliyo juu ya ardhi tukiweka mifumo endelevu fedha hii italeta manufaa kwa ajili ya uchumi wa nchi hii, kwa ajili ya kuondoa umaskini wa watu wetu na kwa ajili ya kuboresha maisha ya Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya tatu iliyonifanya niongee ni kwa sababu, kama nilivyosema, Mkoa wa Shinyanga ndio unaongoza kwa kuwa na mifugo mingi, kwa hiyo, ukikaa hapa Bungeni halafu usiseme kuhusu mifugo sio vizuri. Sisi Shinyanga mifugo, pamba, madini na leo nakamilisha hili lingine la mifugo. Nianze kwa kupongeza juhudi za Serikali kuwezesha kupatikana mwekezaji kwenye kiwanda cha nyama cha Shinyanga ambacho mwekezaji anasubiri maji ya kutoka Ziwa Victoria pamoja na kibali cha Baraza la Hifadhi ya Mazingira ndiyo aweze kuendelea na hatua nyingine zinazofuata.

Napongeze juhudi kubwa za ujenzi wa kiwanda cha maziwa pale Shinyanga cha kwanza Mkoa wa Shinyanga kinachofanywa na Mhashamu Askofi Balina akisaidiwa na Meneja Mikomangwa. Kinajengwa pale Ibadakuli na sasa kuna vituo vya Chibe, Iliapa, Lubaga na Seseko tayari vimeshajengwa vya kukusanya maziwa vinatarajiwa kujengwa vingine vinne Nhelegani, Kolandoto, Ibadakuli na Ndala. Tunahitaji takribani shilingi milioni 100 hivi ili kuweza kuikamilisha hiyo kazi na tungependa wale wapenzi wa Shinyanga na wapenda maziwa kwa ujumla wasaidie katika kuhakikisha kuwa tunakamilisha kazi ya ujenzi wa vituo vinne vya kukusanyia maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Shinyanga ndiyo unaochangia asilimia 25 ya nyama inayoliwa Dar es Salaam. Lakini Mkoa wa Shinyanga pia ndiko kwenye chimbuko la unenepeshaji, kwa hiyo, pamoja na Wamasai kusema wao wana mifugo sijui mikubwa mikubwa, bwana sisi tunanenepesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, mifugo ni mali na kwa hiyo, ni fedha. Hebu fikiria michango ya shule ile ya Sh. 20,000/= kwa mwaka chukua kuku wanne tu mmoja kila baada ya miezi mitatu ni shilingi sio chini ya Sh. 5,000/= kwa hiyo, Sh. 20,000/= unaipata kwa kuku wanne, hiyo ni mifugo. Kuku wanaliwa kweli kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, utajiri huu wa mifugo uko mikononi mwa watu binafsi yaani wafugaji, kama tunavyofahamu. Lakini kwa ujumla wake ni utajiri tulionao hapa nchini. Hivyo utajiri huu kwanza tuuthamini, ndiyo maana nashangaa baadhi yetu tunaposimama tunaanza kutaka kuponda sana mifugo, nashangaa kweli kweli. Hebu jaribu kufanya hesabu ya mifugo yote tuliyonayo katika maana ya fedha uone ni fedha kiasi gani. Sasa suala lisiwe ni kulaumu, bali kusema ni namna gani utajiri huu, fedha hii, tunaweza tukaibadilisha sasa kuwa fedha ya karatasi na ikatusaidia kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia utajiri huu tuutumie kwa kuvuna sio kwa kupunguza. Unaposema kupunguza maana yake ni kwamba hiki kitu hakitakiwi, lakini unavuna kwa sababu unajua ni fedha. Tunavuna pamba, tunapata fedha; tunavuna mifugo, tunapata fedha. Hata hivyo mimi nadhani uvunaji huu ambao unahitaji kuwekewa mfumo ambao utahitaji fedha ndiyo itakuwa ni suluhisho la mwisho katika kuhakikisha kuwa utajiri huu tulionao unaleta faida hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu unapaswa kuzingatia kuwa hatua ya kwanza mfugaji ndiye mwenye ng'ombe, pili, mnenepeshaji wale wenye ranchi wote wanaweza kuwa ni wanenepeshaji wazuri; tatu, viwanda na machinjio; nne, soko lenyewe kwa sababu mfugo hatimaye lazima uliwe. Kwa hiyo, katika mlolongo wote huo kuna fedha inakwenda inatumika pale mpaka mwisho na hatimaye Taifa linaweza likafaidika na mifugo hii tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvunaji wa mifugo ni budi tuzingatie kuwa ili uweze kufanya kazi, tunaposema ni lazima fedha ipatikane na ni Wizara hii katika hatua ya kwanza inayopaswa kupewa fedha ya kutosha kuweza kuweka ule mfumo/mifumo ya kuhakikisha kuwa tunaivuna hii mifugo, siyo kuipunguza, ili iweze kutuletea faida

tunayohitaji. Fedha hii tunaihitaji katika kudhibiti magonjwa ili tuweze kujenga majosho ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu bado tuna upungufu wa majosho sio chini ya 1,200 hapa nchini. Shinyanga ni Mkoa wa kwanza kwa uwingi wa mifugo una upungufu wa majosho 400. Kwa hiyo, usipokuwa na majosho huwezi ukaogesha hata kama ukitoa hizi dawa za ruzuku bado huwezi ukaogesha. Lakini bado tunazihitaji hizi dawa za ruzuku za kuogeshea mifugo. Mimi nikiangalia ruzuku ya shilingi bilioni 1.4 haitoshi. Tunahitaji fedha nyingi zaidi ili kusudi tuwe na mifugo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia fedha hii inahitaji kunenepesha, hivyo tupate malisho bora, maji ya kutosha, suala la malambo linakuja hapa. Bahati mbaya nikiangalia hata Kampuni ya Ranchi za Taifa nayo bado inapewa hela kidogo sana na kwa hiyo, haiwezi ikawa ni chombo muhimu cha kuhakikisha kuwa mifugo mingi waliyonayo wafugaji inanunuliwa, wanainenepesha, inakwenda kwenye viwanda na hatimaye inapatikana nyama. Kwa mfano, lakini niipongeze Serikali kwamba sasa kuna wawekezaji ambao wataingia ubia na *NARCO,* lakini *NARCO* unapoipa bilioni tatu tu ili ije iingie ubia na hawa watu haitoshi. Mimi nasema wakati mwingine tusisubiri hela za bajeti tu, tutumie mtindo wa hatifungani *(revenue bond). NARCO* wanakwenda wanakopa benki kwa dhamana ya Serikali, atazalisha watamlipa yule mwenye benki; baadaye dhamana ya Serikali inaondolewa, unapata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunahitaji uhamilishaji kwa ajili ya kuboresha mifugo kwa siku za baadaye, kutumia madume haya yatakwenda taratibu kidogo, lakini ukitumia mtindo wa uhamilishaji mambo yanakwenda haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji uwepo wa machinjio na viwanda vya usindikaji. Tunahitaji uwepo wa vituo vya kukusanyia ngozi ili zinunuliwe kwa madaraja na kupelekwa viwandani kwa madaraja na kuuzwa kwa madaraja ili tuweze kupata fedha nyingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kutafuta masoko ya ndani na ya nje kwa ajili ya mazao haya ya mifugo ili kusudi ule mtandao uweze kukamilika. Kama haya na mengine hayatTaweza kutekelezwa kikamilifu tutaendelea na dhana ile ya kuchukia mifugo kwa sababu tutaendelea kuwa na mifugo mingi ambayo haileti faida katika ujumla wake katika maisha ya Watanzania na kwa hiyo, tukashindwa kuutumia huu utajiri kwa ajili ya kubadilisha maisha ya wananchi na kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama hatuwezi kuyafanya haya, mtazamo hasi uliopo miongoni mwetu kuhusu mifugo utaendelea, mifugo itachukiwa, wafugaji watachukiwa, lakini utachukiaje utaraji mkubwa wote huu? Tuweke mifumo ya kuwezesha kuvuna na Wizara hii ndiyo ipewe hizo fedha . Nimetoa mifano ya namna ambavyo fedha inaweza ikapatikana. Azma ya kuwa na Wizara kama hatuwezi kuyatekeleza haya ya kuhakikisha kuwa hatimaye mifugo inavunwa kwa kiwango cha kutosha kwa mfano robo ya mifugo hii tuliyonayo ikavunwa kwa mwaka tutapata hela nyingi sana na kwa hiyo, uwepo wa Wizara hii unakuwa na maana, vinginevyo kama

kelele hizi tutakwenda kupiga kwamba inaonekana mifugo haina sababu sana, kwa nini tuendelee kuwa na Wizara hii? Baadaye suala hili litakuja kujitokeza. Pia Ilani ya Uchaguzi ya CCM inasisitiza sana kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kumalizia naunga mkono hoja tena kwa Wizara hii kwa siku za usoni ipate hela nyingi zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye hoja hii nzuri yenye manufaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimekwishaondoka kwenda Jimboni, lakini nilipogundua kwamba leo ni Wizara ambayo imenilea mimi, imenikuza, imenisomesha nikafikia hapa ndipo nikaona nirudi. Nakushukuru sana kwa kunifikiria kunipa nafasi ya kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Mheshimiwa John Magufuli na Mheshimiwa John Magafuli ni jirani yangu, ni mshauri wangu na ni mshawishi wangu kuwa Mbunge, maana yake nisingeona anavyofanya kazi, nisingependa kuwa Mbunge, baadaye nikaona anavyochapa kazi nikaona kumbe Ubunge unaweza kuleta maendeleo yako. Ni kijana mchapa kazi na mchacharikaji, sitaki nimwite mzee kwa sababu kazi zake ni za machachari, amefanya kazi nzuri kwenye Wizara ya Miundombinu na amekwenda kwenye Wizara nyingine, tukaona yaliyotokea na hapa tuna matumaini makubwa ingawa wengine wamesema kwamba labda siyo mzoefu kwenye uvuvi. Labda niwape taarifa Mheshimiwa John Magufuli nusu ya Mji wake upo majini, kwa hiyo, uvuvi kwake nadhani hata kuogelea anazidi watu wengi wanaotoka sehemu za Pwani. Ni mzoefu sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa James Wanyancha naye nampongeza, ni mzoefu, Jimbo lake linaungana na Mto Mara ambao ni sehemu ya Ziwa Victoria, kwa hiyo, ni mzoefu. Katibu Mkuu wa Wizara hii ni mtu wa Mara na Mara imezungukwa na Ziwa Victoria, kwa hiyo, ni mvuvi vilevile na kama siyo mvuvi, basi amekuwa akivuka Ziwa Victoria wakati huo akiwa anapanda meli kwenda kusoma. Hatukuwa na shule za sekondari kule na Naibu Katibu Mkuu nafikiri atakuwa amekwenda Nyumba ya Mungu kule ameona ona maji na yeye. Nimesikiliza sana wachangiaji, wengi wamenipa faraja, lakini baadhi yao wamenyima faraja, lakini siwalaumu, ni kwa sababu hawaelewi mifugo na umuhimu wake katika nchi yetu. Kuna nchi zinaishi kwa kutegemea mifugo na ni tajiri kwa sababu ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi nadhani hatujayaweka vizuri haya masualai. Juzi tulipewa Semina juu ya ngozi tu, kila mtu akashangilia akatamani kufuga ng'ombe na akatamani kufanya biashara ya ngozi. Sasa leo tumesahau vipi? Sasa huyo alizungumzia ngozi: Je, mtu mwingine akizungumzia faida ya gundi kwenye ng'ombe, mwingine akizungumzia nyama na robo tatu wengine hawali nyama humu, lakini wengi tunakula nyama, kama huli nyama unakunywa maziwa, kama hunywi maziwa mbolea yake unaitumia. Sehemu nyingine kuna matatizo hata mkia wa ng'ombe wenyewe ni feni, pembe ni mapambano ndani ya nyumba. Jamani! Wote humu unakuta mkienda

katika Mbuga za Wanyama mnachukua zile pembe, ni mapambo. Mifupa ukiitengeneza katika nchi zilizoendelea wanaitumia kutengeneza chokaa sehemu ambapo hakuna chokaa kwa kutumia mifupa ya ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu wa Rufiji sasa hivi badala ya kula nazi watakula samli, watoto watanenepa, watapata akili na watazaa watoto wengi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ng'ombe ni zao ambalo lina manufaa sana. Niseme tu ndugu zangu, bahati mbaya kwa sababu tunakosa masoko, wengine wanakosa mahali pa kuchungia kwa sababu ya mazingira magumu na kwa sababu ya kukosa majosho imetokea wafugaji wamekuwa wakihama. Lakini nawaomba wale wanaopokea wafugaji wasiwaone kama adui, mbona sisi tumepokea wawekezaji wa kuchimba madini pale Geita, wamebomoa milima yote na nini hatusemi, tunawaona ni wawekezaji, sasa kwa nini wasiwachukue hao Wasukuma au Wamasai wakamwona amekwenda kwao ni mwekezaji? Wawaweke mazingira, hao ni wawekezaji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni mwekezaji, ndugu zangu wa Rukwa hao ni wawekezaji, muweke mazingira mazuri watawasaidia. Nimesikitika kusikia kwamba eti wafugaji kule Shinyanga walileteswa chakula wakati wa njaa. Chakula wakati wa njaa tuliwanyima tukasema kwamba wao angalau walikuwa wanawezaweza, tuliwapa chakula wale ambao hawana ng'ombe. Ninao ushahidi, lakini wale wenye ng'ombe tuliwaambia hebu vumilieni wenzetu wapate angalau nyie mnayo maziwa na mnaweza kuchinja ng'ombe. Kinachotakiwa ni kuwawezesha tuwawekee masoko, tuwatengee maeneo yao, tusiwanyang'anye, tuwashauri namna gani waweze kuvuna mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, yeye anatoka maeneo ya wafugaji. Kuna suala lililotokea Ihefu, kwa kweli linasikitisha. Nia ya Serikali ilikuwa nzuri lakini baadhi ya viongozi wakaharibu zoezi hilo, wakasema wanaondoa wafugaji kumbe wenyewe ndiyo wanaonunua ng'ombe kwa Sh. 5,000/=, Sh. 3,000/=, Sh. 2,000/= unawaondoa namna gani wakati unawachukua wewe. Nasikitika, nasikia kiongozi huyo bado yupo. Jamani, ni mfano gani kwa Serikali yetu? Ni mfano mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ripoti hiyo isomwe, ikiwezekana hatua zichukuliwe, hao wanachafua Serikali yetu. Kiongozi wa namna hiyo ni wa nini wanachafua Serikali yetu? Wafugaji wanamwelewa namna gani? Wewe unachukua ng'ombe 500 unaweka kwako, halafu wewe unamwambia yule mwenye ng'ombe 800 aondoke, wewe unaweka hao ng'ombe kwako halafu anaendelea kuwaongoza wengine. Kweli kuna mtu atamsikia! Kuharibu Serikali ya CCM nzuri ambayo inajali watu na inawajua watu wote! *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili suala la Ihefu tunaomba Mheshimiwa Waziri yeye alikuwa Wizara ya Miundombinu alikuwa anajua vipimo vyote vya barabara, barabara zote za Mijini na barabara za vijijini alikuwa anazijua zote. Najua kwenye uvuvi sasa hivi atafahamu nimekwishamwona ameanza kuhesabu samaki wote, kwa hiyo, ametaja idadi ya samaki, ni hatari yeye kwa kweli na uwezo wake ni mkubwa wa aina ya peke yake. Ingawa

nasikia alisoma *Chemistry* sijui na wale wadudu alikuwa anawahesabu namna gani? Sielewi. Lakini tunaomba hilo aliangalie. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyanyasaji umefanyika hata kwangu umefanyika. Katoro umefanyika, sehemu hata kwako Mheshimiwa Waziri umefanyika kwenye sehemu za wafugaji wa Bwanga na kule, *DC* mmoja wa Biharamulo, viongozi wamekuwa wakiwaambia haya nyie ondokeni, nyie tokeni porini na nyie ni wakimbizi wananunua ng'ombe wao na wanawanyang'anya wametesa hata Karagwe imetokea. Tusingependa hiyo hali iendelee watu wakawa ni wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo wafugaji tunawaona ni watu ambao hawana maana. Lakini nadhani wafugaji ni kwamba tunawa-*mis-handle*. Nasikitika kwa hali iliyotokea Rufiji, lakini niwaombe watu wa Rufiji walipofika wafugaji, nafikiri kuna kitu kimetokea kama walifika watu wakaletwa haya mmewaleta, hakuna ng'ombe asiyekunywa maji, sasa nyie mmewapeleka kule Bondeni mnafikiri wale ni Wamasai na Wakusuma wale hawana akili, wale mmewapeleka katika sehemu ambayo haina maji, wanawafuata nyinyi na wenyewe wanaleta na kwa sababu wa Rufiji wakiona ng'ombe wanakimbia wanaingia mashambani, Msukuma anakaa kimya au mfugaji anakaa kimya, sasa anakuwa na uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakiwekewa mazingira mazuri, wafugaji watakaa, wana akili siyo kwamba hawana akili, wengine wanasomesha watoto na wengine tumesoma kwa mtindo huo na tumesomeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema wafugaji siyo wabaya jinsi wanavyofikiriwa. Wafugaji wamekuwa ni msaada, maeneo mengine baadhi ya *centres* wamekuwa wakifuatwa wanaambiwa kwamba ndiyo wenye mali, ndiyo wanaambiwa wachangie, wanachangia maendeleo ni kuwasaidia tu. Ninaomba tuwajengee kiwanda cha nyama, kiwanda cha kutengeneza mafuta, kiwanda hata cha ngozi na kila kitu. Inasikitisha unapokwenda madukani unakuta, juzi nilikuwa hapa Dodoma kuna Mhindi mmoja anauza nyama anaitwa Kennedy *from South Africa* sijui nini na nini. Jamani nyama Kennedy *from South Africa* wakati kuna nyama nzuri ya mnadani pale kutoka Afrika Kusini na Geita hivyo hivyo na Shinyanga utakuta ni hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama watu watakuwa wanauza kwa bei nzuri inakwenda tu siyo kuwanyang'anya na kuwafukuza na kuwapora hovyo hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nisije nikalisha pua nikasahau mdomo. Naenda Busanda. Busanda wafugaji wangu pamoja na wakulima hawana amani. Naomba wapewe mabwawa. Kuna mabwawa yalikuwepo, yaliachwa na wakoloni, sasa hivi yamekufa, kuna lambo la Chikombe, lambo la Kamena, Nyarugusungu na sehemu nyingine za Geita hata Kasamwa hata kwake Mheshimiwa Waziri pale Bwanga hawana bwawa, kuna wafugaji wengi pale. Ninajua hawezi kujisemea, lazima tumsemee jamani, Serikali msaidieni huyo Mheshimiwa John Magufuli, anapata taabu kweli pale Bwanga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu wafugaji wa Mheshimiwa Waziri John Magufuli na wangu, pale sehemu za Bwanga porini wanafukuzwa, kuna pori la Bwanga pale, halafu kuna pori la Lwamugasa, halafu kuna pori la Chibingo lile halina wanyama wala halina nini, kuna tumbili tu na sisi wafugaji wengi hawali tumbili, waruhusiwe wachuge mle, tuiombe Wizara ya Maliasili na Utalii, juzi walijibu vizuri, sasa Mheshimiwa Waziri anisaidie kuwasukuma hao, amwambie Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwamba awaruhusu wafugaji wetu wachungie mle, wasianze kugombana kusudi watu walime mpunga vizuri na wengine walime pamba yao vizuri, lakini wale wachungie mle, wasiruhusiwe kukataa miti wala kulima, basi. Tuwaruhusu wakae mle. Mimi ninajua yeye ni mwenzangu, atajitahidi kulifanyia hilo kazi na kwingine wapate mfano mzuri, lazima tuanzie kwetu. Usifanye mifano kwingine tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wavuvi, ninajua Mheshimiwa Waziri anachoma moto nyavu akiwa na uchungu kidogo. Bahati mbaya na yeye eneo lake ni la wavuvi, tuwasaidie. Nyavu hizo mimi nilikuwa najiuliza, kwa nini tunachoma moto nyavu? Kwa nini tusichome moto viwanda vinavyotengeneza nyavu hizo? Mvuvi amekwenda dukani, amenunua nyavu, sasa nyie mruhusu gongo, mnywaji mnaanza kumgombeza yeye wakati gongo mnaiona inatengenezwa pale, Polisi anapita pembeni, zinakuja lawama tena. Tuwabane hao! Halafu mnasema watu wengine wadogo sana hapo wanaishi wenyewe hivyo hivyo tu, mimi nadhani tuwabane *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la ujambazi majini. Wavuvi wetu katika Ziwa Victoria wanapata shida na wananyang'anywa mitego. Kuna malalamiko maeneo ya Mganza kwake Mheshimiwa Waziri kule, kuna maeneo yangu ya kwenda sehemu za Kasamwa, ni shida, Bukondo na mpakani pale, kila wanapokwenda ni taabu. Wamenunua simu, lakini jamaa wanawazimisha chini ya maji na wengine hawajulikani wamekufa namna gani. Kwa hiyo, naomba sana wavuvi wasaidiwe. Lakini wajitahidi wajenge kiwanda cha mifugo kwa ajili ya kutengeneza nyama na viwanda kwa ajili ya ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninamuunga mkono ndugu yangu na ninamtakia kazi njema Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba. Sasa anakuja Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hii Wizara nyeti na mpya ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Awali ya yote nianzie kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuwa katika Wizara hii nikiwa na matarajio kwamba tutapata mabadiliko kama ambavyo tumekuwa tukiyaona katika Wizara nyingine ambazo Mheshimiwa Waziri wakati alikuwa akizisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, kwanza kabisa nimesikitishwa sana na utayarishaji wa taarifa ambazo zimo katika bajeti hii kwa hotuba hii, imenionesha wazi kwamba watayarishaji wana taarifa chache sana kuhusiana na uvuvi unaofanyika

katika Ziwa Nyasa. Nasikitika nitakuwa *biased* kwa sababu mimi ni mdau na ni mzaliwa wa Kijiji cha Kihagara kando ya Ziwa Nyasa na uzalendo unaniisha ninapoona kwamba watu wale hawasaidiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu hiki kilichosheheni majedwali chenye kurasa 128 hakika *paragraph* zake ukizijumlisha zote zilizogusa uvuvi katika Ziwa Nyasa hazifiki hata nusu kurasa. Nimenukuu, imegusiwa kidogo katika ukurasa wa tano ambao unazungumzia kwa ujumla ya mapato 40, 41, 74 na ikamalizika. Katika hayo yaliyoandikwa ni kwamba imezungumzwa kwa ujumla wake. Kwa mfano, inazungumza kwamba utafiti umefanyika, samaki katika Ziwa Nyasa wanaonekana kupatikana katika maji ya kina kirefu na inatakiwa kuvuliwa kwa ndoano. Ikaishia hapo. Kwa hiyo, wanashauriwa wavuvi wawahi kuvua asubuhi sana ili wapate hao samaki. Wanavua vipi? Kuna tatizo lipi la ziada? Haijaelezwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha, mara ya mwisho wakati niko kwenye ziara nimepitia maeneo ya Chiwanda, Mtipwili, Kilosa, Mbambabay, Liuli, Kihagara sikuweza kumalizia Ziwa lote la Nyasa. Hali ya watu hawa ni mbaya *as if* hawako Tanzania. Tunaomba muwasaidie Mheshimiwa Waziri. Kando ya Ziwa Nyasa wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyepita ametembelea eneo hilo, ukweli ni kwamba hakuna zao lingine la biashara linalotegemewa zaidi ya uvuvi na mazao yale ya chakula, sana sana ni kidogo mpunga na mihogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa pia nikafanya stadi nikasema, hivi kuna kitu gani katika maeneo ya Mwambao? Ukiangalia maeneo ya Mwambao wa Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na Bahari ya Hindi ukifuatilia kihistoria wale wananchi asilia wanaotoka maeneo hayo, hali zao ni duni, wanaoendeleza maeneo hayo ni wale ambao wanatoka maeneo mengine ndio wanaokuja kuwekeza. Nikajiuliza, kuna mahusiano gani? Je, yawezekana mwinuko wa ardhi *attitude* ina mahusiano na watu wanaokaa maeneo hayo mpaka wakawa labda sio wajasiriamali au wakawa maskini kiasi cha kwamba hali zao zinakuwa duni na mpaka wanakuja wawekezaji wanawafukuza na hawawezi kuwekeza? Tatizo liko wapi?

Sasa bajeti hii inanionyesha wazi kwamba hakuna msisitizo na msimamo katika suala la uvuvi ambalo wao toka asili yao wamejifunza kuvua na kupata mapato yao kutokana na uvuvi. Matokeo yake wanakuja wawekezaji wanawanyang’anya ardhi, wanawekeza vitu vingine, wao wanazidi kusukumwa kama ambavyo tunaona Dar es Salaam wanasukumwa tu wanatoka nje ya mji, wanasukumwa tu kwa sababu hawana uwezo wa kuwekeza wao kama wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi ni kwamba, mara ya mwisho nilipokwenda Malawi ziwa hilo hilo moja, kule kuna samaki, chambo unawapata saa yoyote! Unapofika kwenye hoteli *chambo fish* ndio wako Ziwa Nyasa, lakini kwenye hoteli zetu huwezi kuwapata. Kule Ziwa Nyasa unakuta kama ukitaka kula dagaa, basi ule dagaa wanaotoka Kigoma, wale wa pale hawapatikani. Kwa sababu lile ziwa lina mawimbi makali mno na ndio maana mara ya mwisho nikasema Mheshimiwa Waziri tafadhali tuongozane, mimi nitaendesha mtumbwi mwenzangu tukae mtumbwi mmoja

twende huko halafu nitakuacha upalaze wewe wakati wa kurudi. Kusema kweli hali ni mbaya! Naamini utalia hiyo siku mpaka wakuokoe wale wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, sio kwa ajili ya kutisha, ninaomba nikiwa na uchungu, nalia niko chini ya miguu yako na ndani ya viatu vyako wasaidie wananchi hao, wana hali mbaya! Samaki wana madini muhimu, wana *calcium* ndiyo inatengeneza *brain*, ndiyo maana watu wanaokula samaki kwa wingi wanakuwa na akili nyingi. Kwa nini hatuwawezeshi watu wakavua samaki wa kutosha?

Sasa hivi tunalalamika masuala ya *cholesterol* kutokana na nyama tunasema mafuta tunakimbilia samaki hao, samaki hatuwatoi huko baharini tunafanyaje? Lakini naelewa hii Wizara ni changa, imekuwa haijapewa bajeti ya kutosha. Kwa sababu bajeti iliyowekwa hapa kusema kweli nitasema hivi imezingatiwa nini, kwa sababu bajeti zile tunavyoangalia nafananisha sawa na mwili wa binadamu. Naona kuna kichwa, kuna bajeti zenye sura ya kichwa, kama hakipo unakufa; bajeti za moyo, bajeti za mikono sasa hii sijui ni ya kidole, kiasi kwamba hata kikikatwa mtu ataishi. Kwa hiyo, haina haja ya kupewa umuhimu wa pesa za kutosha. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri awezeshwe, bajeti yake iongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa sababu gani? Tutafikia mahali tutaona kwamba tunakwenda kiuchumi, lakini kuna jamii tunazitenga. Lakini pia katika suala la uvuvi ukiangalia ukurasa wa tano inaonyesha wazi mapato yaliyokusanywa kutokana na uvuvi yalikuwa ni makubwa kuliko yale yaliyotokana na mifugo, tofauti ni kubwa sana. Ziwa Nyasa peke yake ni zaidi ya mara mbili ya yale uliyokusanya kutoka kwenye mifugo.

Lakini nikiangalia huku nyuma katika bajeti na majedwali yaliyoonyeshwa hapa naona tu chanjo, kwa ajili ya majosho, naona kwa ajili ya malambo naona kwa ajili ya mitamba, lakini kwenye uvuvi mimi sioni kitu. Sasa hapo ndio nashtuka, nasema hivi, wale wenzangu waliotangulia walisema kwamba yawezekana Wizara hii kwa sababu wengi mmebobea kwenye ufugaji ndio sababu ambayo imepelekea kabisa uvuvi ukasahaulika hivi. Kwenye uvuvi nimeona hasa katika Mwambao wa Pwani ambao na wenyewe ni mradi unaofadhiliwa kutoka nje.

Kwa hiyo, ni kama vile kuna ushurutishwaji kidogo na tunaomba hata hao wafadhili wasiangalie eneo moja tu. Kule Kigoma kuna ile migebuka iko kule, mizuri kabisa. Maana miradi inakuwa sehemu moja halafu wanatung'ang'aniza katika sura ambazo pengine haziendani na mazingira yetu, mimi naomba tuwashauri kama wana nia ya kutusaidia watusaidie vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimeona katika ukurasa wa 74 naona kidogo Mheshimiwa Waziri niliposema labda twende Nyasa ukaona aah ngoja niweke maboti mawili Ziwa Nyasa. Basi naomba nijaribu kuchangia hapo. Katika maboti hayo mwanzo nilivyoandika barua yangu niliomba utupe maboti angalau hata mawili uwekeze katika yale maeneo ambayo dagaa wanapatikana kwa wingi sana. Lakini sasa kwa sababu naona humu yako mawili tu, basi tupate moja katika kijiji cha Kihagara nilipozaliwa au Liuli, popote Mheshimiwa Waziri atakapoona inafaa. Kwa sababu maeneo hayo toka

asili ni kwamba ndio maeneo yenye kuweza kuvua dagaa kwa wingi sana na hata ndugu zangu walioko huko wananisikia, nasema ukweli.

Kwa hiyo, ni vyema tukawezesha maeneo hayo ili tuweze kusaidia ongezeko la uvuvi katika eneo la Ziwa Nyasa. Kwa hiyo, nimeomba aidha, Mheshimiwa Waziri atupelekee Kihagara au Liuli kadri utakavyoona inafaa, lakini mimi nilizaliwa Kihagara. Kwa hiyo, akiona apeleke Liuli sawa sawa, asije akasema kwamba nimeshurutisha kwa sababu ya sehemu ninayotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kilio changu katika bajeti zinazofuata naomba kwamba bajeti ya Wizara hii iongezeke. Naamini Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kama watawezeshwa kwenye uvuvi, kuna mambo mengi sana ya kufanya na naamini kwamba inawezekana Wizara hii ilikuwa inaonekana kama vile haina *activities* nyingi kwa sababu ya uzito uliokuwa ikipewa na ukifuatilia hata kwenye *data base* zake huenda usipate *literature* nyingi za Wizara hii kwa sababu ilikuwa ni kama ki-*subsidiary* na mpaka nikajiuliza, kuna Wizara ya Kilimo na Chakula tunaipigia kelele sana ipewe bajeti kubwa, sasa nikafikiria hivi nyama na yenyewe sio chakula au samaki sio chakula? Nikaona labda pengine tupate *definition* nzuri ya chakula. Lakini kama chakula kama tunavyokipatia uzito, basi Wizara hii inastahili kupewa bajeti ya kutosha kwa sababu pia ni chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kumchosha sana Mheshimiwa Waziri kwa kunisikiliza maneno yangu ya msingi amenisikia, naomba pamoja na hayo maboti mawili yatakayokuja mwaka huu kwa kweli akumbuke vijiji vile Chiwanda, Mtipwili, Kilosa, Mbamba Bay, Liuli, Ngumbo, Lituhi na Mbaha. Vyote hivyo ambavyo tunategemea Mungu akibariki iwe Wilaya, hawana zao lingine la biashara zaidi ya uvuvi. Tafadhali naomba Mheshimiwa Waziri aiwezeshe ili iwe ni Wilaya ambayo itakuwa na mtazamo wa kuweza kuzalisha na kuwa katika jiografia ya Tanzania na suala la mapambo kutokana na samaki wanaotoka ziwa hilo. Tumeona ameandika, lakini hatujaona *focus* yake ikoje? Naamini mapambo ya samaki hao kama watauzwa nje yangeweza kuingiza pato kubwa zaidi na hivyo kuwezesha wananchi pamoja na Serikali kupata mapato ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mngetutayarishia mpango, jinsi gani sasa hao wajasiriamali ambao watakuwa katika biashara za uuzaji wa samaki wa mapambo waweze kuuza hao samaki ama sivyo watakuwa wanaangalia tu wale vitui wameng'aa kule, wana rangi mpaka za zambarau, za njano, lakini hawataweza kuuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kusema sitaunga mkono hoja nikisubiria maboti hayo na mipango ya baadaye ya kuongezewa yatakuwaje. Naomba Mheshimiwa Waziri naye pia ageukie kwenye uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya. Nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri kwamba Jumatatu usisahau kujibu lile la safari, usije ukakosa kuungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kuna funguo nadhani mojawapo ni ya gari zitakuwa hapa mezani kwa Makatibu, endapo mtu amepoteza funguo zake. Waheshimiwa Wabunge, hoja hii itaendelea hadi Jumatatu tarehe 04 Agosti, 2008 na wachangiaji wapo wa kutosha kwa siku ya Jumatatu ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwakumbusha kwamba kesho asubuhi tutaanza na *VIP Race* kama tulivyotangaza asubuhi na vifaa vyote tayari viko pale ukumbi wa Msekwa endapo kuna Mheshimiwa hajapata vifaa ni vizuri kupitia sasa, itakuwa vigumu kuvigawa asubuhi. Lakini pia kesho baada ya hiyo *VIP Race* ndiyo maana kwenye saa 4.30 tukatangaza kwamba kutakuwa na semina kuhusu Sheria ya Ushindani na Vita Dhidi ya Bidhaa Bandia Nchini. Kwa hiyo, pamoja na kukimbia, kama mtakuwa mmechoka kidogo msisahau kuhudhuria semina hiyo ambayo inatarajiwa kuanza kwenye saa 4.30 hapa hapa Ukumbi wa Msekwa.

Mwisho, naomba kuwashukuru Makatibu kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya siku nzima ya leo na Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mliotupatia, nawatakia kila la kheri kwa *week-end* hii na kwa kuwa basi shughuli zilizokuwa zimepangwa katika meza hii kwa kutwa nzima ya leo zimekamilika, basi naomba kusema kwamba naahirisha Kikao cha Bunge hadi Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,
Tarehe 4 Agosti, 2008 Saa 3.00 Asubuhi)*